

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 24 Aprili, 2019

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI - MSEMADI MKUU WA KAMBI  
RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA  
NCHI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Maswali.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 122

**NEC Kufanya Uhakiki wa Majimbo ya Uchaguzi Zanzibar**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (*ZEC*) imeongeza idadi ya Majimbo ya Uwakilishi kutoka 50 hadi 54, kabla ya ongezeko hilo Majimbo ya Uwakilishi na Ubunge yalikuwa sawa kwa ukubwa, mipaka na idadi ya wapiga kura. Ongezeko hili limefanya Majimbo mawili ya uwakilishi kufanywa Jimbo moja la Ubunge:-

Je, ni lini Tume ya Taifa ya Uchaguzi itafanya uhakiki wa Majimbo ya Ubunge Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA  
NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka

1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) imepewa jukumu la kuchunguza mipaka ya kiutawala na kuigawa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Majimbo ya Uchaguzi wa Ubunge. Kwa kuzingatia Ibara tajwa, Tume imepewa jukumu la kuchunguza na kugawa Majimbo ya Uchaguzi ya Ubunge mara kwa mara; na angalau kila baada ya miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilifanya uhakiki wa Majimbo ya Uchaguzi wa Ubunge mwaka 2015 kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015. Baada ya uhakiki, jumla ya Majimbo 26 yalianzishwa kutokana na maombi 77 yaliyowasilishwa Tume kutoka Halmashauri 37 na Majimbo ya Uchaguzi 40. Hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuhakiki tena Majimbo ya Uchaguzi wa Ubunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Zanzibar baada ya kutangaza kufanya hivyo kwa majibu wa Katiba.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Khamis.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la Majimbo yaliyoongezwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar mwingiliano wake unaleta usumbu na kupunguza kasi ya maendeleo. Nataka kujua: Je, Tume ya Taifa iko tayari kuongeza Majimbo manne ili yaende sambasamba ili tufanye kazi vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı langu la pili *ZEC* ni Wakala wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi; *NEC* kwa Zanzibar kwa Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Wabunge, lakini wanatumia daftari moja, kura inapigwa siku moja katika chumba kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchaguzi wa 2015 *ZEC* walifuta matokeo ya Uchaguzi wakati ambapo Wawakilishi na Madiwani walishatangazwa katika Majimbo yao na

wamepewa hati zao za ushindi, katika mazingira kama hayo, nataka kujua: Je, *NEC* wametumia sheria gani ya kukubali uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Wabunge kutoka Zanzibar? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la kwanza kuhusu Majimbo manne ya Uwakilishi, kama katika majibu yangu ya msingi yalivyo sema, suala hili la ugawaji wa Majimbo yanafanyika kwa mujibu Ibara ya 75(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika maneno yallyotumika ni baada ya kufanya uchunguzi na kugawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mujibu wa Katiba hii, ni kwamba pindi pale matakwa ya Katiba hii na hasa katika Ibara ya 98(1)(b) ambayo inasomwa pamoja na Orodha ya Pili ya Nyongeza *item* Na. 8 ya kwenye Katiba ambayo inahitaji ongezeko la Wabunge wa Zanzibar, lazima pia ipitishwe na theluthi mbili ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wenzetu kutoka Zanzibar. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Katiba, jambo hilo linawezekana baada ya taratibu hizo kufuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusiana na matokeo ya uchaguzi; kwa mujibu wa Katiba yetu inazungumza vyema kabisa kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la kusimamia Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge kwa upande wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, chaguzi nydingine zote zinakuwa chini ya *ZEC* ambao pia kwa mujibu wa Katiba nao wana majukumu ya kusimamia uchaguzi katika ngazi hiyo. Kwa hiyo, jambo ambalo limetokea ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema, maana yake ni kwamba Tume ya Taifa

ya Uchaguzi ilitumia *mandates* yake ya Katiba ambayo inampa mamlaka ya kusimamia uchaguzi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali. *Sorry, Mheshimiwa Nachuma.*

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuna Wilaya ambazo zina Majimbo mawili na Wilaya hizi ziligawanywa Majimbo kwa sababu ya ukubwa wa zile Wilaya na idadi kubwa ya watu, lakini hivi sasa kuna tetesi ambazo zinatembea chini kwa chini huko Serikalini kwamba yale Majimbo ambayo yaligawanywa kutokana na ukubwa lakini pia na wingi wa watu yanataka kurudishwa kuwa Jimbo moja moja.

Je, kama hilo ni kweli, hatuoni kwamba Serikali ita-*hinder* utendaji wa Majimbo hayo? (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge mwenyewe alivyoli-phrase swalı lake kwamba ni tetesi, naomba nami kwa upande wa Serikali tusijibu tetesi, ikiwa rasmi itasemwa kama ni rasmi. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swalı linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini linaelekezwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Massay.

Na. 123

**Serikali Kuwaongezea Mishahara Madiwani**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Madiwani nchini wanafanya kazi kubwa sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongeza posho na mishahara au maslahi yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kazi kubwa wanayofanya Waheshimiwa Madiwani katika kusimamia shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao. Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali imekuwa ikipandisha posho na maslahi ya Madiwani kwa kadri mapato ya Halmashauri yanavyoongezeka. Kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ilipandisha posho ya Madiwani kuititia Waraka wa mwaka 2012 kutoka shilingi 120,000/= hadi 250,000/= kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimia 108.3.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali ilipandisha tena posho za Madiwani kuititia Waraka wa mwaka 2014 kutoka 250,000 hadi 350,000 kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimia 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali inalipa pia posho ya madaraka kwa Wenyevitii wa Kamati kiasi cha shilingi 80,000/= kwa mwezi na posho ya kikao kiasi cha shilingi 40,000/= kwa mujibu wa Waraka wa Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo kikubwa kinachotumika kupandisha posho za Madiwani ni uwezo wa Halmashauri kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri husika. Serikali itaendelea kuthamini na kutambua kazi kubwa na nzuri inayotekelawa na Waheshimiwa Madiwani na kuongeza posho hizo kadri makusanyo ya mapato yanavyoongezeka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Halmashauri hazina uwezo wa kuwalipa Madiwani na mpaka sasa Madiwani wengi wamekopa posho zao; na kwa kuwa mapato madogo na hali hii inapelekea Madiwani kutolipwa stahiki zao: Je, Serikali ina mpango gani kubadilisha namna hii ili Serikali ilipe toka Hazina kama walivyo Watumishi wengine sasa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa Vijiji nao wanafanya kazi sawasawa na Madiwani na Watendaji, hao Ma-*VEOs* na *WEOs* wanalipwa mishahara: Je ni lini sasa Serikali itawaona Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ili kuwalipa posho au mshahara? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Waitara kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Swali lake la kwanza anapendekeza kwamba Waheshimiwa Madiwani walipwe posho kutokea Hazina na kwa maelezo yake anasema kwamba kuna Halmashauri ambazo hazina uwezo. Ukweli ni kwamba Halmashauri ambayo haina uwezo wa kujiedesha inapaswa kufutwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, lazima vyanzo viwe vimeainishwa na vinasimamiwa na hii hatujapata malalamiko rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoelezea ni kwamba Halmashauri kwa mapato yake ya ndani wanajipangia namna ya kuweza kulipa Waheshimiwa Madiwani. Kama Serikali itapata uwezo mkubwa zaidi ya huu uliopo sasa, hili jambo litafanyiwa kazi. Kwa sasa Halmashauri zote zinapaswa kulipa na tunajua kuna Halmashauri ambazo Waheshimiwa Madiwani wanazidai fedha mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaelekeza kila Mkurugenzi ahakikishe kwamba Madiwani wanalipwa stahiki zao kwa sababu wanafanya kazi kubwa. Swali lake la pili, anapendekeza pia kwamba kuwe na mpango wa kulipa Wenyeviti wa Mitaa. Ni kweli, nami ni Mwenyekiti wa Mtaa Mstaafu kule Kivule Dar es Salaam Ukonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maelekezo ya Serikali kwamba kila makusanyo yote ya Halmashauri asilimia 20 inabidi irudi katika Mitaa yetu na Vijiji, inawezekana jambo hili halitekelezwi vizuri. Naomba niwaelekeze Wakurugenzi, Wenyeviti wa Vijiji kwa sasa, ile asilimia ambayo inapaswa kurejeshwa baada ya kodi kukusanya katika eneo lao, ipelekwe na waweze kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuwalipa asilimia nyingine zaidi hii au Serikali Kuu ichukue jukumu hilli, kwa kweli itategemea uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MICH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, asilimia 20 ambayo inatengwa ili irudi kwa ajili ya Wenyeviti wa Mitaa, kuna Halmashauri nyingine hiyo asilimia 20 ni ndogo sana. Ni kwa nini Serikali isitoe *commitment* ili hawa Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Vitongoji wapate mshahara kwa sababu wao ndio wanafanya kazi kubwa sana katika shughuli zote za maendeleo huko tunakotoka? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nia njema ya Serikali tungeweza

kuwalipa Wenyeviti wa Mitaa mishahara. Hapa tunazungumzia hali ya uwezo wa Serikali kufanya kazi. Wenyeviti wa Mitaa ni wengi sana, pamoja na kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoelekeza, pamoja na kwamba hayo mapato ni madogo, kwa kinachopatikana, kuna Wenyeviti wa Mitaa hawalipwi kabisa fedha hizi na tuna malalamiko mengi wameleta. Tumeelekeza Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wahakikishe hawa watu wanalipwa stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kuweza kuwalipa kwa sasa, tumelichukua, tutalifanyia kazi. Uwezo wa Serikali ukiruhusu, hawa viongozi wenzetu watalipwa stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ukweli ni kwamba pamoja na maelekezo yanayoelekezwa kule chini, viongozi hawa wa Mitaa na Vijiji, Vitongoji hawalipwi posho zao; na kwa kuwa Serikali kwa namba ya viongozi hawa kuwa kubwa inashindwa kuongeza posho zao:-

Serikali haioni umefika wakati sasa kufikiria uwezekano wa kuwalipa kiwango fulani cha pesa viongozi hawa pale wanapomaliza muda wao wa Uongozi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona Waheshimiwa Wabunge wanazungumzia posho za Madiwani na posho za Wenyeviti wa Mitaa; naomba nitumie nafasi hii kusema tu kwamba

wakati tunamalizia hoja yetu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, suala la posho za Madiwani zile ambazo zilikuwa zimezungumzwa, Mheshimiwa Waziri ameshatoa maelekezo kwa Madiwani wote wa Halmashauri watapata Waraka wa maelekezo kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuondoa sintofahamu ya posho za Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali alilouliza Mheshimiwa Mkundi, tulipokee; ni kweli kwamba Wenyeviti wa Mitaa baada ya kustaafu kuna kiwango cha fedha wanapaswa kulipwa. Sasa maoni ya Mbunge ni kwamba tuangalie namna ya kuongeza kiwango hiki (*lump sum amount*) kama watasema ni shilingi 500,000/= au shilingi 1,000,000/= kwa mkupuo itaweza kuwasaidia. Jambo hili tunalipokea, tunalfanyika kazi, kadri uwezo wa Serikali utakavyoruhusu, tutalitekeleza kwa sababu ni jambo jema kwa ajili ya viongozi wenzetu hawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa jambo muhimu kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaofanya bidii na kushirikiana na Wabunge ni Madiwani na Wenyeviti katika kuhamasisha maendeleo katika maeneo yao; sasa kama Halmashauri inaweza kuwa na uwezo wa kulipa posho zaidi: Je, Serikali inaweza ikaruhusu Halmashauri ile yenye uwezo kuongeza posho kwa hawa ambaa ndio wanaoweza kuongeza mapato hayo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge sawa na Wabunge wengine wote ambaa wameendelea kuwasemea Waheshimiwa Wenyeviti wa

Mitaa na Waheshimiwa Madiwani, nao ni viongozi wenzetu na hakuna namna ya kuweza kuwapuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza hapa kwamba wakati wa Bajeti kulikuwa na mjadala; na kweli kuna Waraka ambao umepelekwa katika Halmashauri zetu ambao unaelekeza *fixed amount* kulipwa kwenye posho za Madiwani ukiacha ile posho ya mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema Mheshimiwa Waziri aliahidi mbele ya Bunge lako Tukufu na naomba niseme, bado ametoa ametoa maelekezo, ndani ya muda siyo mrefu sana, Waraka kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuititia Katibu Mkuu utaenda kwenye Halmashauri zote na suala hili la kulipana Madiwani kulingana na uwezo wa Halmashauri litatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa Tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Joseph Leonard Haule Mbunge wa Mikumi na linaelekezwa bado kwa Ofisi ya Waziri wa Nchi, TAMISEMI.

Na. 124

### **Uhaba wa Vituo vya Afya Jimbo la Mikumi**

**MHE. JOSEPH L. HAULE** aliuliza:-

Jimbo la Mikumi lina uhaba mkubwa wa Vituo vya Afya na hata pale ambapo kuna Kituo, basi dawa na Wataalamu ni tatizo:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo hilo sugu la uhaba wa Vituo vya Afya na dawa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ina jumla ya vituo vya afya vitano. Kati ya vituo hivyo viwili vipo katika Jimbo la Mikumi ambavyo ni Kituo cha Afya Kidodi na Ulaya. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kituo cha Afya cha Kidodi kilipatiwa jumla ya shilingi milioni 400 za ukarabati na kwa sasa kinatoa huduma za upasuaji kwa akinamama wajawazito. Vilevile Kituo cha Afya Kidodi kimepatiwa vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 95 ili kukiwezesha kuanza kutoa huduma. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019 zahanati ya Mikumi ilipewa jumla ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuongeza majengo ili iweze kukidhi vigezo vya kupandishwa hadhi kwa Kituo cha Afya na mpaka sasa kazi ya ujenzi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi wa Kata ya Malolo inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Afya Malolo kwa kutumia mapato ya ndani ambapo ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje, maabara, jengo la upasuaji na wodi ya wazazi yapo katika hatua ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilipokea kiasi cha shilingi billioni 1.07 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vitendanishi. Vilevile katika mwaka wa fedha 2018/2019 hadi Februari, 2019 Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imepokea shilingi milini 849 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vitendanishi ili kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018 Serikali iliajiri jumla ya wataalam wa afya 8,238 ambapo Halmashauri ya Kilosa ilipata jumla ya wataalam 42 wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kujenga vituo vya afya kote nchini pamoja na kuajiri wataalam wa afya kulinga na upatikanaji wa rasilimali fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Haule.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu hayo ya Serikali, kwenye Kituo cha Afya cha Ulaya nilishauliza hapa mara nyangi kwamba Serikali itatusaidiaje maana ni kituo cha muda mrefu na kimeshachakaa na Serikali iliahidi kwamba itatupatia fedha za kuweza kukarabati kituo hichi cha Ulaya. Je, ni lini sasa Serikali italeta pesa kwenye kituo hiki cha Ulaya ambacho kimechakaa sana na ni kituo muhimu kinachituhudumia Kata za Ulaya, Muhenda, Zombo pamoja na Masanze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kituo cha Afya cha Malolo kinajengwa kwa nguvu za wananchi wakishirikiana na Mbunge na Halmashauri na sasa kimefikia kwenye kiwango cha lenta. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza nguvu za wananchi ambazo sasa hivi zimeonekana ili waweze kujipatia huduma katika kituo cha Afya cha Malolo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Haule Joseph, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo katika swalii lake la nyongeza anaongelea Kituo cha Afya cha Ulaya ambacho kimechakaa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote, ni ukweli usiopingika kwamba vituo vya afya ambavyo vimepatiwa fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi vinaonekana viko bora kuliko vile

ambavyo vilikuwa vyasiku nyingi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vile vituo vyafya ambavyo vilijengwa miaka hiyo na hadhi yake haiendani na vituo vyafya vyasasa, iko katika utaratibu wa kuhakikisha kwamba vinakarabatiwa ili vilingane na hadhi ya sasa. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge aendelee kuiamini Serikali kama ambavyo tumeweza kupeleka fedha katika hivyo vituo vyafya na zahanati yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaongelea jitihada ambazo zinafanya na halmashauri pamoja na nguvu yake mwenyewe nampongeza kwa sababu suala la afya linahusu jamii yote ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Pale ambapo wananchi wamejitoa kwa ajili ya kujenga vituo vyafya Serikali na sisi tunaunga mkono kwa sababu ndio azma ya Serikali nayo iko kwenye ilani yetu ya CCM.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kata ya Mnyagala ni kata ambayo ina idadi ya watu wengi na vijiji kadhaa ambavyo hakuna huduma ya kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moshi Sulemani Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wana hamu vituo vyafya vijengwe na nimepata fursa ya kwenda jimboni kwa Mheshimiwa Kakoso tukaenda mpaka Mwese kule kuna kazi nzuri sana inafanyika ya ujenzi wa kituo cha afya kama

ambavyo kazi nzuri imefanyika Kituo cha Afya Mwese, naomba nimtoe wasiwasi kwamba hata hicho kituo ambacho ana-*propose* kwa kadri nafasi itakavyoruhusu hatua kwa hatua tutahakikisha tunawasogezea wananchi huduma ya kupata matibabu ya afya kwa jirani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Matembe.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Ikungi Mashariki halina kabisa kituo cha afya. Je, ni lini sasa Serikali itajenga vituo vya afya?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Matembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anaongelea Ikungi Mashariki wakati mwingine ataongelea Ikungi Magharibi, lakini niombe tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo tumekuwa tukitekeleza na tumefikisha hivyo vituo vya afya 352, safari tunayo na tutazingatia maeneo yenye uhitaji mkubwa na sasa kama na eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge analitaja kwamba lipo mbali na lina *population* kubwa, naomba nimhakikishie kwamba katika awamu inayokuja tutazingatia maombi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sekta ya afya kwa ujumla wake ina tatizo kubwa sana la watumishi, takribani asilimia 48 hakuna watumishi na hii imeathiri zaidi kwa sababu ya zoezi zima la uhakiki wa vyetii feki, ambapo tuliamiwa baadhi ya vituo ya afya vilifungwa. Nataka kujua nini mkakati wa Serikali

pamoja na kwamba wanajenga vituo, wana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba vituo hivi vya afya vyote vinapata wataalam ili lipunguze tatizo kubwa la akhnamama na watoto ambao wanafariki?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyeekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyeekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba mahali popote ambapo vituo vya afya vinajengwa vinakamilika, zahanati zinajengwa zinakamilika, hayabaki yakawa majengo ambayo tunayatazama, tutahakikisha kwamba vifaa vinapelekwa na wataalam wanapelekwa. Mheshimiwa Lyimo ni shahidi, siku tukiwa ndani ya Bunge hili Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Mkuchika alisema kama yupo Mbunge ye yote ambaye eneo lake zahanati imefungwa au kituo cha afya hakina wataalam kabisa apeleke orodha, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma zinatolewa.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, naomba nikuhakikishie, kuna kipindi ambacho tulitangaza nafasi *especially* kwa ajili ya Madaktari tuliweza kufanya *mopping*, hakuna Daktari hata mmoja ambaye alikuwa ame-*qualify* akabaki bila kuajiriwa. Ikafikia mahali ambapo Madaktari wote wameajiriwa na wengine hawajaripoti. Kwa hiyo pia tuna tatizo juu ya wataalam wenywewe kuwepo maana na *demand* nayo ni kubwa si kwa Tanzania peke yake, wengine wanaenda kutafuta *green pastures outside this country*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Omar Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni Mjini na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Na. 125

## **Hatma ya Kipande cha Barabara ya Handeni – Mziha**

**MHE. OMARI A. KIGODA** aliuliza:-

Je, ni lini hatma ya kipande cha barabara ya Handeni- Mziha ambacho Serikali iliahidi kwamba Mkandarasi akishalipwa ujenzi utaanza, hasa ikizingatiwa kuwa barabara hiyo inaunganisha mikoa miwili?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Handeni- Mziha yenyeye urefu wa kilometra 70.1 ni sehemu ya barabara ya Handeni- Mziha-Turiani-Dumila yenyeye urefu wa kilometra 154.7. Sehemu ya Handeni -Mziha (kilomita 70.1) iko katika Mkoa wa Tanga na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Handeni – Mziha-Turiani umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga jumla ya shilingi billioni mbili kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Handeni- Mziha- Turiani kilometra 104 kwa kiwango cha lami. Aidha, katika mwaka wa Fedha 2019/2020 tumeponga kuitengeta barabara hii fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kuwa nia ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Handeni –Mziha-Turiani ili kuiunganisha Mikoa ya Tanga

na Morogoro kwa lengo la kuchochaea na kuinua uchumi wa maeneo husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigoda,

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza kabisa napenda kuishukuru Serikali kwa kusikia kilio cha Wanahandeni cha muda mrefu kwa kuitengea hela hiii barabara. Barabara ya Mziha - Handeni matatizo yake ni sawasawa na barabara inayotoka Handeni kwenda Kilindi. Barabara hii inaunganisha mikoa karibu minne ambayo ni Tanga, Manyara, Dodoma mpaka Singida. Barabara hii asilimia kubwa wanayoitumia ni wakulima na huwa wanapata tabu sana

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali sasa.

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni lini barabara hii inayotoka Handeni kwenda Kilindi itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omar Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inayo mpango wa kujenga barabara hiii kutoka Handeni kilometra 461 inapita katika maeneo ya Handeni, Kivirashi, Kijungu, Kibaya, Njoro, Mrijo chini inakwenda Chemba hadi Singida. Tunao mpango wa kujenga barabara hii na tayari imeshasanifiwa. Niseme tu kwamba katika mwaka huu wa fedha unaokuja tutapendekeza kwenye Bunge lako ili tuanze kujenga kwa kiwango cha lami barabara hii muhimu kwa

sababu barabara hii itakwenda sambamba na bomba la mafuta ambalo litajengwa. Kwa hiyo ni barabara muhimu sana, kwa hiyo nimwombe tu Mbunge avute subira kwamba tutakuja kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwenye maeneo ambayo ni korofi ambayo yanapita eneo la Kilindi, kwa mfano, eneo la kutoka kwa Luguru kwenda Kibirashi ni eneo ambalo kidogo lina ukorofi, tumepanga katika mwaka unaokuja kwamba wakati tuna harakati za kujenga kiwango cha lami tutaiimarisha eneo hili kwa kujenga daraja katika eneo la Kigwangu. Mheshimiwa Kigua naona anapiga makofi pale anafahamu eneo hili lina changamoto, kwa hiyo tutakuja kuimarisha wakati huo Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kujenga kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Kama nyumba nzima imesimama, Mheshimiwa Chegeni, halafu Mheshimiwa Monko.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda tu kumkumbusha kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi barabara ya kutoka Dutwa Jimboni kwa Mheshimiwa Mwenyekiti kuja Ngasamo kuja mpaka Nyashimo iwekwe kwa kiwango cha lami na maandalizi yameshaanza kidogo kidogo. Nataka tu nipate *comfort* ya Serikali, ni lini sasa utekelezaji halisi wa barabara hii utaanza kwa ajili ya kuweka lami?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Kwandikwa, majibu kwa barabara hiyo muhimu sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Chegeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Chegeni nafahamu barabara hii

tumeizungumza sana, ni barabara muhimu na hatua kama alivyosema mwenyewe kwamba ziko hatua kwenye ujenzi wa barabara hii tumeshazifikia. Kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Chegeni kwamba tunaendelea kuhakikisha kwamba kila tukipata fedha barabara hii tunaijenga ili tuweze kuikamilisha barabara hii muhimu. Kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Chegeni na wananchi wa maeneo yote ya Dutwa na Simiyu kwa ujumla kwamba tunawaunganisha vizuri katika maeneo yao.

**MWENYEKITI:** Sawasawa, Mheshimiwa Monko.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Singida- Ilongero –Ngamu ambayo pia inaunganisha Mkoa wa Manyara ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Singida. Barabara hii ilitangazwa kipande cha kilometra 12.6 kutoka Njuki kwenda Ilongero kujengwa kwa kiwango cha lami tangu mwezi Novemba mwaka jana.

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni lini ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hiyo kutoka Njuki kwenda Ilongero utaanza? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumejipanga kujenga barabara hii muhimu kutoka Singida- Ilongero- Ngamu tunakwenda mpaka Hydom na tumetenga fedha katika mwaka huu wa fedha unaoendelea, zoezi la usanifu ili

kujenga barabara hii yote inaendelea. Hata hivyo, kipande hiki cha barabara anachokizungumza kutoka eneo la Njuki kwenda llongero ni sehemu muhimu sana kwa kuwashudumia wanachi wa Singida Vijijini. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na utaratibu wa harakati za manunuzi, zikikamilika tu tutaanza ujenzi wa barabara hii muhimu, kwa hiyo Mheshimiwa Monkoo avute subira tunakwenda llongero kujenga barabara hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuniona. Matatizo yaliyopo Handeni-Mziha-Kibindu mpaka Mbwewe yanalingana kabisa na hii barabara ya kutoka Handeni kwenda Mziha. Je, ni lini Serikali inakuja kutujengea barabara ile kwa kiwango cha lami kama ambavyo sasa hivi nyumba zote zimepigwa *X*kupisha ujenzi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza...

**MWENYEKITI:** Hapana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliiano, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge anauliza juu ya barabara ya kutoka Mbweni inakwenda Kibindu ikipita kwa Luhombo itaungana na barabara hii niliyojibbia swali la msingi kwa maana ya kwamba kuwaunganisha wananchi wa maeneo haya na barabara hiyo itakuwa inakwenda Tanga na sehemu hii kweli ina uzalishaji mkubwa. Niombe tu Mheshimiwa Ridhiwani kwamba avute subira kwa sababu najua barabara karibu zote zipo kwenye mpango mkakati wetu wa Wizara na ikimpendeza tuonanane baadaye tuitazame hii barabara

kwamba kwenye mpango wetu wa kipindi cha miaka mitano tumekipangia nini kipande hiki cha barabara kwa maana ya kwamba inajengwa kwenye kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sasa tunaiboresha barabara hii na mimi nimeipita mara kadhaa kwamba iko katika kiwango kizuri kwamba inaendelea kuwapa huduma nzuri zinazohitajika wananchi wa maeneo haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum na bado linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 126

**Ndege za Serikali Kufika kila Mkoa wenge Kiwanja Nchini**

**MHE. HALIMA A. BULEMBO (K.n.y. MHE. KHADIJA NASSIR ALI)** aliliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea na zoezi la kununua ndege:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuhakikisha kuwa ndege hizo zinakwenda kila mkoa wenge kiwanja cha ndege pamoja na nchi jirani ili kusaidia kushusha gharama za usafiri?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Eng. Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha kuwa Kampuni ya Ndege Tanzania (*Air Tanzania Company Limited*) inakuwa na ndege za kutosha ili kuweza kutoa huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi kwa ufanisi na tija. Uwepo wa ndege mpya na za kutosha kutaiwezesha *ATCL* kuweza kuhimili ushindani katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi wa mtandao wa huduma za usafiri wa anga katika kila mkoa wenye kiwanja cha ndege na nchi jirani, unatekelezwa kwa kufuata Mpango Mkakati (*Corporate Strategic Plan*) wa *ATCL* wa miaka mitano unaoishia mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Mpango wa Biashara unaoandaliwa kila mwaka. Hadi sasa, *ATCL* inasafirisha abiria katika mikoa tisa (9) na katika nchi tano (5) kama ifuatayo: Kwa Tanzania tunasafirisha Mkoa wa Dodoma, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Mbeya, Kilimanjaro, Zanzibar, Tabora na Mtwara. Pia *ATCL* inatoa huduma za usafiri wa anga kwa safari za Kikanda kama ifuatavyo: Hahaya (Comoro), Harare (Zimbabwe), Bujumbura (Burundi), Entebbe (Uganda) na Lusaka (Zambia). Hivyo, huduma za usafiri wa anga katika kila mkoa wenye kiwanja cha ndege na nchi jirani unatekelezwa kwa kufuata mpango wa upanuzi wa mtandao wa safari za *ATCL* pamoja na uwepo wa abiria wa kutosha ili kuifanya kampuni yetu ijiendeshe kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *ATCL* inatarajia kupokea ndege mbili mpya, *Bombadier* moja na *Boeing* moja mwishoni mwa mwaka huu, matarajio yetu ni kuwa *ATCL* itakuwa na uwezo wa kuongeza mtandao wa safari katika mikoa mingine pamoja na safari za kikanda na kimataifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Bulembo.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nina swali moja tu la nyongeza. Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Shirika letu la Ndege la Taifa, kumekuwepo na malalamiko makubwa ya wananchi hususan kuhusu bei za tiketi. Ni kwa nini Serikali isione kuna

umuhimu wa kupunguza gharama hizi za tiketi ili wananchi wengi waweze kumudu usafiri huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, itapelekea shirika kuongeza *routes* badala ya kuwa na *route* moja kwa siku wanawenza kuwa na *route* mbili mpaka tatu. Mfano Dodoma – Dar es Salaam kuna *route* moja...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo muhimu sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Halima Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za safari za ndege za *ATCL* huwa zinapangwa kutokana na hali ya soko. Ni ukweli usiopingika kwamba *ATCL* wako kwenye ushindani na sisi Serikali tunaendelea kuwa-*encourage* na watu wengine waendelee kutumia usafiri wa anga kupeleka ndege zao maeneo mbalimbali. Sasa hivi wanashindana na watu kama *Precision* na mashirika mengine, kwa hiyo, hayo mashirika mengine kutokana na ushindani huo ndiyo bei inajipanga yenewe, huwa inapangwa kutokana na *market force*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hussein.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa safari za ndani za *ATCL* hakuna mkoa wowote unaoshinda Pemba kwa biashara ya ndege. Mheshimiwa Waziri ulituita mbele ya wadau ukatuahidi kwamba ikifika Novemba/Desemba, 2018 *ATCL* itaanza safari za Pemba. Hadi leo mwezi Aprili, 2019 haijaanza safari kuelekea Pemba, nini kauli yako Mheshimiwa Naibu Waziri?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka jana tuliongea na baadhi ya Waheshimiwa kutoka Pemba kuhusu uwezekano wa *ATCL* kupeleka ndege yao Pemba. Mpaka sasa hivi hatupingi kwamba kuna abiria wa kutosha Pemba lakini ndege zenyewe siyo nyingi kiasi hicho. Naomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine wote waendelee kuvuta subira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Mheshimiwa Rais ametupatia ndege mbili za Serikali, tunaendelea kuzipaka rangi ili zianze kutumika kwa ajili ya abiria. Kwa hiyo, naamini hata Pemba tutawapelekea ndege moja na sehemu nyingine mbalimbali tutaendelea kupanua wigo wa kusafirisha watu kwa usafiri wa anga.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ezekiel Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Wananchi wa Kahama wamekuwa wakiulizia usafiri wa ndege kwa Mkoa wa Shinyanga. Kwa sababu Uwanja wa Ndege wa Shinyanga bado unafanyiwa matengenezo, ni lini *ATCL* itaanza kutua Kahama?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Nditiye, Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ni lini Kahama?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalo ni eneo lingine ambalo Serikali inakiri kwamba kuna abiria wa kutosha hata

*ATCL* inafahamu hivyo lakini bado kuna changamoto kidogo ya uwanja, tunaendelea kurekebisha *runway* iweze kukidhi mahitaji ambapo ndege zetu za *ATCL* zitaweza kushuka. Tayari tumeshamu-*assign TANROADSKwa* ajili ya kufanya *BOQ* ya kurekebisha uwanja huo. Ukiharekebishiwa vizuri tutaanza kutua kwa sababu pale abiria na soko la kutosha lipo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba wake wa Wabunge ama waume wa Wabunge wana haki mbalimbali za kupata huduma kama vile kupita njia za *VIP* lakini cha ajabu ni kwamba wake zetu wanapata shida sana upande wa *VIP*. Je, wana haki ama hawana haki ya kupata huduma upande wa *VIP*, kama vile kwenye feri na viwanja vya ndege? (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Kwenye viwanja vya ndege?

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano viwanja vya ndege pamoa na feri.

**MWENYEKITI:** Haya, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la ndugu yangu wa Nyang'wale, Mbunge mahiri sana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kwamba wake au waume au wenza wa Wabunge wanayo haki yote ya kutumia *VIP* na sijawahi kuona hilo tati zo ninapotembelea viwanja mbalimbali vya ndege. Kwa hiyo, Mheshimiwa kama lilikutokea tunaomba radhi lakini siyo kitu cha kawaida, wenza wa Wabunge huwa wanapata huduma zote stahiki za *VIP*. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Eeeh, haya nitachukua mawili tu, Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa ndege zetu za *Air Tanzania* zimekuwa zikishindwa kutua katika Uwanja wa Ndege wa Arusha kwa kuwa kiwanja hiki ni kidogo na tunaelewa kabisa Arusha ni kitovu cha utalii na nimekuwa nikiongea kila mara na ...

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Serikali imekuwa ikiniahidhi lakini haitimizi, mpaka sasa hivi nimechoka kufuatilia. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupanua Kiwanja cha Ndege cha Arusha?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa *Engineer Nditiye*, Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Kiwanja cha Ndege cha Arusha.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Arusha, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri ukweli kwamba Mheshimiwa Catherine Magige amekuwa akifuatilia sana suala la upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Arusha na nimpongeze kwa sababu kwa kuititia juhudzi zake nimtaarifu rasmi kwamba *TANROADS* sasa hivi wanaandaa *BOQ* kwa ajili ya upanuzi wa uwanja huo kwa mita 200 zaidi lakini pia wanashirikiana na *TAA* katika kuhakikisha kwamba uwanja huo unaendelea kupanuliwa pamoja na kuwekewa *apron* nytingine mpya. Hivi karibuni mkandarasi ataiingia *site* kwa ajili ya upanuzi wa uwanja huo ili ndege kubwa ziweze kuanza kuruka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya Uwanja wa Ndege wa Musoma, nakumbuka Mheshimiwa Rais amefika pale mara mbili na mara zote ameahidi uwanja huo ujengwe kwa kiwango cha lami na uthamini umefanyika, sasa ni zaidi ya miezi sita. Nataka kupata kauli ya Serikali baada ya kuwa kuna sintofahamu, je, mpango wa kujenga uwanja huo upo au haupo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Manyinyi, Mbunge wa Musoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Musoma uko kwenye mipango ya kupanuliwa na kuwekewa *runway* kwa kiwango cha lami na *TAA*. Hivi karibuni nilifanya ziara Mjini Musoma tukakuta kuna changamoto ya fidia ambapo kulikuwa kuna mvutano wa hapa na pale lakini kuna timu ya wataalam imetumwa pale kwa ajili ya kwenda kuhakikisha ile changamoto ya fidia ya shilingi bilioni tatu na milioni mia saba inatatuliwa ili tuweze kulipa fidia na upanuzi uweze kuendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba na linalelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Na. 127

### **Kiwanda cha Saruji cha Dangote kupatiwa Gesi Asilia**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, ni lini kiwanda cha Saruji cha Dangote kitapewa gesi asilia na *TPDC*?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petrol Nchini (*TPDC*)imekamilisha kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gesi asilia katika mitambo ya kuzalisha umeme wa muda katika Kiwanda cha Saruji cha Dangote umbali wa mita 100 kutoka katika Toleo la Kwanza la Gesi (*Block Valve Station No. 1*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya mradi wa kuwezesha matumizi ya gesi kuzalisha umeme kwa Kiwanda cha Dangote ilikamilika na kuanza kufanya kazi Agosti, 2018 ambapo hadi kufikia Aprili, 2019, Kiwanda cha Dangote kimeanza kutumia wastani wa futi za ujazo milioni tano kwa siku kwa kuzalisha umeme.

Awamu ya pili ya mradi inahusu ujenzi wa miundombinu ya bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka BVS 1 kwenda kwenye Kiwanda cha Dangote, umbali wa kilimita 2.7 kwa ajili ya kuwezesha gesi asilia kutumika kama nishati ya kuchoma malighafi ya kuzalisha saruji. Jumla ya gharama za mradi ni shilingi bilioni name na milioni mia mbili. Awamu ya pili ya mradi ilikamilika Desemba, 2018 na sasa Kiwanda cha Dangote kinatumia gesi ya wastani wa futi za ujazo milioni 15 hadi 20 kwa siku kwa ajili ya uzalishaji wa saruji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutimiza ahadi yake kupeleka gesi kwenye Kiwanda chetu cha Saruji cha Dangote. Pamoja na pongezi hizi, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, pamoja na kupeleka gesi kwenye Kiwanda chetu cha Dangote, kuna viwanda vingine Mkoani Mtwara hususan viwanda vya kubangua korosho. Je, Serikali imejipangaje kupeleka gesi kwenye viwanda hivyo ili itumike katika shughuli za uzalishaji katika viwanda hivyo? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni kuhusu usambazaji wa gesi majumbani kwa sababu gesi inayozalishwa ni nyingi lakini matumizi ni kidogo. Je, Serikali imejipangaje kuongeza idadi ya watu watakaotumia gesi majumbani kwa Wilaya ya Nanyamba, Newala, Masasi na Mikoa mingine ili tutumie gesi yetu ipasavyo? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Naibu Waziri, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Subira.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipokee pongezi zake kwa niaba ya Wizara baada ya kukamilisha ahadi yetu ya kumpelekea gesi Kiwanda hiki kikubwa cha Dangote kinachozalisha saruji. Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Chikota kwa kazi nzuri anayofanya katika kufatalia matumizi ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yake mawili ya nyongeza anauliza ni lini Serikali itasambaza gesi katika viwanda ambavyo viko Mkoani Mtwara ikiwemo vya kubangua korosho. Napenda nimtaarifu Serikali yetu inatambua umuhimu wa gesi katika kuwezesha viwanda kuzalisha malighafi kwa kutumia gesi na ina mpango kabambe wa kusambaza gesi katika maeneo ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tuna viwanda zaidi ya 27 ambavyo vinatumia gesi na sasa hivi kuna mradi ambaao unatekelezwa wa kusambaza gesi majumbani na viwandani na hasa maeneo ya Mtwara na Mkuranga. Hivi

ninavyozungumza tayari *TPDC*imeshakamilisha mazungumzo na mkataba wa mauziano ya gesi ya viwanda vyta *KNAUF Gypsum Mkuranga* na *Lodhia Mkuranga*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye viwanda vyta kubangua korosho, naomba niwataarifu wawekezaji wetu wote wenye viwanda katika ukanda huo ambaa bomba la gesi limepita kutoka Mtwara kwamba fursa hiyo ipo, waje tu tuzungumze na *TPDC*. Serikali imejipanga katika uwekezajhi huo na hata katika Mpango wa Matumizi ya Gesi kiasi cha triliioni 8 *cubic fit* zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya viwanda tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili alikuwa anaauliza ni lini usambazaji wa gesi asilia majumbani utafanyika. Nataka nimtaarifu sasa hivi hata Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani alizindua Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa Mtwara na Dar es Salaam. Kazi inayoendelea ni ununuzi wa vifaa mbalimbali na mpaka sasa vimeshanunuliwa vifungashio, vifaa vyta kupunguza mgandamizo wa gesi, vifaa vyta kupimia gesi majumbani. Vifaa vyote hivi vitakamilika ifikapo Mei, 2019.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kazi ya kusambaza gesi katika Mikao ya Mtwara, Lindi na Dar es Salaam inaendelea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali linalofuata linaaulizwa na Mheshimiwa Mattar Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, linalekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 128

### **Watu Wanaowekwa ndani zaidi ya Saa 24**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Jeshi la Polisi lipo kwa mujibu wa sheria na hupaswa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria za nchi. Jeshi la Polisi linapowakamata baadhi ya watu huamuru wawekwe ndani zaidi ya saa 24 na kusababisha usumbufo mkubwa:-

Je, ni kesi zifi mtuhumiwa anapaswa kuwekwa ndani chini ya saa 24.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Engineer Masauni*.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa yote isipokuwa yaliyoainishwa katika kifungu 148(5)(a)-(e) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 yana dhamana. Watuhumiwa wake hawapaswi kukaa mahabusu zaidi ya saa 24. Aidha, watuhumiwa ambao wanakaa ndani zaidi ya saa 24 ilhali makosa yao yana dhamana hutokana na sababu kwamba watuhumiwa hao wameshindwa kutimiza masharti na vigezo vyta kupata dhamana kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa la Jinai Kifungu cha 65 na 66, Sura ya 20 kama ambavyo imefanyiwa mapitio mwaka 2002.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali la kwanza, kuna askari ambao wanawaweka

ndani wananchi wetu bila ya kuwa na makosa ya kuwekwa ndani. Vilevile, wengine wanawaweka ndani zaidi ya saa 24 wakiwa hawana makosa ya kuwekwa ndani saa 24. Je, Wizara yako inatoa kauli gani juu ya Maaskari hawa kuhakikisha wanaepuka kuwaweka ndani wananchi wetu zaidi ya saa 24?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, Watanzania wengi hawana elimu ya sheria hii ya Jeshi la Polisi. Je, Serikali ina mikakati gani ya kutoa elimu kwa wananchi wetu ili waweze kujua haki zao za msingi? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, kwa ufupi tu Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mattar, Mbunge wa Shaurimoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nilieleza kwamba ukiachilia mbali Kifungu 148(5) ambacho Kimeainisha makosa ambayo hayana dhamana, lakini kuna Kifungu cha 65 pamoja na 66 vya sheria hiyo hiyo ambayo vinaeleza ni kwa jinsi gani hayo makosa ambayo yana dhamana itatolewa kwa utaratibu upi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kifungu cha 65 kinaeleza umuhimu wa kufahamu historia na familia ya mhusika lakini kifungu cha 66 kinaeleza kwamba mtuhumiwa huyu ambaye anaomba dhamana anatakiwa aweze kuandika kwa mkono wake kwamba atarudi siku ya kesi yake itakapokuwa imeitwa. Kwa hiyo, pamoja na mambo mengine, dhamira kubwa ni kuona jinsi gani mtu huyu anapoachiwa kwenda nje hawezikuwa hatari kwa usalama wake mwenyewe ama kwa jamii ambayo inamzunguka. Kwa hiyo, inawezekana labda wananchi wanashindwa kufahamu kwamba Polisi wanapomweka mtu zaidi ya saa 24 wakati

makosa yana dhamana kwamba kuna mambo ambayo masharti yake hayajatimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitutoe wito kwa wananchi kuweza kutumia fursa ya Jeshi letu la Polisi pamoja na Serikali kwa ujumla tunapoweza kuzungumza mara kwa mara kuwaelimisha ili wafahamu sheria za nchi yetu na wafahamu haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni jukumu la Wabunge kuweza kuwaelimisha wananchi wetu ikiwemo Mheshimiwa Mattar kupitia mikutano yake mbalimbali katika jimbo lake...

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**...atumie fursa hiyo kuweza kuwawezesha wananchi kufahamu sheria za nchi hii ili waweze kuepuka madhara...

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Waziri wa Mambo ya Ndani alitoa maelekezo mazuri sana kwa trafiki juu ya matumizi ya tochi za barabarani, kutopiga kamerra gari kwa nyuma na kurusha picha kwa wenzao mbele ya safari. Lakini mtindo huu unaendelea na juzi siku ya Ijumaa Kuu walimkamata Diwani wangu wakampeleka polisi pale Himo...

**MWENYEKITI:** Swali, swali Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** ...na kum-*harass*sana. Sasa je, Waziri uko tayari kufanua hayo maelekezo ili yaweze kutumika vizuri wananchi waache kusumbuliwa? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engineer Masauni*.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ya maelekezo ya Mheshimiwa Waziri ambaye ndiyo mwenye dhamana ya mwisho katika Wizara yetu na vyombo ambavyo anavisimamia inapaswa itekelezwe na tulitolea ufanuzi vizuri katika kongamano ambalo tulifanya juzi la usalama barabarani, watu walileta hoja mbalimbali kuhusiana na umuhimu wa kutokuitekeleza hoja ile. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulikuwa tuna vigezo na hoja za msingi za kusimamia maamuzi ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, nisitisize kwamba askari wote nchi nzima waendelee kutii na kufuata maelekezo ambayo tunayatoa kama Wizara. Na sisi tutaendelea kutoa ufanuzi pale ambapo tutapata fursa. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea Waheshimiwa. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Machano Othman Said Mbunge anayetoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, inaelekezwa bado kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 129

**Wizara Inayosimamia Utoaji wa Viza Nchini**

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID** aliuliza:-

(a) Je, ni Wizara ipi inayo wajibika kukusanya fedha za Viza na kusimamia utoaji wa Viza hizo?

(b) Je, kuna mgao wowote kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuititia uwanja wake wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Karume?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Eng. Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Machano Othman Said, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Uhamiaji ndiyo inayowajibika kukusanya fedha za Viza na kusimamia utoaji wa Viza. Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Balozi za Tanzania ndiyo inayo kusanya fedha za Viza na kusimamia utoaji wa Viza katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo yote ambayo yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji Zanzibar kupitia vyanzo vya mapato ikiwemo mapato yatokanayo na Viza kupitia uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume huwasilishwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Machano.

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini pamoja na majibu hayo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wizara mbili zinahusika sana na makusanyo ya Viza katika nchi za nje kupitia Balozi zetu. Je, Wizara ya Mambo ya Ndani inakuwa inafanya nini katika kuhakikisha fedha hizo na zinawekwa katika vitabu vya Wizara gani?

Pili, katika mwaka wa fedha 2018/2019 wa bajeti, Viza kwa upande wa Zanzibar zimekusanywa kiasi gani kwa sababu tuna watalii zaidi ya 500,000 kwa mwaka. Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho kimekusanywa kwa kupitia Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engineer Masauni*.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu hoja ya kwamba kuna Wizara mbili zinashughulikia nataka nimthibitishie tu kwamba baada ya Mheshimiwa Rais kuzindua utaratibu wa kuwa na mfumo wa *e-visa* ambayo inahusisha, tunapuzungumzia *immigration* inahusisha *e-visa e-passport* n.k na sasa hivi nitoe taarifa hii hapo Bungeni kwamba mfumo huu umeshafungwa katika Balozi zetu nchi za nje. Kwa hiyo, sasa ile changamoto ambayo ilikuwepo mwanzo, haipo. Sasa hivi fedha yote tena inaingia katika mfumo na hivyo basi hiyo hoja ambayo Mheshimiwa ameuliza imeshapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na takwimu naomba nimhakikishie Mheshimiwa Machano kwamba nitampatia hizo takwimu baadaye.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Na. 130

**Serikali Kuweka Bei Elekezi ya Pembejeo za Kilimo**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA (K.n.y MHE. CECIL D. MWAMBE)** aliuliza:-

Pembejeo za kilimo ni ghali sana, hivyo wakulima wengi hushindwa kununua na kusababisha kupata mavuno haba. Je, Serikali ipo tayari kupunguza au kuweka bei elekezi iliyo nafuu kwa mkulima ili aweze kupata pembejeo za dawa, mbolea na zana za kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** aliibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha pembejeo za kilimo yaani mbegu, mbolea, viwatilifu na zana za kilimo zinapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu. Hatua hizo ni pamoja na uagizaji wa pamoja, utoaji wa ruzuku, kufuta au kupunguza tozo na kodi zinazochangia kuongezeka kwa bei ya pembejeo na kufanya tafiti katika mnyororo wa thamani wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina utaratibu wa kuweka bei elekezi ya mbolea kuititia mfumo wa ununuzi wa pamoja nchini kwa mbolea za kupandia aina ya *DAP* na kukuzia aina ya *Urea*. Utaratibu huu ulilenga kuhakikisha upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa kipato cha mkulima, Serikali hununua na kusimamia udhibiti na usambazaji wa viuatilifu vya kupambana na milipuko ya visumbufu vya mazao na mimea kama vile kweleakwelea, viwavijeshi, viwavijeshi vamizi, panya, nzige wekundu na nzi wa matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumpunguzia mkulima haribu katika uzalishaji na uongezaji thamani ya mazao, Serikali imeendelea kutoa kutoa mikopo nafuu ya zana za kilimo kuititia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za kilimo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Shirika la Maendeleo la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mbegu na viuatilifu, Serikali inafanya utafiti wa kubaini gharama za uzalishaji wa mbegu kwa kulinganisha na bei za mbegu zilizopo sasa ambazo utaiwezesha Serikali kuamua endapo kuna ulazima wa kuweka bei elekezi katika viuatilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo, Serikali inahamasisha ujenzi wa viwanda vya mbolea, viwatilifu, zana za kilimo na uwekezaji katika mashamba ya mbegu ili kupunguza gharama za pembejeo kwa wakulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa mwaka 2018 kwa maana ya mwaka uliopita Serikali ilipora fedha za wakulima wa korosho zaidi ya bilioni 300 ambazo zilikuwa ni za *export levy* na kusababisha wakulima wa korosho kushindwa kununua *sulphur*. Mwaka huu tumeona uzalishaji wa korosho ulikuwa wa chini sana kwa sababu wakulima wanashindwa kununua *sulphur*.

Je, Serikali ipo tayari sasa msimu huu wa korosho unaokuja kuweza kugawa *sulphur* bure kwa wakulima wa korosho ili tija iweze kuongezeka katika uzalishaji wa korosho? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa bei ya kahawa imeendelea kuwa chini mwaka hadi mwaka na hali hii imetokana na suala la pembejeo kuwa juu sana wakati bei ya kahawa imeendelea kuwa chini kabisa. Je, Serikali iko tayari sasa kuanzisha mfuko wa kuimarisha bei kwenye zao la kahawa yaani *Price Stabilization Fund* ili pale kahawa inaposhuka bei Serikali iweze kufidia kupitia mfuko huo? (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua kuhusu suala la *export levy*, kwanza sio kweli, Serikali haijapora pesa za wakulima wa *export levy*, wakulima wa korosho kule Mtwara. Haya yalikuwa ni mapato ya Serikali kama mapato mengine na tulileta mapendekezo hapa na yalipitishwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, Serikali ilichofanya ni utekelezaji wa sheria ile ambayo ilipitishwa na Wabunge akiwepo Mheshimiwa Haonga. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu kahawa kwamba tuanzishe mfumo wa *price stabilization* kwa ajili ya kufidia pale bei zinapoanguka. Kwanza, ni wazo zuri ambalo na sisi Serikali tunalipokea. Lakini katika mazao sio la kahawa peke yake ambayo yanaanguka katika masoko ya dunia, ni suala la msingi, sio bei. Hatuna uwezo wowote wa ku-control bei katika soko la Kimataifa. Uwezo wetu sisi ambao tumegundua kama Serikali ni tija ndogo wanayoipata wakulima katika mazao kwamba wanatumia gharama kubwa lakini wanachokipata ni kidogo na ndiyo maana sasa hivi tunaimarisha mfumo wa upatikanaji pembejeo ili kuongeza tija kwa wakulima, watumie gharama ndogo wapate mavuno vizuri ili tuweze kushindana katika masoko ya ndani na ya nje ambayo hatuna uwezo wa kupanga bei.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali kuhusu kilimo cha korosho. Juzi wakulima wa korosho wamelipwa fedha chini ya kiwango ni theluthi moja ya haki yao. Je, Mheshimiwa Waziri unawaambia nini wakulima hawa, hizi fedha ndiyo basi au watalipwa zingine na sababu gani ambazo zimefanywa hawakuweza kulipwa hela zote?

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunafahamu malipo yote wanayopaswa kulipwa wakulima wa korosho ni zaidi ya bilioni 723 na mpaka sasa tumelipa zaidi ya bilioni 633. Bado kuna wakulima ambao wanadai Serikali bilioni 100 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wiki iliyopita tulipeleka zaidi ya bilioni 50 na malipo yanaendelea mpaka sasa hivi na kama anachokizungumza, kama tunavyofahamu, wanunuzi wa korosho kabla Serikali hatujaweza kuokoa hali ilivyokuwa, walikuwa zaidi ya 100. Lakini mwaka huu mnunuzi ni mmoja tu na ukizingatia

kwamba hii benki ya maendeleo ya kilimo na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilikuwa haijajiandaa katika ununuzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipaswa mjue kwamba Mbunge ungeipongeza Serikali na Bodi ya Nafaka na Mazao mchanganyiko kwa hatua ilizochukua mpaka leo tumeweza kulipa zaidi ya bilioni 633 na mnunuzi akiwepo mmoja kitu ambacho kilikuwa hakuna kwenye bajeti badala ya kusema kwenda kwenye...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika jibu la msingi la Serikali kwenye suala la pembejeo tunakiri kwamba moja ya sababu ya kupanda na kuongezeka kwa gharama ni kwa sababu pembejeo zinaagizwa kutoka nje. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM, katika Mpango wa Serikali, kulikuwa na ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea Kilwa Mkoani Lindi. Serikali imefikia wapi kukamilisha ahadi hii ya Ilani ya Uchaguzi ili kusaidia upatikanaji wa pembejeo? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri mwenyewe Mbunge. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Naomba nijibu kidogo swali la nyongeza la Mheshimiwa Nape kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi tuliweka ahadi ya kuhakikisha kwamba tunajenga kiwanda cha kuzalisha mbolea pale Kilwa. Naomba nimhakikishie tu kwamba hatua za ujenzi wa kiwanda hicho tuko katika hali nzuri sana. Mpaka sasa hivi wiki mbili zilizopita wataalam kutoka Pakistan, Ujeruman na

Morocco wamekuja kwa ajili ya kuangalia na kufanya tathmini ya mwisho na kufanya mazungumzo na Serikali ili kuhakikisha kwamba kiwanda hiki cha mbolea kinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba baada ya muda mfupi, kiwanda hiki kitaanza kujengwa sambamba na maeneo mengine ya viwanda ambavyo vitajengwa ili kuweza kupunguza gharama za pembejeo hapa nchini. Nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, swali letu la mwisho kwa leo linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Na. 131

### **Migogoro Bainya ya Wananchi na Mbuga za Wanyama**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za kimkakati kuhakikisha kwamba migogoro kati ya wafugaji na wananchi wanaoishi pembezoni mwa mbuga za wanyama inakwisha kabisa?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Kanyasu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kuwepo kwa migogoro mingi baina ya wafugaji na wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi, Mheshimiwa Rais Dkt. John

Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa agizo la kutoviondoa vijiji 396 vilivyoainishwa kuwa na migogoro katika maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Rais kutoa agizo hilo kamati maalum iliundwa kwa lengo la kumshauri juu ya namna bora ya kutekeleza agizo hilo. Kamati hiyo iliongozwa na Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Wizara zingine zilizohusika ilikuwemo Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Ofisi ya Maliasili na Utalii, Mifugo na Uvuvi, TAMISEMI, Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kilimo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imekamilisha utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais na maelekezo ya Serikali kuhusu suala hilo yatatolewa na kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa napenda niishukuru na niipongeze Serikali yangu kwa namna ambavyo imekuwa ikiwajali wananchi hasa wanaoishi vijijini na pia kuangalia namna gani ya kutatua matatizo ya wananchi. Pamoja na pongezi hizo za kupongeza Serikali yangu, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; ni kwa kiwango gani Taarifa ya Wizara hizi ambazo zilikaa kama Kamati ambazo zimeweza kuja na ushauri namna gani ya kutatua matatizo ambayo hasa katika vijiji mfano katika Jimbo langu la Kavuu, vijiji vyangu ambavyo ni vijiji vya lkopa, Itura, Luchima, Sentaunyenye, Iziwasungu, Kabunde na kwagineko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa tuna migogoro mikubwa katika kijiji cha Luchima na mpaka wa TANAPA kwa ajili ya mto wa Kavuu na nilikwishaleta maombi mwaka jana na TANAPA walikwishaanza kujenga kisima kwa ajili ya kupunguza mgogoro uliopo kati ya

wananchi wa Kijiji cha Luchima pamoja na mpaka wao. Je, ni lini sasa hawa ndugu zangu wa *TANAPA* wataweza kumalizia kile kisima ili wananchi wangu wa kijiji cha Luchima waweze kuwa huru katika kufanya shughuli zao za kilimo na uvu vi bila kuingiliwa na askari wa *TANAPA*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kanyasu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akifuatilia kwa karibu sana suala la migogoro baina ya maeneo ya uhifadhi na vijiji ambavyo amevitaja. Naomba nichukue nafasi hii kuwajulisha Wabunge wote ni kwamba taarifa hii ambayo Wizara yetu pamoja na Wizara zingine imeshiriki, itakapokuwa tayari kutumika sasa baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais tutashirikisha Wabunge na viongozi katika Serikali za vijiji vyote na Halmashauri kuangalaia mipaka mipya ambayo tutaiweka ambayo itaondoa migogoro hii ambayo imekuwepo kwa muda mrefu. Kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, swali lake la pili kuhusu *TANAPA* kukamilisha mradi wa kisima cha maji, nawaelekeza *TANAPA* kwa sababu mradi huo walikwishaanza kukamilisha kisima hicho haraka katika mwaka huu wa fedha.

**MWENYEKITI:** Nianze na matangazo.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; tuna makundi mawili kwa wageni waliopo jukwaa la Spika. Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Spika kutoka Chama cha Makatibu Mezani (*SOCATT African Region*) wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, ambao wameambatana na Mwenyeji wao, Katibu wa Kanda wa Umoja wa Mabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola Afrika, Ndugu, Stephen Kagaigai. Tunao huko. (*Makofii*)

Niwatambue wageni wetu hawa, nikianza na Ndugu Cecilia Mbewewe, Katibu wa Bunge la Zambia na Mwenyekiti wa Chama cha Makatibu Mezani Kanda ya Afrika. (*Makof*)

Tunaye pia Ndugu Rana Tiampati Kiteru, Mwakilishi wa Katibu wa Bunge la Kenya, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Makatibu Mezani Kanda ya Afrika. (*Makof*)

Pia tuna Ndugu Thabo Leonard Mofokeng, Katibu wa Bunge la Jimbo la *Free State*, Afrika Kusini ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wahariri ya Makatibu Mezani Kanda ya Afrika (*SOCATT Africa Journal*). (*Makof*)

Tunaye Ndugu Barnabas Bwalya, Msaidizi wa Katibu wa Bunge la Zambia na Afisa Sekretariati wa Chama cha Makatibu Mezani Kanda ya Afrika. (*Makof*)

Tuna Ndugu Elsie Simpamba, Afisa Sekretariati wa Chama cha Makatibu Mezani Kanda ya Afrika. (*Makof*)

Pia tuna Ndugu George Brace, Afisa Sekretariati wa Chama cha Makatibu Mezani Kanda ya Afrika. Karibuni sana wageni wetu. (*Makof*)

Kundi la pili, tunao wageni sita wa Mheshimiwa Spika kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (*TIRA*) hapa nchini ambao ni Dkt. Baghayo Saqware, Kamishna wa Bima; tunaye pia Yusto Tongola Mkurugenzi wa Sheria; tunaye Violet Modechai, Mwakilishi wa Kampuni za Bima; Dkt. Emmanuel Lupilya, Mtafiti Mkuu; tuna Stella Rutaguza, Meneja Kanda ya Kati; na Ndugu Oyuke Phostine, Afisa Uhusiano wa *TIRA*. (*Makof*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Spika kutoka Sweden (*Investors in Tourism and Information Technology Solutions*) ambao ni Ndugu Johan Dahl, Ndugu Steven Humbi Ziota na Ndugu Shija Ramadhani Humbi. Karibuni sana. (*Makof*)

Hayo majina ya Humbi Ziota, nakumbuka *Chief Humbi Ziota* alikuwa Mbunge wetu miaka ya 1970, Mbunge wa Nzega. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, nianze na wageni 93 wa Mheshimiwa Kangi Lugola, Mbunge, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni Meja Jenerali Jacob G. Kingu, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. (*Makofi*)

Tunaye pia Ndugu Ramadhani Kailima, Naibu Katibu Mkuu; Inspeksa Jenerali wa Jeshi la Polisi Nchini, Jenerali Simon Sirro. Karibu sana *IGP*, karibu sana. Tunaye pia Mkuu wa Jeshi la Magereza, Kamshina Jenerali Phaustine Kasike. Tunaye pia Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna Jenerali Thobias Andengenye. (*Makofi*)

Wengine ni Kamishna wa Jeshi Zanzibar, *CP*. Mohamed Hassan; tunaye Kamishna wa Utawala na Fedha, Edward Chogero; Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, *Cl. Johari Sururu*; na Mkurugenzi Mkuu wa *NIDA*, Dkt. Arnold Kihaule. (*Makofi*)

Hawa viongozi wameambatana na Maafisa wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, wakiwemo Mapolisi 65. Sijui wako wapi leo? Mtawaona baadaye. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa *Eng.* Hamad Masauni, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambaye ni mtoto wake, Ndugu Riziki Masauni. Karibu sana mgeni wetu. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango ambao ni Mwalimu Ayoub Sogoi, Mwalimu Tesh Hot, Mwalimu Salm Itukya, Mwalimu Seleiman Halfa, Bi Maarium Bura, Sank Hot na San Hot na Sam Hot. Hawa ni wageni wa Dkt. Ashatu. (*Makofi*)

Tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge

na Waziri wa Kilimo ambaao ni wapigakura wake kutoka Vwawa Mkoani Songwe, Ndugu Imani Mwaipaja na Ndugu Edward Mwamundi. Karibuni sana, (*Makof*)

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mbunge, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi ambaao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Mkuranga wakiongozwa na Ndugu Joseph Mabagala. Karibuni sana kutoka Mkuranga. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga, ambaao ni Diwani Mheshimiwa Khatibu Chitaunga na wapigakura wake kutoka Kata ya Iragga, Ulanga Mkoa wa Morogoro, Ndugu Nestor Lamu na Ndugu Said Kupeleka. (*Makof*)

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Felista Bura, Mbunge, ambaao ni waumini wenzake wa Kanisa la Waadventista Wasabato kutoka Kikuyu Jijini Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Isack Mangire. Karibuni sana Waadventista Wasabato. (*Makof*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge, ambaao ni wapigakura wake kutoka Mbulu Vijiji Mkoani Manyara wakiongozwa na Ndugu Johanson Eliya. (*Makof*)

Wageni walio po Bungeni kwa ajili ya mafunzo, tunao Wanafunzi 32 na Walezi 12 kutoka Shule ya Msingi ya Watoto ya *Ngorika Happyya* Jijini Arusha ambaao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi. Wako wapi hao wanafunzi wetu kutoka Arusha, karibuni sana. (*Makof*)

Wanafunzi 50 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi ya Mzakwe ya Jijini Dodoma ambaao wamekuja kujifunza shughuli za Bunge, karibuni sana. (*Makof*)

Tuna mgeni kutoka Jiji la Arusha naye amekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi, ambaye ni Ndugu Andrew Mbaga, karibu sana Ndugu Mbaga. (*Makof*)

Tuna Watumishi watatu Waandamizi katika Benki ya CRDB Jijini Dodoma, ambao ni Ndugu Jane Ikira, Ndugu Suzan Shuma na Ndugu Shabu Mishwaro. Karibuni sana. (*Makof!*)

Wote karibuni sana. Hao ndio wageni wetu na waliokuja kwa mafunzo.

Matangazo. Nianze na matangazo ya michezo. Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge wa Sengerema, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wanamichezo kuwa mazoezi yanaendelea kwenye Uwanja wa Jamhuri kila siku asubuhi. Pia mnakumbushwa kuwa, *weekend* hii kutakuwa na mechii ya kirafiki siku ya Ijumaa ambayo itakuwa kati ya timu yetu ya Bunge na Balaza la Wawakilishi na Jumapili itakuwa Bunge na *Staff* wa Chuo Kikuu cha *UDOM*.

Kwa hiyo, mnaombwa kufika kwenye mazoezi kwa wingi, lakini pia tunaombwa kufika kushangilia timu yetu ya *Bunge Sports Club* siku hiyo ya Ijumaa na Jumapili. Kwa kuimarisha tu hiyo ya mazoezi ya viungo, Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, anasema, pamoja na mazoezi tunayofanya viwanjani, kwa sasa tunaweza kuimarisha zaidi mazoezi hayo kwa kushiriki mazoezi maalum ya viongo (*gym*) kuititia *gym* iliyoko kwa Mheshimiwa Shabiby inayoendeshwa na Mheshimiwa Venance Mwamoto. (*Makof!*)

*Gym* hii hufunguliwa saa 12.00 asubuhi na hufungwa saa 3.00 usiku kila siku na mazoezi ya *aerobics* huanza saa 12.00 jioni kila siku. Gharama ni nafuu sana, shilingi 4,000/= tu kwa siku. Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu sana kwa faida ya afya zetu tukazingatia hizi *facilities* na fursa ambazo zinatolewa na Bunge letu.

Mwenyekiti wa Jumuia ya *Saint Thomas MO*, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, anawatangazia leo tarehe 24 Aprili, kutakuwa na ibada ya misa kwa Wakristo Wakatoriki mara baada ya shughuli za Bunge kusitishwa mchana, saa 7.00 katika Ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya

pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wote wanaopenda kushiriki ibada hiyo mnakaribishwa.

Hayo ndiyo matangazo ya leo. Ahsanteni.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Lyimo.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kutokana na swalii namba 123 lilitokuwa linahusu nyongeza ya posho kwa Madiwani. Suala hili lina maslahi mapana sana kwa Taifa kwa sababu wote tunajua kazi kubwa wanayofanya Madiwani, lakini katika jibu, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba posho hizo zitategemeana na vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri ameendelea kusema kwamba, kama Halmashauri hazitakuwa na vyanzo hivyo, Halmashauri hizo kisheria zinapaswa kufutwa. Natambua kwamba sheria hii ipo na ilikuwepo kabla vyanzo muhimu sana vya ndani vya mapato havijachukuliwa na Serikali Kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Halamshauri hizi zilikuwa zinategemea kwa mfano *property tax*, lakini vilevile ile *land retention* ya 30% iliyokuwa inabaki, vilevile kodi za mabango na kadhalika fedha zote hizi zimechukuliwa na Serikali Kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, kwa kuwa Madiwani hawa wanafanya kazi kubwa sana na kuwa Serikali Kuu imechukua vyanzo vyote vya mapato; na kwa kuwa sheria inasema sasa kwamba vyanzo hivyo kama Halmashauri haina hivyo vyanzo, maana yake itafutwa:-

Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu sasa, ama warudishe vile vyanzo ili Madiwani wetu waweze kupata posho hii? Kwa sababu tunatambua kwamba hawa Madiwani ni mwakani tu wanaondoka na wengi wamekopa na wamekopwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako tuone ni jinsi gani Serikali Kuu itarudisha mapato hayo ili Madiwani waweze kupata nyongeza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Order Paper* ya leo ya tarehe 25 Mwezi wa Nne, pamoja na maswali ambayo yameshauziliza, kuna Hoja ya Serikali inayohusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni, Serikali imetangaza kwamba watasajili laini za simu kuititia vitambulisho vya Taifa; na vitambulisho vya Taifa viko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani; na sasa kuna malalamiko kwamba, wananchi wengi hawajapata vitambulisho hivyo na wananchi wana wasiwasi kwamba inawezekana laini zao za simu zikafungwa kutokana na kutopata vitambulisho vya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *NIDA* wapo na Wizara ya Mambo ya Ndani ipo ambayo bajeti yao inajadiliwa leo, naomba sasa Serikali iseme na kuwaondoa wananchi wasiwasi kuhusu usajili wa laini zao za simu, kwamba pamoja na kuwa hawajapata hivyo vitambulisho, watoe maelekezo kwa wananchi kwamba laini zao za simu watasajili kwa namna gani kuondoa malalamiko na manung' uniko na hofu kwa wananchi kuhusu simu zao. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, nimeombwa hiyo miongozo miwili. Nianze na hili la Mheshimiwa Susan Lyimo kuhusiana na majibu yaliyotolewa na Serikali kuititia Naibu Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Waitara. Pale aliposisitiza

kwamba Halmashauri yoyote iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria nchini inapaswa iwe na vyanzo vyake nya ndani nya kujitosheleza; na alikazia kwa kusema kwamba kama Halmashauri itafikia hatua ya kushindwa kuwa na mapato yake ya ndani ya kujitosheleza, basi Halmashauri hiyo itafutwa. Nadhani ndiyo ilikuwa *concern* ya Mheshimiwa Lyimo.

Kwa vile lilikuwa ni jibu ambalo limetolewa na Serikali kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI); na lilikuwa ni swali la nyongeza, halikuwa swali la msingi; swali la msingi lilikuwa limejibowi vizuri tu, halafu ndiyo likaja hilo swali la nyongeza.

Sasa, kwa maamuzi ya Kiti, kwamba Mbunge kama wewe unasiliza majibu ya Serikali, au umeuliza swali la nyongeza na ukajiliwa, ukaona kwamba hujisikii vizuri kutokana na majibu uliyopewa na Serikali, mwongozo ambao tumeutoa hapa ni kwamba, wewe una haki ya kwenda sasa kuuliza swali la msingi ili lije llijibiwe vizuri na Serikali. Kama wewe utakuwa umeuliza swali la nyongeza na hukuridhika, Mwongozo ambao tumeweka ni kwamba huwezi tena ukasema kwamba jibu hilo halikujitosheleza kwa sababu tu wewe ukuridhika na majibu ambayo yanetolewa.

Kwa hiyo Mwongozo wangu ni kwamba Mheshimiwa Lyimo, una fursa nzuri tu kwa swali hili ukalijengea hoja kwa kuuliza swali la msingi ili liweze kujiliwa na Serikali sasa namna ya kwenda mbele. Pia ni kweli na nakubaliana na wewe kwamba mapato ya ndani ya halmashauri zetu ikiwa ni halmashauri zangu za Bariadi ya Mjini na ya Wilaya yanaanza kupungua kwa sababu hayo tuliyokuwa tunategemea yamechukuliwa na Serikali Kuu, lakini hayarejeshwi mapema, hoja ni hiyo, yanekuwa yanarejeshwa mapema kwenye halmashauri zetu nadhani malalamiko haya yasingekuwa yanajitokeza. Kwa hiyo tuendelee kuyachukuliwa hayo tuone nini tunaweza tukaboresha zaidi katika hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Bura ni kweli hili zoezi la uandikishaji la Vitambulisho nya Taifa kwa kasi ambalo liliivoanza sasa siyo

ile ambayo inaonekana sasa hivi; lakini vile Serikali wapo hapa labda wanaweza wakatusaidia kulitolea majibu kwa kadri mlivyojipanga. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimlete mbele ya Bunge lako tukufu Mheshimiwa Naibu Waziri anayeshughulikia na sekta hiyo, atatupa maelezo kuhusu Mwongozo aliyouleta mbele yako Mheshimiwa Felister Bura. Kwa idhini yako naomba Naibu Waziri, Mheshimiwa Nditiye atusaidie kutoa ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Injinia Nditiye, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kweli kwamba kuanzia tarehe Mosi Mei, 2019, Makampuni yote ya Simu yatatakiwa kusajili laini za simu kwa kutumia alama za vidole baada ya kujiridhisha na utambuzi wa mtu kupitia kitambulisho cha Taifa. Hatua hizi tumezichukua kwa muda mrefu toka mwaka jana mwezi wa Tatu tulipozindua rasmi usajili kwa kutumia alama za vidole kwa Mikoa ya Dar es Salam, Arusha na Mwanza kwa majoribio na sasa hivi ndiyo tunataka tuanze kulifanya rasmi baada ya kujiridhisha kwamba taratibu zote ziko sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu tulizonazo kama Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia kwa wenzetu wa *NIDA* watu ambao wana namba za vitambulisho wapo milioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hili zoezi litaanza tarehe Mosi mwezi Mei na tutafanya *review* tarehe 30 mwezi wa Septemba kuona ni watu wangapi wamekwishaandikisha na kuna changamoto kiasi gani. Hata hivyo, mwisho kabisa wa zoezi hili itakuwa ni tarehe 31 mwezi wa 12 mwaka huu. Baada ya hapo tutazima laini zote ambazo watakuwa hawajajisajili kwa kutumia alama za vidole.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata  
utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Nadhani, hebu subirini kidogo, Waheshimiwa Wabunge aliyeuliza ni Mheshimiwa Bura, sasa hoja ambayo lazima ijibiwe atusaidie Mheshimiwa Naibu Waziri kujibu; katika tangazo lilitotolewa na *TCRA* wanataka uwe na Kitambulisho cha Taifa, hiyo ndiyo hoja uifafanue vizuri maana maeneo mengi wananchi wetu hawajifikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwhali kusema Bungeni hapa kwamba Mheshimiwa Felister Bura ni kama Esther ambaye alitajwa kwenye Biblia, namna ambavyo anapigania maslahi ya Watanzania. Ndiyo maana Mheshimiwa Felister Bura ameleta Mwongozo huu ili Watanzania Serikali yao iweze kuwapa ufanuzi; Watanzania hawapaswi kuwa na maisha ya wasiwasi, Watanzania lazima waendelee kutumia simu zao kuanzia ambapo anainunua mpaka pale ambapo ataacha kutumia simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NIDA* tulikuwa na lengo la kutambua na kusajili na kutoa vitambulisho milioni 24.5 hayo ndiyo malengo, lakini mpaka sasa *NIDA* tumekwishafanya utambuzi na usajili wa Watanzania wenyewe sifa milioni 16. Tulipoona kwamba wenzetu wa *TCRA* wanataka kubalisha masuala ya kusajili simu ili waweze kutumia alama za vidole na kwamba mwenye kitambulisho cha Taifa ndiye atakayesajiliwa, sisi kuititia *NIDA* tuliweka utaratibu ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Watanzania ambao wamekwishapata vitambulisho watawasilisha vitambulisho vyao. Watanzania milioni 16 tayari wamekwishapatiwa namba inaitwa *NIN - Nation Identification Number*. Kwa hiyo, namba hiyo ambayo inasubiri apewe kitambulisho chake ndiyo atakayoiwasilisha *TCRA*, atabofya kidole chake kwa

namba hiyo na atasajiliwa. Kwa hiyo, maana yake kibindoni tuna Watanzania milioni 16 ambao wana sifa za kusajiliwa kwenye simu na mpaka sasa tunaendelea kumalizia wale walio baki katika kuwapa namba na kuendelea kutoa vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Watanzania hawapaswi kuwa na wasiwasni na pale ambapo sisi kama Serikali tutakuwa hatujatimiza, Mtanzania ambaye anatakiwa apate namba ili aweze kusajili simu, Mtanzania hujo tutampa utaratibu kwa sababu si kosa lake la kutosajiliwa simu, kwa sababu sisi Serikali tuko kwa ajili ya kuwalinda Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo maelezo ya Serikali; Serikali itaendelea kuwepo, wananchi wataendelea kuwepo na pale ambapo zitajitokeza changamoto, ndiyo maana nasema Serikali itafanya *interventions* za haraka za kuweza kunyoosha mambo; tusubiri tuone zoezi lianze na changamoto kama zipo zitatatuliwa. Ahsanteni, Katibu.

#### **NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mtoa hoja, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola, una muda usiozidi saa moja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lipokee, lijadili na lipitishe Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/2019 na Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo haya nitakayoyasoma naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa mezani kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Vilevile, namshukuru sana sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania si mwiningine ni Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kunitfea kusimamia Wizara hii nyeti inayoshughulikia amani, usalama wa raia na mali zao. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake madhubuti ambao umefanikisha utekelezaji wa mambo mbalimbali ikiwemo miradi mikubwa ya kitaifa. Ni dhahiri kuwa wananchi wengi wana imani na matumaini makubwa na Serikali ya Awamu ya Tano inayosimamia Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi niliyonayo hapa mkononi ya mwaka 2015 katika kuelekea kwenye uchumi wa kati unaotegemea viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawapongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa uongozi wao na miongozo ambayo imetoa dira katika kuboresha utendaji wa Wizara na Serikali kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakupongeza wewe binafsi pamoja na Wenyeiti wenzako nampongeza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa uongozi mahiri katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Wajumbe wa Kamati hiyo na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri wao unaolenga katika kuimarisha utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Shughuli za Wizara kwa Mwaka 2018/2019 na Malengo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2019/2020; Mapatona Matumizi ya Fedha. Katika mwaka 2018/2019, Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Shilingi bilioni 945.5. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 521.5 ni kwa ajili ya Mishahara; Shilingi bilioni 385.7 ni za Matumizi Mengineyo na Shilingi bilioni 38.3 ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 fedha zilizopokelewa na Wizara ni jumla ya Shilingi bilioni 813.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 74 zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, Shilingi bilioni 368.8 ni Mishahara na Shilingi bilioni 370.9 zilikuwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya mapato Shilingi bilioni 297. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, jumla ya Shilingi bilioni 204.8 zilikuwa zimekusanya sawa na asilimia 68.9 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafanikio ya Wizara; Wizara inaendelea kutekeleza kazi na majukumu yake, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo:-

(i) Kuendelea kuwepo kwa amani, utulivu na usalama nchini kulikowezesha kuimarika kwa shughuli za uchumi na kijamii, ambapo hali ya uhalifu imeendelea kupungua kwa kiasi kikubwa;

(ii) Kuimarisha usimamizi wa Sheria za Usalama Barabarani kulikosababisha kupungua kwa makosa ya usalama barabarani kwa asilimia 38.7;

(iii) Kukamilika kwa Mkakati wa Kujitosheleza kwa Chakula wa Jeshi la Magereza na kuanza utekelezaji wake;

(iv) Kufungwa kwa mtambo na mashine mpya katika Kiwanda cha kutengeneza bidhaa za ngozi kilichopo Gereza la Karanga Moshi; na

(v) Kufanikiwa kuzima moto na kufanyika kwa uokoaji katika matukio 1,785.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni:-

(i) Kukamilika kwa jengo la kuanzia Ofisi za Makao Makuu ya Wizara eneo la Mtumba Jijini Dodoma;

(ii) Kuzinduliwa kwa mfumo wa kielektroniki wa kutoa vibali vya ukaazi yaani (*e-Permit*), Visa yaani (*e-Visa*);

(iii) Kutunukiwa Tuzo kwa Pasipoti Mpya ya Tanzania ya Kielektroniki kuwa Pasipoti bora katika Ukanda wa Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika;

(iv) Kuanza utaratibu unaowezesha wananchi kupata nakala ya Kitambulisho cha Taifa kuititia Tovuti ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; na

(v) Kukamilika kwa mfumo huu wa kielektroniki wa usajili wa Jumuiya za Kijamii yaani (*Societies Management System*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; katika mwaka 2019/2020, Wizara imewe ka kipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kudumisha usalama wa raia na mali zao kwa kufanya doria, misako na operesheni mbalimbali;

(ii) Kuboresha mazingira ya Ofisi na makazi ya Askari na watumishi raia; na

(iii) Kuwaongezea ujuzi watumishi raia na Askari kwa kuwapa mafunzo ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vingine ni:-

(i) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Jeshi la Magereza wa Kujitosheleza kwa Chakula;

(ii) Kuendelea kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu kwa kuimarisha usimamizi wa sheria husika;

(iii) Kuimarisha utendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza;

(iv) Kununua magari na vifaa vyaa kuzima moto na uokoaji;

(v) Kuimarisha huduma za uhamiaji mtandao yaani (*e-immigration*) kwa kuanzisha *e-border management system* na kuunganisha *e-visa*, *e-permit* na *e-passport* katika Ofisi za Kibalozi nje ya nchi; na

(vi) Kuongeza kasi ya utambuzi, usajili na utoaji wa Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi La Polisi; Hali ya Usalama Nchini; hali ya amani, utulivu na usalama nchini imeendelea kuimarishwa na kuwezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kukua zaidi. Kwa ujumla hali ya uhalifu nchini imepungua kwa kiasi kikubwa. Katika kutimiza jukumu hilo Jeshi la Polisi limeimarisha misako, doria na operesheni kwa kutumia mbinu mbadala za kudhibiti uhalifu sambamba na kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia njia mbalimbali ili jamii ibadilike na kuachana na vitendo vyaa uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya makosa makubwa ya jinai 45,574 yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na makosa 47,236 yaliyotokea katika kipindi kama hicho mwaka wa Fedha 2017/2018. Upelelezi wa makosa hayo umefanyika na kesi 17,631 zikiwa na watuhumiwa 37,267 zilifikishwa mahakamani. Katika kuhakikisha kesi zinapelelezwa kwa haraka, Jeshi la Polisi kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 litaongeza ufanisi katika utendaji wa Maabaraya Uchunguzi wa Sayansi ya Jinai kwa kuongeza vifaa vyaa kisasa na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Askari wapelelezi ndani na nje ya nchi. Aidha, Jeshi

litakamilisha taratibu za kisheria ili maabara yake ya uchunguzi wa vinasaba yaani (*DNA*) isajiliwe na Mkemia Mkuu wa Serikali na kuiwezesha kufanya kazi sambamba na Maabara ya Uchunguzi wa Kikemia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti uhalifu wa matumizi ya silaha, operesheni mbalimbali zimefanyika, ambapo jumla ya silaha 351 na risasi 4,844 za aina mbalimbali zilikamatwa. Aidha, kupitia operesheni hizo jumla ya watuhumiwa 239 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, Jeshi la Polisi kupitia Shirika lake la Uzalishaji Mali litaanza kufanya mafunzo ya matumizi ya silaha za moto kwa Mashirika ya Umma, Kampuni Binafsi za Ulinzi na wamiliki binafsi wa silaha kwa lengo la kuimarisha matumizi sahihi na ulinzi wa maeneo yao. Natoa wito kwa wamiliki na watumiaji wote wa silaha za moto kushirikiana na Jeshi la Polisi kutekeleza matakwa haya ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, katika mwaka wa Fedha 2019/2020, Jeshi la Polisi kupitia Shirika lake la Uzalishaji Mali litaanza kufanya mafunzo ya matumizi ya silaha za moto kwa Mashirika ya Umma, Kampuni Binafsi za Ulinzi na wamiliki binafsi wa silaha kwa lengo la kuimarisha matumizi sahihi na ulinzi wa maeneo yao. Natoa wito kwa wamiliki wote na watumiaji wote wa silaha za moto kushirikiana na Jeshi la Polisi kutekeleza matakwa haya ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Usalama Barabarani; katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019, jumla ya matukio 2,593 yameripotiwa ikilinganishwa na matukio 4,180 yaliyoripotiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa vifo vitokanavyo na ajali za barabarani vimepungua kwa asilimia 38.7. Kupungua kwa ajali na vifo kumetokana na usimamizi mzuri wa Sheria za Usalama Barabarani; ushirikiano na wadau, sambamba na kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, Jeshi litaendelea kusimamia Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, utaratibu wa kupata ridhaa ya Serikali kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 unaendelea vizuri. Muswada wa Sheria hiyo utawasilishwa Bungeni katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Ujenzi wa Makazi, Ofisi na Vituo vya Polisi. Katika kuboresha mazingira ya kazi na makazi ya Askari, Jeshi la Polisi linatekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa nyumba 400 kwa gharama ya shilingi bilioni 10 zilizotolewa mwaka 2018 na Mheshimiwa Rais. Hadi kufikia Machi 2019, awamu ya kwanza ya mradi unaojumuisha ujenzi wa nyumba 148 upo katika hatua ya umalizaji katika mikoa nane ya Dodoma, Katavi, Kaskazini Pemba, Kaskazini Unguja, Kusini Pemba, Njombe, Pwani pamoja na Simiyu. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 252 upo katika hatua mbalimbali za ujenzi katika mikoa 24. Mradi huu umepangwa kukamilika Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kutumia Mfuko wa Tuzo na Tozo, Jeshi la Polisi linatekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 107. Kati ya nyumba hizo, 100 zinajengwa Mkoani Dodoma ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 30 upo katika hatua ya umalizaji na nyumba 70 zitajengwa baada ya awamu ya kwanza kukamilika. Aidha, ujenzi wa jengo moja la kuishi familia saba Wilaya ya Nyang'wale, Mkoani Geita umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa kutumia Mfuko huo, Jeshi la Polisi linaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Polisi, Jijini Dodoma ambao umefikia hatua ya umalizaji. Pia, wananchi na wadau wameendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika ujenzi wa nyumba za kuishi familia 13 na ujenzi wa Vituo vya Polisi 11 katika Mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi litaendelea kushirikiana na kushirikisha wadau mbalimbali katika ujenzi wa Vituo vya Polisi, ofisi na makazi ya Askari kote nchini. Hivyo, natumia

fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika miradi hiyo ili kuweza kuimarissha hali ya ulinzi na usalama katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, Jeshi litaendelea kushirikiana na kushirikisha wadau mbalimbali katika ujenzi wa Vituo vya Polisi, ofisi na makazi ya Askari kote nchini. Hivyo, natumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika miradi hiyo ili kuweza kuimarissha hali ya ulinzi na usalama katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa Vyuo vya Polisi. Katika kuboresha Vyuo vya Polisi nchini, Jeshi la Polisi limefanya upanuzi wa miundombinu ya majengo ya Shule ya Polisi Tanzania (*TPS*) iliyopo Moshi, ujenzi wa mabweni manne yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 320, majengo mawili ya madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 612 na jengo moja la Ofisi limekamilika. Mradi huu umefadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa gharama ya shilingi bilioni 20.4. Hivyo, napenda nitumie fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa kuboresha Shule ya yetu ya Polisi Moshi. Sambamba na hilo, Jeshi la Polisi limeanza ukarabati wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam kwa kutumia shilingi milioni 700 zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza rasilimaliwatu katika Jeshi la Polisi. Katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, Jeshi la Polisi limeajiri Askari wapya 812 kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kazi za Polisi. Askari hao wamehitimu mafunzo ya awali katika Shule ya Polisi Moshi tarehe 9 Aprili, 2019. Aidha, jumla ya Askari 3,725 wanatarajiwa kuajiriwa katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi. Katika kuendelea kuboresha utendaji kazi,

Jeshi la Polisi limepokea magari 144 na makasha (*containers*) tatu ya vipuri kutoka Kampuni ya Ashok Leyland ya India. Jeshi pia limepata magari 18 na pikipi 17 kuitia misaada ya taasisi na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya kutekwa na kuuawa kwa watoto. Mwezi Novemba na Desemba, 2018 yaliibuka matukio ya mauaji na utekaji wa watoto katika Mikoa ya Njombe na Simiyu. Katika Mkoa wa Njombe watoto sita waliuawa na watatu walitekwa, ambapo Jeshi la Polisi lilitanikiwa kuwapata watoto waliotekwa wakiwa hai. Kutokana na matukio hayo, watuhumiwa saba walikamatwa na kufikishwa Mahakamani kwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Mkoa wa Simiyu kulitokea mauaji ya watoto wanne ambao waliuawa na kukatwa baadhi ya viungo. Kufuatia tukio hilo watuhumiwa 12 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Taarifa za kiintelijinsia zilibainisha viini vya matukio hayo ni imani za kishirikina.

Aidha, Wizara kuitia Jeshi la Polisi imeendelea kutoa elimu kwa wananchi, hususan wazazi na walezi kuwa na uangalizi wa karibu kwa watoto wao wanapokwenda na kurudi shulen na wanapokuwa majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa nidhamu za Askari. Katika mwaka 2018/2019, hatua za kinidhamu zimeendelea kuchukuliwa kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari Polisi waliobainika kujihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili mema ya Jeshi la Polisi. Jumla ya Askari 130 wa vyeo mbalimbali, Maafisa 28, Wakaguzi 14 na Askari 88 wamechukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria. Maafisa wawili, Wakaguzi saba na Askari 88 walishaktiwa kijeshi, Askari 35 walipewa adhabu ya kufukuzwa kazi kwa fedheha, Askari watatu walifikishwa Mahakamani na Askari wawili walishushwa vyeo. Aidha, Maafisa 25 na Wakaguzi wanne waliandikiwa barua za onyo na kujieleza pamoja na kutahadharishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara kuititia Jeshi la Polisi itaimarisha upekuzi wa Askari na vijana wanaoomba kujunga na Jeshi ili kuwa na Askari wenye nidhamu na moyo wa dhati wa kulitumikia Jeshi la Polisi na Taifa kwa ujumla. Aidha, Wizara itaendelea kuchukua hatua stahiki kwa Maafisa na Askari wasiozingatia maadili ya Jeshi vikiwemo vitendo vyta kuomba na kupokea rushwa, kubambikiza kesi na kujishirikisha kwenye matukio ya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza, hali ya ulinzi na usalama Magerezani. Wizara kuititia Jeshi la Magereza imeendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika Magereza yote nchini. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 kulikuwa na jumla ya wafungwa na mahabusu 38,501. Kati ya hao, wafungwa ni 19,395 na mahabusu 19,106. Idadi hii imekuwa iksababisha msongamano wa wafungwa na Mahabusu hasa katika Magereza yaliyopo katika miji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani, Wizara inaendelea kutumia njia mbalimbali za kupunguza msongamano huo ikiwemo msamaha wa Mheshimiwa Rais, ambapo jumla ya wafungwa 4,477 walinufaika. Wafungwa 91 walinufaika na utaratibu wa mpango wa *Parole* kuititia Sheria ya Bodi za Parole, Sura ya 400 ya mwaka 2002. Wafungwa 788 walinufaika na utaratibu wa kifungo cha nje, wafungwa 3,629 walihukumiwa kutumikia adhabu zao nje ya Magereza kuititia Programu ya Adhabu Mbadala ya Kifungo cha Gerezani. Takwimu hizo ni kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019. Vilevile, Jeshi la Magereza limekamilisha ujenzi wa Magereza mawili ya Mahabusu ya Chato Mkoani Geita na Ruangwa Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kudhibiti msongamano wa wafungwa Magerezani kwa kutumia njia zilizotajwa hapojuu. Aidha, Jeshi la Magereza limeongeza bajeti ya shughuli za Bodi ya *Parole*

kutoka shilingi milioni 116.5 mwaka wa fedha 2018/2019 hadi shilingi milioni 241.3 mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Wizara inatarajia kuongeza Mikoa ya Katavi, Lindi na Ruvuma katika kutekeleza Programu ya Adhabu Mbadala ya Kifungo cha Gerezani na hivyo kufikia Mikoa yote ya Tanzania Bara. Aidha, Wizara itaendelea kuharakisha uandaaji wa taarifa za uchunguzi ili kuhakikisha wahalifu na wafungwa wa vifungo vya muda mrefu usiozidi miaka mitatu wanatumikia adhabu mbadala nje ya Magereza na hivyo kusaidia kupunguza msongamano Magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi pia limeimarisha upekuzi ili kubaini vitu visivyoruhusiwa kuingizwa Magerezani na kudhibiti vitendo viovu. Katika kufikia azma hiyo, utekelezaji wa mpango wa kufunga mfumo wa kisasa wa ulinzi wa kielektroniki umeanza kutekelezwa katika Magereza makubwa ya Mkoa wa Dar es Salaam (Ukonga, Keko na Segerea). Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Jeshi litakamilisha kazi hii pamoja na kuanza kufunga mfumo huo katika Gereza Arusha na Gereza la Isanga hapa Mjini Dodoma. Zoezi hili litaendelea kutekelezwa katika Magereza yote nchini kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Kujitosheleza kwa Chakula. Katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais, Jeshi la Magereza limeandaa Mkakati wa Miaka Mitano (2018/2019 - 2022/2023) wa Kujitosheleza kwa Chakula cha Wafungwa na Mahabusu. Mkakati huo umejielekeza katika kuzalisha mazao muhimu ya chakula ambayo ni mahindi, mpunga na maharage. Mkakati husika umeanza kutekelezwa katika Magereza kumi ya Arusha, Idete, Kiberege, Kitai, Kitengule, Ludewa, Mollo, Nkasi, Pawaga na Songwe kwa kutenga jumla ya hekari 12,370.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa kilimo 2018/2019, Jeshi la Magereza limelima na kupanda eneo lenye jumla ya hekari 5,395 katika Magereza hayo niliyyoyataja. Matarajio ni kuvuna tani 6,299 za mahindi, tani 3,228 za

mpunga na tani 568 za maharage. Pamoja na Mkakati huo, Magereza mengine yataendelea na shughuli za kilimo ziklwemo mbogamboga na matunda kwa utaratibu wa kuwekewa malengo ya uzalishaji. Hatua nyingine zilizochukuliwa katika kuboresha shughuli za kilimo ni ununuzi wa matrekta 10 na zana zake ambayo yamesambazwa katika Magereza mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Jeshi la Magereza litaendelea kutekeleza Mkakati wa Kujitosheleza kwa Chakula cha Wafungwa na Mahabusu kwa kulima jumla ya hekari 8,150 za mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha makazi ya watumishi wa Jeshi la Magereza na mabweni ya wafungwa na mahabusu. Jeshi la Magereza litaendelea kujenga nyumba za makazi ya Askari katika vituo mbalimbali nchini. Jukumu hili linatekelezwa kuitia mpango unaoelekeza Wakuu wa Vituo kutumila nguvu kazi ya Askari, wafungwa na rasilimali zilizopo katika maeneo yao kwa mpango tunaouita ujenzi wa nyumba za ubunifu. Hadi kufikia Machi, 2019, jumla ya nyumba 129 zimekamilika na nyumba 264 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Gharama za kukamilisha nyumba hizo ni shilingi bilioni 1.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa Jeshi la Magereza. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Jeshi la Magereza linatarajia kuajiri Askari 685. Pia, Jeshi litatoa mafunzo ya muda mfupi ya ndani ya Jeshi kwa lengo la kuboresha utendaji. Mafunzo hayo yatahusisha wataalam wa usimamizi wa rasilimali za Serikali, kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa lengo la kuboresha utendaji ndani ya Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza. Shirika hili limekamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi za kuanzia kwa ajili ya Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu) katika eneo la Mtumba Jijini Dodoma. Aidha, ujenzi wa ukuta wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Jijini Dodoma unaendelea. Kazi zote zilizotajwa zina thamani ya shilingi bilioni 3.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika kupitia Kampuni ijulikanayo kama *Karanga Leather Industries Company Limited* limeboresha kiwanda cha viatu cha zamani kilichopo eneo la Gereza Karanga, Mjini Moshi. Uboreshaji huo umefanyika kwa kuongeza mtambo na mashine mpya. Kwa sasa kiwanda kina uwezo wa kuzalisha jozi 400 za viatu kwa siku ikilinganishwa na jozi 150 zilizokuwa zikilizalishwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza pia linatengeneza samani mbalimbali katika viwanda vyake vilivyopo Ukonga - Dar es Salaam, Uyui - Tabora pamoja na Arusha. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, viwanda hivyo vimepokea zabuni za kutengeneza samani zenyehumla ya Sh.1,339,199,763.97. Zabuni hizo zilitoka katika Taasisi za Serikali na watu binafsi na zitakamilika kabla ya Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshiriki katika kuzima moto na kufanya uokoaji katika matukio 1,785 nchi nzima. Jeshi pia limefanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto katika majengo 34,395 na magari 4,786. Kutokana na ukaguzi huo kiasi cha shilingi bilioni 4.5 kilikusanya. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Jeshi litaendelea na ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto ili kuzuia na kupunguza matukio ya moto hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua za kudhibiti majanga ya moto, elimu imeendelea kutolewa kwa umma kupitia vyombo mbalimbali vyahabari ikiwemo vipindi vyaruninga 45 na vipindi vyaredio 331. Aidha, katika kukabiliana na matukio ya moto katika Shule za Msingi na Sekondari, Jeshi limefungua humla ya Vilabu vyahabari Zimamoto 34 kwa ajili ya kutoa elimu katika Shule za Msingi na Sekondari. Elimu hiyo itaendelea kutolewa kwa umma katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya vitendea kazi vyahabari na uokoaji. Katika kukabiliana na upungufu wa

vitendea kazi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika mwaka 2018/2019 limepata jumla ya magari 16. Vilevile, Jeshi limepokea msaada wa kontena lenye vifaa vya kuzima moto na uokoaji kutoka Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi bilioni 3.75 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari matano ya kuzima moto. Hadi kufikia Machi, 2019 kiasi cha shilingi bilioni 3 kimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa magari hayo ambayo yataletwa nchini mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 4.5 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.75 ni kwa ajili ya ununuzi wa magari mengine matano na shilingi milioni 750 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuzima moto na uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuzima moto pia inahitaji uwepo wa visima vya kuhifadhi maji katika maeneo mbalimbali. Visima vilivyopo kwa sasa ni 2,042 nchi nzima ikilinganishwa na mahitaji ya visima 285,000. Kati ya visima vilivyopo, visima 692 vinafanya kazi na visima 1,350 ni vibovu. Natumia fursa hii kutoa wito kwa Mamlaka za Maji katika Mikoa mbalimbali kutekeleza jukumu lao la kufanya matengenezo ya visima hivyo ili kuwezesha kazi ya kuzima moto kufanyika kwa wakati na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, kazi ya kuzima moto pia inahitaji uwepo wa visima vya kuhifadhi maji katika maeneo mbalimbali. Visima vilivyopo kwa sasa ni 2,042 nchi nzima ikilinganishwa na mahitaji ya visima 285,000. Kati ya visima vilivyopo, visima 692 vinafanya kazi na visima 1,350 ni vibovu. Natumia fursa hii kutoa wito kwa Mamlaka za Maji katika Mikoa mbalimbali hapa nchini kutekeleza jukumu lao la kufanya matengenezo ya visima hivyo ili kuwezesha kazi ya kuzima moto kufanyika kwa wakati na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa Maafisa na Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimaliwatu, mwaka wa

fedha 2019/2020, Jeshi la Zimamoto na uokoaji linatarajia kuajiri Askari 500. Pia, Jeshi litawapandisha vyeo Maafisa na Askari 1,343 kwenye ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za uhamiaji. Utekelezaji wa Mradi wa Uhamiaji Mtandao. Tarehe 26 Novemba, 2018, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa alizindua mfumo wa kielektroniki wa kutoa vibali vya ukaazi (*e-permit*) pamoja na viza (*e-visa*). Mfumo huo unamwezesha mteja kutuma maombi yake kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mfumo wa kudhibiti watu wanaoingia na kutoka nchini *yaani (e-border Management Control System)*. Mfumo huu utaanza kutumika mwezi Julai, 2019 na utasaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka yetu pamoja na kuongeza udhibiti wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Vilevile, katika mwaka 2019/20 Serikali itaunganisha *e-visa, e-permit na e-passport* katika ofisi za kibalozi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huo wa kielektroniki wa huduma za uhamiaji umeanza kuonesha mafanikio sio tu ndani ya nchi bali hata nje ya nchi. Katika kudhihirisha mafaniko hayo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Pasipoti mpya ya Tanzania ya Kielektroniki imetunukiwa Tuzo ya kuwa Pasipoti bora katika Ukanda wa Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika, kwa kukidhi viwango vya ubora wa kiusalama vinavyopendekezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia Usafiri wa Anga. Tuzo hiyo ilitolewa katika sherehe zilizofanyika katika Kisiwa cha Malta tarehe 26 Machi, 2019 na ilikabidhiwa kwa Idara ya Uhamiaji kwa niaba ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie mfumo huo wa kielektroniki wa huduma za uhamiaji umeanza kuonesha mafanikio sio tu ndani ya nchi bali hata nje ya nchi. Katika kudhihirisha mafaniko hayo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Pasipoti mpya ya Tanzania ya Kielektroniki imetunukiwa Tuzo ya kuwa Pasipoti bora katika Ukanda wa

Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika, kwa kukidhi viwango nya ubora wa kiusalama vinyopendekezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia Usafiri wa Anga. Tuzo hiyo ilitolewa katika sherehe zilizofanyika katika Kisiwa cha Malta tarehe 26 Machi, 2019 na ilikabidhiwa kwa Idara ya Uhamiaji kwa niaba ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Ulinzi na Usalama Mipakani, hali ya ulinzi na usalama mipakani imeendelea kuwa shwari kutokana na kuimarisha udhibiti wa watu wanaoingia na kutoka nchini. Kazi hii inafanyika kwa kushirikiana na vyombo vingine nya Ulinzi na Usalama pamoja na wananchi wenye nia njema na nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Misako, Doria na Ukaguzi. Misako, doria na ukaguzi umeendelea kufanyika katika sehemu mbalimbali ili kuwabaini wageni wanaolishi nchini kinyume cha sheria. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya watuhumiwa wa uhamiaji haramu 9610 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Idadi hii imepungua kwa asilimia 28.2 ya wahamiaji haramu 13393 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka wa fedha 2017/18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 03 hadi 04 Aprili, 2019 Jijini Dar es Salaam ulifanyika mku الوا kimataifa uliozikutanisha nchi tatu za Tanzania, Kenya na Ethiopia pamoja na Washirika wa Maendeleo. Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mku الوا huo uliokuwa na lengo la kutafuta mbinu mbalimbali za kukabiliana na wahamiaji haramu wanaoingia nchini. Kufuatia mku الوا huo nilitoa agizo kwa Idara ya Uhamiaji kuhakikisha kwamba inawasaka na kuwatia mbaroni madalali wa wahamiaji haramu ili waweze kukamatwa na kufunguliwa mashitaka. Majina ya madalali hao yameanza kupokelewa na yanafanyiwa kazi na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudiekufuatin mku الوا huo nilitoa agizo kwa Idara ya Uhamiaji kuhakikisha kwamba inawasaka na kuwakamata madalali wa wahamiaji haramu ili waweze kufikishwa na kufunguliwa mashitaka

kwenye vyombo vya kisheria. Majina ya madalali hao yameanza kupokelewa na yanafanyiwa kazi na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020 Serikali itaendelea kusimamia Sheria na Kanuni za Uhamiaji ili kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu katika maeneo ya mipaka na vituo vya kuingilia nchini. Aidha, misako, doria na kaguzi zitaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuwabaini na kuwadhibiti wahamiaji haramu pamoja na madalali, wasafirishaji, wanaowahifadhi na wote wanaoshiriki kwa namna moja au nytingine katika uhalifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Wizara kuitia Sekretarieti ya Kupambana na Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu imeokoa jumla ya wahanga 31 na kuwapatia misaada. Baadhi ya wahanga hao wameunganishwa na familia zao na wengine taratibu za kuwaunganisha na familia zao zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020 Wizara itakamilisha marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu ya Mwaka 2008. Moja ya maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika sheria husika ni kuongeza wigo wa adhabu kwa wahalifu wa biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Vitambulisho vya Taifa. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inaendelea na zoezi la usajili, ambapo hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya watu 19,934,708 walikuwa wamesajiliwa sawa na asilimia 82 ya lengo la kusajili watu 24,295,468. Aidha, Mamlaka imetoa namba za utambulisho wa Taifa kwa Wananchi 11133095. Mamlaka pia imechapisha vitambulisho 4,850,724 na kugawa kwa wananchi 4,503,769. Hata hivyo, ili kuongeza kasi ya kuchapisha vitambulisho, Mamlaka ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za ununuzi wa mashine mpya mbili (2) zenye uwezo wa kuchapa vitambulisho 9,000

ikilinganishwa na vitambulisho 750 kwa saa vinavyochapishwa na mashine zilizopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia NIDA imeanzisha utaratibu wa kuvipeleka Vitambulisho vya Taifa katika ofisi za Watendaji wa Kata kwa ajili ya kuongeza kasi ya ugawaji wa vitambulisho kwa wananchi. Pia, Mamlaka inashirikiana na taasisi nyingine kutumia Namba za Utambulisho wa Taifa katika kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kuliaarifu Bunge lako Tukufu kuwa NIDA imeanzisha utaratibu unaowezesha wananchi kupata nakala ya Kitambulisho cha Taifa kupitia Tovuti ya Mamlaka hiyo uyaani ([www.nida.go.tz](http://www.nida.go.tz)). Sambamba na utaratibu huo, wananchi wanaweza kupata Namba ya Utambulisho wa Taifa kupitia simu zao za viganjani kwa kupiga namba \*152\*00# halafu kuchagua namba 3 na kufuata maelekezo. Kupitia namba hiyo ya Utambulisho wa Taifa wananchi wanaweza kupata huduma mbalimbali zikiwemo, usajili wa kampuni ya biashara, usajili wa laini za simu, huduma za fedha zitolewazo na benki, ulipaji wa kodi za Serikali, kupata mikopo ya elimu ya juu, na kupata pasipoti. Maelezo haya ndio yanaungwa mkono na muongozo uliotua hapa Bungeni ulioombwa na Mheshimiwa Felister Bura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/20 Wizara kupitia Mamlaka hiyo itaendelea na zoezi la usajili ili kufikia wananchi 25,237,954. Pia, NIDA itakamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa ofisi 25 za usajili za Wilaya, Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka Jijini Dodoma pamoja na mifumo ya TEHAMA. Kati ya ofisi hizo 22 zitajengwa Tanzania Bara na tatu (3) zitajengwa Zanzibar (Wilaya ya Micheweni - Kaskazini Pemba, Wilaya ya Mkoani - Kusini Pemba na Wilaya ya Magharibi - Mjini Magharibi). Kazi hizo zitatekelezwa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea ambapo Shilingi 9,645,489,600 zimetengwa katika mwaka 2019/20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma kwa wakimbizi. nchi yetu imeendelea kupokea na kuhifadhi wakimbizi na

waomba hifadhi kutoka nchi mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Tanzania ilikuwa inawahudumia waomba hifadhi na wakimbizi 321,642. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya wakimbizi 28,662 kutoka Burundi walirejeshwa nchini mwao kwa hiari yao. Idadi hiyo inafanya wakimbizi walirejeshwa nchini mwao tangu zoezi hilo lilitivoanza mwaka 2017 kufikia 63,167 kati ya 83,676 waliojiandikisha sawa na asilimia 73.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeendelea na zoezi la kuwahamishia katika nchi ya tatu wakimbizi waliopo nchini. Hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya wakimbizi 2,583 walihamishiwa katika nchi za Marekani, Canada, Australia na Uhlanzi. Serikali inatekeleza majukumu hayo kwa kushirikiana na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNHCR na IOM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masoko ya Pamoja kati ya Wananchi na Wakimbizi. Wizara imetekeleza agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuyahamishia ndani ya makambi masoko ya pamoja. Katika kutekeleza agizo hilo Wizara imehamishia masoko mawili ndani ya Kambi za Nduta na Mtendeli yanayotumiwa na wananchi pamoja na Wakimbizi ili kuimarisha usalama na kudhibiti utoro wa wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kuwahifadhi wakimbizi waliopewa hadhi hiyo kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu, kuwatafutia suluhisho la kudumu ikiwa ni pamoja na kuwarejesha katika nchi zao za asili kwa hiari na kuwahamishia nchi ya tatu. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha udhibiti na kudumisha hali ya usalama katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuhifadhi wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usajili na Usimamizi wa Jumuiya za Kijamii. katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya maombi ya usajili ya jumuiya 150 yamepokelewa, ambapo 77 ni ya Jumuiya za Kidini na 73 ni Jumuiya za Kijamii. Kutokana na maombi hayo, jumla ya

Jumuiya 69 zilisajiliwa, kati ya hizo 38 ni za Kijamii na 31 ni za Kidini. Maombi ya Jumuiya 81 yanaendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na shughuli za usajili, Wizara imekamilisha mfumo mpya wa usajili wa Jumuiya za Kijamii ujulikanao kama *Societies Management System*. Mfumo huo utawezesha shughuli za usajili kufanyika kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shukurani natoa shukurani kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wangu wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni, ambaye ni Mbunge wa Kikwajuni - Zanzibar kwa msaada wake anaonipa katika kusimamia majukumu ya Wizara na hata pale ambapo anakuwa anatekeleza majukumu yake ni Naibu Waziri wa pekee ambaye nakuwa sina wasiwasi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. (*Makofii*)

Vilevile, nawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu Meja Jenerali Jacob Gideon Kingu na Naibu Katibu Mkuu Ramadhan K. Kailima kwa uongozi wao madhubuti katika kusimamia utekelezaji wa kazi na majukumu ya Wizara. Huyu ni Katibu Mkuu wa Wizara na Naibu wake ambao nimewaona kwamba wanafanya kazi oiliyotukuka na hivyo wanasaidia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kunisaidia mimi kufanya kazi zangu kwa ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Wakuu wa Vyombo vyaya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi IGP Simoni Nyakoro Silo, CGP Faustine Kasike, CGF Andengenyé na CGI Dkt. Makakara. (*Makofii*)

Vilevile, niwashukuru Makamishna wa vyombo vyote vyaya ulinzai na usalama na Makamishna Wasaidizi pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo, Askari na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuendelea kutekeleza shughuli za Wizara kwa weledi na ufanisi na ndio maana katika hotuba yangu nimesema uhalifu unaendelea

kupungua kwa sababu ya kazi nzuri zinazofanywa na watendaji hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatoa shukurani kwa wahisani zikiwemo nchi Austria, *Belgium*, *Egypt*, Jamhuri ya Watu wa China, India, Japan, Korea Kusini, Morocco, Urusi, Ujerumani pamoja na Taasisi na Mashirika ya Kimataifa ya ASA, EU, RESA, IOM, UNDP, UNHCR, UN-Women, UNICEF, WFP, Vyombo vyta Habari, Jumuiya za Kijamii na wananchi kwa ujumla. Wadau wote hawa wamekuwa nguzo muhimu katika kutoa misaada ikiwemo ya ujenzi wa ofisi, vituo vyta Polisi na makazi ya Askari, kutupatia vitendea kazi pamoja na kutoa taarifa mbalimbali ambazo zinasaidia kubaini na kudhibiti na kuzuia uhalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa napenda kuishukuru familia yangu, ikiongozwa na mtoto wangu mkubwa Marieta ambao wamekuwa msaada sana kuniweka katika mazingira ya kulitumikia Taifa langu Tanzania. Nawashukuru pia ndugu, marafiki pamoja na wananchi, hususan na kwa aina ya kipekee wapiga kura wangu waliotukuka wa Jimbo langu la Mwibara kwa namna ambavyo wanashirikiana na mimi katika kujiletea maendeleo kwa namna ambavyo wanatifagilia kwamba mimi ni Mbunge ambaye ni jembe nawashukuru sana wana Mwibara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho, Wizara itaendelea kulinda amani, usalama wa nchi hii kwa kushirikiana na vyombo vingine vyta dola nchini pamoja na wadau mbalimbali. Kuwepo kwa utulivu ambao watanzania na wananchi kwa ujumla wanauona hapa nchini hutaendelea kuwezesha vyombo vyta ulinzi na usalama na hakika shughuli za maendeleo kwa sekta mbalimbali zitaendelea kuimarika na hivyo kuipaisha nchi yetu na kufikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepanga kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka Shilingi 297,014,614,300 mwaka wa fedha 2018/19 hadi Shilingi

471,893,927,000 mwaka wa fedha 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 58.8. Ili kufikia lengo hilo Wizara itatumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Mapato ya Serikali (*GePG*); kuendelea kuhuisha viwango vya tozo na ada mbalimbali ili viendane na wakati.

Kuendelea kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto katika maeneo mbalimbali nchini, na kuimarisha huduma za uhamiaji mtandao. Matumizi Mengineyo ya Shilingi 517,040,341,000 ni Mishahara. Fedha za Miradi ya Maendeleo ni Shilingi 31,938,414,279 kati ya fedha hizo Shilingi 21,500,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 10,438,414,279 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kubwa mbele ya Bunge lako Tukufu sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHE.  
KANGI ALPHAXARD LUGOLA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YAFEDHA KWA  
MWAKA 2019/20 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja kwamba kufuatia Taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19 na lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2019/20.
2. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba hii kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Vilevile, namshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kunateua kusimamia Wizara hii nyeti

inayoshughulikia amani, usalama wa raia na mali zao. Aidha, nampongeza Mhe. Rais kwa uongozi wake madhubuti ambao umefanikisha utekelezaji wa mambo mbalimbali ikiwemo miradi mikubwa ya kitaifa. **Ni dhahiri kuwa wananchi wengi wana imani na matumaini makubwa na Serikali ya Awamu ya Tano inayosimamia Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 katika kuelekea kwenye uchumi wa kati unaotegemea viwanda.**

**3. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, nawapongeza Makamu wa Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.) kwa uongozi wao na miongozo ambayo imetoa dira katika kuboresha utendaji wa Wizara na Serikali kwa ujumla.

**4. *Mheshimiwa Spika*,** pia nakupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa uongozi wenu mahiri katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, namshukuru Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.) Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Wajumbe wa Kamati hiyo na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri wao unaolenga katika kuimarisha utendaji wa Wizara.

**B. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA KWA MWAKA  
2018/19 NA MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA  
MWAKA 2019/20**

**Mapato na Matumizi ya Fedha**

**5. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19 Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 945,555,651,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 521,544,490,810** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 385,725,478,187** ni za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 38,285,682,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

**6. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia mwezi Machi, 2019 fedha zilizopokelewa ni jumla ya **Shilingi 813,705,781,313**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 74,000,577,005** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 368,771,225,943** ni Mishahara na **Shilingi 370,933,978,365** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**7. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19 Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya mapato ya **Shilingi 297,014,614,300**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya **Shilingi 204,762,550,114** zilikuwa zimekusanyaawa sawa na **asilimia 68.9** ya lengo.

### **Mafanikio ya Wizara**

**8. *Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kutekeleza kazi na majukumu yake, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo: kuendelea kuwepo kwa amani, utulivu na usalama nchini kulikowezesha kuimarika kwa shughuli za uchumi na kijamii, ambapo hali ya uhalifu imepungua kwa kiasi kikubwa; kuimarisha usimamizi wa Sheria za Usalama Barabarani kulikosababisha kupungua kwa makosa ya barabarani kwa **asilimia 38** na vifo vitokanavyo na ajali za barabarani kwa **asilimia 38.7**; kukamilika kwa Mkakati wa Kujitosheleza kwa Chakula wa Jeshi la Magereza na kuanza utekelezaji wake; kufungwa kwa mtambo na mashine mpya katika Kiwanda cha kutengeneza bidhaa za ngozi kilichopo Gereza Karanga Moshi; na kufanikiwa kuzima moto na kufanyika kwa uokoaji katika matukio 1,785.

**9. *Mheshimiwa Spika***, mafanikio mengine ni kukamilika kwa jengo la kuanzia la ofisi za Makao Makuu ya Wizara eneo la Mtumba Jijini Dodoma; kuzinduliuwa kwa mfumo wa kielektroniki wa kutoa vibali vya ukaazi (*e-Permit*) na Viza (*e-Visa*); kutunukiwa Tuzo kwa Pasipoti Mpya ya Tanzania ya Kielektroniki kuwa Pasipoti bora katika Ukanda wa Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika; kuanza utaratibu unaowezesha wananchi kupata nakala ya Kitambulisho cha Taifa kuititia Tovuti ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; na kukamilika kwa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa Jumuiya za Kijamii (*Societies Management System*).

### **Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2019/20**

**10. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Wizara imeweka kipaumbele katika maeneo yafuatayo: kuendelea

kudumisha usalama wa raia na mali zao kwa kufanya doria, misako, operesheni mbalimbali; kuboresha mazingira ya ofisi na makazi ya Askari na watumishi raia; na kuwaongezea ujuzi watumishi raia na Askari kwa kuwapa mafunzo ya ndani na nje ya nchi.

**11. *Mheshimiwa Spika*,** vipaumbele vingine ni kuendelea kutekeleza Mkakati wa Jeshi la Magereza wa Kujitosheleza kwa Chakula; kuendelea kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu kwa kuimarisha usimamizi wa Sheria husika; kuimarisha utendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza; kununua magari na vifaa vya kuzima moto na uokoaji; kuimarisha huduma za uhamiaji mtandao (*e-immigration*) kwa kuanzisha *e-border management system* na kuanganisha *e-visa, e-permit na e-passport* katika ofisi za kibalozi nje ya nchi; na kuongeza kasi ya utambuzi, usajili na utoaji wa Vitambulisho vya Taifa.

**12. *Mheshimiwa Spika*,** maeneo hayo ya kipaumbele yameainishwa kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Awamu ya Pili ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 –2020/21; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2019/20; Mpango Mkakati wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi 2016/17 – 2020/21; Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti na Kuzuia Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto 2017/18 – 2021/22; Maagizo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi Wakuu wa Kitaifa yaliyotolewa kwa nyakati tofauti; na Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

## **JESHI LA POLISI**

### **Hali ya Usalama Nchini**

**13. *Mheshimiwa Spika*,** hali ya amani, utulivu na usalama nchini imeendelea kuimarishwa na kuwezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kukua zaidi. Kwa ujumla hali ya uhalifu nchini imepungua kwa kiasi kikubwa. Katika kutimiza jukumu

hilo Jeshi la Polisi limeimarisha misako, doria na operesheni kwa kutumia mbinu mbadala za kudhibiti uhalifu sambamba na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuititia njia mbalimbali ili jamii ibadilike na kuachana na uhalifu.

**14. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya makosa makubwa ya jinai 45,574 yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi nchini ikilinganishwa na makosa 47,236 yaliyotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Kupungua kwa makosa hayo kumetokana na kupatikana mapema kwa taarifa za uhalifu kwa kutumia Askari wa Intelijensia; ushirikishwaji wa wananchi kuititia Polisi Jamii katika udhibiti wa uhalifu nchini; kuimarika kwa doria, misako na operesheni maalum mijini, vijijini na majini; na ushirikiano na vyombo vingine vya dola.

**15. *Mheshimiwa Spika*,** kati ya makosa makubwa ya jinai yaliyopotiwa hapo juu upelelezi umefanyika na kesi 17,631 zikiwa na watuhumiwa 37,267 zilifikishwa mahakamani. Kesi zilizobaki 27,943 zipo katika hatua mbalimbali za upelelezi na zitakapokamilika watuhumiwa watafikishwa Mahakamani. Katika kuhakikisha kesi zinapelelezwa kwa haraka, Jeshi la Polisi kwa mwaka 2019/20 litaongeza ufanisi katika utendaji wa Maabara ya Uchunguzi wa Sayansi Jinai kwa kuongeza vifaa vya kisasa na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Askari wapelelezi ndani na nje ya nchi. Aidha, Jeshi litakamilisha taratibu za kisheria ili maabara yake ya uchunguzi wa vinasaba (DNA) isajiliwe na Mkemia Mkuu wa Serikali na kuiwezesha kufanya kazi sambamba na Maabara ya Uchunguzi wa Kikemia.

**16. *Mheshimiwa Spika*,** katika kudhibiti uhalifu wa matumizi ya silaha, operesheni mbalimbali zimefanyika ambapo jumla ya silaha 351 zilikamatwa kwa mchangano ufuatao: SAR 1; Uzi Gun 1; Shot Gun 45; G.3 1; Pistol 25; Air Gun 2; Rifle 58 na AK 47(SMG) 16, Mark IV 1 na Gobore 201. Aidha, kuititia operesheni hizo jumla ya risasi 4,844 za aina mbalimbali zilizokuwa zikimilikiwa kinyume cha sheria zilikamatwa. Jumla ya watuhumiwa 239 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani, ambapo wanaume ni 229 na wanawake 10.

**17. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Jeshi la Polisi kuititia Shirika lake la Uzalishaji Mali (*Tanzania Police Force Corporation Sole – TPFCS*) litaanza kufanya mafunzo ya matumizi ya silaha za moto kwa Mashirika ya Umma, Kampuni Binafsi za Ulinzi na wamiliki binafsi wa silaha kwa lengo la kuimarisha matumizi sahihi na ulinzi wa maeneo yao. **Natoa wito kwa wamiliki na watumiaji wote wa silaha za moto kushirikiana na Jeshi la Polisi kutekeleza matakwa haya ya kisheria.**

**18. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao kwa kubaini na kuzuia uhalifu kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Aidha, Jeshi litaendelea kutoa elimu ya utambuzi wa makosa mbalimbali kwa kushirikiana na wananchi na wadau wa ndani na nje ya nchi.

#### **Hali ya Usalama Barabarani**

**19. Mheshimiwa Spika**, matukio makubwa ya ajali za barabarani yameendelea kupungua. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya matukio 2,593 yameripotiwa ikilinganishwa na matukio 4,180 yaliyoripotiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Takwimu hizi zinaonesha kuwa matukio 1,587 yamepungua ikiwa ni sawa na **asilimia 38**.

**20. Mheshimiwa Spika**, matukio hayo yalisababisha vifo 1,216 ikilinganishwa na vifo 1,985 vilivyotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Hii inaonesha vifo 769 vimepungua sawa na **asilimia 38.7**. Vilevile, idadi ya majeruhi imepungua kwa **asilimia 40.7** kutoka majeruhi 4,447 mwaka 2017/18 hadi majeruhi 2,639 mwaka 2018/19.

**21. Mheshimiwa Spika**, kupungua kwa ajali na vifo kumetokana na usimamizi mzuri wa Sheria za Usalama Barabarani; ushirikiano na wadau, sambamba na kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuzingatia utii wa Sheria. Katika kudhibiti ajali za barabarani Jeshi la Polisi lilitifanya ukaguzi kwa mabasi 247,514 ambapo mabasi 26,219 yaligundulika kuwa mabovu.

Mabasi hayo hayakuruhusiwa kuendelea na safari na wamiliki wake walitakiwa kuyatengeneza. Aidha, jumla ya madereva 72 wa mabasi ya abiria walifungiwa leseni zao baada ya kufikishwa Mahakamani.

**22. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi hicho pia jumla ya madereva 7,271 walifikishwa mahakamani wakiwemo madereva wa magari 1,436 na waendesa pikipiki 5,835. Madereva wengine 95,081 walipewa adhabu ya kulipa faini kwa kukiuka Sheria ya Usalama Barabarani. Katika mwaka 2019/20 Jeshi litaendelea kusimamia Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, utaratibu wa kupata ridhaa ya Serikali kuhusu mapendekazo ya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 unaendelea. Muswada wa Sheria hiyo utawasilishwa Bungeni katika mwaka 2019/20.

#### **Miradi ya Ujenzi wa Makazi, Ofisi na Vituo vya Polisi**

**23. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuboresha mazingira ya kazi na makazi ya Askari Jeshi la Polisi linatekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za makazi 520, ujenzi wa Vituo vya Polisi 11 na Jengo la Makao Makuu ya Polisi Dodoma.

**24. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi la Polisi linaendelea na mradi wa ujenzi wa nyumba 400 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 10** zilizotolewa mwaka 2018 na Mhe. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Nyumba hizo zinajengwa katika Mikoa ya Dodoma 88, Pwani 40, Dar es Salaam 18, Kigoma 9, Mara 15, Morogoro 7 na Shinyanga 9. Katika Mikoa ya Geita, Katavi, Njombe, Simiyu na Songwe zinajengwa nyumba 20 kila Mkoa. Vilevile, zinajengwa nyumba 6 kila Mkoa katika Mikoa ya Arusha, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Singida, Tabora, Tanga, Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba.

**25. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia mwezi Machi 2019, awamu ya kwanza ya mradi unaojumuisha ujenzi wa nyumba 148

kwa gharama ya **Shilingi bilioni 3.7** upo katika hatua ya umaliziaji katika mikoa nane (8) ya Dodoma, Katavi, Kaskazini Pemba, Kaskazini Unguja, Kusini Pemba, Njombe, Pwani na Simiyu. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 252 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 6.3** upo katika hatua mbalimbali za ujenzi katika mikoa 24. Mradi huu umepangwa kukamilika mwezi Juni, 2019.

**26. Mheshimiwa Spika**, vilevile, kwa kutumia Mfuko wa Tuzo na Tozo Jeshi la Polisi linatekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 107. Kati ya nyumba hizo 100 zinajengwa mkoani Dodoma eneo la Medeli East ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 30 upo katika hatua ya umaliziaji na nyumba 70 zitajengwa baada ya awamu ya kwanza kukamilika. Aidha, ujenzi wa jengo moja la kuishi familia saba (7) Wilaya ya Nyang'wale mkoani Geita umekamilika. Pia, kwa kutumia Mfuko huo Jeshi la Polisi linaendelea na ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu ya Polisi Jijini Dodoma ambao umefikia hatua ya umaliziaji. Vilevile, Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi katika mwaka 2019/20 litaanza ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari 350 katika ngazi za wilaya nchini.

**27. Mheshimiwa Spika**, wananchi na wadau wameendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika ujenzi wa nyumba za kuishi familia 13 zilizopo mikoa mbalimbali. Nyumba mbili (2) katika eneo la Kanoge Mpanda - Katavi zimekamilika na kukabidhiwa kwa Jeshi. Pia, ujenzi wa nyumba tano (5) mkoani Kigoma unaendelea ambapo nyumba moja (1) imekamilika na kuanza kutumika, nyumba moja (1) ipo hatua za umaliziaji na tatu (3) zipo hatua ya msingi. Aidha, ujenzi wa jengo moja la kuishi familia nne (4) Kaskazini Pemba umefikia hatua ya linta na jengo moja la kuishi familia mbili (2) Kusini Pemba limepauliwa.

**28. Mheshimiwa Spika**, wananchi na wadau pia wameshiriki katika ujenzi wa Vituo vya Polisi, ambapo katika mwaka 2018/19 Jeshi limepokea vituo viwili (2) ambavyo ni Mburahati (Daraja A) na Kiluvya Magogoni (Daraja B) vilivyopo Jijini Dar es Salaam. Aidha, ujenzi wa vituo viwili (2) katika Mkoa wa Mjini Magharibi maeneo ya Kombeni na Amani umefikia

hatua ya kufunga linta na vituo vinne (4) katika Mkoa wa Lindi maeneo ya Mtama, Londo, Mchinga na Nanjilinji ujenzi wake umefikia hatua ya umalizaji. Vilevile, vituo vitatu (3) vya Polisi Daraja C vinajengwa kwa ufadhilli wa *United Nations High Commissioner for Refugees* (UNHCR) katika Mkoa wa Katavi maeneo ya Kanoge, Kakese na Karema na ujenzi umefikia hatua ya kupaua.

**29. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Jeshi la Polisi litaendelea na ujenzi wa jengo moja la kuishi familia (12) za Askari Buyekera Kagera kwa gharama ya **Shilingi 1,400,000,000** na Kituo cha Polisi Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa gharama ya **Shilingi 500,000,000**. Pia, Wizara itakamilisha miradi iliyoanza kutekelezwa kwa nguvu za wananchi ambapo **Shilingi 50,000,000** zimetengwa katika mradi wa ujenzi wa nyumba nne (4) za kuishi Askari Wilaya ya Meatu – Simiyu na **Shilingi 50,000,000** zitatumika katika mradi wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Mbalizi – Mbeya.

**30. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Jeshi la Polisi litakamilisha taratibu za kuhamisha Makao Makuu ya Kikosi cha kutuliza Ghasia (*Field Force Unit Headquarters*) kutoka eneo la Ukonga - Dar es Salaam kwenda maeneo ya Pera na Malivundo Wilaya ya Chalinze Mkoa wa Pwani. Zoezi hili litafanyika ili kupisha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (*Standard Gauge Railway - SGR*).

**31. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi litaendelea kushirikisha wadau mbalimbali katika ujenzi wa Vituo vya Polisi, ofisi na makazi ya Askari nchini kote. **Hivyo, natumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika miradi hiyo ili kuweza kuimarisha hali ya ulinzi na usalama katika maeneo husika.**

#### **Uboreshaji wa Vyuo vya Polisi**

**32. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuboresha Vyuo vya Polisi nchini, Jeshi la Polisi limefanya upanuzi wa miundombinu ya majengo ya Shule ya Polisi Tanzania (Tanzania Police School - TPS) iliyopo Moshi. Ujenzi wa mabweni manne (4) yenye uwezo

wa kuhudumia wanafunzi 320, majengo mawili (2) ya madarasa lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 612 na jengo moja (1) la ofisi umekamilika. Mradi huu umegharimu kiasi cha **Shilingi 20,381,380,000** kwa ufadhilli wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. **Hivyo, natumia fursa hii kwa niaba ya Serikali kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa kuboresha Shule ya Polisi Moshi.**

**33. *Mheshimiwa Spika*,** sambamba na hilo Jeshi la Polisi limeanza ukarabati wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam kwa kutumia **Shilingi 700,000,000** zilizotolewa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Joseph Magufuli. Fedha hizo ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa wakati akifunga Mafunzo ya Maafisa na Wakaguzi Wasaidizi wa Polisi tarehe 21 Desemba, 2018 katika Chuo cha Taaluma cha Polisi – Dar es Salaam. Kazi zilizoanza ni pamoja na: ujenzi wa bweni lenye vyumba 32 vyenye uwezo wa kuhudumila wanafunzi 128; ujenzi wa jengo lenye madarasa mawili (2) lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 70 kila moja; na stoo moja (1) ya kuhifadhia vifaa mbalimbali.

#### **Kuungeza Rasilimaliwatu na Rasilimalifedha katika Jeshi la Polisi**

**34. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19 Jeshi la Polisi limeajiri Askari wapya 812 kwa ajili ya kuungeza ufanisi wa kazi za Polisi. Askari hao wamehitimu mafunzo ya awali katika Shule ya Polisi Moshi tarehe 09 Aprili, 2019. Aidha, jumla ya Askari 3,725 wanatarajiwा kuajiriwa katika mwaka 2019/20.

**35. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Serikali imeliongezea Jeshi la Polisi fedha za matumizi mengineyo kiasi cha **Shilingi 82,541,040,238.77** nje ya bajeti kwa ajili ya kulipa deni la wazabuni na watoa huduma. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,199,617,311.18** zimelipwa kwa watoa huduma (TANESCO, Mamlaka za Maji, Kampuni za Simu na Kantini za Polisi) na **Shilingi 67,341,422,927.59** zimelipwa kwa wazabuni 28.

**36. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi pia limelipa deni la **Shilingi 392,197,000** kwa watumishi 113. Jumla ya **Shilingi 2,509,995,000**

zimelipwa zikiwa ni fidia kwa Askari 376 walioumia wakiwa kazini pamoja na wasimamizi wa mirathi kwa Askari 58 waliopoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu ya Jeshi. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za mashujaa wetu mahali pema peponi Amina.

### **Upatikanaji wa Vitendea Kazi kwa Jeshi la Polisi**

**37. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuendelea kuboresha utendaji kazi, Jeshi la Polisi limepokea magari 144 na makasha (*containers*) matatu (3) ya vipuri kutoka Kampuni ya Ashok Leyland ya India. Kati ya hayo magari 47 yaligawiwa katika Taasisi nyingine za Serikali kama ifuatavyo: Ofisi ya Waziri Mkuu manne (4), Jeshi la Wananchi Tanzania (15), Jeshi la Magereza (10), Jeshi la Zimamoto matano (5), Idara ya Uhamiaji matano (5), Idara ya Usalama wa Taifa matatu (3), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa moja (1), Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevyia mawili (2) na Wizara ya Maliasili na Utalii mawili (2). Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya magari 497 yamepokelewa ikiwa ni sehemu ya magari 777 yaliyopo katika mkataba husika.

**38. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi pia limepata magari 18 na pikipiki 17 kupitia misaada ya taasisi na wadau mbalimbali wa usalama ambao ni Mamlaka ya Mapato Tanzania tisa (9); Ubalozi wa Marekani manne (4); Ubalozi wa Japani moja (1); Mkuu wa Mkoa wa Mbeya mawili (2); Mahakama moja (1) na kutoka *Tanzania Association of Tourist Operators* (TATO) - Arusha moja (1). Vilevile, Jeshi limetengeneza Magari 1,327 na pikipiki 90.

### **Kushiriki katika Kuimarisha Amani na Usalama katika Nchi Mbalimbali**

**39. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19 jumla ya Maafisa na Askari 55 wanashiriki operesheni za Ulinzi wa Amani katika nchi mbalimbali. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wamepelekwa Askari watano (5); Sudani Kusini 14; Sudan – Darfur 24; Sudani – Abyei 10; Ethiopia mmoja (1); na Lesotho mmoja (1) chini ya Umoja wa Mataifa.

**40. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarisha mashirikiano ya kikanda Jeshi la Polisi lilikuwa mwenyeji katika mashindano ya pili ya Shirikisho la Majeshi ya Polisi Ufanda wa Afrika Mashariki (*Eastern Africa Police Chiefs Cooperation Organization – EAPCCO*) yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 6 hadi 12 Agosti, 2018. Katika mashindano hayo Jeshi lilikuwa mshindi wa pili hivyo **natumia nafasi hii kulipongeza Jeshi la Polisi kwa Ushindi huo uliojengea sifa Taifa** letu.

#### **Matukio ya Kutekwa na Kuuawa kwa Watoto**

**41. *Mheshimiwa Spika*,** mwezi Novemba na Desemba, 2018 yaliibuka matukio ya mauaji na utekaji wa watoto katika Mikoa ya Njombe na Simiyu. Matukio hayo ni uhalifu mpya kutokea katika mikoa hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2012. Katika Mkoa wa Njombe watoto sita (6) waliuawa na watatu (3) walitekwa, ambapo Jeshi la Polisi lilifanikiwa kuwapata watoto walitekwa wakiwa hai. Kutokana na matukio hayo, watuhumiwa saba (7) walikamatwa na kufikishwa mahakamani kwa hatua za kisheria.

**42. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile katika Mkoa wa Simiyu kilitokea mauaji ya watoto wanne (4) ambao waliuawa na kukatwa baadhi ya viungo. Kufuatia tukio hilo watuhumiwa 12 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Taarifa za kiintilijinsia zilizokusanywa na Jeshi la Polisi zilibainisha viini vya matukio hayo ni imani za kishirikina. Aidha, kupitia vyombo vya habari, Jeshi la Polisi limeendelea kutoa elimu kwa wananchi, hususan wazazi na walezi kuwa na uangalizi wa karibu kwa watoto wao wanapokwenda na kurudi shulenii na wanapokuwa majumbani.

#### **Matukio ya Mauaji ya Vikongwe na Watu wenye Ulemavu wa Ngozi (Albino)**

**43. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi pia limedhibiti mauaji ya vikongwe kutoka mauaji 117 yaliyopotiwa mwaka 2017/18 hadi 57 mwaka 2018/19. Hali hii inaonesha mauaji ya vikongwe yamepungua kwa **asilimia 51.3.** Matukio hayo

yamejitokeza katika Mikoa ya Geita (7), Iringa (1), Kigoma (2), Lindi (1), Mbeya (3), Mwanza (6), Njombe (3), Rukwa (2), Ruvuma (2), Shinyanga (3), Simiyu (4), Songwe (7) na Tabora (16). Aidha, vitendo vya mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) vimedhibitiwa kikamilifu na hakujatokea tukio la aina hiyo katika kipindi husika. Udhibithi huu utaendelea kufanyika katika mwaka 2019/20.

### **Mafunzo katika Jeshi la Polisi**

**44. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali katika mwaka 2018/19 imeendelea kuwapatia mafunzo Maafisa na Askari ili kuwajengea uwezo kiutendaji. Jumla ya Maafisa, Wakaguzi na Askari 5,335 walipata mafunzo mbalimbali katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, Askari 5,279 walipata mafunzo ndani ya nchi na 56 walipata mafunzo nje ya nchi katika nchi za China 40, Japan 4, Misri 4, India 4, Botswana 1, Ethiopia 1, Kenya 1 na Msumbiji 1. Vilevile, mafunzo ya mbinu za medani na operesheni za Makamanda yalifanyika Tanga mwezi Novemba, 2018 kwa kushirikisha nchi tano 5 za Afrika Mashariki. Nchi zilizoshiriki ni Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda na mwenyeji Tanzania.

**45. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 jumla ya Askari 10,870 watahudhuria mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kati ya hao Maafisa, Wakaguzi na Askari 470 watahudhuria mafunzo ya kitaaluma ngazi ya shahada, stashahada na astashahada katika vyuo mbalimbali nchini na 10,400 watahudhuria mafunzo ya utayari.

### **Usimamizi wa Nidhamu za Askari**

**46. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19 hatua za kinidhamu zimeendelea kuchukuliwa kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari Polisi waliobainika kujihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili mema ya Jeshi la Polisi. Jumla ya Askari 130 wa vyeo mbalimbali, Maafisa 28, Wakaguzi 14 na Askari 88 wamechukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria. Maafisa wawili (2), Wakaguzi saba (7) na Askari 88 walishtakiwa kijeshi, Askari 35 walipewa adhabu ya kufukuzwa

kazi, Askari watatu (3) walifkishwa Mahakamani na Askari wawili (2) walishushwa vyeo. Aidha, Maafisa 25 na Wakaguzi wanenye (4) waliandikiwa barua za onyo, kujieleza na tahadhari.

**47. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, Jeshi la Polisi limetambua watendaji wazuri kwa kuwapa tuzo, sifa na pongezi. Jumla ya Maafisa, Wakaguzi na Askari 55 wamefaidika na utaratibu huu, ambapo Askari saba (7) walipewa zawadi ya malipo ya jumla ya **Shilingi 700,000**, Askari sita (6) wamepewa yeti, Askari watatu (3) wamepewa barua za pongezi na Askari 39 wamepandishwa vyeo.

**48. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Wizara kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kutoa tuzo na zawadi kwa Askari, Wakaguzi na Maafisa wanaotekeleza majukumu yao ipasavyo. Vilevile, Wizara italmarisha upekuzi wa Askari na vijana wanaoomba kujunga na Jeshi ili kuwa na Askari wenye nidhamu na moyo wa dhati wa kulitumikia Jeshi na Taifa kwa ujumla. Aidha, Wizara itaendelea kuchukua hatua stahiki kwa Maafisa na Askari wasiozingatia maadili ya Jeshi vikiwemo vitendo vya kuomba na kupokea rushwa, kubambikiza kesi na kushiriki kwenye matukio ya uhalifu.

## **JESHI LA MAGEREZA**

### **Huduma za Magereza**

**49. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi la Magereza limeendelea na jukumu la kuwahifadhi wafungwa na mahabusu. Aidha, Jeshi hilo limeendelea kuwarekebisha tabia wafungwa ili wamalizapo vifungo vyao wawe raia wema wenye kutii sheria na uwezo wa kuchangia maendeleo ya uchumi nchini.

### **Hali ya Ulinzi na Usalama Magerezani**

**50. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Jeshi la Magereza imeendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika magereza yote nchini. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 kulikuwa na jumla ya wafungwa na mahabusu 38,501. Kati

ya hao, wafungwa ni 19,395 na mahabusu 19,106. Idadi hii imekuwa ikitababisha msongamano wa wafungwa hasa katika mageresa yaliyopo katika miji mikubwa.

**51. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukabiliana na msongamano wa wafungwa magerezani, Wizara kuititia Jeshi la Magereza inaendelea kutumia njia mbalimbali za kupunguza msongamano huo ikiwemo: msamaha wa Mhe. Rais, ambapo jumla ya wafungwa 4,477 walinufaika, wafungwa 91 walinufaika na utaratibu wa mpango wa Parole kuititia Sheria ya Bodi za Parole Sura ya 400 ya mwaka 2002; na wafungwa 788 walinufaika na utaratibu wa kifungo cha nje. Takwimu hizo ni kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019.

**52. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, Jeshi limekamilisha ujenzi wa magereza mawili ya Mahabusu ya Chato – Geita na Ruangwa - Lindi. Kukamilika kwa awamu hii ya kwanza ya ujenzi wa magereza haya kumesaidia kusogeza huduma za magereza pamoja na kupunguza msongamano mkubwa uliokuwepo katika Gereza Nachingwea na Gereza Muleba. Kwa sasa Gereza Chato limeshahapeka jumla ya wafungwa na mahabusu 417 na Gereza Ruangwa limepokea wafungwa na mahabusu 115. Jeshi la Magereza litaendelea kujenga magereza katika wilaya zisizokuwa na magereza kwa lengo la kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi.

**53. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Jeshi la Magereza litaendelea kudhibiti msongamano wa wafungwa magerezani kwa kutumia njia zilizotajwa hapo juu. Aidha, Jeshi la Magereza limeongeza bajeti ya shughuli za Parole kutoka **Shilingi 116,518,000** mwaka 2018/19 hadi **Shilingi 241,300,000** mwaka 2019/20.

#### **Programu ya Adhabu Mbadala ya Kifungo cha Gerezani**

**54. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea kusimamia Sheria ya Huduma kwa Jamii Sura ya 291 ya mwaka 2002 na Sheria ya Majoribio na Ujenzi wa Tabia Sura ya 247 ya mwaka 2002 ili kutekeleza Programu ya Adhabu Mbadala ya Kifungo cha Gerezani. Hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya Taarifa za

Uchunguzi wa Kijamii 3,850 ziliandaliwa na kuwezesha wafungwa 3,629 (Wanaume 2,769 na Wanawake 860) kutumikia adhabu zao nje ya magereza, hivyo kupunguza msongamano wa wafungwa na kuokoa jumla ya **Shilingi 2,100,000,000** ambazo Serikali ingezitumia kwa ajili ya kugharamia chakula cha wafungwa hao. Katika kipindi hicho, wafungwa **1,990** wamemaliza adhabu zao na kurudishwa kwenye jamii kuungana na familia zao.

**55. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Wizara inatarajia kuongeza mikoa mingine mitatu katika kutekeleza Programu ya Adhabu Mbadala ya Kifungo cha Gerezani. Mikoa hiyo ni Katavi, Lindi na Ruvuma, hivyo kufanya wigo wa matumizi ya adhabu mbadala kufikia mikoa yote ya Tanzania Bara. Aidha, Wizara itaendelea kuharakisha uandaaji wa taarifa za uchunguzi ili kuhakikisha wahalifu na wafungwa wa vifungo vya muda mfupi usiozidi miaka mitatu wanatumikia adhabu mbadala nje ya magereza na hivyo kusaidia kupunguza msongamano magerezani.

**56. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi pia limeimarisha upukuzi ili kubaini vitu visivyoruhusiwa kuingizwa magerezani na kudhibiti vitendo viovu. Katika kufikia azma hiyo, utekelezaji wa mpango wa kufunga mfumo wa kisasa wa ulinzi wa kielektroniki umeanza kutekelezwa katika Magereza makubwa ya Mkoa wa Dar es Salaam (Ukonga, Keko na Segerea). Katika mwaka 2019/20 **Shilingi 50,000,000** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi hii pamoja na kuanza kufunga mfumo huo katika Gereza Arusha na Gereza Isanga - Dodoma. Zoezi hili litaendelea kutekelezwa katika Magereza yote nchini kulingana na upatikanaji wa fedha.

### **Mkakati wa Kujitosheleza kwa Chakula**

**57. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Jeshi la Magereza limeandaa Mkakati wa miaka mitano (2018/19 – 2022/23) wa Kujitosheleza kwa Chakula cha Wafungwa na Mahabusu. Mkakati huo umejielekeza katika kuzalisha mazao muhimu ya chakula

ambayo ni mahindi, mpunga na maharage. Mkakati husika umeanza kutekelezwa katika magereza kumi (10) ya Arusha, Idete, Kiberege, Kitai, Kitengule, Ludewa, Mollo, Nkasi, Pawaga na Songwe kwa kutenga jumla ya ekari 12,370.

**58. *Mheshimiwa Spika*,** katika msimu wa kilimo 2018/19, Jeshi la Magereza limelima na kupanda eneo lenye jumla ya ekari 5,395 katika magereza hayo. Katika eneo hilo, ekari 3,455 zimepandwa mahindi kwa matarajio ya kuvuna tani 6,299, ekari 1,230 zimepandwa mpunga na matarajio ni kuvuna tani 3,228 na ekari 710 zimepandwa maharage kwa matarajio ya kuvuna tani 568. Pamoja na Mkakati huo, magereza mengine yataendelea na shughuli za kilimo zikiwemo mbogamboga na matunda kwa utaratibu wa kuwekewa malengo ya uzalishaji.

**59. *Mheshimiwa Spika*,** hatua nyingine zillizochukullwa katika kuboresha shughuli za kilimo ni ununuzi wa matrektu kumi (10) na zana zake ambayo yamesambazwa katika Magereza ya Idete na Kiberege – Morogoro (2), Isupilo – Iringa (1), Kitai – Ruvuma (1), Kwitanga - Kigoma (2), Ludewa – Njombe (1), Mollo – Rukwa (1), Mugumu – Mara (1) na Songwe (1). Aidha, Jeshi la Magereza limeyafanya matengenezo matrektu ya zamani 13 ili kuongeza nguvu katika shughuli za kilimo.

**60. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Jeshi la Magereza litaendelea kutekeleza Mkakati wa Kujitosheleza kwa Chakula cha Wafungwa na Mahabusu kwa kulima jumla ya ekari 8,150 za mazao mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao: mahindi ekari 5,450 kwa matarajio ya kuvuna tani 9,810, mpunga ekari 1,675 kwa matarajio ya kuvuna tani 4,397 na maharage ekari 1,025 kwa matarajio ya kuvuna tani 615.

**61. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza maagizo ya Mhe. Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuhusu kuzalisha miche bora ya michikichi na kuanzisha kiwanda cha kuzalisha mafuta yatokanayo na zao hilo, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali limeanza kuendeleza kilimo hicho katika Gereza Kwitanga mkoani Kigoma. Wadau hao ni pamoja na Tanzania Agricultural Research Institute (TARI),

Tanzania Industrial Research and Development Organization (TIRDO), Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) na Halmashauri ya Kigoma Vijijiini. Katika kilimo hicho Gereza Kwitanga lenye ukubwa wa ekari 1,100 litakuwa shamba la mfano kwa kuzalisha miche bora na kuza kwa wananchi. Pia, wananchi watapata soko kwa kuza chikichi kama malighafi katika kiwanda kitakachojengwa kwa ajili ya kuzalisha mafuta ya mawese na mise.

**62. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Jeshi la Magereza litaendelea na kazi za kilimo cha chikichi na kuzalisha mbegu bora za zao hilo. Aidha, kazi ya upembuzi yakinfu wa kiwanda cha kuzalisha mafuta ya mawese na mise inayofanyika kupitia TIRDO itakamilishwa.

**63. *Mheshimiwa Spika*,** sambamba na zao la chikichi, Jeshi la Magereza pia limepeewa jukumu la kuzalisha miche bora ya korosho na kuisambaza kwa wakulima wa Mkoa wa Dodoma. Katika kutekeleza jukumu hilo, jumla ya miche 360,000 imezalishwa na kusambazwa kwa wananchi kupitia Vituo vya Gereza Mpwapwa na Gereza Kongwa.

**64. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi la Magereza pia linashirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo (Agriculture Seed Agency – ASA) nchini kuzalisha na kusambaza mbegu bora kwa wakulima. Katika mwaka 2018/19, jumla ya ekari 872 zimelimwa katika magereza mbalimbali kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora za mahindi, maharage, mpunga na ufuta. Matarajio ni kupata tani 200 za mbegu bora za mazao hayo. Katika mwaka 2019/20 Jeshi la Magereza litaendelea kushirikiana na Wakala huyo kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora.

#### **Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira katika Maeneo ya Magereza**

**65. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19 Jeshi la Magereza limeendelea na juhudzi za utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 eneo la ukubwa wa ekari 300 limepandwa

miti aina ya milingoti na pine katika Magereza ya Isupilo na Mgagao yaliyopo mkoani Iringa. Katika mwaka 2019/20 Jeshi kwa kushirikiana na Tanzania Forest Fund (TFF), lilaendelea na utunzaji wa Mazingira kwa kupanda miti 555,000 katika vituo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na kutunza miti 2,217,828 iliyopo.

### **Kuboresha Makazi ya Watumishi wa Jeshi la Magereza na Mabweni ya Wafungwa na Mahabusu**

**66. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi la Magereza lilaendelea kujenga nyumba katika vituo mbalimbali nchini. Jukumu hili linatekelezwa kuititia mpango unaoelekeza Wakuu wa Vituo kutumia nguvu kazi ya Askari, wafungwa na rasilimali zilizopo katika maeneo yao. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya nyumba 129 zimekamilika na nyumba 264 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Gharama za kukamilisha nyumba hizo ni **Shilingi 1,815,517,293**.

**67. *Mheshimiwa Spika*,** ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Magereza eneo la Ukonga, Dar es Salaam unaendelea, ambapo majengo ya utawala na maabara yamekamilika. Majengo ya stoo ya kuhifadhi dawa na wodi za kulaza wagonjwa yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, majengo ya hospitali ya rufaa yaliyokuwa yanajengwa katika Gereza Segerea yamebadilishwa matumizi na kuwa mabweni ya kulala wafungwa na mahabusu. Uamuzi huu umetokana na Jeshi la Magereza kujenga Hospitali ya Rufaa katika eneo la Ukonga na hivyo kutokuwa na uhitaji wa Hospitali nyingine ya rufaa. Majengo mawili (2) ya mabweni kati ya manne (4) yamewekewa sakafu, milango na mfumo wa majitaka. Kwa kufanya hivyo, nafasi 800 za kuhifadhi wafungwa na mahabusu zimeongezeka na kusaidia kupunguza msongamano.

### **Mafunzo na Ajira kwa Jeshi la Magereza**

**68. *Mheshimiwa Spika*,** mafunzo ya ndani ya Jeshi yameendelea kutolewa ambapo Askari 61 wanaendelea na mafunzo katika ngazi ya cheti cha sheria. Aidha, wanafunzi

29 wamehitimu taaluma ya urekebishaji katika ngazi ya cheti kwenye Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Ukonga Dar es Salaam na Askari 37 wamehitimu kozi za ufundi katika fani mbalimbali kwenye Chuo cha Ufundi Ruanda - Mbeya.

**69. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Jeshi la Magereza linatarajia kuajiri Askari 685. Pia, Jeshi litatoa mafunzo ya muda mfupi ya ndani ya Jeshi kwa lengo la kuboresha utendaji. Mafunzo hayo yatahusisha wataalam wa usimamizi wa rasilimali za Serikali, Kumbukumbu na Nyaraka za Serikali kwa lengo la kuboresha utendaji ndani ya Jeshi la Magereza.

#### **Kuboresha Huduma za Usafirishaji katika Jeshi la Magereza**

**70. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha utoaji wa huduma, Jeshi la Magereza limepata jumla ya magari makubwa 13 aina ya "Ashok Leyland T/Carrier" kutoka Jeshi la Polisi (10) na Jeshi la Wananchi Tanzania (3). Magari hayo yanatumika katika shughuli za usafirishaji wa mizigo. Hatua hii imesaидia kupunguza tatizo la usafirishaji na uchukuzi katika Jeshi la Magereza.

#### **Ushiriki wa Jeshi la Magereza katika Ulinzi wa Amani chini ya Umoja wa Mataifa na Mahusiano ya Kikanda**

**71. *Mheshimiwa Spika***, Maafisa wanne (4) na Askari watano (5) wa Jeshi la Magereza wapo katika nchi za Sudani Kusini na Sudan – Darfur wakishiriki ulinzi wa amani. Jeshi pia, linashirikiana na nchi ya Seychelles katika masuala yanayohusiana na magereza, ambapo Maafisa watano (5) na Askari 15 wako nchini Seychelles wakiendelea kubadilishana uzoefu.

#### **Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza**

**72. *Mheshimiwa Spika***, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza (Prisons Corporation Sole - PCS) kuititia Kikosi cha Ujenzi limekamilisha ujenzi wa maghala mawili (2) ya kuhifadhiya silaha kwa ajili ya Jeshi la Polisi katika maeneo ya FFU Ukonga

- Dar es Salaam na TPS Moshi - Kilimanjaro. Maghala hayo tayari yamekabidhiwa kwa Jeshi la Polisi. Vilevile, Shirika limekamilisha ujenzi wa majengo ya ofisi za kuanzia kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu katika eneo la Mtumba Jijini Dodoma. Aidha, ujenzi wa ukuta wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Jijini Dodoma unaendelea. Kazi zote zilizotajwa zina thamani ya **Shilingi 3,556,378,436.32**.

**73. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, Kampuni Hodhi ya Mkulazi ambayo ni ya ubia kati ya Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza na NSSF imelima jumla ya ekari 2,150 na kupanda miwa katika eneo la Gereza Mbigiri. Matarajio ni kuvuna tani 103,200 za miwa ifikapo mwishoni mwa mwaka 2019 ambazo zitauzwa katika Kiwanda cha Sukari Mtibwa. Utaratibu huu ni wa mpito wakati ununuzi wa mitambo na ujenzi wa kiwanda kipyta cha kuzalisha sukari ukiendelea. Aidha, Kamati Elekezi (*Steering Committee*) imeundwa kwa ajili ya kuharakisha taratibu za ujenzi wa kiwanda. Shirika limetoa ardhi yenye jumla ya ekari 12,294.5, kati ya hizo ekari 12,000 ni kwa ajili ya shamba la kulima miwa, ekari 239.5 kwa ajili ya kujenga kiwanda kipyta na ekari 55 eneo la makazi ya watumishi. Ardhi hiyo itatumika kama mchango wa shirika katika ubia huo ambapo majadiliano ya kiasi cha hisa kwa wabia hao yanaendelea na yatakamiliwa kabla ya mwezi Juni, 2019.

**74. *Mheshimiwa Spika*,** kama Wizara ilivyoahidi katika Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2018/19, Shirika kuititia Kampuni ijulikanayo kama Karanga Leather Industries Company Limited limeboresha kiwanda cha viatu cha zamani kilichopo eneo la Gereza Karanga Moshi. Kampuni hiyo inaendeshwa kwa ubia kati yake na *Public Service Social Security Fund (PSSSF)*. Uboreshaji huo umefanyika kwa kuongeza mashine mpya 55 za aina mbalimbali na mtambo mmoja (1) wa kutengeneza viatu. Kwa sasa kiwanda kina uwezo wa kuzalisha jozi 400 za viatu kwa siku ikilinganishwa na jozi 150 zilizokuwa zikilizalishwa awali.

**75. Mheshimiwa Spika**, kufuatia hali hiyo, Kiwanda hicho kilitengeneza na kukabidhi jumla ya jozi 15,000 za viatu kwa ajili ya Jeshi la Polisi zenyе thamani ya **Shilingi 1,237,666,600**. Kati ya jozi hizo, buti ni jozi 10,000 na viatu vya kawaida (*staff shoes*) jozi 5,000. Aidha, viatu vya aina mbalimbali vyenye thamani ya jumla ya **Shilingi 277,664,000** vilitengenezwa kwa ajili ya wateja mbalimbali.

**76. Mheshimiwa Spika**, pia Shirika limeingia mkataba na Kampuni hiyo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vipyा vinne (4) vitakavyojengwa katika eneo la Gereza Karanga. Viwanda hivyo vitahusika na kuchakata ngozi, kutengeneza soli, kutengeneza viatu na bidhaa nyingine za ngozi kama mikanda na mikoba. Ujenzi wa viwanda hivyo umepangwa kukamilika ifikapo mwezi Julai, 2020.

**77. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza pia linatengeneza samani mbalimbali katika viwanda vyake vilivyopo Ukonga - Dar es Salaam, Uyui - Tabora na Arusha. Katika mwaka 2018/19 viwanda hivyo vimepokea zabuni za kutengeneza samani zenyе jumla ya **Shilingi 1,339,199,763.97**. Zabuni hizo zilitoka katika Taasisi za Serikali na watu binafsi na zitakamilika kabla ya Juni, 2019.

**78. Mheshimiwa Spika**, ukarabati wa Kiwanda cha Samani Arusha unaendelea kutohana na kukumbwa na janga la moto mwezi Novemba, 2018. Katika hatua ya awali, mashine zilizoungua zimefanyiwa ukarabati na tayari zinaendelea kufanya kazi ya kutengeneza samani. Aidha, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza lina mpango wa kujenga kiwanda kipyा katika eneo hilo kuititia mkopo wa **Shilingi 475,000,000** kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania (*Tanzania Investment Bank - TIB*). Majadiliano kati ya Shirika na Benki hiyo yanaendelea na yatakamilika kabla ya mwezi Juni, 2019.

**79. Mheshimiwa Spika**, Shirika pia linayo miradi mingine ya viwanda vidogo vidogo vya sabuni, ushonaji, uhunzi na chumvi ambayo inaendelea na uzalishaji kwa zabuni na kwa ajili ya kuuza sokoni. Kwa mwaka 2018/19 mauzo ya jumla ya

bidhaa za miradi hii midogo midogo yalifikia kiasi cha **Shilingi 248,500,000**.

**80. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza limeandaa Rasimu za Mpango Mkakati wa miaka mitano (2019/20 – 2023/24) na Mpango wa Biashara (*Business Plan*) wa miaka mitatu (2019/20 - 2021/22). Mipango hiyo ina lengo la: kuongeza ufanisi na kuimarisha utendaji wa shughuli za Shirika; kuwa na uwezo endelevu na usimamizi bora wa fedha; kuboresha miundombinu na vitendea kazi; kuboresha matumizi ya ardhi kwa kuyapima na kuyapatia hati; kuimarisha rasilimaliwaitu; kuimarisha mifumo ya mawasiliano; na kuweka muundo wa utawala utakaoimarisha utekelezaji wa shughuli za Shirika. Rasimu hizo zitakamilishwa katika mwaka 2019/20 baada ya kushirikisha wadau muhimu.

### **JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

**81. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na jukumu la kukinga, kuokoa majeruhi, mali na uharibifu mbalimbali unaotokana na moto, mafuriko, ajali za barabarani na majanga mengine.

**82. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Jeshi limeshiriki katika kuzima moto na kufanya uokoaji katika matukio 1,785 nchi nzima. Matukio hayo ni pamoja na uokoaji wa watu na mali katika ajali ya Kivuko cha MV Nyerere kilichotokea katika Kisiwa cha Ukara; kuzima moto na kufanya uokoaji katika Kiwanda cha Kutengeneza Viatu cha Bora kilichopo eneo la Tazara - Dar es Salaam; na Kiwanda cha Kutengeneza Samani - Arusha kinachomilikiwa na Jeshi la Magereza. Aidha, Jeshi lilifanya uokoaji kwa watu waliofukiwa na kifusi katika mgodi wa Inyenze Wilaya ya Nyang'wale - Geita.

**83. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pia limefanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto katika maeneo mbalimbali nichini. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya majengo 34,395 na magari 4,786 yalikaguliwa. Kutokana na ukaguzi huo kiasi cha **Shilingi**

**4,516,875,000** kilikusanywa. Katika mwaka 2019/20 Jeshi litaendelea na ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto ili kuzuia na kupunguza matukio ya moto nchini.

**84. *Mheshimiwa Spika*,** katika hatua za kudhibiti majanga ya moto elimu imeendelea kutolewa kwa umma kuititia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo vipindi vya runinga 45 na vipindi vya redio 331. Aidha, katika kukabiliana na matukio ya moto katika shule za Msingi na Sekondari, Jeshi limefanikiwa kufungua jumla ya Vilabu vya Zimamoto 34 kwa ajili ya kutoa elimu katika shule za Msingi na Sekondari. Vilabu 26 vipo katika shule za Sekondari kwenye Mikoa ya Dar es Salaam (8), Dodoma (4), Iringa (4), Katavi (2), Mwanza (4), Mtwara (1), Shinyanga (1) na Tanga (2); na vilabu nane (8) vipo katika shule za msingi katika Mikoa ya Dodoma (4) na Mwanza (4). Elimu hiyo itaendelea kutolewa kwa umma katika mwaka 2019/20.

#### **Hali ya Vitendea Kazi vya Kuzima Moto na Uokoaji**

**85. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuendana na kasi ya ukuaji wa miji nchini unaoambatana na ujenzi wa majengo marefu pamoja na viwanda, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linapaswa kutoa huduma katika wilaya zote nchini na kuwa na vifaa vya kisasa. Hata hivyo, Jeshi linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa vitendea kazi, hususan magari na vifaa vya uokoaji.

**86. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukabiliana na upungufu wa vitendea kazi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika mwaka 2018/19 limepata jumla ya magari 16. Kati ya magari hayo, tisa (9) yamepokelewa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA (magari matano (5) ni ya kuzima moto na manne (4) ni ya utawala); gari moja la kuzima moto kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya; gari moja la kuzima moto kutoka Serikali ya Austria; na malori matano (5) kutoka Jeshi la Polisi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Vilevile, Jeshi limepokea msaada wa kontena lenye vifaa vya kuzima moto na uokoaji kutoka Ujerumani.

**87. Mheshimiwa Spika**, kupitia bajeti ya mwaka 2018/19 jumla ya **Shilingi 3,750,000,000** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari matano (5) ya kuzima moto. Hadi kufikia Machi, 2019 kiasi cha **Shilingi 3,000,000,000** kimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa magari hayo. Mzabuni husika amepatikana ambaye ni Kampuni ya Marce Fire Technology kutoka Afrika ya Kusini. Katika mwaka 2019/20 magari hayo yataletwa nchini. Aidha, jumla ya **Shilingi 4,500,000,000** zimetengwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 3,750,000,000** ni kwa ajili ya ununuzi wa magari mengine matano (5) na **Shilingi 750,000,000** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuzima moto na uokoaji.

**88. Mheshimiwa Spika**, vilevile Wizara imeandaa Rasimu ya Mpango wa Maboresho ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (2019/2020 - 2024/2025). Mpango huo pamoja na mambo mengine una lengo la kuboresha upatikanaji wa magari na vifaa vya kuzima moto na uokoaji. Mpango husika umegawanywa katika awamu tano (5) na gharama za utekelezaji wake zinakadiriwa kuwa **Shilingi 205,676,903,000**. Rasimu ya mpango huo imewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua zaidi.

**89. Mheshimiwa Spika**, kazi ya kuzima moto pia inahitaji uwepo wa visima vya kuhifadhia maji (*Fire Hydrants*) katika maeneo mbalimbali. Visima vilivyopo kwa sasa ni 2,042 nchi nzima ikilinganishwa na mahitaji ya visima 285,000. Kati ya visima vilivyopo, visima 692 vinafanya kazi na visima 1,350 ni vibovu. **Natumia fursa hii kutoa wito kwa Mamlaka za Maji katika mikoa mbalimbali, kutekeleza jukumu lao la kufanya matengenezo ya visima hivyo ili kuwezesha kazi ya kuzima moto kufanyika kwa wakati na ufanisi.**

**Mafunzo, Ajira na Upandishwaji wa Vyeo kwa Maafisa na Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**90. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimaliwatu, mwaka 2019/20 Jeshi la Zimamoto na uokoaji linatarajia kuajiri Askari 500. Pia, Jeshi litawapandisha vyeo Maafisa na Askari 1,343 kwenye ngazi mbalimbali.

**91. *Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ujuzi wa utendaji, Askari 92 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wamepatiwa mafunzo (*Refresher Course*) katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo – Handeni, mkoani Tanga. Pia, Askari wanne (4) wamepata mafunzo ya uzimaji moto na uokoaji nchini Kenya.

**Ukarabati na Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**92. *Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza agizo la kuhamia Makao Makuu Jijini Dodoma, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepewa **Shilingi 1,506,148,300** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya muda ya Makao Makuu. Ujenzi wa jengo hilo la ghorofa nne (4) umefikia hatua ya umaliziaji. Vilevile, Jeshi limepata Kiwanja Na. 15 Kitalu 'A' kilichopo Jijini Dodoma kwa ajilli ya ujenzi wa ofisi ya kudumu ya Makao Makuu.

**HUDUMA ZA UHAMIAJI**

**Utekelezaji wa Mradi wa Uhamiaji Mtandao**

**93. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Idara ya Uhamiaji imeendelea kutoa huduma za uhamiaji kupitia mfumo wa kielektroniki (*e-immigration*) kwa kuanza kutoa Pasipoti za kielektroniki.

**94. *Mheshimiwa Spika***, tarehe 26 Novemba, 2018 Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa alizindua mfumo wa kielektroniki wa kutoa vibali vya ukaazi (*e-permit*) pamoja na Visa (*e-Visa*). Mfumo huo unamuwezesha mteja kutuma maombi yake kwa njia ya mtandao. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mfumo wa kudhibiti watu wanaoingia na kutoka nchini (*e-border Management Control System*). Mfumo huu utaanza kutumika mwezi Julai, 2019 na utasaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka yetu pamoja na kuongeza udhibiti wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Vilevile, katika mwaka 2019/20 Serikali itaunganisha *e-visa*, *e-permit na e-passport* katika ofisi za kibalozi nje ya nchi.

**95. *Mheshimiwa Spika*,** mfumo huo wa kielektroniki wa huduma za uhamiaji umeanza kuonesha mafanikio sio tu ndani ya nchi bali hata njie ya nchi. Katika kudhihirisha mafaniko hayo, **napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Pasipoti Mpya ya Tanzania ya Kielektroniki imetunukiwa Tuzo ya kuwa Pasipoti bora katika Ukanda wa Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika, kwa kukidhi viwango vya ubora wa kiusalama vinavyopendekezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia Usafiri wa Anga (International Civil Aviation Organization-ICAO).** Tuzo hiyo ilitolewa katika sherehe zilizofanyika katika Kisiwa cha Malta tarehe 26 Machi, 2019 na ilikabidhiwa kwa Idara ya Uhamiaji kwa niaba ya Serikali.

**96. *Mheshimiwa Spika*,** Tuzo hizo huandaliwa kila mwaka na Taasisi iitwayo RECONNAISSANCE, ambayo pamoja na mambo mengine, huzingatia ubora na usalama wa uchapishaji nyaraka za kielektroniki kama vile Vitambulisho vya Taifa, fedha za noti na Pasipoti. Vigezo viliviyotumika kuipatia tuzo Pasipoti ya Tanzania ni pamoja na: ubora wa alama za usalama (*Security Features*); Teknolojia iliyotumika; na ubunifu wa michoro, picha na alama mbalimbali zinazobeba historia, rasilimali na utambulisho wa nchi yetu. Ushindi wa Pasipoti yetu katika kipengele cha usalama, unaashiria kufikiwa kwa lengo kuu la Uhamiaji Mtandao la kuimarisha ulinzi na usalama nchini.

#### **Hali ya Ulinzi na Usalama Mipakani**

**97. *Mheshimiwa Spika*,** hali ya ulinzi na usalama mipakani imeendelea kuwa shwari kutokana na kuimarisha udhibiti wa watu wanaoingia na kutoka nchini. Kazi hii inafanyika kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama pamoja na wananchi wenye nia njema.

**98. *Mheshimiwa Spika*,** kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya wageni 957,977 waliingia nchini ikilinganishwa na wageni 1,021,071 waliongia katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Aidha, jumla ya wageni 950,507 walitoka nchini ikilinganishwa na wageni 954,926 waliotoka mwaka 2017/18. Katika kipindi hiki, jumla ya wageni 293 walizuiliwa

kuingia nchini kutokana na sababu mbalimbali za kiusalama na kutokidhi vigezo mbalimbali nya kiuhamiaji. Vilevile, jumla ya Watanzania 1,015 waliokwenda nje ya nchi kinyume na taratibu za kiuhamiaji walirudishwa nchini na wahamiaji haramu 5,604 waliondoshwa nchini.

### **Misako, Doria na Ukaguzi**

**99. Mheshimiwa Spika**, misako, doria na ukaguzi umeendelea kufanyika katika sehemu mbalimbali ili kuwabaini wageni wanaoishi nchini kinyume cha sheria. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya watuhumiwa wa uhamiaji haramu 9,610 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Idadi hii imepungua kwa **asilimia 28.2** ya wahamiaji haramu 13,393 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka 2017/18. Idadi kubwa ya wahamiaji haramu hao walitoka katika Mataifa ya Ethiopia na Eritrea.

**100. Mheshimiwa Spika**, tarehe 03 - 04 Aprili, 2019 Jijini Dar es Salaam ulifanyika mukutano wa kimataifa uliozikutanisha nchi tatu za Tanzania, Kenya na Ethiopia pamoja na Wadau wa Maendeleo (*Development Partners*) ambao ni Balozi za Uingereza, Marekani, Ujeruman, Norway, Ubelgiji, European Union (EU), United Nations – Resident Coordinator Office (UN-RCO), Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (International Organization for Migration - IOM) na International Committee of Red Cross (ICRC). Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mukutano huo uliokuwa na lengo la kutafuta mbinu mbalimbali za kukabiliana na wahamiaji haramu wanaoingia nchini.

**101. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengine, mukutano huo uliazimia: kuweka mikakati ya pamoja katika kushughulikia changamoto ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu; kuangalia namna bora ya kubadilishana taarifa za wasafirishaji; mikakati ya kuwaondoa nchini wahamiaji haramu na kuhakikisha hawarejei tena bila kufuata taratibu. **Kufuatia mukutano huo nilitoa agizo kwa Idara ya Uhamiaji kuhakikisha kwamba inawasaka madalali wa wahamiaji haramu ili waweze kukamatwa na kufunguliwa**

**mashitaka.** Majina ya madalali hao yameanza kupokelewa na yanafanyiwa kazi na Wizara.

**102. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Serikali itaendelea kusimamia Sheria na Kanuni za Uhamiaji ili kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu katika maeneo ya mipaka na vituo vyta kuingilia nchini. Aidha, misako, doria na kaguzi zitaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuwabaini na kuwadhibiti wahamiaji haramu pamoja na madalali, wasafirishaji, wanaowahifadhi pamoja na wote wanaoshiriki kwa namna moja au nyingine katika uhalifu huo.

### **Pasipoti na Hati Nyingine za Kusafiria**

**103. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya Pasipoti 73,416 zilitolewa kwa Watanzania walotaka kusafiri nje ya nchi. Pasipoti hizo zilitolewa katika makundi yafuatayo: Pasipoti za Kawaida 72,842, Pasipoti za Kibalozi 418 na Pasipoti za Kiutumishi 156. Idadi hiyo imeongezeka kwa **asilimia 59.7** kutoka jumla ya Pasipoti 45,965 zilizotolewa mwaka 2017/18. Ongezeko hilo limetokana na kuboreshwa kwa Mfumo wa Utoaji wa Pasipoti na kuongezeka kwa uhitaji wa Pasipoti kwa raia wa Tanzania.

**104. *Mheshimiwa Spika*,** pia, Hati za Safari za Dharura 190,170 zilitolewa katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 ikilinganishwa na Hati za Safari za Dharura 109,726 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2017/18. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la Hati za Safari za Dharura 80,444 sawa na **asilimia 73.3**. Katika mwaka 2019/20 Wizara kuititia Idara ya Uhamiaji itaendelea kutoa Pasipoti na hati nyingine za kusafiria kwa raia wa Tanzania wenye mahitaji hayo.

### **Vibali Vilivyotolewa kwa Wageni Wakaazi**

**105. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya vibali vyta ukaazi 9,878 (daraja "A" 1,032; daraja "B" 5,596; na daraja "C" 3,250) vilitolewa kwa wageni walioingia nchini kwa malengo mbalimbali. Aidha, katika

kipindi husika jumla ya Hati za Mfuasi 725 na Hati za Msamaha 2,037 zilitolewa. Katika mwaka 2019/20 vibali vyatuaazi na hati mbalimbali za kuingia nchini zitaendelea kutolewa kwa wageni wenye tija kwa Taifa.

### **Wageni Walioomba na Kupewa Uraia wa Tanzania**

**106. *Mheshimiwa Spika***, jumla ya wageni 94 walipewa uraia wa Tanzania katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019. Idadi hii ni ndogo kwa **asilimia 30.4** ikilinganishwa na wageni 135 waliopewa uraia katika kipindi kama hiki mwaka 2017/18. Wageni waliopewa uraia wa Tanzania ni kutoka nchi za Burundi (2); India (39); Kenya (9); Lebanon (7); Lesotho (1); Morocco (1); Pakistan (8); Rwanda (2); Somalia (4); Uganda (2); Uingereza (6); Yemeni (12); na Zambia (1).

### **Watanzania Waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine**

**107. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Watanzania 37 wamepoteza hadhi ya kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Sura ya 357 Rejeo la mwaka 2002 kwa kupata uraia wa mataifa mengine. Watu hao wamepata uraia katika mataifa yafuatayo: Afrika Kusini (1), Austaria (2), Botswana (1), Canada (1), Denmark (3), Grenada (1), India (1), Kenya (1), Marekani (3), Norway (4), Uganda (1), Uingereza (5) na Ujeruman (13). Katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2017/18 Watanzania 60 waliukana uraia wao.

### **Mafunzo kwa Watumishi wa Idara ya Uhamiaji**

**108. *Mheshimiwa Spika***, mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo kiutendaji Maafisa na Askari 625 ndani na nje ya nchi yamefanyika, kati ya hao 604 walipatiwa mafunzo ndani ya nchi na 21 nje ya nchi. Katika mwaka 2019/20 Idara ya Uhamiaji itaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa Maafisa, Askari na Watumishi raia ili kuwaongezea ujuzi. Aidha, Askari 500 wanatarajia kuajiriwa kwa Idara hiyo.

### **Uboreshaji wa Mazingira ya Ofisi na Vitendea Kazi Muhimu**

**109. *Mheshimiwa Spika***, Serikali ilitoa magari nane (8) kwa Idara ya Uhamiaji ambayo wamiliki wake walishindwa kulipia

kodi. Vilevile, Jeshi la Polisi limetoa magari matano (5) na Ubalozi wa Marekani umetoa msaada wa magari manne (4) kwa ajili ya matumizi ya Idara. Magari hayo yamegawiwa katika mikoa mbalimbali. Aidha, Idara pia imenunua magari manne (4) kwa ajili ya Viongozi waliopo Makao Makuu kuititia ruzuku iliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Ofisi ya Uhamiaji Zanzibar. Hivyo, hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Idara ya Uhamiaji imepata jumla ya magari 21. Katika mwaka 2019/20 Serikali itaendelea na juhudi za kupata vitendea kazi muhimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi.

#### **Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji Jijini Dodoma**

**110. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea na taratibu za ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji Jijini Dodoma. Hadi sasa Mshauri elekezi amepatikana ambaye ni Chuo Kikuu cha Ardhi na atashirikiana na Bureau of Industrial Cooperation (BICO) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vilevile, Mkandarasi wa ujenzi SUMA JKT tayari amekabidhiwa eneo la mradi kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kazi nyingine zilizokamilika ni upimaji wa udongo, usanifu wa jengo pamoja na michoro. Jengo hili litakuwa la ghorofa nane (8) na nafasi ya ofisi za watumishi 1,200 na litagharimu jumla ya **Shilingi 30,000,000,000**.

**111. *Mheshimiwa Spika*,** sehemu ya fedha za ujenzi wa mradi huo zinatokana na ahadi ya **Shilingi 10,000,000,000** ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyotoa tarehe 31 Januari, 2018 wakati wa uzinduzi wa huduma ya Uhamiaji Mtandao. Kazi za ujenzi zitaendelea katika mwaka 2019/20 na mradi utakamilika ndani ya miezi 18.

#### **VITA DHIDI YA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI WA BINADAMU**

**112. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kuititia Sekretarieti ya Kupambana na Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa

Binadamu imeokoa jumla ya wahanga 31 na kuwapatia misaada. Kati ya wahanga hao, 23 ni wa ndani ya nchi na 8 kutoka nje ya nchi (Malaysia 1, Thailand 6 na Uganda 1). Baadhi ya wahanga hao wameunganishwa na familia zao na wengine taratibu za kuwaunganisha na familia zao zinaendelea.

**113. *Mheshimiwa Spika*,** tarehe 30 Julai, 2018 Tanzania iliungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha siku ya Kimataifa ya Kupinga Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu. Maadhimisho hayo yalifanyika Kitaifa Jijini Dar es Salaam na jumla ya washiriki 500 walihudhuria. Lengo la maadhimisho hayo ni kutoa elimu na kuhamasisha jamii kupinga biashara hiyo. Aidha, katika maadhimisho hayo Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu 2018 – 2022 (*Anti-Trafficking in Persons National Action Plan*) ulizinduliwa.

**114. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Machi, 2019 mafunzo yalitolewa kwa Maafisa 108 wanaohusika katika utekelezaji wa Sheria ya kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu ya Mwaka 2008. Mafunzo hayo yalitolewa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar. Maafisa walioshiriki walikuwa Polisi 9, Uhamiaji 9, Waendesha Mashtaka 14, Majaji/Mahakimu na Wasajili wa Mahakama 49, Maafisa Ustawi wa Jamii 11, Watendaji Kata 4 na Maafisa 12 kutoka Taasisi zisizokuwa za Serikali (Non-Governmental Organizations - NGO's). Lengo ni kuendelea kuwajengea uwezo watekelezaji wa Sheria husika nchi nzima ili waweze kuitekeleza kikamilifu.

**115. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara pia imeendelea kutoa elimu kwa umma, hususan kwa wanawake na watoto, juu ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu ili kuwaepusha kurubuniwa na kuingia katika mikono ya wahalifu wa biashara hii. Elimu hii pia imeisaidia Wizara kupata taarifa za mitandao inayojihusisha na uhalifu huu kutoka kwa raia wema.

**116. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kikanda wa Nchi Wanachama wa Jumuiya

ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (Southern African Development Community – SADC) uliohusu mapambano dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu. Mku الوا huo ulifanyika tarehe 21 – 24 Agosti, 2018 Jijini Dar es Salaam. Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Mohamed Abood – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Zanzibar. Miiongoni mwa maazimio ya mku الوا huo ni: kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa taarifa zinazohusu biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu na kuingizwa kwenye kanzidata ya SADC; kuimarisha utoaji wa takwimu za robo mwaka kwenye Sekretarieti ya SADC; na nchi wanachama ambazo hazijaanza kutumia Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu zihakikishe zinakamilisha Sheria husika na kuanza kutumika.

**117. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Wizara itakamilisha marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu ya Mwaka 2008. Marekebisho hayo yanafanyika kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Sheria hiyo ili kuongeza udhibiti wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu hapa nchini. Moja ya maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika sheria husika ni kuongeza wigo wa adhabu kwa wahalifu wa biashara hiyo.

#### **MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA Mradi wa Vitambulisho vya Taifa**

**118. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (National Identification Authority - NIDA) imeendelea na zoezi la usajili na utambuzi wa raia wa Tanzania, wageni wakaazi pamoja na wakimbizi, wenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Hadi kufikia Machi, 2019 Mamlaka imefanikiwa kusajili jumla ya watu 19,934,708 ikiwa ni sawa na **asilimia 82** ya lengo la kusajili watu 24,295,468. Aidha, Mamlaka imetoa namba za Utambulisho wa Taifa kwa Wananchi 11,133,095 ikiwa ni sawa na **asilimia 55.8** ya watu waliosajiliwa. Mamlaka pia imechapisha vitambulisho 4,850,724 na kugawa kwa wananchi 4,503,769. Hata hivyo, ili kuongeza kasi ya kuchapisha vitambulisho, Mamlaka ipo

katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za ununuzi wa mashine mpya mbili (2) zeny uwezo wa kuchapa vitambulisho 9,000 kwa saa ikilinganishwa na vitambulisho 750 kwa saa vinavyochapishwa na mashine zilizopo sasa.

**119. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia NIDA imeanzisha utaratibu wa kuvipeleka Vitambulisho vya Taifa katika ofisi za Watendaji wa Kata kwa ajili ya kuongeza kasi ya ugawaji wa vitambulisho kwa wananchi. Pia, Mamlaka inashirikiana na taasisi nyingine kutumia Namba za Utambulisho wa Taifa katika kutoa huduma. Mionganoni mwa Taasisi hizo ni Idara ya Uhamiaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Usajili wa Biashara (BRELA), Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa (NHIF), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Taasisi za Fedha. Aidha, jumla ya Taasisi 47 za Serikali na Binafsi zimeunganishwa katika Mfumo wa Usajili na Utambuzi wa Watu nchini.

**120. *Mheshimiwa Spika***, Mamlaka pia imeunganisha ofisi mbili (2) za usajili za Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma na Busega Mkoani Simiyu katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na hivyo kufanya jumla ya ofisi zilizounganishwa kufikia 119. Kati ya ofisi hizo 112 zipo Tanzania Bara na saba (7) zipo Zanzibar.

**121. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Wizara kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa itaendelea na zoezi la usajili ili kufikia wananchi 25,237,954 kwa kuzingatia takwimu za ukuaij wa ongezeko la watu watakaofikia umri wa miaka 18 zilizotolewa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa (National Bureau of Statistics - NBS). Aidha, Wizara itaendelea na programu ya kuelimisha umma juu ya umuhimu wa Kitambulisho cha Taifa.

**122. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Wizara kupitia NIDA itakamilisha upembizi yakinifu (*feasibility study*) wa ujenzi wa ofisi 25 za usajili za wilaya, Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka Jijini Dodoma pamoja na mifumo ya TEHAMA. Aidha, ujenzi wa ofisi hizo na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA utaanza mara baada ya kukamilika kwa upembizi yakinifu. Kati ya ofisi hizo 22 zitajengwa Tanzania Bara na tatu (3) zitajengwa Zanzibar (Wilaya ya Micheweni - Kaskazini Pemba,

Wilaya ya Mkoani - Kusini Pemba na Wilaya ya Magharibi - Mjini Magharibi). Kazi hizo zitatekelezwa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea ambapo **Shilingi 9,645,489,600** zimetengwa katika mwaka 2019/20.

**123. *Mheshimiwa Spika*,** kazi nyingine zitakazotekelezwa kuititia mradhi huo ni: kuendelea na utoaji wa Vitambulisho vya Taifa katika mikoa yote nchini; kukamilisha mfumo wa mawasiliano katika wilaya 32 na Makao Makuu; kuunganisha Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa pamoja na mifumo ya taasisi nyingine 45 ili iweze kusomana kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma za utambuzi katika taasisi hizo; kuandaa Rasimu ya Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu; kununua vifaa vya usajili na vitendea kazi kwa ajili ya ofisi za wilaya pamoja na magari matano (5). Katika mwaka 2019/20 jumla ya **Shilingi 10,000,000,000** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea kutekeleza kazi hizo.

**124. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeanzisha utaratibu unaowezesha wananchi kupata nakala ya Kitambulisho cha Taifa kuititia Tovuti ya Mamlaka hiyo ([www.nida.go.tz](http://www.nida.go.tz)). Sambamba na utaratibu huo, wananchi wanaweza kupata Namba ya Utambulisho wa Taifa kuititia simu zao za viganjani kwa kupiga namba \*152\*00# halafu kuchagua namba 3 na kufuata maelekezo. Kuititia namba hiyo ya Utambulisho wa Taifa wananchi wanaweza kupata huduma mbalimbali zikiwemo: usajili wa kampuni ya biashara; usajili wa laini za simu; huduma za fedha zitolewazo na benki; ulipaji wa kodi ya Serikali; kupata mikopo ya elimu ya juu; kupata hati za viwanja; na kupata pasipoti.

## **HUDUMA KWA WAKIMBIZI**

**125. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kutoa huduma kwa Wakimbizi nchini kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Wakimbizi ya Mwaka 2003, Sheria Na. 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998 na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia.

**126. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imeendelea kupokea na kuhifadhi wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Tanzania ilikuwa inawahudumia waomba hifadhi na wakimbizi 321,642 ambapo kati ya hao Warundi walikuwa 239,164, Wakongo 81,887, Wasomali 150 na 441 kutoka nchi za Eritrea, Ethiopia, Iran, Kenya, Nigeria, Rwanda, Sudani Kusini, Syria, Uganda na Yemen.

**127. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa kimataifa inaendelea kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi wanaohifadhiwa hapa nchini ikiwemo kuwarudisha katika nchi zao za asili mara baada ya usalama katika nchi hizo kuimarka. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya wakimbizi 28,662 kutoka Burundi walirejeshwa nchini mwao kwa hilari yao. Idadi hiyo inafanya wakimbizi waliorejeshwa nchini mwao tangu zoezi hilo liliivoanza mwaka 2017 kufikia 63,167 kati ya 83,676 waliojiandikisha sawa na **asilimia 73.3.**

**128. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali imeendelea na zoezi la kuwahamishia katika nchi ya tatu wakimbizi waliopo nchini. Hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka 2018/19 jumla ya wakimbizi 2,583 walihamishiwa katika nchi za Marekani (2,149), Canada (188), Australia (245) na Uholanzi (1). Serikali inatekeleza majukumu hayo kwa kushirikiana na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNHCR na IOM.

#### **Masoko ya Pamoja kati ya Wananchi na Wakimbizi**

**129. Mheshimiwa Spika**, Wizara imetekeleza agizo la Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipofanya ziara ya kikazi Mkoani Kigoma kuhusu kuyahamishia ndani ya makambi masoko ya pamoja. Katika kutekeleza agizo hilo Wizara imehamishia masoko mawili (2) ndani ya Kambi za Nduta na Mtendeli yanayotumiwa na wananchi pamoja na Wakimbizi ili kuimarisha usalama na kudhibiti utoro wa wakimbizi.

**Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira katika Kambi za Wakimbizi**

**130.** *Mheshimiwa Spika*, shughuli za uhifadhi wa mazingira ndani ya kambi za wakimbizi na maeneo ya vijiji vinavyozunguka kambi hizo zinaendelea kufanyika. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika ni ujenzi wa nyumba za matofali na mabati 1,590, nyumba zinazohamishika 328, kugawa mitungi 28,815 ya gesi kwa wakimbizi kwa ajili ya kupikia na ujenzi wa majiko banifu 25,670 ya kupikia.

**131.** *Mheshimiwa Spika*, shughuli nyingine zilizofanyika ni kupanda miti 560,121 ndani ya kambi pamoja na vijiji jirani vinavyozunguka kambi za wakimbizi, kuweka alama za mipaka (*beacon*) ndani ya mita 60 za Kingo za mito na kununua mashine tano (5) kwa ajili ya kuzalisha mkaa unaotokana na mabaki ya miti na mazao kwa ajili ya kupikia. Shughuli hizi zilifanyika kwa kushirikiana na Shirika la UNHCR na Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Kakonko na Kibondo.

**132.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kutoa kipaumbele katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwenye maeneo ya kambi za wakimbizi na vijiji vinavyozunguka kambi hizo. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na UNHCR katika kufanya tathmini ya athari za shughuli za wakimbizi kwenye mazingira (*environmental audit*) katika kambi za Nyarugusu, Nduta na Mtendeli. Tathmini hiyo itawezesha kutekeleza mikakati endelevu ya kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira katika maeneo husika.

**133.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kuwashafadhi wakimbizi waliopewa hadhi hiyo kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu, kuwatafutia suluhisho la kudumu ikiwa ni pamoja na kuwarejesha katika nchi zao za asili kwa hiari na kuwashamishia nchi ya tatu. Aidha, Wizara itaendelea kuimarishe udhibiti na kudumisha hali ya usalama katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuhifadhi wakimbizi.

**KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO**

**134.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi dhidi ya utendaji wa

Idara na vyombo vya usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya malalamiko 234 yalipokelewa kutoka kwa wananchi kuititia njia ya barua, simu, barua pepe, nukushi (*Fax*) pamoja na mahojano ya ana kwa ana. Kati ya malalamiko hayo, 191 yalihusu Jeshi la Polisi, 11 Jeshi la Magereza, 4 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 14 Uhamiaji, 3 Wakimbizi, na 4 NIDA. Aidha, malalamiko 7 yalihusu taasisi zilizopo nje ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na hivyo yaliwasilishwa kwenye taasisi husika kupatiwa ufumbuzi.

**135. *Mheshimiwa Spika*,** kati ya malalamiko hayo, 129 yalipatiwa ufumbuzi na watusika kujulishwa na mengine 105 yanashughulikiwa. Katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kupokea, kushughulikia na kufuatilia malalamiko ya wananchi ili kuhakikisha ufumbuzi wake unapatikana kwa wakati na hatimaye haki kutendeka.

#### **USAJILI NA USIMAMIZI WA JUMUIYA ZA KIJAMII**

**136. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kusajili na kufanya ufuatiliaji wa uendeshaji wa Jumuuya za Kijamii. Aidha, Wizara imekuwa ikitatua migogoro inayojitokeza kwenye Jumuuya hizo kwa lengo mahususi la kuhakikisha amani na utulivu unakuwepo katika jamii. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya maombi ya usajili ya jumuuya 150 yamepokelewa, ambapo 77 ni ya Jumuuya za Kidini na 73 ni Jumuuya za Kijamii. Kutowana na maombi hayo, jumla ya Jumuuya 69 zilisajiliwa, kati ya hizo 38 ni za Kijamii na 31 ni za Kidini. Maombi ya Jumuuya 81 yanaendelea kushughulikiwa.

**137. *Mheshimiwa Spika*,** sambasamba na shughuli za usajili, uhakiki wa jumuuya unaendelea kuimarishwa ikiwa ni pamoja na kuboresha kanzidata ya jumuuya zote ambazo zinakidhi vigezo vya kuendelea kuwepo kwa mujibu wa Sheria ya Jumuuya Sura ya 337. Vilevile, Wizara imekamilisha mfumo mpya wa usajili wa Jumuuya za Kijamii ujulikanao kama *Societies Management System*. Mfumo huo utawezesha shughuli za usajili kufanya kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato yanayotokana na ada ya maombi na ada ya uandikishaji.

## **MAENDELEO YA RASILIMALIWATU MAKAO MAKUU YA WIZARA**

**138.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Wizara ilipokea watumishi wapya saba (7) kutoka Sekretarieti ya Ajira. Wizara pia, iliwapandisha vyeo watumishi 16 wa kada mbalimbali na kuwabadilisha kada watumishi saba (7). Aidha, watumishi watano (5) kutoka Makao Makuu ya Wizara walipelekwa kwenye mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada na Stashahada. Katika mwaka 2019/20 Wizara imepanga kuwawezesha watumishi 74 kutoka Makao Makuu ya Wizara kupata mafunzo katika fani mbalimbali. Kati ya watumishi hao, 24 watahuduria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili na watumishi 50 watahuduria mafunzo ya muda mfupi.

### **C. SHUKURANI**

**139.** *Mheshimiwa Spika*, natoa shukurani kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Mhandisi Hamad Masauni kwa msaada wake anaonipa katika kusimamia majukumu ya Wizara. Vilevile, nawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu Meja Jenerali Jacob G. Kingu na Naibu Katibu Mkuu Ramadhan K. Kailima kwa uongozi wao madhubuti katika kusimamia utekelezaji wa kazi na majukumu ya Wizara.

**140.** *Mheshimiwa Spika*, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Wakuu wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Inspeksa Jenerali wa Jeshi la Polisi, Simon N. Sirro; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Dkt. Phaustine Kasike; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias E. Andengenye; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala; na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Dkt. Arnold M. Kihuale. Vilevile, nawashukuru Makamishna; Makamishna Wasaidizi; Wakuu wa Idara na Vitengo; Askari na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuendelea kutekeleza shughuli za Wizara kwa weledi na ufanisi.

**141.** *Mheshimiwa Spika*, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatoa shukurani kwa nchi wahisani

zikiwemo Austria, Belgium, Egypt, Jamhuri ya Watu wa China, India, Japan, Korea Kusini, Morocco, Urusi, Ujerumanii pamoja na Taasisi na Mashirika ya Kimataifa ya ASA, EU, RESA, IOM, UNDP, UNHCR, UN-Women, UNICEF, WFP, Vyombo vya Habari, Jumuiya za Kijamii na wananchi kwa ujumla. Wadau wote hawa wamekuwa nguzo muhimu katika kutoa misaada ikiwemo ya ujenzi wa ofisi, vituo vya Polisi na makazi ya Askari, vitendea kazi pamoja na kutoa taarifa mbalimbali ambazo zinasaidia kubaini na kuzuia uhalifu. Pia, naishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia "Press A" kwa kuchapisha hotuba hii kwa ubora na kwa wakati.

**142. *Mheshimiwa Spika***, kipekee naishukuru familia yangu, ndugu, marafiki na wananchi, hususan wa Jimbo langu la Mwibara kwa ushirikiano wao katika kuchangia maendeleo ya jimbo letu.

#### D. HITIMISHO

**143. *Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kulinda amani na usalama kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola nchini pamoja na wadau mbalimbali. Kuwepo kwa utulivu nchini kutaendelea kuwezesha utekelezaji wa shughuli za maendeleo na hivyo kuimarisha uchumi wa nchi.

**144. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imepanga kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka **Shilingi 297,014,614,300** mwaka 2018/19 hadi **Shilingi 471,893,927,000** mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la **asilimia 58.8**. Ili kufikia lengo hilo Wizara itatumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuimarisha matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Mapato ya Serikali (*Government Electronic Payment Gateway - GePG*) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango katika kutoa elimu elekezi kwa watumiaji wa mfumo huo.

**145. *Mheshimiwa Spika***, mipango mingine ya ukusanyaji wa mapato itakayotekeliza na Wizara ni: kuongeza idadi ya wahasibu kwenye ofisi za Wizara katika ngazi za wilaya; kuendelea kuhuisha viwango vya tozo na ada mbalimbali ili viendane na wakati; kuendelea kufanya ukaguzi wa

tahadhari na kinga ya moto katika maeneo mbalimbali nchini; kuimarisha huduma za uhamiaji mtandao; na kufanya kaguzi za mara kwa mara za Vyama vya Kijamii ili viweze kulipa ada husika kwa wakati.

**146. *Mheshimiwa Spika***, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 921,247,033,279** kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2019/20. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 889,308,619,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 372,268,278,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 517,040,341,000** ni Mishahara. Fedha za Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 31,938,414,279** kati ya fedha hizo **Shilingi 21,500,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 10,438,414,279** ni fedha za nje.

**147. *Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa Hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba kuhusu Utaratibu kwa kurejea kanuni zetu za Bunge ambazo nitaenda kuzitaja.

**MWENYEKITI:** Niambie kanuni Mheshimiwa iliyokiukwa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 64(1) na vifungu vyake vyote.

**MWENYEKITI:** Yaani vyote vile nivisome vyote vimekiukwa ehe!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi unisikilize ambao nitaenda kukiiongea. Nimekuomba kuhusu utaratibu na kikakwambia nitarejea kanuni tatu tofauti sio ile kwamba nilikuwa ninampa utaratibu Mheshimiwa Kangi lakini kuhusu utaratibu wa kanuni zetu za Bunge na ambacho kinaenda kujili. Kwa hiyo, ningeomba unipe muda nirejee hizi kanuni halafu utatoa mwongozo wako kwa sababu najua wewe ni Mwanasheria mbobezi.

**MWENYEKITI:** Hili ni suala la utaratibu nenda tu kwenye kanuni iliyokiukwa basi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 15(2), Kanuni ya 99(9) sanjali na Kanuni ya 64(1).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko wewe ni Mbunge mzoefu twende polepole, niambie Kanuni ya 15 imekiukwa vipi?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 15(2) inasema kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni atateua Wabunge wa chama chake au Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambao watakuwa Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara zilizopo kwenye Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 99(9) inasema, “*baada ya Waziri kuwasilisha hotuba ya bajeti kwa mujibu wa fasili ya (1) Mwenyekiti wa kamati iliyopitia makadirio husika na Msemaji wa Kambi ya Upinzani watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika 30.*” Watatoa maoni yao; na hapa ndiyo nafanya rejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Kambi Rasmi ya Upinzani tulipeleka hotuba yetu, maoni yetu Kambi Rasmi ya Upinzani kwenda kuchapishwa. Tumeletewa hiki kijitabu ambacho kimeshachapishwa, ukiangalia mle kuna fasili nyingi sana zimeondolewa ambapo maneno ambayo yameondolewa, ndiyo maana ya kurejea kwenye 64(1) na vipengele vyake vyote ambavyo vinazuia mambo ambayo hayaruhusiwi Bungeni. Inasema, "*Bila kuathiri masharti ya lbara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge,*" na ameeleza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukirejea Kanuni ya 15(2), 99(9) na hapa na hotuba ambazo kwa mfano nikikusomea kipengele kimoja cha 9 ambacho mmekiondoa kinasema, "*demokrasia ni msingi wa haki na amani wa nchi yetu. Hata hivyo, Jeshi la Polisi limeendelea kuzuia kazi za siasa nchini kinyume na sheria za nchi, hususan mikutano ya hadhara na ile ya ndani.*"

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maoni yetu sisi, kwa nini mnaya-*edit*? Inatakiwa Serikali iyasikie iyafanyie kazi na siyo ku-*edit* maoni ya Upinzani. Haya ni maoni yetu sisi, mnatumia kanuni gani kufanya *editing?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nataka mwongozo wako. Wewe ni Mwanasheria mbobezi, utendee haki utaratibu ambao unavunjwa. Ni Mwanasheria mbobezi, tendea haki Watanzania, wanahitaji kupata maoni mbadala. Tumekuwa tukifanya hivi kipindi cha Bunge la Kumi chote, sasa hivi awamu hii Bunge la Kumi na Moja Serikali inaogopa kupata maoni ya Upinzani. Nasi mhimili ambao unategemewa na wananchi tunajibeba, tunafanya haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikubaliki. Tunaomba utuongoze na upitie yote yaliyoondolewa uruhusu yasomwe

ili Serikali ije ijibu. Tusikimbie kivuli cha maoni ya Upinzani, ifanyie kazi kwa mustakabali wa nchi yetu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko nimekuvumilia uyaseme yote uliyonayo. Ndiyo maana nilikuomba unionongoze kwenye kanuni ni zipi ambazo zimekiukwa. Sasa sijaona mahali ambapo kanuni imekiukwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa nisikilizeni. Tunaongozwa na kanuni. Sasa nikurejeshe kwenye kanuni ya 72, "Spika atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni na uamuzi wa Spika kuhusu jambo lolote kwa utaratibu, utakuwa ni wa mwisho." (*Makofi*)

Hotuba ambayo ipo kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani ninayo hapa pamoja na ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Hizi ndiyo zimewasilishwa rasmi hapa na nje ya hapo sitaruhusu kitu kingine. Huo ndiyo uamuzi wangu kuhusiana na suala la kanuni. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa niaba yake, Mheshimiwa Mbena, una muda usiozidi dakika 30.

**MHE. PROSPER J. MBENA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mabo ya Ndani ya Nchi, Fungu 14, 28, 29, 51 na 93 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani, upande wa upinzani, naomba utulivu Bungeni. Naomba utulivu tu. Fanyeni mashauriano, lakini kwa staha.

**MHE. PROSPER J. MBENA (K.n.y. MHE. MUSSA A. ZUNGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** ...kwa mwaka wa fedha 2019/

2020. Naomba taarifa hii yote kama ilivyowasilishwa Mezani iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kukubali, kisha kuidhinisha bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3)(c) cha Nyongeza ya Nane za Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hili ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na JKT. Aidha, Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinatoa mamlaka kwa Kamati zote za kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia majukumu hayo ya kikanuni, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 26 na 27 Machi, 2019 ili kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu hili la uchambuzi wa bajeti lilienda sambamba na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoishia, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kutokana na utekelezaji wa jukumu hilo, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi mitatu iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inajumuisha Mafungu matano ya kibajeti; Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Fungu 28 – Jeshi la Polisi; Fungu 29 – Jeshi la Magereza; Fungu 51 – Wizara Makao Makuu ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*); na Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu sehemu nne zifuatazo; Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelezo Kuhusu Miradi ya Maendeleo Iliyokaguliwa. Kamati ilitembelea na kukagua miradi mitatu ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ukaguzi wa miradi hiyo ulitekelezwa kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 20 Machi, 2019 katika Mikoa ya Morogoro na Dodoma. Miradi iliyokaguliwa; ukarabati wa Chuo cha Polisi Kidatu Morogoro, ujenzi wa kiwanda cha samani katika Gereza la Msalato Dodoma pamoja ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilikagua mifumo na mitambo ya mawasiliano katika Makao Makuu ya Jeshi la Polisi na kuridhika na hali ya mitambo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuliarifu Bunge lako katika mafungu yote matatu, yaani Fungu 28 – Jeshi la Polisi; Fungu 29 – Jeshi la Magereza; na Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji; hakukuwa na fedha zozote za maendeleo zilizotolewa kutoka katika bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kutotolewa kwa fedha za maendeleo kutoka Hazina kumeendelea kuwa changamoto kubwa na ya muda mrefu inayoathiri utekelezaji wa miradi hiyo iliyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Kamati kuishauri Serikali mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kutoa fedha hizo, bado fedha zimekuwa hazitolewi. Kutokanana changamoto hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi umegawanyika katika makundi matatu kama yalivyooneshwa katika ukurasa wa 3 - 7 wa taarifa ambayo imegawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kama ilivyobainika wakati wa ziara ya ukaguzi, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(1) Kutokelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kunaathiri ratiba ya utekelezaji wake.

(2) Kutokeleza miradi ya ukarabati kwa wakati kunasababisha uchakavu uliokithiri wa majengo, jambo ambalo linaongeza gharama ya ukarabati kuwa kubwa.

(3) Mwenendo mzima wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya mafungu ya Wizara hii, hususan Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto; Fungu 28 – Jeshi la Polisi; Fungu 29 – Jeshi la Magereza; na Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji kunahitaji kuboreshwa zaidi.

(4) Manufaa ya miradi ya maendeleo inayotekelawa na Wizara hii yataonekana tu pale ambapo Serikali itakapotoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa ukamilifu ili kukamilisha miradi iliyosimama na inayoendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Mapato kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2019 kiasi kilichokusanya kilikuwa ni shilingi bilioni 185.5 sawa na asilimia 62.4 ya makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2018/2019. Makusanyo hayo yameongezeka kwa asilimia 15.4 ikilinganishwa na makusanyo yaliyokusanya katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo yalikuwa shilingi bilioni 160.68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa makusanyo hayo yameongezeka katika mafungu; 28 – Jeshi la Polisi; 29 – Jeshi la Magereza; na 51 – Wizara ikilinganishwa na makusanyo ya mafungu hayo kwa kwa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebainisha kwamba mchanganuo wa makusanyo hadi kufikia mwezi Februari, 2019 kama inavyoonekena katika Jedwali Na. 1 katika taarifa hii, ulinganisho huo wa makadirio na makusanyo kwa kila fungu, ikilinganishwa na mapato halisi ya kila fungu umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mafungu yote ya Wizara ni wa kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la kupongezwa kwa sababu kila fungu liliweza kukusanya zaldi ya asilimia 50 ya makadirio ya malengo yaliyowekwa hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati inaamini hadi robo ya nne itakapokamiliika lengo la makusanyo liliowekwa litakuwa limefikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Wizara, hususan fedha za maendeleo, umeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu. Katika kipindi cha 2016/2017 na 2017/2018 Kamati illendelea kuishauri Serikali kupitia Hazina kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo kama zinavyoidhinishwa. Hata hivyo, mtiririko wa fedha kwa Wizara hii umeendelea kuwa siyo wa kuridhisha.

(1) Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 79.4 tu ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara.

(2) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari, 2019 asilimia 98.61 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na asilimia 1.39 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(3) Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 96 ya bajeti ya matumizi mengineyo iliyoidhinishwa na asilimia 24.6 tu ya bajeti ya maendeleo.

(4) Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 mafungu mawili tu; Fungu la 14 – Jeshi la Zimamoto na Fungu 51 – Wizara, ndio yaliyokuwa yamepokea fedha za maendeleo. Fungu 14 lilipokea asilimia 66 na Fungu 51 lilipokea asilimia 49.6 ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa kila fungu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni wa kuridhisha. Hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo hauridhishi bado, hususan kwa Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka minne mfululizo Kamati imekuwa ikishauri kuhusu Mafungu 14 – Zimamoto; 29 – Magereza na 93 – Uhamiaji kupewa kipaumbele katika kupelekewa fedha za maendeleo, lakini ushauri huo wa Kamati umezingatiwa katika Kifungu 14 tu katika mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za maendeleo unaathiri mpango na ratiba ya utekelezaji wa miradi hiyo chini ya mafungu hayo ambapo baadhi yake imesimama kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutotolewa kwa ukamilifu kwa fedha za maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais na Amiri jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kutambua uhitaji wa fedha za maendeleo kwa mafungu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 shilingi bilioni 6.3 zilitolewa kwa ajili ya awamu ya

kwanza ya mradi wa ujenzi wa nyumba 400 za makazi ya Askari Polisi katika mikoa minane nchini ikiwemo Njombe, Dodoma, Rufiji, Simiyu, Geita, Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba. Shilingi milioni 700 kwa ajili ya ujenzi wa ukarabati wa Chuo cha Polisi *Kilwa Road*, *Dares Salaam* na shilingi bilioni 55.56 kwa ajili ya kulipa deni la Mkandarasi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Kamati ilishauri masuala 21 yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu bajeti. Katika masuala yaliyotolewa ushauri yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, yapo ambayo yanaendelea kutekelezwa na yapo ambayo ikiwemo uhaba wa fedha, kama ilivyoonekana katika ukurasa wa 13 hadi 15 hayajazingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 471.89. Kiasi kinachotarajiwa kukusanya ni ongezeko la asilimia 58.8 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo yalikuwa shilingi bilioni 297.01. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 28 – Jeshi la Polisi kwa asilimia 33 na Fungu 93 – Uhamiaji kwa asilimia 49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi kuhusu ongezeko hilo Kamati ilibaini pia kuwa, tozo na ukiukwaji wa Sheria za Usalama Barabarani ilitarajiwa kuwa shilingi bilioni 118.32 sawa na asilimia 93 ya makadirio ya makusanyo ya Fungu hilo. Aidha, kwa Fungu 93 kamati ilibaini kuwa ongezeko hilo litachangiwa na makusanyo ya *Visa* ambapo awali yalikuwa yanakusanya na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mchangano wa lengo la makusanyo hayo unaonekana na kufafanuliwa zaidi katika Jedwali Na. 2 la Taarifa ambayo imesambazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufanuzi huo ni dhahiri kuwa Fungu 28 – Jeshi la Polisi na Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji,

ndio yanayotegemewa katika makusanyo ya Wizara hii. Kamati imebaini kuwa wakati makadirio ya makusanyo ya Mafungu ya Zimamoto, Magereza na Wizara yamepungua, Makadirio ya makusanyo ya Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji yanatarajiwa kuwa mazuri, hivyo kuongeza makadirio ya mapato ya Wizara nzima kwa asilimia 58.87 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka unaoishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza mafungu hayo kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa na umuhimu katika makusanyo ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mafungu haya yalitarajiwa kukusanya zaidi kuliko mafungu mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi. Ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia kasma, vifungu na mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha unaoishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi huo, kamati ilibaini mambo yafuatayo: Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imepungua kwa shilingi bilioni 24.31 ambayo ni pungufu ya asilimia 2.64 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019. Upungufu huu upo katika matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo kutokana na ukomo (*ceiling*) uliyowekwa. Bajeti inayoombwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imepungua kwa asilimia 19 kwa bajeti ya maendeleo. Mishahara imepungua kwa asilimia 0.6 na imepungua kwa asilimia 3.5 katika matumizi mengineyo ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, bajeti inayoombwa kwa ajili ya matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imepungua kwa asilimia 19 kwa bajeti ya maendeleo. Mishahara imepungua kwa asilimia 0.6 na imepungua kwa asilimia 3.5 katika matumizi mengineyo ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji, haijapangiwa fedha zozote kwa ajili ya miradi ya maendeleo na hivyo kutoa picha kuwa hakuna mpango wowote uliopo wa kuendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Lindi, Geita, Manyara na ukamilishaji nyumba ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji iliyoko Masaki, Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nne; fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo kwa Fungu 51 upande wa *NIDA* zimepungua kwa shilingi billioni tano sawa na asilimia 33 ikilinganishwa na shilingi billioni 15 zilizotengwa kwa mwaka 2018/2019. Fedha za matumizi mengineyo kwa Fungu 28 zimepungua kwa asilimia 2.79 ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati libaini kuwa kiasi cha shilingi billioni 7.15 kimepungua katika maeneo ya posho ya *ration* ya chakula, posho ya msamaha wa kodi na fedha za kikosi cha kupambana na matukio makubwa ya kiharifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati kusisitiza kuhusu Serikali kutenga shilingi billioni 2 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liliopo eneo la Mchicha, Dar es Salaam. Kwa miaka mitatu mfululizo 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019, Serikali haijatenga bado kasma yoyote kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo hilo katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa hospitali na jiko katika Gereza la Segerea licha ya Kamati kuendelea kusisitiza kwa muda wa miaka mitatu mfululizo kuhusu kutengwa kwa fedha hizo hasa kwa kuzingatia umuhimu wa hospitali hiyo kwa Gereza la Segerea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho; hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa miradi ya majengo ya Uhamiaji hususan katika Mkoa wa Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa maoni na ushauri mahususi kwa kila Fungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 14 - Jeshi la Zima Moto; Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa shilingi bilioni tatu katи ya shilingi bilioni 4.5 zilizotengwa kwa ajii ya ununuzi wa magari matano pamoja na vifaa vya kuzima moto na uokoaji. Suala hili ni la kupongeza kwa sababu tangu mwaka 2016/2017, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutoa fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu hili lakini zimekuwa hazitolewi kwa kiasi cha kuridhisha. Pamoja na kuipongeza Serikali, Kamati inaishauri Serikali itoe fedha zillizobaki yaani shilingi bilioni 1.5 ili kutekeleza shughuli iliyokuwa imepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Jengo la Zimamoto liliopo eneo la Mchicha, Wilaya ya Temeke, Jijini Dar es salaam ambalo ujenzi wake ulisimama tangu mwaka 2013. Jengo hilo lenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 linahitaji shilingi bilioni nane ili likamilike kwa mujibu wa makadirio ya mwaka 2016/2017. Jengo hili likikamilika linaweza kutumika kama kitega uchumi na kuiingizia kipato Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya matumizi mengineyo kiasi cha shilingi bilioni mbili ikilinganishwa na bajeti ya matumizi mengineyo iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019. Fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya posho ya chakula kwa askari na fidia ya msamaha wa ushuru wa kodi katika samani na vinywaji kwa askari wapya. Pamoja na pongezi hizi, Kamati inashauri fedha hizo zitolewe kwa ukamilifu wake katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; kwa kuwa Fungu hili limekuwa likipata mgao pungufu wa fedha za matumizi mengineyo na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya jeshi, Kamati inashauri Serikali itoe fedha kiasi cha shilingi milioni 253.06 ambacho bado hakijatolewa katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 28 – Jeshi la Polisi; Serikali itoe kiasi cha shilingi bilioni 596.64 zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Jeshi la Polisi. Fedha hizi zikitolewa kabla ya tarehe 30 Juni, 2019 ili iwezeshe utekelezaji wa shughuli zilizokuwa zimepangwa ikiwa ni pamoa na kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia, kuanzisha elimu ya juu ya vitendo vyta ukatili kwa kushirikisha dhana ya Polisi Jamii na ukarabati wa vyoo vyta polisi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; Kamati inatambua juhudzi za Serikali katika kuhakikisha kuwa changamoto ya makazi ya Askari Polisi inapata ufumbuzi. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu wake ili kuwezesha ujenzi wa makazi ya Askari Polisi ambao wengi wao wanaishi nje ya kambi jambo ambalo linaweza kuathiri maadili na utekelezaji wa majukumu yao. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kiasi cha shilingi bilioni 1.4 kilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa makazi Tanzania Bara na Zanzibar lakini hadi kufikia mwezi Februari, 2019 kiasi hicho cha fedha kilikuwa bado hakijatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; Kamati inapongeza juhudzi za Serikali katika usimamiaji wa Sheria ya Usalama Barabarani. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Jeshi la Polisi linatarajiwani kukusanya shilingi bilioni 118.42 ikiwa ni kadriro la makosa ya barabarani milioni 3.1. Kamati inashauri elimu zaidi kuhusu sheria za barabarani iendelee kutolewa kwa wananchi ili kupunguza makosa ya ukiukwaji wa sheria. Sambamba na hilo, ushauri ulitolewa hapo, inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha mchakato wa Sheria ya Usalama Barabarani ambao umechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitatu mfululizo, Jeshi la Magereza limekuwa likipokea fedha kidogo za matumizi mengineyo, jambo ambalo limeathiri utendaji wa jeshi hilo kwa kiwango kikubwa. Hivyo, tunashauri jeshi hlo lipewe fedha zaidi kwa kuzingatia umuhimu wake. Serikali ione umuhimu wa kuongeza ukomo wa bajeti kwa ajili ya fungu hilo. Serikali itoe shilingi bilioni mbili zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kiwanda cha samani kilichopo Msalato, Dodoma. Kamati imekuwa ikishauri Serikali mara mara kuhusu hilo lakini bado hajiatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika taarifa hii yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Kangi Lugola; Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Hamad Masauni; Katibu Mkuu, Meja Jenerali Jacob Kingu; Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ramadhan Kailima pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano na mchango wao mkubwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge.

Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhani Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na mto hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (FUNGU 14, 28, 29, 51 NA 93) KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mto Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na JKT. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia.

Kufuatia majukumu hayo ya Kikanuni, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 26 na 27 Machi, 2019 ili kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, jukumu hili la uchambuzi wa Bajeti lilienda sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoishia kwa Mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kutokana na utekelezaji wa Jukumu hilo, naomba kutoa Taarifa kuwa Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi mitatu iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inajumuisha Mafungu matano (5) ya kibajeti yafuatayo:-

- i) Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji,
- ii) Fungu 28- Jeshi la Polisi,
- iii) Fungu 29- Jeshi la Magereza,
- iv) Fungu 51- Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Talfa-NIDA; na
- v) Fungu 93- Idara ya Uhamiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu sehemu nne zifuatazo:-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

**2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO  
ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA  
2018/2019**

**2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo mitatu (3) iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Ukaguzi wa miradi hiyo ulitekelezwa kuanzia tarehe 15 hadi 20 Machi, 2019, katika Mikoa ya Morogoro na Dodoma.

Miradi iliyokaguliwa ni:-

**a) Fungu 28- Jeshi la Polisi**

Mradi Na. 6303 kuhusu Ukarabati wa Chuo cha Polisi Kidatu, Morogoro

**b) Fungu 29- Jeshi la Magereza**

Mradi Na. 4002 kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Samani katika Gereza la Msalato, Dodoma

**c) Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Mradi Na. 6301 kuhusu Ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji, Dodoma

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilikagua Mifumo na Mitambo ya Mawasiliano katika Makao Makuu ya Jeshi la Polisi na kuridhika na hali ya Mitambo iliyopo.

**2.2 Matokeo ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kuhusu Miradi ya maendeleo na maeneo yaliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hali ya utekelezaji wa Miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kiliarifu Bunge lako kuwa, katika mafungu yote matatu yaani Fungu 28- Jeshi la Polisi, Fungu 29- Jeshi la Magereza na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji, hakukuwa na fedha zozote za Maendeleo zilizotolewa kutoka katika Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Hata hivyo, ipo miradi ya Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji ambayo ilipelekewa fedha za maendeleo nje ya Bajeti iliyoidhinishwa katika Bajeti ya Wizara, ikiwemo mradi wa Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kutoka Hazina kumeendelea kuwa changamoto kubwa na ya muda mrefu inayooathiri utekelezaji wa miradi iliyochini ya Wizara hii. Licha ya Kamati kuendelea kuishauri Serikali mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kutoa fedha hizo, bado fedha hizo zimekuwa hazitolewi.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa Miradi umegawanyika katika makundi matatu kama yanavyoelezwa hapa chini.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la kwanza ni Miradi ya muda mrefu ya ukarabati ambayo utekelezaji wake umesimama. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo hazijatolewa kwa muda mrefu licha ya kuwa kuna mahitaji makubwa ya ukarabati. Mfano wa Miradi hii ni Mradi Na. 6303 kuhusu ukarabati wa miundombinu ya Vyuo vya Polisi nchini. Maelezo yaliyotolewa na Serikali yalibainisha kuwa katika Mwaka 2018/2019 Mradi huu ilitengewa jumla ya Shilingi **1,027,000,000/=**.

Katika fedha hizo, Vyuo vyote vya Polisi kikiwemo Chuo cha Maafisa wa Polisi Kidatu vilitengewa Shilingi **205,400,000/=** kila kimoja kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Ofisi, Mabweni na makazi ya Watumishi wa Chuo. Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Machi, 2019 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji na kubaini kuwa ukarabati uliofanyika katika Chuo cha Maafisa wa Polisi Kidatu ulifanyika

kwa mara ya mwisho Mwaka 2011/2012 ikiwa ni takribani miaka saba iliyopita. Kamati ilielezwa kuwa kwa sasa Chuo kina uwezo wa kuchukua Wanafunzi 250. Endapo Chuo kingekarabatiwa kingekuwa na uwezo wa kuchukua Wanafunzi 500 na hivyo kuongeza mapato ya Chuo kuitia tozo ya ada ya mafunzo.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilielezwa kuwa, kutohana na kutokukarabatiwa tangu mwaka 2012, Shilingi Bilioni 2.6 zitahitajika kwa ajili ya ukarabati kutohana na uchakavu mkubwa wa miundombinu na majengo katika Chuo hicho.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la pili ni Miradi mipyä iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 lakini fedha hizo hazijatolewa. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, kutokutolewa kwa fedha zilizoidhinishwa kumeathiri kuanza utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati uliopangwa.

Mfano wa miradi hiyo ni Mradi Na. 4002 wa Ujenzi wa Kiwanda cha Samani katika eneo la Gereza la Msalato, Jijini Dodoma. Kamati ilielezwa kuwa, Mradi huu ni mpyä na umebuniwa ili pamoja na mambo mengine, kuzingatia matarajio ya uhitaji mkubwa wa bidhaa za samani kutohana na Makao Makuu ya Nchi kuhamia Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Shilingi Bilioni 2 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Kiwanda, uingizaji wa miundombinu ya maji na umeme, na ununuvi wa mashine mbalimbali za uzalishaji. Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Machi, 2019 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa jambo ambalo linachelewesa Mradi huu kuanza.

Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha 2017/2018, Kiwanda cha samani cha Jeshi la Magereza- Ukonga kilipokea maombi kutoka kwa wateja mbalimbali wa Dodoma, ya kutengenezewa samani zenye thamani ya Shilingi 1,195,840,664. Maombi hayo yanatoka katika baadhi ya Wizara, Taasisi za Serikali na watu binafsi. Hii inadhihirisha kuwa yapo mahitaji makubwa ya samani katika Jiji la Dodoma hivyo ni muhimu Serikali ikatoa kipaumbele katika kuhakikisha

kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda hiki cha kutengeneza bidhaa za Samani zinatolewa ili ujenzi wake uanze mapema.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la tatu ni miradi ambayo kutokana na umuhimu wake, fedha za utekelezaji zilitolewa nje ya bajeti ya maendeleo. Mfano wa miradi hiyo ni Mradi Na. 6301 kuhusu ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji, Jijini Dodoma. Kamati ilielezwa kuwa Mradi huo unatekelezwa kufuatia ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ya kiasi cha Shilingi Bilioni 10 aliyoitao wakati wa uzinduzi wa huduma ya Uhamiaji Mtandao tarehe 31 Januari, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara yalibainisha kuwa fedha hizo zimekwishatolewa na hatua za awali za utekelezaji wa mradi huo zimeshaanza. Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuona umuhimu wa kuwa na Jengo la Makao Makuu ya Uhamiaji mapema iwezekanavyo katika Jiji la Dodoma ambalo linakuwa kwa kasi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nzuri zilizofikiwa katika maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo, Kamati ina mashaka kama fedha zilizotolewa zitaweza kukamilisha Jengo linalotarajiwa kujengwa. Ni rai ya Kamati kuwa michoro ya majengo inayopendekezwa iendane na uhalisia wa rasilimali fedha ili kuepusha changamoto za kifedha katika kukamilisha miradi muhimu kama huo.

### **2.3 Maoni kuhusu Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kama ilivyobainika wakati wa ziara za ukaguzi, Kamati ina maoni yafuatayo:-

- i) Kutokutolewa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati kunaathiri ratiba ya utekelezaji wake;

- ii) Kutokutekeleza miradi ya ukarabati kwa wakati kunasababisha uchakavu uliokithiri wa majengo jambo linaloongeza gharama ya ukarabati kuwa kubwa;
- iii) Mwenendo mzima wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Mafungu ya Wizara hii, hususan Fungu 14- Jeshi la Zimamoto, Fungu 28 - Jeshi la Polisi, Fungu 29- Jeshi la Magereza, na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji unahitaji kuboreshwa zaidi;
- iv) Manufaa ya Miradi ya Maendeleo inayotekelzeza na Wizara hii yataonekana pale tu Serikali itakapotoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa ukamilifu ili kukamilisha miradi iliyosimama na inayoendelea kutekelezwa.

### **3.0      UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

#### **3.1      Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ulizingatia makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo lililokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mafungu yote matano ya Wizara. Vilevile, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi cha Agosti na Oktoba, 2018, Januari 2019, na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

##### **3.1.1    Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi

**297,014,614,300/=** ikilinganishwa na Shilingi **293,822,132,859/=** zilizokadiriwa kukusanya katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia Mwezi Februari 2019, kiasi kilichokusanya kilikuwa ni Shilingi **185,526,900,792.62** sawa na asilimia 62.4 ya Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka 2018/2019. Makusanyo hayo yameongezeka kwa asilimia 15.4 ikilinganishwa na makusanyo yaliyokusanya katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo yalikuwa Shilingi **160,687,217,400/=**.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Makusanyo hayo yameongezeka katika Mafungu 28-Jeshi la Polisi, 29- Jeshi la Magereza, na 51-Wizara ikilinganishwa na makusanyo ya Mafungu hayo kwa Mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebainisha mchanganuo wa makusanyo hadi kufikia mwezi Februari, 2019 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01 hapa chini.

#### Jedwali Na.01: MCHANGANUO WA MAPATO

FUNGU	MAKADIRIO	%YAJUMA YALENGO	MAKUSANYO	%YA JUMA YA MAKUSANYO
14- Zimamoto	9,250,003,000	3.1	4,055,295,000	22
28- Pdls	84,687,904,000	28.5	70,383,978,860.39	37.9
29-Magereza	1,800,000,000	0.6	1,356,069,925	0.7
51-Wzara	926,601,000	0.3	473,889,309.41	0.3
93-Idara ya Uhamiaji	200,350,106,300	67.5	109,257,667,697.82	589
<b>JUMA</b>	<b>297,014,614,300</b>	<b>100</b>	<b>185,526,900,792.62</b>	<b>100</b>

**Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

- i) Makusanyo ya Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 3.1 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 14 limechangia kwa asilimia 2.2 ya kiasi kilichokusanya;
- ii) Makusanyo ya Fungu 28- Jeshi la Polisi, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 28.5 na Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 28 limeshachangia kwa asilimia 37.9 ya kiasi kilichokusanya;
- iii) Makusanyo ya Fungu 29- Jeshi la Magereza, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.6 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 29 limechangia kwa asilimia 0.7 ya kiasi kilichokusanya;
- iv) Makusanyo ya Fungu 51- Wizara, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.3 na Taarifa ya Makusanyo ilionesha Fungu hilo limechangia kwa asilimia 0.3 ya kiasi kilichokusanya;
- v) Makusanyo ya Fungu 93- Jeshi la Uhamiaji, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 67.5 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu hilo limeshachangia asilimia 58.9 ya kiasi kilichokusanya.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho huo wa makadirio ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na mapato halisi ya kila fungu, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Mafungu yote ya Wizara ni wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili ni la kupongezwa kwani Kamati ilibaini kuwa kila Fungu liliweza kukusanya zaidi ya asilimia 50 ya makadirio ya malengo yaliyowekwa hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kamati inaamini hadi robo ya nne itakapokamilika, lengo la makusanyo liliowekwa litakuwa limefikiwa.

### **3.1.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**


**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Wizara hususan fedha za maendeleo umendelea kuwa changamoto ya muda mrefu. Katika kipindi cha Mwaka 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019 Kamati iliendelea kuishauri Serikali kupitia Hazina kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo kama zinavyoidhinishwa na Bunge, hata hivyo mtiririko wa fedha kwa Wizara hii uliendelea kuwa si wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia changamoto hiyo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2019. Kupitia uchambuzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

- i) Hadi kufikia mwezi Februari 2019, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 79.4 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara.
- ii) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari 2019, asilimia 98.61 ilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na asilimia 1.39 tu ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.
- iii) Hadi kufikia mwezi Machi 2019, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 96 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo iliyoidhinishwa na asilimia 24.6 ya bajeti ya Maendeleo.
- iv) Hadi kufikia mwezi Februari 2019, Mafungu wawili tu yaani Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Fungu 51- Wizara yaliyopokea fedha za maendeleo. Fungu 14 lilipokea asilimia 66 na Fungu 51 lilipokea asilimia 49.6, ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa kila Fungu husika.

**Mheshimiwa Spika**, ili kupata picha halisi kuhusu uwiano wa upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Mishahara, Mengineyo

na Maendeleo, Kamati ililinganisha Kasma za matumizi hayo kwa Mafungu yote matano ya Wizara hii na kuwianisha kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.



### **Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ni wa kuridhisha. Hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo haqidhishi hususan kwa Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji. Kwa miaka minne mfululizo, Kamati imekuwa ikishauri kuhusu Mafungu 14- Zimamoto, 29- Magereza na 93- Uhamiaji kupewa kipaumbele katika kupelekewa fedha za maendeleo, lakini ushauri huo umezingatiwa kwa Fungu 14 tu katika Mwaka huu wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za maendeleo unaathiri Mpango na Ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mafungu hayo, ambayo baadhi yake imesimama kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kutokutolewa kwa ukamilifu kwa fedha za maendeleo kama zinavyoidhinishwa na Bunge, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu

kwa kutambua uhitaji wa fedha za maendeleo kwa Mafungu ya Wizara hii. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Shilingi **6,300,000,000/=** zilitolewa kwa ajili ya Awamu ya kwanza ya Mradi wa ujenzi wa nyumba 400 za makazi ya Askari Polisi katika Mikoa 8 Nchini ikiwemo Njombe, Dodoma, Rufiji, Simiyu, Geita, Kaskazini Unguja, Kaskazini Pemba, Shilingi Milioni 700 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Chuo cha Polisi Kilwa road Dar es Salaam na Shilingi **55,558,077,005/=** kwa ajili ya kulipa deni la Mkandarasi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa NIDA.

### **3.2 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati ilishauri masuala ishirini na moja (21) yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo kwa Mafungu yote matano. Masuala hayo yalihusu mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- i) Serikali itoe fedha za maendeleo zilizokuwa zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha miradi ya muda mrefu iliyosimama hususan ya Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji;
- ii) Serikali ishirikiane na Mashirika yake ya Nyumba na Mifuko ya Jamii kutekeleza miradi ya ujenzi kwa mikopo yenye riba nafuu katika kujenga nyumba za askari wa vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Wizara;
- iii) Serikali ilipe madeni ya huduma za maji na umeme zinazotolewa kwa Majeshi ya Polisi na Magereza;
- iv) Serikali ikamilishe ujenzi wa Jengo lilioluwa la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto katika eneo la Mchicha, TAZARA Jijini Dar es Salaam;

- v) Serikali itenye na kutoa fedha za ujenzi wa nyumba za askari Polisi na kuendelea kubuni utaratibu mpya wa kujenga makazi ya askari;
- vi) Serikali iweke Mpango Mkakati wa kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwa na vyanzo vya Mapato vya uhakika kuitia kazi zao za kilimo na ufugaji;na
- vii) Serikali itenye fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali, mabweni ya wafungwa na jiko katika Gereza la Segerea ambalo ulianza tangu miaka ya 1990.

**Mheshimiwa Spika**, katika masuala yaliyotolewa ushauri, yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, baadhi yanaendelea kuzingatiwa na mengine ambayo hayajazingatiwa kikamilifu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhaba wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya ushauri uliozingatiwa kikamilifu na Serikali ulihusu Serikali kutoa Shilingi Bilioni 10 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa utoaji wa Vitambulisho vya Taifa. Taarifa iliyotolewa na Wizara ilieleza kuwa Serikali ilitoa fedha zote shilingi Bilioni 10 katika robo ya nne ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa iliyowasilishwa ilionesha kuwa Serikali imeendelea kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusu kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za askari Polisi na kubuni taratibu nyinginezo za kuwezesha ujenzi wa nyumba za askari. Kamati ilielezwa kuwa katika kwa Mwaka 2018/2019, Mheshimiwa Rais alitoa Shilingi Bilioni **6,300,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 400 katika Mikoa nane nchini na tayari utekelezaji wake umeanza.

Aidha, Jeshi la Polisi limeendelea kutumia Mfuko wake wa Tuzo na Tozo katika kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba za askari. Maeleo yaliyotolewa yalibainisha kuwepo kwa mkandarasi wa ujenzi wa nyumba 200 za askari Jijini Dodoma katika eneo la Medeli ambapo awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa nyumba 30 ipo katika hatua za umalizaji.

**Mheshimiwa Spika**, ushauri mwagine uliotolewa ulihusu Serikali kutoa Shilingi **5,791,630,000/-** zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji za Mikoa, Wilaya na Vituo hususan kwa majengo ambayo ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu. Ushauri haukuzingatiwa kwani hakuna fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya shughuli hiyo.

**4.0      UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO  
NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**4.1      Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa  
Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo. Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na:-

- i) Kulinda usalama wa Raia na mali zao;
- ii) Kusimamia marekebisho ya tabia kwa wafungwa ndani na nje ya magereza na katika maeneo ya Jamii;
- iii) Kutoa huduma za zimamoto na uokoaji;
- iv) Kuwezesha na kudhibiti uingiaji na utokaji nchini kwa Raia na wageni; na
- v) Kuimarisha na kusimamia Mfumo wa Taifa wa Utambuzi na Usajili wa Watu Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopitia majukumu hayo ya Wizara kwa kulinganisha na Bajeti inayoombwa, ilibainika kuwa utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake utaimarishwa endapo Serikali itatoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara.

#### **4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **471,893,927,000/=**. Kiasi kinachotarajiwa kukusanya ni ongezeko la asilimia 58.8 ikillinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo yalikuwa Shilingi **297,014,614,300/=**. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 28 Jeshi la Polisi kwa asilimia 33 na Fungu 93- Uhamiaji kwa asilimia 49.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi kuhusu ongezeko hilo, Kamati ilibaini kuwa tozo ya ukiukwaji wa Sheria ya usalama barabarani inatarajiwa kuwa Shilingi **118,317,470,683** sawa na asilimia 93 ya makadirio ya makusanyo ya Fungu hilo. Aidha, kwa Fungu 93, Kamati ilibaini kuwa ongezeko hilo linachangiwa na makusanyo ya Visa ambapo awali yalikuwa yanakusanya na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mchanganuo wa lengo la makusanyo unaonekana katika Jedwali Na. 2 hapa chini.

#### **Jedwali Na.02: MAKADIRIO YA MAPATO**

FUNGU	MAKADIRIO	% YAJUMLA YA LENO
Fungu 14 - Zimamoto na uokoaji	9,250,003,000	2
Fungu 28 - Jeshi la Polisi	127,031,856,000	26.9
Fungu 29 - Jeshi la Magereza	1,887,002,000	0.4
Fungu 51 – Wizara	726,606,000	0.2
Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji	332,998,460,000	70.5
<b>Jumla</b>	<b>471,998,460,000</b>	<b>100</b>

#### **Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo:-

- i) Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linategemewa kukusanya asilimia 2 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 3.1, ki-uwiano ikiwa ni pungufu kwa asilimia 1.1;
- ii) Fungu 28- Jeshi la Polisi linategemewa kukusanya asilimia 26.9 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 28.5 kiasi ambacho ki-uwiano ni pungufu kwa asilimia 1.6;
- iii) Fungu 29- Jeshi la Magereza linategemewa kukusanya asilimia 0.4 ya makusanyo ikiwa ni pungufu ki-uwiano asilimia 0.2 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 0.6;
- iv) Fungu 51- Wizara linategemewa kukusanya asilimia 0.2 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 0.3; Kiasi hiki ni pungufu katika uwiano kwa asilimia 0.1;
- v) Fungu 93- Jeshi la Uhamiaji linategemewa kukusanya asilimia 70.5 ya makadirio ya makusanyo ikiwa ni ongezeko katika uwiano kwa asilimia 3 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo lilitegemewa kukusanya kwa asilimia 67.5.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ufanuzi huo, ni dhahiri kuwa Fungu 28- Jeshi la Polisi na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji, ndio yanayotegemewa katika makusanyo ya Wizara hii. Kamati imebaini kuwa wakati makadirio ya makusanyo ya Mafungu ya Zimamoto, Magereza na Wizara yamepungua, makadirio ya makusanyo ya Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji yanatarajiwu kuwa mazuri hivyo kuongeza makadirio ya Mapato ya Wizara nzima kwa asilimia 58.87 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka unaoishia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Mafungu hayo kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa na muhimu katika

makusanyo ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, mafungu haya yalitarajiwa kukusanya zaidi kuliko mafungu mengine.

#### **4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mhesimiwa Spika**, maelezo ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwaa kwa mafungu yote matano ni Shilingi **921,247,033,279/=**. Kati ya fedha hizo Shilingi **517,040,341,000/=** sawa na asilimia **56.12** ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi **372,268,278,000/=** sawa na asilimia 40.41 ni Matumizi Mengineyo na Shilingi **31,938,414,279/=** sawa na asilimia **3.47** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwaa, Shilingi **21,500,000,000/=** sawa na asilimia 67 ni fedha za ndani na Shilingi **785,682,000/=** sawa na asilimia 33 ni fedha za nje.

**Mhesimiwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma, Vifungu na Mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha unaoishia. Katika uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

- i) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imepungua kwa Shilingi **24,308,617,721/=** ambayo ni pungufu ya asilimia 2.64 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Upungufu huu upo katika Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kutokana na Ukomo (ceiling) uliowekwa.
- ii) Bajeti inayoombwaa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imepungua kwa asilimia 19 kwa Bajeti ya Maendeleo, Mishahara imepungua kwa asilimia 0.6 na imepungua kwa asilimia 3.5 katika matumizi mengineyo ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- iii) Fungu 93- Idara ya Uhamiaji hajapangiwa fedha zozote kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na hivyo kutoa picha kuwa

hakuna mpango wowote uliopo wa kuendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Lindi, Geita, Manyara na ukamilishaji wa Nyumba ya Kamishna Generali wa Uhamiaji Masaki- Dar es Salaam.

iv) Fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya Maendeleo kwa Fungu 51 upande wa NIDA zimepungua kwa Shilingi Bilioni 5 sawa na asilimia 33 ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 15 zilizotengwa kwa Mwaka 2018/2019.

v) Fedha za Matumizi Mengineyo kwa Fungu 28 zimepungua kwa asilimia 2.79 ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kamati ilibaini kuwa kiasi cha Shilingi 7,150,800,000/= kimepungua katika maeneo ya posho ya resheni ya chakula, posho ya msamaha wa kodi na fedha za kikosi cha kupambana na matukio makubwa ya kihalifu.

vi) Pamoja na Kamati kusisitiza kuhusu Serikali kutenga Shilingi Bilioni 2 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lililopo eneo la Mchicha, Dar es Salaam kwa miaka mitatu mfululizo 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019, Serikali haijatenga Kasma yoyote kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Jengo hilo katika Mwaka wa Fedha 2019/2020;

vii) Hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali na jiko katika Gereza la Segerea licha ya Kamati kuendelea kusisitiza kwa muda wa miaka mitatu mfululizo (2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019) kuhusu kutengwa kwa fedha hizo hasa kwa kuzingatia umuhimu wa Hospitali hiyo kwa Magereza ya Segerea; na

viii) Hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa miradi ya majengo ya uhamiaji hususan katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyoainishwa hapo juu yanatokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kuititia na kujadili Randama za Mafungu matano ya Wizara ya Mambo

ya Ndani ya Nchi kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mapema leo hii.

## **5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa maoni na ushauri mahsusini kwa kila Fungu kama ifuatavyo:-

### **5.1 Ushauri Mahsusini**

#### **5.1.1 Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

i) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa Shilingi Bilioni 3 katil ya Shilingi Bilioni 4.5 zilizetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari matano (5) ya kuzima moto na vifaa vya kuzima moto na uokoaji. Suala hili ni la kupongeza kwasababu tangu Mwaka 2016/2017 Kamati imekuwa ikishauri Serikali kutoa fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu hili lakini zimekuwa hazitolewi kwa kiasi cha kuridhisha.

Pamoja na kuipongeza Serikali, Kamati inaishauri Serikali itoe fedha zilizobaki Shilingi Bilioni 1.5 ili kutekeleza shughuli iliyokuwa imepangwa.

ii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Jengo la Zimamoto liliopo eneo la Mchicha, Wilaya ya Temeke Jijini Dar es Salaam ambalo ujenzi wake ulisimama tangu Mwaka 2013. Jengo hilo lenye thamani ya Shilingi **1,696,286,613.72** litahitaji Shilingi Bilioni 8 ili likamilike kwa mujibu wa makadirio ya Mwaka 2016/2017. Jengo hili likikamilika linaweza kutumika kama kitega uchumi na kuingizia kipato Serikali.

iii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Matumizi Mengineyo kiasi cha Shilingi Bil 2 ikilinganishwa na Bajeti ya Matumizi Mengineyo iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya posho ya chakula kwa Askari na fidia ya msamaha wa ushuru na kodi katika samani na vinywaji kwa Askari wapya.

Pamoja na pongezi hizi, Kamati inashauri fedha hizo zitolewe kwa ukamilifu wake katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

iv) Kwa kuwa Fungu hili limekuwa likipata mgao pungufu wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Jeshi, Kamati inashauri Serikali itoe fedha kiasi cha Shilingi **253,059,900/=** ambacho bado hakijatolewa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

### **5.1.2 Fungu 28- Jeshi la Polisi**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa Jeshi la Polisi katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa Raia na mali zao, Kamati inashauri yafuatayo:-

i) Serikali itoe kiasi cha Shilingi 596,638,468,000/= zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Jeshi la Polisi. Fedha hizi zitolewe kabla ya tarehe 30 Juni, 2019 ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizokuwa zimepangwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia, kuanzisha elimu juu ya vitendo vya ukatili kwa kushirikisha dhana ya Polisi Jamii na ukarabati wa Vyuo vya Polisi nchini.

ii) Kamati inatambua juhudhi za Serikali katika kuhakikisha kuwa changamoto ya makazi ya Askari Polisi inapata ufumbuzi. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu ili kuwezesha ujenzi wa makazi ya Askari Polisi ambao wengi wao wanaishi nje ya Kambi jambo ambalo linaweza kuathiri maadili ya utekelezaji wa majukumu yao. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kiasi cha Shilingi **1,400,000,000/=** kilitengwa kwa ajili ya

ujenzi wa makazi Tanzania Bara na Zanzibar lakini hadi kufikia Mwezi Februari, 2019 kiasi hicho kilikuwa hakikutolewa.

iii) Kamati inapongeza juhudzi za Serikali katika kukusanya mapato makubwa yatokanayo na tozo ya ukiukwaji wa Sheria ya Usalama barabarani. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Jeshi la Polisi linatarajiwa kukusanya Shilingi **118,317,470,683/=** ikiwa ni kadirio la makosa Milioni 3.1. Hata hivyo, Kamati inashauri elimu zaidi kuhusu Sheria ya Usalama Barabarani iendelee kutolewa kwa Wananchi ili kupunguza makosa ya ukiukwaji wa Sheria za barabarani ambayo yanababishi ajali nyingi na wakati mwingine vifo.

iv) Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha mchakato wa Sheria ya Usalama Barabarani ambao umechukua muda mrefu. Sheria itakapofanyiwa marekebisho, pamoja na mambo mengine, itasaidia kudhibiti na kupunguza makosa ya barabarani ambayo yanababishi ajali na hatimaye ulemavu na vifo.

### **5.1.3 Fungu 29- Jeshi la Magereza**

**Mhesimiwa Spika**, kwa miaka mitatu mfululizo Jeshi la Magereza limekuwa likipokea fedha kidogo za Matumizi Mengineyo jambo ambalo limeathiri utendaji wa Jeshi hilo kwa kiwango kikubwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kununua sare za Maafisa, Askari na Wafungwa. Aidha, Jeshi hilo limekuwa likipewa fedha pungufu za maendeleo na wakati mwingine fedha hizo kutokutolewa kabisa. Kwa kuzingatia haya, Kamati inashauri ifuatavyo:-

i) Serikali ione umuhimu wa kuongeza ukomo wa bajeti kwa ajili ya Fungu hili ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Ukomo mdogo usioendana na uhalsia umeathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kusababaisha ulimbikizaji wa madeni ya watoa huduma mbalimbali magerezani. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2019 deni la Jeshi la Magereza liliolahakikiwa lilikuwa Shilingi **55,121,737,785.83/=**.

- ii) Serikali itoe Shilingi Bilioni 2 zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kiwanda cha Samani- Msalato, Dodoma.
- iii) Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwekeza katika Kilimo na hatimaye kujitosheleza kwa chakula lakini ushauri huo haujazingatiwa kikamilifu. Kwa Mwaka 2018/2019 Bunge liliidhinisha Shilingi Bilioni 3 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Gereza la Idete na kuboresha shughuli za kilimo lakini hadi kufikia Mwezi Februari, 2019 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha hizo ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Gereza hilo.
- iv) Kamati inapongeza juhudzi za Serikali katika kutatua tatizo la Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu magerezani kwa kujenga Magereza mapya ya Wilaya pamoja na kuanzisha *mobile courts* zinazoongeza kasi ya usikilizwaji wa kesi. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutumia utaratibu wa parole na vifungo vyatoto nje ili kupunguza msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani.

Aidha, Jeshi la Polisi liendelee kuwezesha ili kutoa elimu kwa umma hususan vijana ambao idadi yao ni kubwa magerezani, kuhusu kujiepusha na vitendo viovu. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Jeshi la Polisi halikupelekewa fedha hizo japokuwa zilitengwa.

Vilevile, kuhusiana na msongamano wa Wafungwa na Mahabusu, Kamati inaendelea kushauri Serikali kumuwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka ya Makosa ya Jinai (Director of Public Prosecution-DPP) kuzungukia Magereza mengi zaidi ili kesi nyingi ziweze kutolewa maamuzi mapema jambo ambalo litachangia kupunguza msongamano husika kwa kiasi kikubwa.

- v) Kamati inaipongeza Serikali kwa kununua magari 10 kuititia Mpango wa ununuzi wa magari 777. Hata hivyo, kutokana

na changamoto ya upungufu wa magari unaolikabili Jeshi la Magereza hususan uhitaji wa magari 1247 ambayo kati ya hayo 480 ni kwa ajili ya usafirishaji wa mahabusu, Serikali iweke Mpango mahususi wa kuliwezesha Jeshi kupata magari zaidi ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kukosekana kwa magari ya kusafirisha mahabusu kumeendelea kuchelewesha haki za baadhi ya mahabusu za kusikilizwa kesi zao kwa tarehe zilizopangwa kutokana na kukosa usafiri wa kwenda Mahakamani.

#### **5.1.4 Fungu 51- Wizara**

- i) Serikali itoe fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa adhabu mbadala kwa wafungwa kupitia Sheria ya Probesheni na Huduma kwa Jamii. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2019 kiasi cha Shilingi **107,785,718.45** sawa na asilimia 41.54 tu ya fedha zilizoidhinishwa ndicho kilichotolewa. Kutolewa kwa fedha hizo kutasaidia wafungwa wengi zaidi kutumikia adhabu nje ya Magereza na hatimaye kusaidia kupunguza msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani.
- ii) Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kuhakiki wakimbizi waliopo nchini na kuwatafutia suluhihilo la kudumu. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2019 Wizara ilipokea asilimia 33 tu ya fedha zilizoidhinishwa jambo ambalo linaathiri ratiba ya kushughulikia masuala ya Wakimbizi ikiwa ni pamoja na kuratibu urudishwaji wa Wakimbizi hao katika nchi zao kwa hiari.

#### **5.1.5 Fungu 93- Idara ya Uhamiaji**

- i) Wakati wa kujadili Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Mwaka 2018/2019, Kamati iliishauri Serikali itoe fedha za maendeleo Shilingi **5,791,630,000/=** zilizoidhinishwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji za Mikoa, Wilaya na Vituo. Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Juni, 2018 fedha hizo hazikutolewa. Aidha, kiasi cha Shilingi Bilioni 10 kilichotengwa kwa Mwaka 2018/2019 hakikutolewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2019.

Kutotolewa kwa fedha hizo kumesababisha miradi ya Ujenzi wa majengo ya Ofisi na makazi ya Uhamiaji kusimama kwa muda mrefu. Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kutekeleza miradi hii ili kutatua changamoto ya upungufu wa majengo na nyumba za Watumishi wa Uhamiaji. Idadi ya Ofisi za Uhamiaji ni asilimi 39 tu ya mahitaji halisi ya majengo 146 na asilimia 18.4 tu ya mahitaji halisi ya nyumba 2664 ya nyumba za Watumishi.

- ii) Kwa kuwa Watumishi wa Fungu 14- Zimamoto, Fungu 28- Polisi na Fungu 29- Magereza wanapata **package** mbadala iliyokuwa inatolewa na maduka ya majeshi ambayo kwa sasa hayapo, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutoa **package** hii pia kwa Idara ya Uhamiaji ambao mazingira yao ya kazi yanaendana na ya Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii.
- iii) Serikali ione umuhimu wa kuongeza ukomo wa bajeti kwa Idara hii ili kuwezesha shughuli za misako na doria, kuwezesha kuwaondoa nchini wahamiaji haramu na kununua sare za Maafisa na Askari ambazo hazijanunuliwa kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Hadi kufikia Mwezi Februari, 2019 jumla ya wahamiaji haramu 3260 walikuwa wanashikiliwa katika Magereza mbalimbali nchini wakiwa wameshamaliza vifungo vyao jambo ambalo linachangia msongamano usio wa lazima Magerezani na vilevile kuongezea Serikali gharama za kuwatunza wahamiaji hao.

## **6.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard):-

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb, **Mwenyekiti**

2. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb, **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
4. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
5. Mhe. Prosper J. Mbenya, Mb
6. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
7. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
8. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
9. Mhe. Bonnah Mosses Kaluwa, Mb
10. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb
11. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
12. Mhe. Gerson Hosea Lwenge, Mb
13. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
14. Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
15. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
16. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
17. Mhe. Shally Joseph Raymond, Mb
18. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
19. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
20. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
21. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
22. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
23. Mhe. Augustino Manyanda Masele, Mb
24. Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb
25. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
26. Mhe. Dkt. Charles John Tizeba, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Kangi Alphard Lugola (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Eng. Hamad Massauni (Mb), Katibu Mkuu Meja Jenerali Jacob Kingu, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ramadhan Kailima pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na

Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu, Mb  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO**  
**YA NJE, ULINZI NA USALAMA**  
Aprilii, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbena kwa kuwasilisha vizuri kwa niaba ya Kamati.

Sasa tupokee taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Msigwa lakini naomba uzingatie maelekezo yangu kwamba utasoma hiki kilichowasilishwa mezani tu. Huo ndio uamuzi wangu kuhusiana na utaratibu ulioombwa na Mheshimiwa Esther Matiko. Karibu, una muda usiozidi dakika 30.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara hiyo kwa mwaka

wa fedha 2019/2020. Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Godbless Jonathan Lema, napenda kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma hotuba hii kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kufuatia adhabu ya Bunge hili kwake dhidi ya maoni yake aliyojatao Bungeni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaamini kwamba maoni yake yalipaswa kulindwa chini ya Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Tunamtakia kila la kheri kwa vile tunakumbushwa Mheshimiwa Jonathan Lema kwamba mapambano ya haki dhidi ya utawala wa sheria yataendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawatia moyo viongozi wakuu wa CHADEMA wanaokabiliwa na kesi katika mahakama mbalimbali nichini, wakiongozwa na Mheshimiwa Freeman Mboge na viongozi wengine waandamizi tunawaombea na kuwatia moyo kwa kauli mbiu ya kwamba kesho ni imara kuliko jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma maoni haya katika kipindi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa unanielewa mimi huwa sipendi matani, nenda kwenye *paragraph* ya pili inayoanza aidha...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*)

**MWENYEKITI:** Nasema hivi hayo ndio maelekezo yangu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*)

**MWENYEKITI:** Hapana, Mheshimiwa ndio maana, nilyonayo ni hii...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*)

**MWENYEKITI:** Hapana siwezi kukusikiliza wewe upo pale kusoma, soma kile ambacho kimewasilishwa mezani.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni hayo ya Serikali yametolewa, hayo yanaletwa angesoma Kangi, hayo sio ya kwetu, sio ya Upinzani. Yaani hayo unayosema tungechanganya kwenye hotuba ya Mheshimiwa Kangi. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Unabishana na mimi sasa?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** *No, sibishani kwa sababu sisi kama Upinzani tumeandaa maoni yetu haya, hayo unayoyasema ungechanganya kwenye hotuba ya Serikali akasome; tuliyonayo sisi ni haya.* (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Naomba ukakae kwanza. Waheshimiwa Wabunge wala tusichukue muda mrefu hapa, taarifa au hotuba ya Msemaji ndio hii;

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*)

**MWENYEKITI:** Hiyo ni ya kwako. Hii niliyonayo mimi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Basi kama huna kingine cha kuwasilisha basi.

**MHE. MICH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali imetoa maoni, kanuni zinatufundisha tuna maoni ya Kambi ya Upinzani, mnatupa maoni yenu wenyewe, sasa tumekuja kufanya nini sisi hapa? Yaani hapa *what are we doing? Why should we be doing your job?* Hiyo ni kazi yenu ninyi, sisi tumetengeneza maoni yetu... (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Unaona nimesimama sijasimama?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** *Ooh, I am sorry.*

**MWENYEKITI:** Anhaa!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko usinifikishe mahali nikakuonesha mamlaka ya Kiti.

Sasa Mheshimiwa Msigwa kama unataka kuendelea na Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani zingatia hayo ambayo na umepewa sio kwamba...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Arudishe maji Msigwa. (*Kicheko*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani na kwa dhamira yangu mwenyewe nitakuwa silitendei haki Taifa hili kama nitasoma hotuba ya Serikali badala ya maoni ya Kambi ya Upinzani.

Nami humu ndani ya Bunge nimeletwa na watu wanaojua mimi natoka Kambi ya Upinzani, kwa hiyo nisipoleta maoni ya Kambi ya Upinzani, dhamira inanisuta, nitakuwa sitendi haki. Hayo mnayoyataka mtamkabidhi Kangi kwenye kambi ya Serikali watasoma, sisi hatutasoma. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Rudisha maji, rudisha maji.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu. Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu, huo ndio uamuzi wenu.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** *(Alizungumza bila kutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh unafahamu nakusikia mpaka hapa?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, wachangiaji wetu tena tuna muda wa kutosha. Tunaanza na Mheshimiwa Catherine Ruge, kama hayupo naendelea na nafasi hataipata tena, naendelea, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba nimepata nafasi ya kuchangia kama Mbunge kwa kuwa maoni yetu kama Kambi Rasmi ya Upinzani yameshindikana, tutayatumia kwa kuongea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani - Fungu 28 tunalolizungumza leo ikiwepo Polisi na wenzao kuna

upungufu mwingu sana unaotokea katika Wizara hii. Nikianza kwanza na suala la wakimbizi. Kuna sare za kijeshi zilikamatwa kwenye mipaka, zile sare zilienda zikachomwa, nakubali, lakini najiuliza wafanyakazi wetu wa Uhamiaji waliachaje zile sare zikaingia katika nchi yetu. Nataka kujua, mambo yapo mawili; kama Taifa la Tanzania tulikuwa na utaratibu wa kutoa taarifa tunapokuwa na watu wasiofaa katika jamii inayotuzunguka na kama kuna kitu kibaya kinatokea, sisi kama Watanzania na Jeshi la Polisi likiwemo na *Immigration* walikuwa wanapewa taarifa na wananchi, je, mahusiano yetu kama Jeshi la Uhamiaji yapo sawasawa na wananchi, ilikuwaje hizo sare zikapita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi imekuwa ni chama kingine cha siasa, kimejificha nyuma ya Chama Tawala Chama cha Mapinduzi. Sisi kama chama kilichosajiliwa CHADEMA na wenzetu wa *CUF, ACT* na vyama vingine tunahitaji kufanya siasa kwa ajili ya kuongeza wanachama na ni wajibu wa kikanuni na Kikatiba kwa sisi kufanya kazi ya siasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana neno wanatumia intelijensia. Intelijensia ipo kwa Wapinzani na wala sio kwa Chama Tawala. Nataka niwakumbushe Jeshi la Polisi, Tanzania hii amani iliyopo sio kwa sababu tuna jeshi kubwa, sio kwa sababu tuna siasa nyingi, lakini kwa sababu watu wote tumeamua kuipenda nchi yetu na tumeamua kukataza watu wetu watulie na siku ikibidi polisi hawawezi kutushinda kwa maana Watanzania pia ni wengi kama vile Polisi wanafikiri wao wanatuweza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafanya mkutano *Area A, Area D CCM* inafanya mkutano, unakujaje kwenye ofisi yangu kwenye mkutano wa ndani umeshika *tear gas* kuja kunizua na CCM hujawazuia? Polisi tunawaonya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua mnatumika kwenye chaguzi kuja kubandika matokeo ambayo siyo kazi yenu. Mheshimiwa Siro nakuheshimu, naomba simamia taaluma ili uweze kuwazuia askari wako kwa sababu mwisho wa siku

hawa ni ndugu zetu, tunaishi nao uswahilini, tunasoma nao na tunakwenda nao sokoni. Naomba tusifike tukagombana kwa sababu ya siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linazuia Wabunge wenye majimbo kufanya siasa. Mheshimiwa Kubenea wiki mbili zilizopita kazuiwa kwa kitu kinaitwa intelijensiia lakini Mheshimiwa Mchengerwa anafanya mkutano intelijensia haipo. Nchi yetu ni ya umoja, tumeishi kama ndugu, msitutenge. Kama mnataka siasa vueni vyeo ingjeni kwenye siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitambulisho vya Taifa. Walioandikishwa ni 19,000 mpaka sasa ni milioni nne tu ndiyo wamepata vitambulisho hivyo na hawa watu wameshindwa kwa sababu hawana pesa, wanadaiwa na mkandarasi. Serikali hajatoa hela, uzalishaji wa vitambulisho ni kidogo, leo hii mnalazimisha matumizi ya Kitambulisho cha Taifa wakati wajibu wa Serikali kutoa pesa hamfanyi. Serikali yako iseme hapa tarehe hiyo 1 Mei waliyoweka ya matumizi ya kitambulisho wazue mpaka haki ya Watanzania ya kupata vitambulisho ipatikane. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni iliyochukua tenda ya kutengeneza mashine za hivyo vitambuliso kutoka Malaysia wameleta mashine ambayo uzalishaji wake ni mdogo na mpaka leo kuna watu waliwekwa ndani, sina uhakika kesi zinakwendaje. Mheshimiwa Waziri akija kujibu atuambie hatua zilizochukuliwa, pesa za Watanzania zilizopotea na wale waliosababisha ufanisi mbovu wamechukuliwa hatua gani mpaka leo. (*Makof*)

*Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi tena kwenye Polisi maana yake hawa ndiyo cancer ya Taifa. (*Makof*) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni kanuni ipi na ni njia gani inayotumika Polisi ambao wanajua kazi yao ni kulinda mali za Watanzania lakini Polisi hao hao wanakwenda

kuwagawa Watanzania kwa itikadi za kisiasa. Ma-*OCD*, ma-*RPC*, wote wanasimamia kazi za kiasasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Wabunge wote wa Upinzani wakitembelea majimbo yao *OCD* yuko mgongoni. Tunakubali, tunahitaji ulinzi, tunafanya kazi kwa sheria na sisi tumejipanga kuwa waaminifu lakini wanatuchokoza na muda mwangi sana tumewavumilia. Tunafanya mikutano wanashinda na kamera kuturekodi, mikutano ya CCM mbona hawarekodi? Tunawatangazia Uchaguzi wa Serikali za Mitaas na Vitongoji na Uchaguzi Mkuu, tunajua kuna maelezo toka juu kama yapo na sisi tutayafanyia kazi maelezo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku Jeshi la Polisi litueleze shilingi bilioni 16 za sare za Polisi ambapo pesa zilitolewa na mwisho wa siku kuna *uniform* hewa, ziko wapi? Hii ni kwa mujibu wa *CAG*.

Naomba kujua matumizi ya fedha hizo na ambazo walipata kutoka kwa wahisani ili kujenga vituo vyta mifano ambapo Polisi imeshindwa kufanya. Tunaoma watuambie na hasa Mheshimiwa Kangi Lugola, uje utupe majibu sio ya kisiasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kangi Lugola ni Mbunge mwenzetu lakini toka ameingia Jeshi la Polisi amekuwa na matamko zaidi ya 20 hata moja hakuna lililoteklezeka. Kuna wakati anatoa matamko kumbe amekosea, sijamuona akirudi hadharani na kuomba msamaha. (*Makof*)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Kangi hajaingia Jeshi la Polisi, ameingiaje Jeshi la Polisi?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kangi mara nyingi ameonekana akishusha watu vyeo labda huyo mtu kakosea lakini si haki kwa Jeshi la Polisi kumdhaliisha hadharani, kuna njia sahihi za kufanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongelea habari ya Magereza, Magereza kuna msongamano mkubwa na kibaya zaidi magereza ya wanawake wafungwa maeneo ya kuwahifadhi na kujihifadhi nayo ni madogo na wanapata shida sana. Tunaomba Magereza watazamwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jengo la Mchicha kwa Zimamoto, nimelizungumzia mara nyingi. Ni kitu kibaya kutumia pesa za Watanzania tukazi-dump pale Mchicha halafu tunashindwa kufanya mipango ya miaka mingi, tunatumia akili zetu nyingi kuzuia Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea suala la *uniform* za wafungwa. *Uniform* ni haki kwa mfungwa... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Kigua na Mheshimiwa Kiula ajiandae.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa ya kusimama leo kuweza kuchangia katika Hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Maafisa wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Wizara hii ina changamoto nyingi sana lakini lazima tukiri kwamba kuna kazi kubwa inafanyika na lazima tuwapongeze. Nayasema haya kwa sababu Watanzania ni mashahidi wameona kwa kiasi kikubwa kwamba ajali na

uhalifu umepungua kwa kiasi kikubwa sana. Zamani tulikuwa tunashuhudia uhalifu unafanyika katikati ya Dar es Salaam pale Kariakoo lakini sasa hivi hali hiyo imepungua. Ni lazima tulipongeze Jeshi la Polisi katika hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimponeze Waziri, Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla kwa jitihada kubwa ambazo wanachukua kuhakikisha kwamba wanajenga vituo vya polisi pamoja na magereza. Changamoto ni kubwa kila maeneo, hususan wa wilaya mpya. Binafsi nikushukuru Mheshimiwa Waziri, tumepata shilingi milioni 150 kwa ajili ya kujenga nyumba za Polisi Wilaya ya Kilindi. Bado tuna changamoto ya kituo cha kisasa, wilaya ile ni ya muda mrefu, toka 2002 hatuna kituo cha kisasa. Naibu Waziri ni shahidi alifika Kilindi, nikuombe Mheshimiwa Waziri muiangalia Wilaya ya Kilindi tuwe na Kituo cha kisasa cha Polisi, vituo vya kata vilivybaki tutajenga sisi wenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Katika ukurasa wa 57 umezungumzia Vitambulisho vya Taifa. Hapa pana shida kwa sababu zoezi hili linakwenda taratibu sana. Juzi tumepata taarifa kwamba kuanzia tarehe 1 Mei kila aliye na Kitambulisho cha Taifa ndiye atakayesajiliwa laini, sasa hili ni tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Wizara ya Mambo ya Ndani iliingia mkataba na Kampuni inaitwa *Iris Corporation Berhad* ya Malaysia, ilisainiwa Septemba, 2014 na ulikuwa unakwenda hadi 2016 lakini wakaongezewa tena mkataba hadi Septemba, 2018. Jambo hili ni lazima tuseme kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani lazima mlifanyie kazi. Vitambulisho vya Taifa ni haki ya msingi na ni lazima muongeze *speed* mhakikishe kwamba vitambulisho vinapatikana katika ngazi ya vijiji hadi mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu tunapata malalamiko kutoka vijijini huko kwamba vitambulisho hivi bado. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri lisimamie hili ili Watanzania waweze kupata vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie juu ya ujenzi wa vituo vya polisi. Nimezungumzia Kituo cha Polisi Kilindi hapa lakini kulikuwa na utaratibu au mkataba na Kampuni ya STAKA ambao walitakiwa kujenga vituo vya Polisi Tanzania nzima. Sasa hapa pametokea changamoto japokuwa naipongeza Serikali iliweza kuchukua hatua kwa wale ambao hawakuweza kutekeleza majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, moja ya mapungufu makubwa katika mkataba huu ni kwamba ujenzi wa vituo hivi ulikuwa chini ya kiwango lakini pia waliweza kubadili mipango ya ujenzi. Mahali pengine ni kwamba hapakuwa na mikataba ya ujenzi. Nitoe mfano mmoja tu, ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Lushoto kwa Mheshimiwa Shangazi ambao uligharimu takribani milioni 500 haukwenda sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakuamini sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na uongozi mzima pamoja na Katibu Mkuu, nina imani pamoja na mapungufu yote haya yaliyofanyika basi wale ambao hawakutekeleza wajibu wao ipasavyo lazima wachukuliwe hatua. Fedha za umma lazima zifanyiwe kazi, haiwezekani pesa zitolewe labda na wadau halafu watu wafanye ndivyo sivyo. Mimi naamini kabisa Mheshimiwa Waziri ulishakuwa Polisi, majukumu haya unayajua vizuri na Katibu Mkuu na viongozi wote wataweza kusimamia vizuri eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la kisera zaidi kwa sababu naiona Wizara hii ni kubwa sana. Afisa Masuuli ambaye ndiyo mwenye wajibu wa kusimamia fedha za umma ana maeneo makubwa sana ya kusimamia. Hili siyo la kwako Waziri, ni suala la Serikali kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuchukue mfano mdogo tu, tuichukulie *NIDA* yenyewe ambayo inasimamia Vitambulisho vya Taifa, Jeshi la Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Polisi, Katibu Mkuu ni mmoja tu, anaweza vipi ku-manage? Hebu naomba Waheshimiwa Wabunge na

Serikali kwa ujumla tuangalie namna ya kufanya *restructuring* ya Wizara hii. Kwa sababu ukiangalia *NIDA* yenyewe na hizi taasisi ni takribani Wizara tano. Mimi nadhani wakati umefika tukupunguzie lawama na malalamiko ili Serikali iweze kufanya vizuri katika maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, pengine niseme tu kwamba kuna mambo ambayo kwa kweli si Polisi wote ambao siyo waadilifu. Kuna tukio moja limetokea Wilaya ya Kilindi, nina Mzee wangu mmoja ambaye yeye amenunua gari kupitia mnada na Mheshimiwa Waziri unalifahamu vizuri sana hili. Cha kushangaza ni kwamba baada ya kununua kwenye mnada yule Mzee amenyang'anywa gari. Mzee yule miaka karibia 40 ametafuta pesa kanunua gari lakini amenyang'anywa. Suala hili liko kwenye Wizara yako, nisingependa kutoa maelezo marefu, naomba wale ambao wanashughulikia suala hill walishughulikie kwa dhati kabisa wampe huyu Mzee haki yake kwa sababu kama mtu ni mhalifu lazima afikishwe kwenye vyombo nya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo machache, nakushukuru sana, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Hakuna cha mwongozo, kaa chini. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Kiula.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nishukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu. Awali kabisa niseme naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niwapongeze viongozi; Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya. Pongezi hizi msingi wake mkubwa ni kwamba watu wengi tunasema hakuna amani lakini ukilala ukiamka salama maana yake amani ipo, hiyo ndiyo tafsiri yake kubwa. Sasa twende kwenye *issues* useme wapi umekwazwa au wapi hapaendi sawa, lakini ukitoa *statement ya generalization* haileti afya kwa Taifa hili wala haileti afya kwa Polisi wetu ambao wanatulinda mchana na usiku. Tukitoka hapa tunakwenda kuchoma nyama hapo Chako ni Chako baadaye tunakwenda kulala halafu unasema Polisi hawakulindi. Sasa sisi tutoke wenyewe tuanze kujilinda kama ni hivyo. Kwa hiyo, kazi ya Polisi ni ya kutukuka na tunawapongeza na tunaomba waendelee kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni pongezi kwa Polisi wote lakini pongezi kwa Polisi wa Usalama Barabarani. Taarifa yetu imetuonesha ajali na vifo vinapungua. Tumekuwa tukiwalaumu sana Polisi wetu wa Usalama Barabarani kwa kutubana sisi madereva maana yake sisi wenyewe Wabunge hapa wote ni madereva, sasa lazima tufike mahali tufuate sheria za barabarani, tusiendeshe sisi kama wafalme. Sheria tumetunga inauma kotokote, huwezi kuwatungia sheria watu ambao wako nje ya Bunge, sheria ikitungwa na sisi inatugusa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nichangie hoja hii ya Waziri. Jambo la kwanza, amezungumza mzungumzaji aliyepita suala la kisera. Mimi niko Kamati ya PAC, katika hoja zetu nyingi ambazo tumekuwa tukizipitia tumekuwa tukimpa taabu sana Afisa Masuuli. Tulichogundua ni kwamba Afisa Masuuli ana kazi kubwa sana na ana *risk* kubwa sana kwa maamuzi yote na vitu vyote vinavyopita mezani kwake. Asimamie Fungu 14, Fungu 28, Fungu 29, Fungu 51, Fungu 93; inakuwa ni kazi kubwa sana. Tunashauri Wizara iangalie namna bora ya kupunguza *risk* hii kwa Afisa Masuuli mmoja anayesimamia mafungu matano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo nafikiri Wizara ya Fedha inahusika, wataliangalia waone ufanisi unapatikana vipi katika mazingira kama hayo. Hata changamoto za mikataba mbalimbali iliyoingiwa na ufuatiliaji wake, tumeona kwamba mwisho wa yote ufanisi unapungua kwa sababu Afisa Masuuli ana kazi kubwa, anatakiwa awe na jicho kama la mwewe, yaani awe anaona kila sehemu. Kwa hiyo, hilo ni jambo muhimu, liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala zima la *NIDA*. *NIDA* sasa hivi ndiyo habari ya mjini wanassema, kwa sababu Serikali imeamua kila Mtanzania apate kitambulisho. Kama kila Mtanzania inabidi apate kitambulisho basi Wizara inatakiwa isimamie jambo hili na tuhakikishie wote wamepata vitambulisho. Huko vijiji tumeona ofisi zimefunguliwa, Maafisa wa *NIDA* wamekwenda hawana vitendeakazi, wamepiga watu picha huko kwenye kata, watu wanauliza vitambulisho lakini vitambulisho havionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuangalie tatizo limeanza wapi, ni kwenye mkataba wa uzalishaji vitambulisho. Tunaomba Waziri atakapokuja hapa atuambie mwarobaini wa vitambulisho ni upi? Watanzania wote watakuwa wamepata lini vitambulisho, tupate *commitment* ya Wizara. Hilo ni jambo muhimu sana na sasa hivi tumeona *transactions* zote zinazofanyika ukifika kitu cha kwanza unaulizwa Kitambulisho cha Taifa, kwa hiyo, hii ni agenda kubwa na ni agenda ambayo inatakiwa iwe katika *boardroom*, viongozi wetu wa juu wasimamie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni vituo vya Polisi. Nimeona kwenye hotuba ya Waziri amehamasisha wananchi kujitolea kujenga vituo. Pamoja na wananchi kujenga vituo na sisi tunawahamasisha huko kwenye mikutano yetu na kwenye kazi tunazofanya, isipokuwa bado upo ule Mkataba wa STAKA, hatujapata majibu yake ndani na nje ya Bunge, naomba tupate majibu. Maana kuna vituo vimejengwa vimeachwa, kama Mkalamama kituo pale kinaanza kuoza sasa, kilikuwa cha ghorofa, kinaharibika, pesa nyngi zimeshawekwa. Manyoni kuna kituo, kilikuwa kijengwe kituo

kingine lkungi na maeneo mengine mbalimbali, Lushoto imetajwa kama mfano. Hilo ni jambo kubwa na vile vituo umefika wakati wake vimalizike. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali au Wizara utuambie ni lini vituo hivyo vitakamilika na ituambie kwa uhakika kabisa na usahihi. Kwa sababu hiyo inakuwa ni pesa iliyotupwa. Hata kama ilikuwa ni pesa ya kimkataba lakini ni pesa ambayo inatakiwa iwe *accounted for*, tujuue kwamba vituo hivyo vitamalizika lini, pamoja na kuhamasisha kwamba bajeti zaidi itengwe kwa ajili ya kujenga vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo ambalo wananchi nalo wanataka wajue, yaani kuna wingu zito. Limezungumzwa ndani na nje ya Bunge na kwenye vyombo vya habari nalo ni suala zima la mikataba ya Lugumi, mikataba wa *AFIS*, tupate kauli ya Wizara, inasemaje, hilo jambo limeishia wapi? Kwa sababu zipo fununu pia kwenye Jeshi la Magereza ipo mikataba mingi inayomhusu Lugumi ambayo na yenyewe ni mikataba tata. Tunaomba Wizara itueleze hapa ili wote kwenye ukurasa mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa suala la malipo yasiyo na nyaraka timilifu. Hata hoja nyingi za Mkaguzi Mkuu wa Serikali zinaibuliwa kwa sababu ya ukosefu wa nyaraka, unaanza kutafuta waraka mmojammoja. Limezungumzwa suala la sare hewa, sisi tunaamini katika mazingira ya kawaida Jeshi la Polisi siyo eneo la kujifichia, siyo kichaka pale. Kwa hiyo, tunaamini kwamba hizo sare zilinunuliwa na hili suala la nyaraka hewa, mafunzo hewa, sare hewa, Waziri utatuambia ufanuzi tuweze kujua kinachoendelea ni kitu gani. Jeshi kwa ujumla wake lina nidhamu ya hali ya juu, tunatarajia kwamba nidhamu ianzie jeshini. Kwa hiyo, nidhamu ikiwa nzuri huko hata Wizara zingine na maeneo mengine watainga mfano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala vitendea kazi tupongeze Wizara, wameleta magari na mimi Mkalama nimepata gari la polisi japo tunahitaji magari zaidi lakini tunashukuru kwa hicho tulichopata. Nimshukuru Naibu Waziri

Mheshimiwa *Engineer* Masauni alifika kule na aliongea na wananchi na walifurahia sana kwa hiyo, tunapongeza sana kwa kazi hiyo kubwa inayofanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira, tumeona humu ndani askari wataajiriwa, tunaamini kwamba mnawapeleka mikoani, Mko ma-RPC wanawapangia vituo kulingana na uhitaji. Tumeona Wizara ya Elimu wamechukuwa hatua nzuri sana kujua mahitaji ya ualimu kwa kila shule kwa hiyo wanapanga huku walimu wanakwenda moja kwa moja kwenye shule husika. Sasa nafikiri na hata jeshi la polisi liige mfano huo na magereza wawe wanapanga wafanyakazi kutoka huku huku. Kwa sababu wakienda tunawaachia ma-RPC wanapanga siyo kwamba hatuwahamini wakati mwingine tunaona kuna baadhi ya wilaya au kuna baadhi ya maeneo yanahitaji polisi wengi zaidi alafu wanakuwa hawapatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za askari kuna pesa ambazo zimetolewa za kujenga nyumba za askari, tunaomba hiso pesa nazo mgao wake usimamiwe kutoka Makao Makuu. Tunatambua kwamba mmekasimu madaraka hayo kwa ma-RPC mikoani, lakini mjaribu kuangalia kwa sababu zipo wilaya ikiwepo Mkalama, hakuna hata nyumba moja ya askari. Sasa hiso pesa na zenyewe zinufaishe maeneo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii naunga mkono hoja tena ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiula. Mheshimiwa Nsanzugwako na kama muda utakuruhusu Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ngoja kidogo Ally Saleh. (*Makof*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Labda nianze moja kwa moja kwa kuwapa hongera sana viongozi katika Wizara hii, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, na makanda wote wa Jeshi la Polisi hongereni sana. Lakini kwa namna ya pekee na chukua nafasi hii kumpongeza *RPC* wa Mkoa wa Kigoma ndugu Otieno na ma-*OCD*wake kwa kazi kubwa wanayoifanya kule Kigoma ukizingatia Kigoma ni Mkoa wa mpakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na wewe binafsi nikushukuru kwa kufanya ziara katika Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya ya Kasulu ulikuja tukakutembeza maeneo mbalimbali ukaenda mpaka Kitanga ukashuhudia mauaji yaliyotokea hongera kwa kazi, na karibu sana katika Mkoa wetu wa Kigoma.

Labda Mheshimiwa Waziri nikukumbushe jambo moja, Mkoa wa Kigoma unapakana na nchi nne ndiyo mkoa pekee katika nchi hii ambao unapakana na nchi nne, unapakana na Zambia upande wa maji, unapakana na Congo DRC, tunapakana na Burundi na Rwanda. Na nchi zote hizo Mheshimiwa Waziri unajuwa ukiacha tu nchi ya Zambia nchi zilizobaki *DRC*, Burundi na Rwanda hali yake ya usalama si shwari sana hali ni tete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge wa Mkoa wa Kigoma tumekaa na wewe zaidi ya mara moja tukikuomba utumie mamlaka yako kwa mujibu wa *instrument* uliyonayo, uyatamke maeneo yenye uhalifu mkubwa ili yaweeze kuwa na kikosi maalum cha polisi au mnahita kama Rarya ya Tarime ile Kanda Maalum ya Kipolisi. Na Mheshimiwa Waziri tunakusisitiza Kanda hii inaweza ikawa ni *enclave* ya Ngara, Biharamuro, Kakonko, Kibondo, Kasulu, na maeneo ya Buhigwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri unaposema hali ya usalama katika nchi yetu ni nzuri tena unaweka nzuri sana sisi wakazi wa maeneo yale tuna sema hali si shwari. Utekaji ni mwingu, ujambazi ni mwingu na

tunaomba kabisa kabisa Mheshimiwa Waziri jambo hili mlipe kipaumbele. Nina hakika eneo hili likiongezewa rasilimali tukawa na Kanda Maalumu la Jeshi la Polisi na polisi wengine wakaendelea kuwepo katika maeneo yao hali ya usalama inaweza ikawa ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza hivi na Waziri unajuwa utekaji unaendelea katika maeneo ya Kakonko, maeneo ya Biharamuro, maeneo ya Nyakanazi, maeneo ya Kasulu, maeneo ya Kibondo na ule mpaka wetu ni mkubwa sana. Mheshimiwa Waziri ule mpaka unajuwa ni zaidi ya kilomita elfu 2000 kwa hiyo, ni muhimu sana Kanda hiyo Maalum ukaanza kufikiria na ningependa uje utueleze humu ndani mnajipangaje kuweza kupunguza uwalifu katika maeneo yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ningependa nilisemehe ni upungufu wa askari katika Mkoa wa Kigoma, taarifa nilizonazo na wewe unazo kwamba Mkoa wa Kigoma unaupungufu wa askari kati ya 120 mpaka 150 na wewe Waziri unajuwa, wakimbizi wote wa nchi yetu wapo katika Mkoa wa Kigoma. Wakimbizi wapo Kasulu, wakimbizi wapo Kibondo, wakimbizi wapo Kakonko lakini kuna upungufu mkubwa sana wa askari pamoja na vitendea kazi. Sasa mtu ye yote mwenye akili angeweza kudhani kwa sababu Mkoa wa Kigoma upo mpakani unapakana na nchi nne hatupaswi kuwa na uhaba wa askari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haina maana unakuwa na askari wengi katikati ya nchi, unakuwa na askari wengi Dodoma, unakuwa na askari wengi Singida, unakuwa na askari wengi Tabora, unakuwa na askari wengi Shinyanga, wakati ujafunga mpaka, tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba ualifu na wahalifu na silaha sinatoka nje ya nchi, zinapitia Kigoma kuingia kati kati hasa kwa akili ya kawaida nilidhani na nina amini wewe Mheshimiwa Waziri na timu yako na RPC ananisikia, *RPC* Sirro ananisikia haiwezekani Mkoa amba kama *shield* yetu ndiyo ngome yetu tuhangaike..

**MBUNGE FULANI:** *IGPSirro umesema RPC.*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO:** *IGPSirro ndiyo, aah IGPSirro ni mtani wangu angeelewa tu hivyo hivyo. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *IGP Sirro* ananisikiliza haina maana nasema tena inakuwa na askari wengi katikati ya nchi, lakini kwenye mpaka ambao unaingiza silaha haramu unawakimbizi haramu, una watu chungu mzima kumeachwa wazi. Nadhani busara ya kawaida ya polisi ingetumika na wewe Mheshimiwa Waziri kwamba tufunge mpaka, ule mpaka ni mrefu sana silaha zinaingia kutoka Burundi, silaha zinaingia kutoka Rwanda, silaha zinaingia kutoka Kongo na ndiyo zinapita katikati ya nchi yetu.

Sasa Mheshimiwa Waziri uioni kama ni busara kawaida tu? Ukaanza kusini mpaka kule of couse ulivyosema mkisheana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, ingawaje wanajeshi wengi walioko katika *detach* zile wao wanasema wanakazi yao maalum. Lakini mshirikiane kwa karibu ili mpaka ule uweze kuwa salama na wananchi wa maeneo yale tuweze kuhishi kwa amani na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ningependa nilisemehe na msema kweli mpenzi wa Mungu nimeshangaa kwenye kitabu chako hata hukugusia ujenzi wa *barracks* nilokwenda kukutembeza, Mheshimiwa Waziri tumekunywa chai pale Kasulu tukaenda kutembea wewe na mimi tukaenda kwenye *barracks* za Kasulu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *barracks* ya Kasulu ile inauwezo wa kuifadhi familia za askari zaidi ya 50 tumekwenda pale sasa nimeshangaa kwenye kitabu chako hiki hata kugusia katika miradi inayoendelea na cha ajabu Mheshimiwa Waziri zile nyumba zimejengwa pia kwa msaada wa Jeshi la Polisi, Magereza wameshiriki pale na jambo hili hata Kamanda IGP Sirro nimewai kumueleza una-*priority* gani kama uwezi kuhifadhi askari katika maeneo ya mipakani, kwenye kitabu chako *not even a mention* hata kutamka tu umeona *barracks* hili mambo ya ajabu haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unasema unajenga nyumba tano Kigoma, Kigoma mjini unajenga nyumba tano

tunazungumzia maeneo ambayo yamekithiri kwa uhalifu, hawa askari wanakaa mitaani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu chako kabisa uelezi hata kutaja kwamba umetembelea *barracks* ile na wewe mwenyewe umeona zile blocks zile ni kubwa ni nydingi. Sasa nimeshangaa sana Mheshimiwa Waziri ningependa kwa kweli nipate maelezo kwanini? *Unless ukutambua ile nguvu iliyofanyika pale kuna nguvu ya wafanyabiashara, kuna nguvu ya wananchi, kuna nguvu ya Magereza, kuna nguvu ya polisi nimeshangaa sana Mheshimiwa Waziri kwenye mpango wa maendeleo 2019/2020 hata kutaja kwamba kuna barracks inajengwa umesahau kutaja.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa nilizungumze ni uhamiaji tunashukuru sana Kamanda wa Uhamiaji, Kamanda wa uhamiaji tunamshukuru na wenzake na timu yake zile *harassmentza* kutambua watu kwa sura zimepungua sana angalau zimeanza kutumia weledi. Na sisi Mheshimiwa Waziri kupitia kwako niwashukuru sana wenzetu wa uhamiaji ule umbumbu wa kutambua watu kwa sura zao eti kutambua watu kwa rafudhi zao kwa kweli vituko vile vimepungua kwa kiwango kikubwa, tunaomba waendeleze weledi, wahamiaji haramu watambuliwe kwa namna ambayo ni ya kisayansi zaidi kuliko kuangalia sura zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake sura za watu wa Congo, sura za watu wa Zambia, sura za watu wa Burundi na Rwanda zinafanana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hiyo lakini naomba hayo yote yazingatiwe Mwenyekiti nashukuru ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Tunashukuru sana. Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nitazungumzia mambo matatu kwanza kuhusiana na mikutano ya kisia, pili kuhusiana na Mashekhe ambao wapo jela sasa, ramadhani sita wapo jela, kisha nitazungumzia juu ya ajira ya askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote humu tumeapa kuheshimu katiba pamoja na viongozi ambao hawapo humu ndani, na katiba yetu maeneo mengi inaeleza juu ya haki, usawa, uwadilifu, ya namna ya *ku-treat* haki za watu na mambo mengine. Lakini pia inatupa fursa ya namna ya kujikusanya kujieleza, kuijunga, uhuru huo umetolewa, lakini pia nchi yetu imejiunga na mikataba mbalimbali imesaini mikataba mbalimbali ya kimataifa juu ya haki ya kujikusanya na kujieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mwaka 92 kwa hiari yetu tulikubali kwamba tunaingia katika mfumo wa vyama vingi, na CCM kwa nafasi yake iliyokuwa ilikuwa inaweza kukataa kutokuingia katika vyama vingi. Kwa sababu kwanza wale walisema wanataka vyama vingi walikuwa ni kidogo 20 percent lakini ikaonekana busara kwamba 20 percent hawa wanaweza wakawa wamenyimwa haki yao kwahivyo tuwape haki na tukakubaliana tuingie kwenye mfumo wa vyama vingi. Lakini *seven year on haionekani infact it is even going to the extreme*. Kwamba CCM sasa wanakataa kilekile ambacho wao walituingiza ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa unashangaa nchi hii kwamba inaamini katika demokrasia, inaamini katika siasa za *pluralism* kwa sababu haielekei kwamba inaamini hivyo kwa matendo, ndani ya katiba ndani ya sheria tunasema kama tunafuata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tutazungumza habari ya mikutano ni *simple logic it doesn't need Ph.D au rocket science*, kwamba ili mtu afanye siasa lazima aweze kuchanganyika na watu, ili mtu afanye siasa lazima aweze kujikusanya na watu, aweze kuzungumza na watu, aweze kupiga *propaganda* na sera zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumesema mara nyingi kama mnahisi hamuwezi bado mna-*majorit just call it off* semenii tu mnazo kura za kutosha humu za kusema kuanzia leo hakuna vyama vingi basi tujuwe hakuna vyama vingi tusisumbuane tusitaabishane tusipatishane tabu, kwamba mnataka vyama vingi inaelekeaje mnataka vyama vingi mtu mmoja anasema siasa msimu mpaka msimu mnataka vyama vingi lakini bado hamruhusu watu wafanye mikutano, mnataka vyama vingi lakini bado mnakuja na *excuse lame excuses intelligentsia* sijui kitu gani kitu gani jamani kama *intelligentsia* umeipata si ndiyo wewe wakuifanyia kazi? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *you're a failure* ukiwa na *intelligency you're a failure* sasa kama Waziri unakubali uitwe *failure is horrible* kama unakubali uitwe *failure* kila siku unakubali polisi wako wakuwa *intelligentsia you don't question* kama *intelligentsia* kwanini usiwapo wape *option*. Juzi ulisema hapa katika kujibu swalii moja ulisema kwamba kama mkutano leo haufanyiki unakuwa kesho kutwa ufanye nafikiri ilikuwa katika *briefing* hebu nikuulize, siku gani upinzani walipewa siku mbadala ya kufanya mkutano? Hata siku moja! (Makof)

Mheshimiwa mwenyekiti, sitaki kuzungumza habari ya CCM wala nazungumzia kuwakilisha wapinzani kwahiyo kama mnahisi hamuwezi *call it off*. Leo leteni Muswada na sisi tutaunga mkono tutafanya kazi nyingine siyo lazima kuwa wapinzani si lazima kuwemo humu ndani hatukuzaliwa kuwa Wabunge wa upinzani tumezaliwa tuishi tu kuwemo humu ni *coincidence* tu, kwa hiyo, siyo lazima tubakie humu kama hamtaki wacheni semenii hakuna vyama vingi katika nchi hii mtakutana nao mabwana wa dunia (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu mashekhe nimesema hapa kwamba hii ni ramadhani ya sita *its six ramadhan they are spending in lockup* hata kesi haijaanza kushughulikiwa *six years shame on this country, shame on our system.* (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnatuambia tuiseme nje, tunaitukana nchi yetu humu ndani *shame* kwa nchi yetu, *shame* kwa Serikali zetu kwamba miaka sita mtu anachunguzwa hata kesi aijaanza jamani fikirini hata kesi haijaanza fikirini jamani wale binadamu kama sisi *next it could be you, it could be mwanao, it could be mtu mwingine*, jamani watu wanasema sheria haina huruma miaka sita inatosha jamani, inatosha, inatosha, inatosha miaka sita. Waamulieni kama wana makosa waukumuni hakuna mtu anayesema anaunga mkono ugaidi, nataka kama ugaidi miaka 50 mia 200 wafungwe lakini wawe wameukumiwa kesi *i-move*, kesi *haija-move* mnataka nini tuambieni halafu mnasema mna tunza haki nyie watetezi wa wanyonge ninyi *its rubbish, hamfanyi chochote* kwa haki ya nchi hii. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh unayemwambia *rubbish* ni nani? Hebu mimi nakuheshimu sana hebu tumia ile lugha ya Kibunge tu, futa hiyo kitu.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya mwisho namalizia juu ya habari ya kichakaa, kichakaa ni kama utani kule pemba kuna msemo mmoja umesema uchumi wa mudu, uchumi wa panga, panga hutumika kwa kukatakata vitu vingi kulima kufanya nini lakini mwisho hutupwa lisionekane mpaka msimu ujao. Ni sawa sawa na hawa polisi wetu manawatumia katika uchaguzi, mnawatumia katika *operation*, mnawatumia kuzuia mikutano yetu lakini vyeo vyao hamuwapi haki zao hamwapi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi wa nchi hii wanatumika vibaya wanatumika visivyo lakini haki yao basi *minimum* wapeni haki zao, wapandisheni vyeo kwa wakati sio kwa kuwa hawana pa kusema, sio kwa kuwa wanapiga *salute* hawa mabwana wanaitikia mkaona hawasemi wanatuambia mnawafanya vibaya hamuwapi haki zao hata tukisema mara nydingi polisi wa nchi hii wana lala pabaya hawana mahali pa kulala hawana matunzo mengine

yanayostahiki askari jamani vibayeni wanasema wapemba vibayeni, vibayeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WABUNGE FULANI:** Vibayeni, vibayeni

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, haya niseme moja tu, Waheshimiwa Wabunge mko nadhifu sana hasa ambao wamevaa *Western suit*, kwa sababu haya ni mazoea na huwa tunajifunza kila wakati kama umevaa *suit* kama mlivyo wengi humu, acha Kaunda *suit*, siongelei Kaunda *suit*, *etiquette* zinatutaka hivi, ukisimama unataka kuongea kile kifungo unakifunga ndiyo utaratibu ukimaliza unataka kuketi unakifunga tena upate nafasi ukae vizuri. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sichoki kuwafundisha haya, na la mwisho kama *jacket* lako lina vifungo vitatu una *option* cha katikati wengi unaweza ukakifunga ukakiacha cha chini na cha juu lakini huwezi ukafunga vyote vitatu. Unaweza ukafunga cha kwanza na cha pili ukaacha cha tatu ndiyo utaratibu wa mavazi. (*Makofi*)

Nayasema haya kwa sababu nyinyi ni viongozi mnasafiri *imege* ya Tanzania nyinyi ndiyo mnaipeleka nje mabalozi wetu nataka uonekane mmekaa vizuri.

Sasa baada ya kusema hayo niwataje Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao mchana nikushukuru sana Mheshimiwa Ally Saleh na umepewa uhuru Ibara ya 100 ya katiba ndiyo huo lakini tumia vizuri, basi usilete mambo ya kukashifu watu lugha chafu tu lakini jenga hoja watu watakusikia ndiyo maana mnalindwa *nothing is gonna happen*, ukishatoka hapa hakuna atakayekugusa. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** ....Hoyeee. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Fakharia Shomar ajiandae na wengine

watafuata. Sina matangazo kwa maana hiyo nasitisha shughuli za Bunge.

*(Saa 7:00 mchana Bunge ilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge ilirudia)*

**MWENYEKITI:** Niliwatataj Waheshimiwa Wabunge watatu tutakaoanza nao. Nianze na Mheshimiwa Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na baadaye Mheshimiwa Fakharia Shomari.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nami kuniruhusu nichangie hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani vifungu 28, 29, 51 na 93.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais Joseph Pombe Magufuli kwa kuliwezesha Jeshi la Polisi kufanya kazi kubwa ambayo linafanya. Pia pongezi kwa Wizara nzima ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Polisi hasa kwa kuendeleza amani na utulivu hapa nchini, kwa kulinda raia na mali zao lla nina jambo la kusema leo ambalo limenisumbua sana.. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, upande wa pili kule wanaye Mnadhimu Mkuu au Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Mnadhimu huyu, Mheshimiwa Tundu Lissu amekuwa anasema maneno mabaya kuhusu nchi hii, kuhusu Serikali, kuhusu Mheshimiwa Rais na wenzetu hawa wamekaa kimya. Huyu ndiye Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Kwa hiyo, anayoyasema kule ndiyo haya haya ambayo hawa wanayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka hawa waseme leo: Je, ni kweli mnamuunga mkono Tundu Lissu au mko tofauti? Mseme ili wananchi wajue mko upande wa watu wanaochukia Tanzania, wanaomchukia Mheshimiwa Rais, wanaochukia Serikali, wanaochukia maendeleo yote; wanachukia miradi ya nchi hii inayoletwa na Serikali ya

Awamu ya Tano. Mseme wananchi wawajue ili wasiwape kura kwenye uchaguzi unaokuja. Hamfai kuongoza nchi. haiwezekani muishi kama popo upande huu mko ndani ya Bunge mnasema mnaipenda Serikali ya Jamhuri ya Muungano, mnachangia mtu anayekosoa Serikali. Sasa hivi mnawasema vibaya hawa hawa. Haiwezekani mkia uwe tofauti na kichwa kiseme tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii wakati ilipofika Wizara ya Sheria na Katiba, wamesoma hotuba ya Mheshimiwa Tundu Lissu. Kwa hiyo, wanamuunga mkono yote anayoyasema, lakini nje hamwambii wananchi kwamba ninyi hamuipendi nchi hii, semeni. Msiendelee kukaa kimya, upande wa pili mnasema watu, nchi za nje ziinyime misaada Serikali yetu, lakini vilevile hamtaki misaada yoyote ije kwa watu ambao wanawasaidia, Serikali inayowasaidia dada zetu, mama zetu na kaka zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana upande wa Upinzani leo useme kwamba anayoyasema Mheshimiwa Tundu Lissu ni ya kwao au ni ya kwake? Ili wananchi wajue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa naomba nichangie. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani anipelekee salamu zangu kwa Mheshimiwa Rais za kuwapa pole familia za Askari waliofariki wakitetea amani na usalama wa nchi yetu. Askari hawa ambao wanabezwa na upinzani wamefanya kazi kubwa sana. Hakuna mtu kati yetu Bungeni humu aliyejitlea kufa ili jirani yake aishi. Askari wetu wamekufa. Wamekufa Rufiji, hata juzi wamekufa, wanapambana na majambazi ili kuleta usalama wa raia na mali zao. Iko haja ya kuwasifia sana lakini kutoa pole kwa familia zinazobaki, waliokuwa wanawategemea Askari wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ya *NU* imefanya kazi ya kukagua miradi yote muhimu ya Jeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ikiwemo miradi muhimu, lakini kote kumekuwa na kilio, hakuna fedha iliyopelekwa kwenye

maendeleo hata kidogo. Fedha iliyopelekwa ni kidogo, haiwezi kumalizia miradi ambayo ipo. Naiomba Serikali, Wizara ya Fedha iwapatie fedha miradi hii katika Jeshi la Polisi, Idara ya Zimamoto, Idara ya Magereza na Uhamiaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la Sheria ya Sekta Binafsi ya Ulinzi. Sheria hii niliileta nikaipeleka kwa Mheshimiwa Spika na baadaye Serikali ikaiomba kwamba yenye we itaileta kwa sababu ilikuwa inahusishwa kuanzishwa chanzo cha kupata kodi na Mamlaka ya Sekta ya Ulinzi Binafsi, (*Private Security and Authority*). Sasa zilikuwa siku, ikawa wiki, ikawa miezi, mwisho imekuwa ni miaka mitatu tangu sheria imechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri atapokuja alieleze Bunge hili, ni lini sheria hii italetwa? Sheria hii ni muhimu sana kwani italeta *win win situation* kwa makampuni yanayoendesha biashara hii ya ulinzi binafsi lakini pia Serikali itapata kodi kwa kudhibiti mapato yanayotengenezwa na makampuni ya ulinzi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo iwapo sitasemea suala linalompata mwenzetu Mheshimiwa Kadutu katika makazi ya wakimbizi kule Ulyankulu. Sisi tumekuwa na makambi ya wakimbizi kule Ulyankulu, Mishamo, Katumba na kwingineko. Wakimbizi hawa wanavyoishi na wanavyotenda ni kama vile wameanzisha nchi nyingine ndani ya nchi ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakimbizi hawa wamefikia kiwango cha kuchagua nani awe kiongozi wao wa kisiasa kwa nafasi zote; Diwani, Katibu nani, hata Mbunge wanayemtaka wao. Vilevile bahati mbaya Mwenyekiti iko haja kubwa ya kuangalia maslahi wanayopata hawa wakimbizi ambayo sasa wako kama raia wa Tanzania; na hawa wanapata elimu bure, wanapata maji bure, wanapata chochote ambacho Watanzania wanapata. Imekuwa mbaya zaidi, inahofiwa kwamba hawa wanaongezeka kwa wingi sana lakini pia wanasona sana wanapata hata mikopo ya elimu ya juu na vilevile kuingia katika nafasi za kazi muhimu

sana kwa ajili ya Tanzania. Hii ni hatari kwa usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo ya kuchangia. Nakushukuru sana kwa muda ulionipa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maige. Tunaendelea na Mheshimiwa Ritta Kabati halafu Mheshimiwa Fakharia Shomari na Mheshimiwa Kakoso wajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Namtanguliza Mwenyezi Mungu katika mchango wangu, lakini nami niungane na mchangiaji aliyepita kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwachagua hawa Mawaziri na viongozi wote waliopo katika Jeshi hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Kangi Lugola; Naibu Waziri, Mheshimiwa Masauni; Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze makamanda wote kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya, *IGPSirro*, *SGPKasike*, *Zimamoto*, *SGPAndengenye* na *Uhamiaji SGI AP Dkt*. Makakala ambaye kwa kweli ni mwanamke aliyetuwalikisha wanawake wote na amefanya kazi nzuri sana. Katika ripoti ya Mheshimiwa Waziri tumeona amepewa tuzo katika *passport*. Kwa hiyo, tunaona kwamba sisi wanawake tumewakilishwa vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kazi nzuri ya mama huyu, nafikiri hata mtandao wa Polisi, sasa uangalie wanawake na wenyeve wale wanaoweza, basi wapatiwe vyeo vya juu ili waendelee kutuwakilisha vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu wanafanya kazi nzuri sana lakini tukikutana na bajeti finyu wamekuwa wakifanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iwaangalie, kuna changamoto ambazo wanakumbana nazo. Wanadai posho zao muda mrefu, uhaba wa watumishi, pensheni zao zilipwe kwa wakati, *promotion* zao wapatiwe kwa wakati ili kuwatendea haki na wawe na ari ya kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais pia kwa kuona changamoto zilizopo katika nyumba za Maaskari wetu, naona ameanza kuzifanyia kazi pale Ukonga. Nami namwomba katika Mkoa wetu wa Iringa Askari wetu wanakaa katika nyumba chakavu sana. Ukiangalia pale Iringa Mjini, Mufindi, kule Kilolo ndiyo hakuna kabisa nyumba za Askari Polisi na wengine wanakaa nje ya makambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iangalie. Pamoja na uchakavu walionao, kuna akina mama kuna watoto ambao wamekuwa wakiishi kwenye mazingira magumu sana. Kwa hiyo, tunapozungumzia makazi ya Polisi, tunaangalia hata akina mama na watoto walioko katika nyumba zile. Kwa hiyo, naomba hili lizingatiwe kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yetu ya Kilolo, toka ianzishwe Makao Makuu ya Wilaya, *OCD* hajawahi kujengewa Ofisi katika Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hiyo, kumekuwa na changamoto kubwa sana. Tunawashukuru sana *TAZAMA Pipeline* ambao wamempatia ofisi, lakini ni mbali sana na ilipo Mahakama. Kwa hiyo, utakuta wakati mwininge wanapata shida sana kuwapeleka mahabusu kwenda kwenye Mahakama kwa sababu ni karibu kilomita 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waangalie, kuna gharama kubwa kila siku zinatumika. Wangeangaliwa changamoto ili yopo katika Wilaya ya Kilolo ili Mahakama ijengwe yalipo Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nikizungumzia Jeshi la Zimamoto wana changamoto nyingi sana na wanafanya kazi vizuri sana katika mkoa wetu lakini pia posho zao wanakuwa hawalipwi kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uhaba wa magari ya Zimamoto. Utaona katika Wilaya ya Mufindi kuna msitu ambapo mara nyingi moto umekuwa ukitokea lakini hakuna gari la Zimamoto. Vilevile Wilaya ya Kilolo hakuna gari la Zimamoto na mara nyingine kumekuwa kukitokea ajali nyingi katika mlima Kitonga na hakuna hata gari la uokozi (*crane*) kwa ajili ya kusaidia kunapotokea ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna upungufu mkubwa wa Askari katika Wilaya zote. Jeshi la Magereza vilevile kuna madeni ya posho, kuna madeni ya Wazabuni ambao wamekuwa wakisaidia kuwalisha wale wafungwa, gharama za kuwasafirisha mahabusu na wafungwa wanaostahili kwenda kusikiliza kesi zao pia ni tatizo. Kwa hiyo, naomba Serikali ingeangalia pia haya Majeshi ili wapatiwe fungu la kutosha katika Mkoa wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu sasa. Naomba nitoe ushauri kwa Serikali kuhusiana na Jeshi la Zimamoto. Zile pesa za makusanyo (*fire inspection fee*) kwenye nyumba, biashara, viwanda, ma-guest, migodi, pengine ingekuwa hata asilimia kumi zinaenda kununua hivi vifaa vya Zimamoto ingeweza kusaidia upungufu ambaou po katika hili Jeshi la Zimamoto kuliko ambavyo sasa hivi pesa zote zinachukuliwa na Serikali wakati wao wenyewe wanakuwa wana matatizo kabisa ya upungufu wa vifaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Jeshi la Magereza, Magereza iwe kama Chuo cha Mafunzo, waongezewe vifaa vya mafunzo ili wale wafungwa waliopo kule wawe wanapatiwa mafunzo. Vilevile wapewe vifaa vya kilimo kama matrektta, yatasaidia; na waweze kufundishwa hata uvuvi na wapatiwe mkopo usiokuwa na riba ili waweze kujiendesha wenyewe. Kwa hiyo, itasaidia.

Mheshimiwa Mweyekiti, nimeona hata Mheshimiwa Rais anasema kwamba haya Magereza yanegkuwa yanajijendesha yenyewe katika kulisha wafungwa na kusaidia changamoto zilizopo. Kwa hiyo, kama tukiziwezesha kupata mikopo, inaweza ikasaidia sana zikawa zinajijendesha yenyewe; na wapewe kazi za ujenzi. Kwa hiyo, utaona kwamba tutakuwa tumezisaidia, tutakuwa hatutumii tena ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutoa mfano, nimeshatembelea pale Magereza nikakuta wana kiwanda, lakini wana changamoto ya fedha. Namshukuru Mkurugenzi aliweza kuwakopesha shilingi milioni kumi na sasa hivi wanajijendesha tu vizuri katika gereza letu la Mkoa wa Iringa. Kwa hiyo, iwe mfano hata katika Magereza nyingine, bado tunaweza tukaziwezesha Magereza zikaweza zikajijendesha yenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine, Mkoa wetu una changamoto ambao kuna mwingiliano mkubwa sana kati ya Gereza la Mkoa na Hospitali ya Mkoa. Hili nimekuwa nikilizungumzia mara nyngi sana; na ningeomba labda sasa hivi hebu mlipe kipaumbele kwamba kwa sababu Gereza lina eneo kubwa nje ya mkoa, basi lihame ili kupisha hospitali iweze kujenga majengo na nyumba za Madaktari iweze kusaidia wagonjwa wetu na msongamano uliopo katika Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Jeshi la Magereza liwe linawapatia hati maalum wadau wanaosaidia Jeshi la Polisi. Kwa mfano, katika mkoa wetu kuna wadau ambao wameweza kusaidia sana ujenzi wa Vituo vya Polisi, ujenzi wa madawati, wamekuwa wakisaidia hata ukarabati wa majengo mbalimbali, kwa mfano, yuko huyu Mheshimiwa ASAS ambaye ni mmiliki wetu pale Mkoa wa Iringa, kuna Besania, kuna Mbarak kuna *Ruaha National Park*, Zakharia Hanspop ambaye pia kwa kweli ametupatia magari ya Zimamoto na *Ambulance*. Sasa uwepo utaratibu mzuri wa kuwapatia hati ambayo inatambulika kwamba wamesaidia Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi mwenyewe nilijenga Kituo cha Polisi pale Kihesa, pia ni vizuri nikatambulika mchango wangu kwa kupatiwa hati maalum kwa sababu nimelisaidia Jeshi la Polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie kuhusiana na vitambulisho vya Taifa. Hivi vitambulisho nafikiri Wabunge walio wengi pia wamezungumzia kwamba wengi walishakwenda kupiga picha, wamefanyiwa kila kitu, lakini sasa vitambulisho bado havijawafikia; na mara nyingi sasa hivi kila sehemu unatakiwa uwe na hicho kitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna ufinyu wa bajeti, basi Serikali iangalie uwezekano wa kutoa pesa ya kutosha ili kuhakikisha kwamba hivi vitambulisho wananchi wanapewa haki yao, kwa sababu kila unapotaka kwenda lazima uwe na kitambulisho. Hata ukisafiri nchi za nje lazima uwe na kitambulisho cha Taifa. Vilevile ukitaka labda kuomba *passport* lazima uwe na kitambulisho. Kwa hiyo, wananchi wamekuwa wakipata shida sana wanapotakiwa kupata hivi vitambulisho.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wetu ndiyo huo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Naomba niunge mkono hoja hii. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Fakharia Shomari, Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa John Kadutu wajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza sina budi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP*na Makamishna na hasa Kamishna wangu Mohamed Hassan wa Zanzibar, ambaye hivi karibuni kulitokea tokeo la vikosi kuingiliana katika

majukumu ya kazi na wakaweza kulidhibiti na kukaa salama na shwari. Lazima niwapongeze kwa kazi yao nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo watu wanapenda kusema ambao nitausema hapa leo, "domo, nyumba ya maneno." Sisi watu wa Pwani tunapenda sana kuzungumza. Kuna baadhi ya watu wanapenda kusema mambo mengi wakailaumu Serikali, wakasema ovyo, baadaye wakamtafuta mchawi, kumbe mchawi anakuwa yeche mwenyewe ambaye amejidhuru kwa kauli zake alizozisema na hilo linatendeka humu ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna msemo mwengine unasema hivi, "kwa shujaa huenda kilio, kwa mwoga huenda kicheko." Sasa baadhi yetu humu yakija yakiwakuta, wanapiga kelele kumbe amejifanya shujaa, yamemkuta, akina siye tuliokuwa waoga, tunamwangalia tunacheke. Sasa jamani tunapokuwa tunataka kusema mambo, lazima ufikirie kwanza nini athari yake ya mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kuhusu ujenzi wa nyumba za Askari. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa majeshi hapa Tanzania kwa huruma zake kwa Wizara hii ambapo aliweza kuwapatia shilingi bilioni 6.3 kwa ujenzi wa nyumba 400 za askari, pia mkachagua mikoa minane katika mikoa minane na Zanzibar wakapata Unguja na Kaskazini Pemba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo la fahari, la kujivunia, kwa uwezo iliyokuwanao Tanzania na kujali wapiganaji wake. Naomba Wizara pia mjiongeze. Mjipongeze vipi? Kwa sababu tunayo mifuko yetu ya jamii, mngekuwa mnazungumza nayo wakaweza kuwapatieni mkopo wa riba nafuu, mkaweza kujiongeza kwa kuwawezesha kujenga nyumba na katika mikoa mingine pia nao wakapata nyumba, Askari wetu wakajisitiri katika makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia Jeshi la Magereza, Mheshimiwa Waziri alizungumzia katika ukurasa 28 na 29, Jeshi la Magereza kubuni ili kuweza kuzalisha chakula na pia kuzalisha mazao ya biashara. Sasa nasema wangejlongeza na wakatafuta na mifugo kwa sababu tayari wanao vijana, wanaingia kwenye magereza yetu hodari, wana nguvu, wana uwezo, ni shabab kabisa, takribani wengi wanakuwa vijana sio wazee. Sasa hawa isiwe kazi yao ni kula na kulala, wawatumie waweze kufanya kazi ili waweze kuzalisha na kuipunguzia mzigo magereza au kuipunguzia mzigo Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika mwaka 2017/2018, zilitengwa bilioni 5.8 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mikano, Wilayani vituo na kadhalika. Hata hivyo, hizi pesa hazikutoka, ujenzi haujakamilika, mfano tukienda Lindi na Mtware, yale majengo hali yake ni mbaya, hayajamalizwa, ile ni hasara kwa pesa za wananchi na ni kodi zao. Kwa sababu ukienda ukiyaona hali ni mbaya na humjui umkamate nani uchawi? Tuwakamate Wizara ya Fedha, tuwakamate Wizara ya Mambo ya Ndani au tuwakamate Magereza, lakini hali ni mbaya na hili jambo lazima walingalie kwa upeo mrefu na liweze kufanyiwa kazi hiyo ya matengenezo ila majengo hayo watu wakae na kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitanzungumzia dawa za kulevyu kwa upande wa Zanzibar. Hivi karibu Mheshimiwa Naibu Waziri alikwenda Zanzibar akazungumza na Wanahabari. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kazi alioifanya ni nzuri na akagundua udhaifu uliokuwepo na akasema udhaifu ulikuwa kwa viongozi wetu watendaji na kuna maneno alizungumza akasema na itakuwa si mbaya baadaye hili jambo akalizungumza kwa mapana tukaelewa sote kwa sababu wanaopata tabu ni watoto wetu na wanatajirika ambao wanaiharibu nchi kwa kutaka manufaa yao ya kupata hela. Sasa hilo jambo azidi kulismamia ili huu udhaifu uondoke, kama amegundua kiongozi, basi huyo kiongozi ashughulikiwe au amegundua taasisi, hiyo taasisi

ishughulikiwe, lakini hili jambo liweze kuangaliwa kwa mapana na tuweze kupata nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kuhusu jengo letu au pale Mkoa wa Mjini Magharibi kuna sehemu panaitwa bomani, hilo boma ambalo ndio kambi kubwa ya mwanzo tulikuwa tunaitegemea pale Zanzibar maana ipo kwenye historia, maana hata wakizungumza hayo Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964 lazima boma lile lina historia. Hata limetungiwa nyimbo katika historia, lakini wanaliacha, boma lile majumba ndani hayapo sawa halishughulikiwi, njia zilipo ndani haziko sawa hazishughulikiwi. Utakuta mlango mkubwa kuna askari kasimama analinda. Sasa analinda nini wakati ule uzio wote mbovu, utaingia utatoka askari hana habari, utafanya unalotaka, askari hana habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba safari hii katika bajeti ya maendeleo watakayoomba, kama mwaka huu hawakuomba, wataomba mwakani wangefanya uzio na huo uzio usiwe wa waya, uwe wa matofali. Nasema hivyo kwa sababu pale pamezungukwa na majumba, zamani palikuwa nje ya mji, lakini sasa katikati ya mji, majumba yote yamezunguka, wanaloofanya mle ndani mtu wa nje anawaona, sasa hiyo siri hapo iko wapi? Sasa naomba wakapaangalia, ile historia iliyokuwepo mle wakaiweka sawa na wanajua ili watu waliokuwepo mtaani, au waliokuwa nje au mtu akidhamiria kufanya jambo kidogo apate shida ya kuingia mle ndani, asiingie kwa urahisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Sulemani Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa John Kadutu, Mheshimiwa Mattar Salum na Mheshimiwa Selemani Bungara ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa

kazi kubwa anayoifanya ya kulinda amani ya nchi hii. Pia nimpongeze Waziri mwenye dhamana na Msaidizi wake kwa kufanya kazi kubwa ya kusimamia Wizara ambayo ni kubwa na ina majukumu mapana sana. Tuwapongeze Wakuu wa Vyombo vya Usalama, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto. Wamefanya kazi kubwa, naamini kila mwananchi anashuhudia ile kazi ambayo imefanyika chini ya uzimamizi wa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wamefanya kazi kubwa sana, wamedhibiti mianya ya uingizaji wa madawa kuleyya na kufuta kabisa nchi yetu iliyokuwa inaonekana kwamba ni eneo la uchochoro wa kupitisha madawa ya kuleyya, hapa wamefanya kazi kubwa sana, tunawapongeza kwa dhati. Hata hivyo, wamedhibiti matukio ya ujambazi nchini ambayo yallikuwa yameshamiri kwa muda mrefu sana. Jeshi la Polisi wamefanya kazi ya kudhibiti hivyo vitendo na sasa hivi matukio yamepungua kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado katika eneo hilo la Jeshi la Polisi wamedhibiti vitendo vya kuhujumu uchumi wa nchi yetu. Tumeshuhudia Jeshi la Polisi likidhibiti utoroshwaji wa dhahabu ambao ulikuwa unafanywa na raia wasioitakia mema nchi yetu. Wamefanya kazi ambayo kimsingi Serikali imedhibiti vile vitendo ambavyo vilikuwa vinadhoofisha uchumi wetu. Pamoja na hayo Jeshi la Polisi pamoja na jitihada linalofanya na kazi inazolifanya ni kubwa, lakini bado kuna changamoto kubwa ambazo zinatakiwa zifanyiwe kazi, vitendea kazi hawana, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri tuangalie kwenye maeneo ya vitendea kazi. Jeshi la Polisi hawana magari ya kutosha, Jeshi la Polisi hawana nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwenye eneo la jimbo langu, tumeshukuru Serikali wanajenga nyumba za askari zipo sita, lakini bado pamoja na kwamba wanajenga hizo nyumba, lakini hakuna Kituo cha Polisi cha Wilaya. Niombe sana Mheshimiwa Waziri alingalie hili na naamini ninachokiongea anakifahamu, alishafika kwenye maeneo

husika, tunaomba kituo cha polisi. Zile nyumba anazojenga hazitakuwa na maana kama hakutakuwa na kituo cha polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vituo vya polisi ambavyo vipo mpakani, tuna Kituo cha Polisi Ikola na Kituo cha Polisi Karema, hivi vituo ni ambavyo havina hadhi inayofanana, tuombe sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe hivi vituo wanavipelekea vitendea kazi. Hata hivyo, baadhi ya vituo vya polisi hata uwezo wa kupeleka silaha hakuna, askari polisi analinda kituo akiwa na rungu, kwa sababu hana nyumba ya kuweza kuhifadhi silaha. Naomba Mheshimiwa Waziri apeleke silaha kwenye maeneo ambayo ni mpakani ili yaweze kulindwa, na ajenge mazingira ambayo yatakuwa salama kwa ajili ya vile vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie Jeshi la Magereza, Jeshi la Magereza linafanya kazi kubwa na jimboni kwangu Wilaya ya Tanganyika tuna Gereza la Kilimo la Kalila Nkulukulu. Gereza hili ni la muda mrefu, ni chakavu, tunaomba likafanyiwe ukarabati sambamba na kujenga nyumba za watumishi hasa askari wanaofanya kazi kwenye gereza hili. Yapo maeneo mengine ukifika unawaonea huruma, hata hao watumishi unaowapeleka kwenye eneo hilo, unajua tu kwamba wanafanya kazi kwa sababu ni wito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Gereza la Kilimo la Kalila Nkulukulu lina eneo kubwa sana la uzalishaji. Kwa bahati mbaya sana vitendea kazi hawana. Tulikuwa tunaomba Waziri wanunulie treka Gereza la Kilimo la Kalila Nkulukulu ili liweze kuzalisha chakula cha ziada. Tuna matumaini makubwa sana wakiwapelekea vifaa na vitendea kazi watafanya kazi kubwa ambayo itawasaidia kuzalisha na kupata ziada ya chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu nina wakimbizi, lipo eneo la Mishamo lina wakimbizi zaidi 60,000, kati ya hao walio wengi walishakuwa raia na wengine hawajakubaliana na kuwa raia wa nchi hii. Sasa kuna vitu ambavyo vinakuwa tofauti kwenye eneo moja, kwa maana linakuwa na utawala wa aina mbili; utawala wa makazi

unaosimamiwa na Afisa anayetambuliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani lakini utawala mwagine ni ule ambao ni wa kawaida. Kwa hiyo kuna tawala mbili kwenye eneo moja, mkuu wa makazi analinda wale wakimbizi wachache waliobaki. Kwamba ni mali ya kwake, wanatambuliwa na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe Serikali itoe maamuzi, wale wachache ambao hawakuchukua uraia wawahamishe wawapeleke kwenye maeneo mengine ambapo watacaa kwenye maeneo rasmi. Tukiwaacha hiyo tuna mashaka makubwa sana baadaye, tutaendelea kupokea wakimbizi kuititia hawa hawa ambao wapo kitu ambacho hatukitegemei tena. Si Mishamo tu, hata Katumba wapo. Kwa hiyo tunaomba hili walishungulikie na tunapata wakati mgumu kwenye Serikali za Mitaa katika uchaguzi ujao. Kuna hati hati ya kutokushiriki wananchi hao wa Mishamo, Katumba, Ulyankulu wanaweza wasishiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa sababu ya mwiningiliano wa utawala. Naomba hili walishughulikie na walifanyie kazi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa John Kadutu atafuatiwa na Mheshimiwa Bungara na Mheshimiwa Amina Makilagi ajiandae.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Chief nikushukuru* sana kwa kunipa nafasi hii, leo nina jambo moja mahususi. Bahati nzuri mapacha wa wakimbizi tupo watatu hapa, mwenzangu amekwishaanza kuligusia. La kwanza nimpongeza rafiki yangu Mheshimiwa Kangi Lugola kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii. Ni Wizara kubwa yenye changamoto nyingi, panataka utulize kichwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe darasa kidogo, mwaka 1972 kulitokea vita kwa wenzetu Burundi, enzi za utawala wa Mchombelo, kundi kubwa likakimbilia

Tanzania wakati ule Waziri wa Mambo ya Ndani alikuwa mzee Maswanya, wakaangalia maeneo ambayo yana nafasi kwa hiyo wakaamua wakimbizi kundi kubwa liletwe Ulyankulu, Mishamo na Katumba, nasi tukasema njoo tuwasaidie katika hali ya kibinadamu, sasa tumekaa nao miaka 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014, Serikali ya Awamu ya Nne ikatoa uraia ikiwa tarehe 14 Oktoba, nami nikiwa Mwenyekiti wa Halmashauri, lakini kwa ahadi, wale waliokuwa wakimbizi wakaahidi kuwa watifuli kwa Serikali mbele ya Mheshimiwa Kikwete, kwa hiyo walipata uraia. Baada ya hapo kumekuwa na mazungumzo je, zifungwe kambi hizi zote tatu au ziendelee kuwepo? Bahati nzuri Kamati ya Ulinzi na Mambo ya Nje imejadili sana jambo hili. Mabunge yaliyopita ilifika hatua, kuna Wabunge humu walikuwa wanasmama humu kukataa watu hawa wasipelekwe katika maeneo yao, kwa sababu mkishawapa uraia ile sio kambi tena ya wakimbizi, ni sehemu halali ya kuishi au kambi ifungwe na watu wahame. Analosema Mheshimiwa Kakoso, wapo watu walikataa Utanzania, walikataa kurudi Burundi, wanataka nchi ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya kwa taarifa yenu wakimbizi wa uraia wa Ulyankulu wanazaliana sana kuliko eneo lolote Tanzania. Kwa maana hiyo tunapongea hapa ile idadi ya wakimbizi waliokuwa wamebaki hawana uraia imekwishaongezeka, lakini Serikali yetu inapata kigugumizi kila wakati, ukiwagusa ndugu zangu wa TAMISEMI ndio kabisa hawataki kuleta majibu ya kueleweka, bado unamfuata Kadutu kagombee, utagombeaje kama watu hawahudumii watu wako. Watu wale wananipenda sana, lakini hawajatekelezewa, huduma za Serikali hazifiki kule. Sasa kwa nini Serikali isiwe na kigugumzi juu ya jambo hili, kwani wakisema kambi imefungwa, bahati mbaya kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri eneo lile la Idara ya Wakimbizi limeguswa kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu 70% ndio wapigakura wa Ulyankulu, ndio wapigakura waliomchagua Kadutu na Magufuli, lakini wakakataliwa kuchagua

Madiwani, lakini ajabu kwa Kakoso kule na kwa Mbogo wamechagua Madiwani. Hebu waniambie hasira waliyonayo itakuwaje? Hivi viongozi hawallioni hill? Serikali hawaoni? Tunaenda kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa, mle ndani kuna Serikali mbili; kuna mkuu wa makazi ana mamlaka yake, halafu TAMISEMI inaingia kwa kuviziavizia, Serikali yetu halafu tunaingia kwa kuviziavizia, ya wapi hiyo? Kwa nini tusiwe na mamlaka kabisa tunaviziavizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa lakini mle ndani kuna Serikali mbili. Kuna Mkuu wa Makazi ambaye ana mamlaka yake halafu TAMISEMI inaingia kwa kuviziavizia. Serikali yetu tunaingia kwa kuviziavizia, kwa nini tusiwe na mamlaka kabisa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme Serikali ifike mahali ileze, kama tunadhani Mheshimiwa Kikwete alikosea, tu-review uamuzi kwa sababu wapo watu walikuwa tayari kurudi Burundi lakini walipopata fursa ya kuchagua kurudi Burundi au Tanzania wakasema sisi ni Watanzania. Hata hivyo, kuna jambo ninyi hamlijui, hawa wenzetu tayari wamo kwenye Wizara zenu, iwe Wizara ya Fedha, Mambo ya Ndani, TAMISEMI na ninyi mnakaa nao hamjui kumbe huyu Mrundi, huyu hivi, huyu hivi, wamo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mnasema mna Idara nzuri ya Usalama wa Taifa, Polisi lakini mnakaa nao. Pakitokea jambo Ulyankulu tayari, ndiyo watu wanasema huku bado hapajakaa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesema nitachangia suala hilo hilo tu, niwasih sana Serikali, Kamati ya Ulinzi na Mambo ya Nje mbona imesema na imeshauri muda mrefu, kwa nini tusiwe na uamuzi? Tunafunga kambi ili wale ambao wamejidai kutafuta nchi ya tatu waondoke tubaki na wale walio tayari basi! Baada ya hapo tutakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwani ukiwaambia chagueni Diwani kuna tatizo gani? Mbona Kadutu wamemchagua? Mbona Mheshimiwa Rais Magufuli

wamemchagua? Kuna shida gani wao wasichaguane? Zamani watu walikuwa wanasema, ooh, misitu, sasa misitu kwenye kura, ni jambo la ajabu hili. Jamani tutafute sababu nyininge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chifu Kadutu, umelieleza vizuri, ni changamoto ambayo Serikali wameisikia, tutapata jawabu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mattar Salum.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake yote pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Alhaj Masauni kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ambayo nataka niyazungumze, nataka Mheshimiwa Masauni anisikilize vizuri.

**MWENYEKITI:** Unasemaje Mheshimiwa?

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri sana.

**MWENYEKITI:** Eeeh, ndiyo Waziri mwenye hoja.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar kuna Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ambapo leo ndani ya Bunge hili ni mara ya pili kuvizungumzia kwamba havitumiki katika kupata *passport* na leo vilevile havitumiki kupata hata laini ya simu. Sioni sababu kwa nini Vitambulisho hivi vya Mzanzibari Mkaazi haviwezi kutumika kwa sababu ya kupata *passport* ya Mtanzania wakati vitambulisho hivi ni halali ambavyo Serikali

ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa pesa za walipa kodi kuhakikisha vitambulisho hivi wanavitumia Watanzania. Tunaomba Waziri wakati wa kuhitimisha atupe majibu mazuri kuhusu Vitambulisho hivi nya Mzanzibari Mkaazi ili Wazanzibari wapate fursa ya kuvitumia kusajili laini pamoja na kupata *passport*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kushangaza leo tuna *NIDA* hapa ni kwa nini Vitambulisho hivi nya Mzanzibari Mkaazi haviunganishwi kwenye *system* kwa wakati ili vikapata hadhi yake? Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, Serikali yetu imefanya kazi kubwa na tuipongeze sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhakikisha Wazanzibar wote wanapata vitambulisho hivi. Leo tunashangaa kitambulisho hiki kina kasoro gani mpaka hakiwezi kutumika katika matumizi hata ya kusajili */line*? Mheshimiwa Waziri naomba tuhakikishe kitambulisho hiki kinaweza kufanya kazi kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni miradi ya Wizara hii, bado ni changamoto kubwa. Wizara hii ya Mambo ya Ndani wanapoanzisha miradi hasa ya Jeshi la Polisi mfano majengo hayamalizwi kwa wakati. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha alichukue suala hili ili Wizara hii aipatie fedha za kutosha ili ikamilishe miradi yake kwa wakati. Tukifanya nusu na fedha zikipelekwa nusu inasababisha miradi hii kutokamilika na hizi fedha zinaweza kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha atoe fedha kwa wakati kuhakikisha miradi hii inamalizika kwa wakati. Kama haikuwezekana kutoa fedha kwa wakati, nimwombe sana Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Kangi Lugola badala ya kutekeleza miradi yote basi achague miradi muhimu ili iishe kwa wakati tusibakishe majengo tu yasiyoisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuna majengo ya kufanya kazi hayakaliki, hayawesi kufanya kazi. Siku moja nilikuwa sehemu moja katika Mkoa wa Kusini Unguja,

nimekwenda katika Ofisi ya *RPC* haifai kufanya kazi. Jengo lile ni la zamani na *plan* ya kujenga jengo lingine haijawa tayari. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kulichukua suala hili, alitembelee jengo hili na kama kuna uwezekano wa kujenga jengo lingine wafanye haraka kujenga lingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, wapo askari wanastaafu wakiwa na vyeo vya *Sergeant* lakini mafao yao wanalipwa na vyeo vya *Corporal* hawapati haki zao husika. Sasa Mheshimiwa Waziri ikiwa askari hawa wamefanya kazi na mmewapandisha vyeo wamefika wakati wa kustaafu kwa nini hawapati mafao yao ya cheo husika cha kustaafia?

Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ulichukue hili na ulifanyie kazi na askari hawa waliostaafu ambao hawajapata haki zao kwa ukamilifu utoe haki kwa ukamilifu ili askari wetu waweze kulitumikia Taifa letu kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Selemani Bungara atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi na Mheshimiwa Ruge ajiandae.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha leo kuwa na afya na kuongea katika Bunge Iako Tukufu. Pili, nawashukuru wapiga kura na tatu nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na mikutano ya hadhara. Sisi sote pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeapa kuilinda, kuitetea na kuienzi Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Cha ajabu Serikali hii ya Awamu ya Tano wanazuia mikutano ya hadhara na maandamano kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi hata pale Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Maguful aliporuhusu kwa kusema kwamba sisi Wabunge tunaruhusiwa kufanya mukutano kwenye majimbo yetu lakini Jeshi la Polisi sisi Wabunge nao wanatuzuia. Mimi mmojawapo nimezuiliwa mikutano na polisi inayofika mitano. Nikiandika barua ya taarifa wao wazuia, mwisho juzi nimeandika barua nikazuiwa kwa kusema kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Mpina amechoma nyavu za wavuvi pale ukifanya mukutano basi hali ya hewa itakuwa siyo nzuri.

Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali sikuvi, iruhusu mikutano ya hadhara kwa mujibu wa sheria za nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza zaidi ndani ya Bunge hili kuna Kamati ya Katiba na inaona Katiba inasiginwa imekaa kimya. Hatusemi Bunge dhaifu lakini kuna tatizo kidogo kwamba Kamati ya Katiba isimamie jambo hili. Hilo ni jambo la kwanza nililotaka kulizungumzia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunasema nchi yetu haina matatizo, ina usalama na amani, lakini mimi naona si sahihi. Kwa mfano, tarehe 20 Aprili, 2019, kuna kijana wangu amekamatwa na amepelekwa Mtwara na sijui kama atarudi. Kwa sababu mwaka jana katika Bunge hili hili nilisema kuna vijana wangu watatu walikamatwa Ali Shari, Yusuph Kipuka na Ali Yusuph Kipuka mpaka leo hatujui walipo. Niliomba sana na Waziri wa Mambo ya Ndani wakati huo alikuwa rafiki yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba lakini hawajapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa wale wanaosema kwamba kuna utulivu na amani katika nchi hii ni kwa kuwa majimboni kwao hawajapata matukio kama haya. Kwa sisi Wapinzani matukio haya yapo, tunaombwa Serikali kijana huyu Rashid Salio Rashid aliyepelekwa Mtwara Mheshimiwa Kangi Lugola leo piga simu Mtwara Mheshimiwa huyu kijana aachiwe asipotee kama waliopotea mwanzo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema nchi hii ina matatizo. Katika Uchaguzi Mdogo Kilwa Kivinje walitekwa watu watatu na taarifa tukatoa na Mheshimiwa Kangi Lugola ukanielekeza nikafungue kesi, kesi imefunguliwa KLK RB.397 ya 2014. Cha kusikitisha sana walioteka watu hawa wanajulikana, gari ambayo imewateka ya Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Liwale inajulikana na kuna gari lingine ambalo lilisaidiana lenye namba T693DDD Toyota Passo ya Mheshimiwa Prosper Rweikiza inajulikana lakini kwa bahati mbaya zaidi...

## TAARIFA

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara, nitakulindia dakika zako subiri tusikilize taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji asipotoshe Bunge kwa sababu Bunge ni chombo maalum/mahsus. Gari analolitaja kwamba ni la Mheshimiwa Kuchauka ndiyo liliteka watu si kweli.

**WABUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, gari yangu mimi ilikuwa na namba T324 na namba ambayo illingizwa kwenye mtandao kwamba imehusika na utekaji ule ni namba T024. Sasa namba hizo ni tofauti na tofauti.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, gari anayoitangaza kwamba ni gari yangu siyo kweli. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosema taarifa nimetoa Polisi na hiyo gari ilikuwepo Kilwa, haikukamatwa kwa sababu walikuwa wanamlinda huyo Mheshimiwa na kama ingekuwa siyo kweli kwa nini isikamatwe? Hiyo namba anayosema ni kweli ilikuwa namba hiyo na tulivyoipeleka ikaoneka gari ya *Scania* siyo *Toyota Land Cruiser*. Kwa hiyo, ile gari namba iliyowekwa ilikuwa ya bandia lakini ile gari ni namba yake na ndiyo maana hawakuikamata kwa sababu ilikuwa na namba ya bandia. Mimi naendelea, taarifa yako sikuipokea, ni gari yako na ushahidi upo na kila kitu kipo sahihi kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari nyngine ni T.693 DDD Toyota Passo ya Mheshimiwa Prosper Rweikiza. Taarifa nilitoa Polisi, gari haikukatwa na watu wamepigwa mapanga na watu wao, hii inaonyesha kwamba amani hakuna. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Kangi Lugola fuatilia jambo hili na barua niliandika kwa *RPC* na wewe nikakupa nakala na ninayo hapa, barua hii hapa na Mwenyekiti nitakupa nakala. Mimi sisemi maneno kwa ujinga ujinga na uhakika. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, tulitoa taarifa kwamba kuna watu walipigwa risasi kule Chumo katika Msikiti na Mheshimiwa Mwingulu aliniambia niende kwa Waziri Mkuu. Kwa Waziri Mkuu nikaeenda na barua niliandika nikampelekea Waziri Mkuu. Yeye aliwaambia wale watu atawaita mpaka leo hajawaita na nakala Mheshimiwa Lugola unayo. Naomba Waislamu wale waliopigwa risasi Chumo muwaite muwape fidia kama sivyo tunasema Serikali ya CCM wauaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tukio la utekaji katika Uchaguzi Mdogo, nakuomba Mheshimiwa Lugola uniambie na ushahidi upo. Kama hiyo gari Mheshimiwa Kuchauka anasema sio yake ailete *Toyota Cruiser* hiyo Kilwa na kwa nini haikukamatwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuthibitisha kwamba Serikali ya CCM inawalinda majambazi, gari hii inayoteka

watu ikamchukua iliyemteka wakampeka Polisi na Polisi wanajua kwamba gari hii ndiyo iliyomteka. Pia kwa ushahidi TAKUKURU wakati anatekwa huyo Juma Gondaye walikuwepo na gari walionia. Mimi nashangaa sana ninyi mnavyosema nchi hii ina amani wananchi mliwapiga risasi, mmewatoa macho, mmewachoma moto kama nao wasingekubali sasa hivi nchi ingekuwa siyo ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Mashekhe wa Uamsho. Mwaka jana alisimama hapa Mheshimiwa Kabudi akasema upelelezi unakamika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bungara muda wako umeisha.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hili la Mashekhe lishughulikiwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimshukuru Mwenyenzi Mungu muweza wa yote aliyenipa fursa ya kuweza kusimama kutoa mchango katika Wizara hii nyeti, Wizara ambayo kwangu mimi naiita moyo wa taifa kwa sababu bila amani hakuna chochote tunachoweza kufanya katika taifa letu. Naomba nipingane na wale wote wanaosema majeshi yetu ikiwepo Jeshi la Polisi kwamba ni ugonjwa wa kansa, mimi naendelea kusema Mwenyezi Mungu awasamehe kwa sababu hawajui watendalo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na naomba nipingane na wale wote wanaosema majeshi yetu ikiwemo Jeshi la Polisi kwamba ni ugonjwa wa kansa, naendelea kusema Mwenyezi

Mungu awasamehe kwa sababu hawajui watendalo. Na wote hawa wanaozungumza ni kwa sababu hawajawahidi kuchimba handaki, hawajawahidi kulala kwenye handaki, hawajahidi kushuhudia vita ndio maana leo wakisikia mtu amekamatwa wanasema amani hakuna lakini kumbe kuna watu ambao hawalali kwa ajili yetu na si wengine Jeshi la Polisi ni Jeshi la magereza, jeshi la uhamiaji ni jeshi la zima moto. Ninawaomba muwasamehe maana hawajui watendalo na akutanaye hakuchagulii tusi na ukiwa kwenye maji unaoga akija mwendawazimu haumfukuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kangi Lugola na timu yake yote kwa kazi njema wanayoifanya. Kusema ukweli mnyonge mnyongeni haki yake apewe, Mheshimiwa Kangi na timu yako na taasisi zako zote mnafanya kazi nzuri na ndio maana leo Wabunge tunazungumza tutakavyo kwa sababu amani imedumishwa mnalinda mali na raia, mnazima moto tunapopata majanga, mnatalinda na katika mipaka yetu ndio maana leo tunasema Mungu awape Baraka zake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Kangi kwa kuandaa ripoti nzuri na timu yake kwa kweli taarifa hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani imeandaliwa vizuri, imechanganuliwa vizuri ninapongeza kweli inajieleza yenewewe na sio tu na kazi inafanyika vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi pia naishukuru Serikali kwamba kwa bajeti iliyokwisha 2018/2019 ilipeleka fedha vizuri kwenye Wizara ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kiwango cha asilimia 86 nimejaribu kupiga heshabu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nitoe ushauri. Wizara hii ya Mambo ya Ndani ndio moyo wa Taifa letu, ninaomba Serikali mko hapa mnisikie tutenge fedha za kutosha kwa ajili ya wizara hii. Wizara hii ina majukumu makubwa sana ya dharura ambayo hata hayatarajiwi, unamkuta *OCDyuko* Kiteto anaongoza kilometra zaidi ya 200

lakini mafuta anayopewa kwenye gari ni lita 100 kwa mwezi. Lakini unakuta hata *service* za magari wanatakiwa kwenda doria watulinde Wabunge, walinde doria, watembee kwenye mipaka yetu, watembee kulinda ujambazi na amani itokee lakini hata magari na matairi yao ya magari hayana uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine hata *service* zenyeewe na hata namna wenyeewe wanavyoweza kujikimu na hata kulala kwenye majanga kwenye maeneo mengine. Kwa kweli naomba na Waziri wa Fedha namwona yuko hapa na Kamati ya Bajeti mko hapa nawaomba wizara hii hebu iangalieni kwa jicho la pekee kwa sababu fedha zinazotengwa hazilingani na kazi wanayoifanya na ugumu wa kazi walijonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia magari ya zima moto ni magari ya zamani yamechoka. Juzi mliona moto hapa Dodoma unatokea hayafanyi kazi sawasawa wanaunulieni magari ya kisasa, tunaona kabisa Serikali imenunua magari nchi nzima imepeleka karibu Ma-OCD wote wana magari. Lakini hata matairi ni yale mapya yaliyokuja nayo hata mafuta ya kuweka kwenye hayo magari hakuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba jamani hebu tupigie kelele Serikali yetu na najua Serikali yetu ni sikuvi na Rais wetu amekuwa mstari wa mbele kulinda vyombo vyetu hivi kama ambavyo anavyofanya kwenye majeshi na vyombo vyta ulinzi na usalama jeshi la polisi, magereza, zimamoto watendewe haki kwa kuongezewa bajeti na hata fedha walijotengewa mwaka jana yote iende kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimejielekeza kuongelea maslahi ya askari, hata anayezungumza na mimi na maslahi na askari. Familia yote ya Mzee Makilagi tuko watoto 24 mimi peke yangu ndio raia na mimi niliponea chupuchupu. Kwa hiyo, nachozungumza hapa nazungumza tukiwa ndani ninaomba nitoe ushauri askari wetu wote wa polisi magereza,

zima moto, uhamiaji wanafanya kazi ngumu katika mazingira magumu. Ninaomba sisi kama Bunge hebu tuielekeze Serikali tujariibu hata kuwaongezea mishahara na hasa askari wa kiwango cha chini. Mishahara yao ni ya zamani kwa kweli haiendani na mazingira ya sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile askari wetu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, posho zao za kujikimu, posho zao za likizo, posho zao za uhamisho hawapati. Askari anakwenda kila baada ya miaka mitatu anakwenda likizo lakini sasa hivi hata nauli wakati mwengine wanajitegemea tunapeleka wapi jeshi, tunawasaidiaje hawa vijana wetu ambaio ndio walinzi wa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie kwa macho ya huruma kwa sababu askari tumewaambia wasichukue rushwa, askari huyu hana muda hata wa kufanya biashara, hana muda wa kukaa wa kufanya mambo yake binafsi muda wote anatalinda sisi, sasa anapokwenda mpaka likizo anajitegemea kwa kweli sio sawasawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie posho zao. Posho zao tunamshukuru Rais wetu na hata Awamu ya Nne, na hata Awamu ya Tano wanapata posho kujikimu ya chakula kila tarehe 15 wanapata shilingi 300,000.

Sasa hivi umekuja utaratibu eti wanapewa kila mwezi ninaomba ule utaratibu wa kupewa kila tarehe 15 ya kila mwezi wawe wanapewa kwa sababu ile tarehe 15 anapopata ile fedha inawasaidia kupunguza zile changamato ndio maana hawatakwenda kukamata huko ndio maana hawatajilingiza kwenye mambo mabaya lakinii unapolimbikiza mpaka mwisho wa mwezi sio nzuri. Ninaomba tuwaongeze pia kwa sababu tangu tulipowaongeza ilikuwa ni mwaka 2010 sasa ni 2015 tuwaongeze askari wetu toka hii 300, 000 ifike hata ikiwezekana 500,000 kwa sababu wanafanya kazi nzuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka nizungumzie ni ma...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninataka nimshauri Mheshimiwa Kangi tena nafurahi kwa sababu wewe...

**MWENYEKITI:** ngoja

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nani kanipa taarifa huyo nani alete.

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba pamoja na kwamba anasema askari wanapewa posho lakini ye ye ali kuwa mi mongoni mwa Wabunge walio kataa maaskari kuongezewa mshahara hapa Bungeni na wafanyakazi wote kwa ujumla. Kwa hiyo, ni taarifa tu kwamba anapozungumzia hilo akumbuke kwamba alikataa wafanyakazi kupandishiwa mishahara na maaskari wakiwa ni mi mongoni mwa wafanyakazi katika nchi hii. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Makilagi

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya huwa siongeagi na watoto nimekusikia, kwa hiyo, ataongea na *size yake* mimi sio *size yake*. Mimi naongea na baba yako umesikia mwanangu eeh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwa kusema kwamba askari wetu tuangalie maslahi yao kwa sababu wanalinda Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuzungumzie maslahi ya askari, vitendea kazi sasa hivi ipo changamoto kwa *uniform* za askari na sio kwa jeshi la polisi peke yake

mpaka zimamoto, magereza, ukikutana na askari sio kama yule wa zamani *uniform* zake zinatofautiana. Ninaomba kwenye fedha za OC kwa ajili ya shughuli mbalimbali hebu tuongeze bajeti hii ili vyombo vyetu vya Serikali viweze kununua *uniform*... (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza nao wanasema wakati mwingine hata wanaambiwa wanunue wao wenyewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini kuhusu utaratibu kanuni ya ngapi.

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba utaratibu kwa mujibu wa kanuni ya 64(1)(g) mzungumzaji wakati anajibu taarifa alisema kwamba haongei na watoto. Sasa licha ya kwamba hii sio kauli ya kibunge lakini kama kiongozi wa Kambi hii siongozi watoto, ninaongoza Wabunge, watu wazima na watoto wamebaki nyumbani. Sasa i baba yao ninaomba ieleweweke hivyo... (*Kicheko*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Makilagi endelea.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa sababu Mbunge anayezungumza ndio baba mwenyewe ninayemzungumza tutakaa pamoja kuwalea watoto kwa pamoja. Na ndio jukumu letu sisi kama wazazi ndani ya Bunge hili kuwalea watoto ili wazazi wanapokuwa wanazungumza watoto wanakuwa na utulivu na wanaweka heshima kwa wazazi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya askari, leo nimesema najielekeza kwenye maslahi ya askari wetu, Rais wetu anawapenda askari kila anapopita mniamwona anawapenda askari na alipokwenda Arusha mwaka jana alitoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kujenga nyumba za askari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa mujibu wa taarifa ya waziri nyumba zinaendelea kujengwa na baadhi yake nimezitembelea kwa kweli nichukue nafasi hii kumshukuru Rais kwa kazi njema. Ushauri wangu katika jambo hili pamoja na kazi nzuri ya kutenga hizo fedha bilioni kumi nataka nimwambie Mheshimiwa Kangi tena ambaye ni askari na wewe hebu sasa njoo na mkakati wa kujenga nyumba za askari za kutosha kwa nchi nzima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushauri kila unapofanya ziara usiache kutembelea kambini fika na pale *feed force* Mkoa wa Mara, fika na pale Mwanza Mabatini, fika na hapa Dodoma uone askari wako mahala wanapolala. Ninaomba mje na mkakati maalum na sisi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sisi Wabunge wa CCM tuko wengi na wengi tunapenda askari tuko tayari kuitisha mpango huu ili nyumba za askari zijengwe nchi mzima na zilete tija kwa askari wetu walale mahala pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nawashauri pia hata ramani ya nyumba za askari ziangaliwe tena kwa sababu nyumba zilizojengwa zamani zilikuwa ni kwa ajili ya familia ambazo hazina watoto, sasa hivi askari wetu wanaishi vizuri wana watoto vile vinyumba haviwastahili hebu njooni na ramani ambayo inavutia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri kuna kitengo cha ujenzi kwa upande wa magereza na kwa upande wa polisi. Sifurahii kuona kuna kazi imetokea jeshi la polisi, kazi wanapewa jeshi la wananchi, sifurahii kama mtoto wa askari kwa sababu nimeshiriki kujenga handaki, nimeshiriki kujenga hata nyumba za askari. Zamani familia za askari tukishirikiana na magereza, tukishirikiana na kitengo cha ujenzi

tulikuwa tunajenga nyumba wenyewe. Hiki kitengo kimekwenda wapi? Na bahati nzuri jeshi la polisi lina wataalam waliobobeaa katika weledi wa ujenzi, lina *Engineer*, lina wachoraji, lina kila kitu, mageraza ina rasilimali watu, Mheshimiwa Waziri hebu sasa uache *legacy* katika nchi hii. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Makilagi

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana naunga mkono hoja (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Catherine Ruge, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Ryoba Chacha Marwa jiandae.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia. Tunaitazama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na mafungu yake yote kwa maana ya Fungu la 93 ambalo ni Uhamiaji, Fungu 29 Jeshi la Magereza, Fungu 28 Jeshi la Polisi, Fungu 51 Makao Makuu ya Wizara na Fungu 14 Jeshi la Uokoaji na Zima moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka miwili mfululizo Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali alipata fursa ya kukagua wizara hii pamoja na mafungu yake yote. Mwaka 2016/2017 *CAG* aliibua hoja kumi za ukaguzi kutoka kwenye wizara hii ambazo ziliikuwa na thamani ya shillingi bilioni 128.6. Ukaguzi wa mwaka 2017/2018 *CAG* aliibua hoja 12 za ukaguzi zilitokuwa na thamani ya shillingi bilioni 180.2. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 40 ya thamani ya hoja zote za ukaguzi kwa maana ya *total value of audit queries*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara hii imekuja mbele ya Bunge lako tukufu kuomba tena kuidhinishiwa bajeti kwa ajili ya matumizi kwa mwaka ujao. Ninashangaa wizara hii bila woga imeweza kufanya hivyo wakati ikiwa na hoja lukuki za ukaguzi ambazo hazijapatiwa majibu kwa kipindi cha miaka miwili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2017/18 Bunge hili lilipitisha bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya shilingi bilioni 930. Lakini shilingi bilioni 180.2 zinahojwa najiuliza wanapata wapi *confidence* ya kusogea mbele ya Bunge hili na kuomba tena fedha kwa ajili ya matumizi ikiwa kuna hoja nzito sana za ukaguzi ambazo zimekosa majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni kama hii wizara ina hadhi ya kuja kuomba pesa tena wakati imeshindwa kujibu ujisadi na pesa nyngi za walipa kodi wanyonge Watanzania zimetumika kwa ubadhirifu mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mifano michache, ujisadi wa kutisha kwenye ununuzi wa mfumo wa utambuzi wa alama za vidole au afisi katika jeshi la polisi. Kulikuwa na manunuzi ya mtambo wa utambuzi wa gharama kwa alama za vidole. Kwanza Jeshi la polisi halikuwa na bajeti, lakini hazina ilichepusha kinyemela shilingi bilioni 40.3 kwenda jeshi la polisi kwa kutumia fomu ambazo hazikuwa halisia, afisa aliyehamisha hizo fedha alikuwa hausiki, sasa basi sawa zimekwenda basi zitumike vizuri, maajabu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 1.7 ambazo zilikuwa zitumike kufunga vifaa vya utambuzi kwenye magereza 35 hayakufanyika. Malipo hewa ya huduma ya matengenezo na uwezeshaji shilingi bilioni 3.3, malipo ya mafunzo hewa shilingi milioni 600.4, malipo ya vifaa hewa shilingi milioni 594 kulikuwa na vifaa vyenye uwezo sawa, mahitaji sawa na sifa sawa lakini zilikuwa *quoted* kwa gharama tofauti, kwa bei tofauti na hii ikapelekea jeshi la polisi kulipa zaidi ya shilingi milioni 556. Huku ni kupoteza na ni matumizi mabaya ya pesa za walipa kodi. Wote tunafahamu na tunatambua mkandarasi au mzabuni alikuwa ni nani? Alikuwa ni Lugumi *enterprises*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nashangaa mpaka leo sioni hatua zilizochukuliwa dhidi ya Lugumi. Nakumbuka mwaka jana Mheshimiwa Kangi ulivyoteuliwa kuwa Waziri ulikuja na kauli nzito na mkwara mzito kweli kuhusu Lugumi na ulim-*summon* kuja ofisi kwako *within 24 hour*. Lakini baada

ya wiki mbili kuna kitu gani, *who is behind* Lugumi, tunataka Serikali ituambie mmechukua hatua gani dhidi ya Lugumi na maafisa wote wa Jeshi la Polisi waliohusika na huu ubadhirifu tunataka majibu ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mweyekiti, nasema hivi kwa sababu Serikali hii imekuwa ikijipambanua kwamba ni Serikali ya kupinga ujisadi ya kutetea wanyonge hivi ni ujisadi gani sasa ambao mnaupinga huu sio ujisadi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye hoja nyininge, hoja ya Idara ya Uhamiaji. Idara ya Uhamiaji imekuwa ikipata hati zenyе mashaka kwa miaka miwili mfululizo. Mwaka huu hati yenye mashaka imesababishwa na Idara ya Uhamiaji kutokurekodi thamani ya ule mfumo ulionunua waki-electronic wa *e-migration*.

*Tunatambua mfumo huu ulinunuliwa, manunuzi yalifanyika kwenye ofisi ya Rais, nashangaa manunuzi makubwa siku hizi yanafanyika kwenye Ofisi ya Rais. Rais amekuwa ndio afisa manunuzi mkuu wa taifa au procurer in chief wakati tunafahamu hatuvezi... [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote tunafahamu mambo yafuatayo kwa mujibu wa kanuni ya 61(1)(e) lakini kwa mujibu pia wa kanuni ya 61(1)(a). Jambo la kwanza ninalotaka kusema manunuzi ya umma yana sheria yake na yanafata taratibu za kisheria zilizowekwa na Serikali hii. Taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara

ya 34 inampa mamlaka Rais ya uteuzi wa viongozi watakaowajibika na kusimamia majukumu mbalimbali ya Serikali. Lakini Kanuni ya kwanza, Kanuni ndogo niliyoisema ya (e) inayovunjwa na Mheshimiwa Mbunge anapoleta tuhuma nzito ndani ya Bunge hili, kwamba Rais wetu sasa amekuwa Afisa Manunuzi na anasimamia manunuzi ndani ya Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili halivumiliki, siyo jambo la kweli, ni uongo uliopitiliza. Namwomba Mheshimiwa Mbunge athibitishe wapi? Lini? Kwa namna gani? Kwa vigezo vipi Mheshimiwa Rais amefanya hivyo? Ninao ushahidi kama Mjumbe wa Baraza la Mawaziri na ninafahamu Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akizingatia taratibu na sheria na kuzisimamia sheria za nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba mjumbe afute kauli yake, kama hataki kufuta kauli hii, alete vielelezo vyta kuthibitisha kwamba Mheshimiwa Rais sasa amekuwa Afisa Manunuzi Mkuu na amekuwa akisimamia na kufanya manunuzi yeze mwenyewe. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge,...

**MBUNGE FULANI:** Kanuni zinasema athibitishe mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Hapana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ndio naongoza shughuli na Kanuni ndiyo zenyewe.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kasimama vizuri sana kwenye *point* ya utaratibu na ametaja hizo Kanuni ambazo kwa sababu ya muda sitachukua, niseme tu moja ili mjue yeze yuko katika nafasi ya Waziri na kwa mujibu wa nafasi hiyo, ana nafasi

pana sana na uwanja mpana sana wa kupata taarifa na ndiyo maana amelielezea Bunge hili taratibu ambazo zinatumika kwa upande wa manunuzi, kwamba haiwezekani hata siku moja, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania afanye shughuli za manunuzi kama inavyodaiwa. (*Makofî*)

Kwa maana hiyo, kwa mujibu wa Kanuni hiyo ya 63 ambayo ndiyo inahamisha jukumu sasa, mimi naridhika kabisa kwamba kwa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa *Chief Whip* wa upande wa Serikali, yanalifanya Bunge liamini kwamba ana taarifa za uhakika. Sasa Mheshimiwa Ruge Catherine una *option* mbili, na mimi kama *Presiding Officer* nakupa *option* ya kufuta kauli yako ili twende mbele au sasa tuingie hatua ya kukutaka uthibitishe.

Nakupa *option* ya kufuta kauli.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta kauli. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, endelea.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuchangia. Kwa sababu mtambo huu wa kielektroniki wa *e-Immigration* haukuwa kwenye hesabu za Idara ya Uhamiaji, ilimnyima nafasi Mkaguzi kuweza kukagua manunuzi ya mtambo huu na hivyo kupelekea Idara ya Uhamiaji kupata hati yenyé mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anakuja ku-*wind up* atueleze ni kwa nini fedha hizi au thamani ya mtambo huu ambao ulinunuliwa kwa shilingi bilioni 127 haukuweza kuonekana kwenye hesabu za Idara ya Uhamiaji kwa sababu hilo ni takwa la kisheria la *IPSAS* 31. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2018 hapa, tuliambiwa *e-Immigration* ilikuwa na *component*nyingi sana zaidi ya nne ikiwemo *e-passport*, *e-border*, *e-gate* na vitu vingine. Ningependa kufahamu mchakato huu umefikia

wapi? Baada ya *e-passport* zile *components* nyingine ziko katika hatua gani kwenye mchakato? Kwa sababu nimejaribu kupitia kitabu chake na sijaona amelizungumzia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzingumzia manunuzi ya sare hewa ya Jeshi la Polisi ya shilingi bilioni 16. Naitaka Serikali iweze kutoa majibu juu ya suala hili. Pia kuna fedha shilingi milioni 800 ambazo zilitoka Jeshi la Polisi zikawalipa watu ambao siyo Polisi. Tunataka tuambiwe watu hao ni akina nani kama siyo Polisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Ryoba Chacha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijalia uzima na leo nasimama kuchangia maoni yangu kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo ni Wizara muhimu sana kwa ustawi wa jamii yetu ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia kwanza kabisa kuhusu Vitambulisho vya Taifa, maana yake leo asubuhi iliongelewa sana hapa Bungeni. Majibu ambayo Serikali imetoa asubuhi Bungeni ni majibu ambayo ni mepesi sana kwa Watanzania kuyasikia na hayana uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa kwamba Serikali inadaiwa zaidi ya dola 30,000 za Kimarekani na Mkandarasi *Alice* ambaye amesitisha *production* ya hivi vitambulisho kuanzia Januari, 2019. Sasa haya mambo ambayo wamekuja hapa asubuhi wanaeleza ooh, watakwenda kutambuliwa kwa sababu ya usajili wa simu kwa kutumia namba, tutambue kwamba Watanzania wanahitaji vitambulisho vya Taifa, siyo kwa usajili wa simu tu. Kuna sehemu nyingi Watanzania wakienda wanaombwa vitambulisho vya Taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ituambie Bunge hili, ni lini itaenda kumlipa Mkandarasi huyu hizi takribani shilingi billioni 69 ili Mkandarasi aendelee na *production*, aendelee kuandikisha Watanzania na wapate hivyo vitambulisho ambavyo ni muhimu? Mtueleze ni lini mtamlipa Mkandarasi huyu hizi shilingi bilioni 69. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ndiyo maana tukikaa tunasema lazima Serikali iwe na vipaumbele. Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa, mlikuwa na *target* ya kuandikisha Watanzania milioni 25, leo waliopata ni milioni nne tu. Mkandarasi amesitisha uzalishaji, Kisa, hamjalipa fedha; lakini fedha nyngine mnapeleka kwenye sehemu ambazo hata hazina tija kwa maendeleo ya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nitaenda kuzungumzia Jeshi la Polisi; na hapa tukizungumzia Polisi, tunazungumzia wale ambao wanakiuka miiko na maadili ya kazi zao. Maana yake Wabunge wa CCM mkisimama huko mna *generalize* sijui mnafikiri nini. Tuko hapa kulisimamia Taifa, kulisimamia Jeshi la Polisi likienda kinyume. Nao wanatambua sisi ndiyo tunapigania maslahi yao hapa, lakini hatuwezi kuacha kuwasema wakienda kinyume. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji wa raia wanapokamatwa na Jeshi la Polisi; tumeshuhudia raia wanapigwa, wengine wanafariki. Juzi nimesikia Mwanga kuna kijana amefariki kwenye kituo cha Polisi. Yaani haiwezi kupita mwezi, miezi minne hatujasikia kuna raia amepigwa na Polisi, amefia Kituo cha Polisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu, nilipokuwa Segerea kuna mabinti walikuja wamekamatwa kwenye Vituo vya Polisi, wamebakwa, wameingiliwa kinyume na maumbile, wengine wameambukizwa magonjwa ya UKIMWI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumza hapa, tunataka Jeshi la Polisi liwajibishe hawa Askari. Majina ya Maaskari nawajua na nilitaja kwamba Kituo cha Sitaki Shari, Kituo cha Kawe na Kituo cha Mabatini. Wanakaa na mabinti

hawa zaidi ya mwezi, wiki tatu, miezi miwili wanawafanya kinyume na maumbile. Binti amekuja pale ameoza huku nyuma. Halafu tukizungumza, mnasema kwamba tuna..., *come on!* Lazima tusimamie hawa Polisi wasiende kinyume. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, kubambika kesi raia. Unamkamata raia kwa uzururaji, unampa amri *robbery*. Asipokuwa na fedha ya kukupa kitu kidogo, unambambika. Lazima tukemee hili ili Jeshi la Polisi, wananchi ambao ni walipa kodi ndiyo wanawalipa kuwepo; wanatakiwa wawalinde raia na usalama wao na siyo kuwageuza vinginevyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kabla sijaendelea hapo hapa katika kuwanyanya raia; tumekuwa tukisia matamko kwa kweli ambayo hata hayakemewi. *RPC* wa Dodoma, mwaka 2018 wakati nachangia nilimsema. Mwaka 2018 alisema kipigo cha mbwa koko; mwaka huu wakati *ACT Wazalendo* wanasema wataandamana, ambapo ni haki yao Kikatiba, akatoka kabisa *confidently* anaongea atawapiga mpaka wachakae. Kweli mnawachakaza Watanzania, maana yake mmewachakaza mpaka mnawaua. Kama hamkemei hili, mnafikiri ni sifa mnaua Watanzania, hakika hiyo laana itawarudia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni mlundikano wa mahabusu kwenye Magereza yetu. Nashangaa Tanzania ni nchi ya ajabu. Nyie mnafurahia kuwalundika raia Gerezani, raia ambao wangekuwa ni wazalishaji kwenye Taifa letu, mnaweka mzigo kwenye Taifa kwa kuwalundika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Segerea unakuta zaidi ya asilimia 80 ni mahabusu, tena mahabusu kesi zao nyingine zinachechesha. Kuna kesi moja alikuwa ni mfanyakazi wa ndani, anatuhumiwa eti ameiba shilingi 800,000/=, tena ni mfanyakazi wa kigogo mkubwa sana Wizarani. Eti, akaenda kufuatwa Bukoba, ametoka Dar es Salaam; wamechukua gari Mwanza wamemfuata Bukoba ndani ndani huko, amekuja wamepandishwa ndege mpaka Dar es Salaam kwa

shilingi 800,000/= mnasema kwamba mnasimamia matumizi ya walipa kodi masikini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukemee haya. Lazima tukemee haya. Watanzania wanaozea kule mahabusu Gerezani kwa kesi za kitoto sana. Wanakaa miaka mingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi imekuja hii ya utakatishaji. Nikiwa Segerea kuna Watanzania vijana ambao wamejajiri kwenye hizi *Travel Agents*, wanasemekana sijui wametakatisha shilingi milioni 10 za *ATCL*. Wamekamatwa vijana zaidi ya 11, wamesafirishwa kutoka Mwanza. Kuna mahakama kule! Usiku wamesafirishwa kutoka Mwanza na Maaskari wameletwa Segerea. Shilingi milioni 10 mnawaita watakatishaji, mnawanyima dhamana, vijana ambao ni wazalishaji zaidi ya 12 na kuna mama ana katoto ka miezi miwili. Yaani, basi, kama ni laana tunaipata kama Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sare za Magereza. Nimekuwa nikizungumza hili. Hawa Askari Magereza...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa!

## TAARIFA

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji, kusema kweli amtaje ambaye alitumia hiyo ndege na gari ili tumjue achukuliwa hatua za kisheria. Bila kumtaja haiwezekani. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Hiyo siyo taarifa. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema hao Maaskari ni wabaya tunataka tusafishe hili jeshi liwe jeshi ambalo linatumikia wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu 2012 mpaka leo Askari wa Magereza hawajapewa *uniform*, wanajinunulia. *This is a shame.* Watu hawa wanawajibika kutunza watu mnaosema ni majambazi sugu, ni manani, wanaji-*sacrifice* wanawatunza, hata kuwapa *uniform* zao, hamna! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, tumekuwa tukiona majeshi yetu yanaingiliwa. Niliona hivi karibuni *TISS* wanatumika kukamata raia badala ya Polisi. Kwa hili / *have the evidence*. Hiki ni kuingilia mihimili mingine. Haya majeshi, *TISS* wanatakiwa wafanye kazi zao, Jeshi la Polisi lifanye kazi yake. Pia kuna malalamiko yalikuja na hata raia tuliona.

Mheshimiwa Rais alisema kabisa kwamba wakati anakwenda kukagua nyumba ambazo zinajengwa kule Ukonga na *TBA* ambazo Magereza hawahusiki kabisa, allitakiwa awawajibishe wale *TBA*, lakini kauli ya kusema *CGP* atatokana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa kweli ile kauli mpaka kesho sijui inamaanisha nini. Kwamba *CGP* wa Magereza atokane na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hii ina-*demoralize* hawa Askari wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwa haraka haraka ni kuhusu Askari Magereza kutumia fedha zao za mfukoni kusafirisha mahabusu na wafungwa, kama wanatoka mkoaa mmoja kwenda mwингine. Hii fedheha kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Wekeni utaratibu wa kuweza kuwasafirisha hawa mahabusu na wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wanatumia fedha zao halafu hamwalipi, inakuwa ni deni. Hii ni aibu. Askari hawa wanadai madeni ya likizo, hamwapi, wanadai na madai kibao. Mshahara hamjawapandishia, pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais alisema kwenye kampeni zake, akishinda ataongeza mishahara ili wasiwe wanaiza vitumbua, wasiwe wanafanya mambo ya rushwa, kitu kimekuwa ni kunyume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa nne tunaenda hamjawapandisha mshahara, mnasubiri mwakani

mpandishe; na hiyo itakuwa ni rushwa. Mlitakiwa mwapandishie kuanzia mwanzo, siyo msubiri ikifika mwakani sasa mnapandisha ili kuwasogeza karibu, maana yake kule kwetu huwa... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ryoba, atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Innocent Bilakwate ajiandae.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii. Nina mambo machache na ninamwomba ndugu yangu Mheshimiwa Kangi Lugola, Waziri wa Mambo ya Ndani anisikilize. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kangi Lugola, ni moja ya Mawaziri wanaofanya vizuri sana, hilo halina ubishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Askari ambao hawana nidhamu walikuwa wanajaribu kuharibu Wizara ya Mambo ya Ndani; na Mheshimiwa Kangi Lugola bila aibu amekuwa akisema wazi wazi. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache. La kwanza naomba Kituo cha Polisi cha Mugumu na nyumba za Askari ni za siku nyingi. Kwa mfano, nyumba ambayo anakaa *OCS*, *OCCID* imechakaa sana. Naomba kwenye bajeti hii tusaidieni Polisi Mugumu waweze kukarabatiwa kituo na nyumba za Polisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge nimejitalidi, kulikuwa na shida ya choo, kuitia fedha zangu za Mfuko wa Jimbo niliwasaidia tukajenga choo na kibanda cha mlinzi. Halikadhalika Magereza walikuwa na nyumba zao tatu, mimi kama Mbunge niliwapa mabati na mbao wakapaua. Sasa Mheshimiwa Waziri niunge mkono tuwasaidie Magereza na Polisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Zimamoto. Mheshimiwa Waziri watu wetu wa Zimamoto pale hawana ofisi, hawana vitendea kazi. Gari wallonalo limechoka ni la miaka mingi. Kama tunaweza tukapata msaada pale Serengeti, gari la Zimamoto lenye uwezo la kisasa itapendeza zaidi, maana nyumba zinaungua lakini kwa sababu ya udogo wa gari lile haliwezi kuhimili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ni kuhusu Wakisii wanaoishi Rwamchanga. Jamii hii ya Wakisii imekuwepo kabla ya Uhuru, lakini hawajapewa nafasi ya kuwa raia wa Tanzania, wanaishi kwa vibali na hawaruhuswi kupiga kura. Namwomba Mheshimiwa Waziri, ifikie wakati hawa Watanzania wenzetu wapewe fursa ya kuwa Watanzania kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma biblia kuna andiko linasema, utawezaje kukitoa kibanzi cha ndugu yako ilhali wewe bado una kibanzi? Labda tu nisome eneo hili, anasema, "basi mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii? Au utawezaje kumwambia ndugu yako, ndugu yangu niache niktoe kibanzi kilicho ndani ya jicho lako, nawe huiangalii boriti ya ndani ya jicho lako mwenyewe. Mnafiki wewe, itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe, ndipo utakapoona vyema kukitoa kile kibanzi kilichomo ndani ya jicho la ndugu yako." (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza kule ng'ambo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kuna ufisadi mkubwa ndani ya Jeshi la Polisi, CAG amekagua. Nami niwafulize, lile gari la CHADEMA mnafahamu ufisadi mlioufanya? Kama hamfahamu, acha niwaambie leo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasemwa kuna ujisadi mkubwa ndani ya Jeshi la Polisi, CAG amekagua. Nami niwaulize, lile gari la CHADEMA wanafahamu ujisadi walioufanya? Kama hawafahamu, acha niwaambie leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari linalosemwa alikopeshwa mwanachama fedha anunue gari ni uongo! Lile gari ni la CHADEMA, lile gari alipewa fedha Mbunge fulani yuko humu simtaji kwa sasa ila wakitaka nitamtaja; akapewa fedha kwamba ye ye ndiyo anaenda kununua gari ili akwepe kodi. *Kwa hiyo, chama kimekwepa kulipa kodi kwa kumtumia Mbunge kununua gari lile na ndiyo maana gari lile liko mpaka leo pale!* Sasa niwaulize, mimi nimekuwa CHADEMA, ni lini chama kimekuwa na utaratibu wa kuwakopesha wanachama wake fedha? Lini? Eh, tuambiane hapa, wamekwepa kodi! (*Makofi*) [**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba...

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampa mzungumzaji anayeeleza kwamba kuna hoja inatolewa humu kwamba askari wameshindwa kulipa mishahara. *Sasa kama chama husika na watu husika wanakwepa kodi, mishahara ya watumishi wanaowasema itatoka wapi? Nataka nimpe Taarifa.* (*Makofi*) [**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**]

**MWENYEKITI:** Ahsante. Endelea Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ile Taarifa ya CAG ni ya kweli. *Alikopeshwa Mbunge mmoja hapa wa Viti Maalum tena ananiangalia yuko pale, alipewa hela, akaenda kuinunulia CHADEMA gari. Wamekwepa kodi na mkiletu mchezo nitamtaja hapa!* (*Makofi/Kicheko*) [**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**]

**MBUNGE FULANI:** Mtaje.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani si ni Sophia Mwakagenda?

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu Utaratibu...

**MWENYEKITI:** Subiri Mheshimiwa Ryoba. Kanuni ya ngapi? Kanuni kwanza niambie. Nitajie Kanuni kwanza.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa Kanuni ya 64(1) kwamba Mbunge hatasema mambo ya uongo, yasiyokuwa ya ukweli ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Elezea basi vizuri niweze kuridhika kama kweli ameenda nje maana wewe ndiyo unalijua zaidi hilo suala.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya *CAG*inaleza vizuri kwamba katika moja ya *queries* ambazo zilitolewa kwam ba Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kilinunua gari ambayo imesajiliwa kwa jina la mwanachama wake mmoja, lakini aliyetoa fedha ni chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukweli ni kwamba anachokieleza Mheshimiwa Mbunge anayechangia sasa hivi ni uongo kwa sababu ukweli hauko hivyo, vitabu vya *CAG* vipo.

Sasa sisi tunamwomba au mimi namwomba athibitishe, alete huo ukweli kwamba chama kilitaka kukwepa kodi ndiyo kikatoa hizo fedha kupitia kwa huyo mwanachama na kama hatafanya hivyo ili taratibu ziweze kutumika, kwa sababu anachosema ni uongo. (*Makofi*)

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ni masuala ya kanuni haya 64(1)(a) ulioisoma lazima uisome na kanuni ya 63 kwa sababu aliyekuwa anaongea alikuwa ni Mheshimiwa Ryoba, amesema kitu ambacho kikafanya wewe ujisikie kwamba usimame kwa mujibu wa Kanuni ya 63(3) Kuhusu Utaratibu kwamba yeye hajasema kitu kilicho sahihi. Wewe kwa mujibu wa Fasili ya (4), Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa Fasili ya Tatu ya Kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuridhisha Bunge. Sasa huo wajibu au ule mzigo wa kuthibitisha sasa ulihama kutoka kwa Mheshimiwa Ryoba kuja kwako. Umejaribu kuelezea lakini hukufikia sasa kile kiwango cha kutofautisha pale ambapo yeye yupo tayari kumtaja maana hoja hapa ni kwamba ilikuwa ni *scheme* ya kukwepa kodi. Sasa tusaidie hapo ili sasa nirejee kwake. (*Makofi*)

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *source* yake ni CAG kama alivyosema. Katika Taarifa ya CAG hakuna mahali popote ambapo CAG amesema CHADEMA ilitaka kukwepa kodi na CHADEMA imetoa maelezo kwamba kuna mwanachama ambaye aliagiza gari akashindwa kulikomboa, chama kikamkopesha fedha akalinunua na hilo gari liko pale kwenye Chama na CAG ameliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala hapa ni kwa nini halijahamishwa kutoka kwa yule mwanachama aliyekopeshwa kuja kwenye chama, lakini hakuna suala la kukwepa kodi. Sasa hiyo ya kukwepa kodi anatoa wapi? Hiyo ndiyo tunataka athitishe na akishindwa kuthibitisha afute hiyo kauli, vinginevyo atakuwa anasema kitu ambacho sio sahihi. (*Makofi*)

**MWENYEKTI:** Ahsante. Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Komu yuko sahihi kabisa na bahati nzuri Mheshimiwa Komu na Mheshimiwa Kubenea wako kwenye matazamio chini ya Kamati Kuu, maana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, jibu tu hilo.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amenisaidia. Ni kweli kwamba alikopesha mwanachama na alikwepa kodi, kwani si Sophia Mwakagenda, alilipa wapi? Kama mimi ni mwongo, gari hilo mpaka leo liko kwenye chama, ni la chama sio la mwanachama! *Mwanachama katumika tu kukwepa kodi! Kama mimi mwongo thibitisha wapi mlilipa kodi. (Makof) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme Komu na Kubenea walitoa tuhuma dhidi ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Mbewe, kwamba anakula ruzuku!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** ... na wako chini ya Kamati Kuu kwa uangalizi na wakavuliwa nafasi zao zote! *(Makof)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona huo sio utaratibu mzuri wa matumizi ya muda wetu wa Bunge. Ningependa sasa Mheshimiwa Ryoba, nisaidie tu kwa sababu na mimi lilikuwa linanisumbua sana hilo suala la kwamba kulikuwa na *scheme* ya kukwepa kodi. Sasa kama kwenye *CAG Report* hakuna kitu cha namna hiyo, nisaidie tu ondoa hiyo *scheme* ya kukwepa kodi, tubaki tu katika utaratibu wetu.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haina shida kwa sababu jinsi gari liliivoingia...

**MWENYEKITI:** Ondoa tu hiyo nanihii. Nisaidie ondoa hiyo ya kukwepa kodi.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Naondoaa, lakini tutafuatilia zaidi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kwa hiyo niseme huwezi ukawa unanyoosha tu kidole, ondoa boriti ya kwako kwanza. Sasa wewe hujaondoa ya kwako unasema! Hapa ngoja nikwambie, hawa Wabunge wewe unaowaona kule ng'ambo wana shida! Mbunge wa Viti Maalum kila mwezi shilingi 1,500,000 na hawajui zinafanya kazi gani na tunavyoongea hata matumizi ya ruzuku niambieni Katibu gani wa CHADEMA wa Jimbo au wa Wilaya anayelipwa na ruzuku ya CHADEMA? Hela inaliwa na wachache pale Makao Makuu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Hongoli.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti tafadhali.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa kwa ajili ya kuchangia hii Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Kwanza nianze kuishukuru sana Serikali hasa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani na maaskari wote kwa namna walivyodhibiti mauaji ya watoto katika Mkoa wa Njombe na Simiyu, nawashukuru sana. Naomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na aendelee kuwalinda ili tuweze kudhibiti tabia za namna hii na hatimaye Watanzania wasiweze kupotea kupitia mauaji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa namna wanavyofanya kazi zao hasa katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Kazi ni ngumu, kubwa sana, inahitaji weledi na pia inahitaji ustaarabu mkubwa. Nashukuru Mwenyezi Mungu

anawatia nguvu wanaendelea kumudu na hatimaye tunaona matokeo ya kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie juu ya makazi. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutoa zile bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 400 za askari wetu nchini. Tumeona zimegawanywa kwenye baadhi ya mikoa, kuna mikoa inapata nyumba 88 na mingine nyumba 20 na mgawanyo umeenda karibu kila mkoa ambao una upungufu mkubwa sana wa nyumba za askari wetu. Mkoa wa Njombe nimpongeze Mheshimiwa Rais ametupa nyumba 20 kwa ajili ya askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu wanafanya kazi kubwa sana usiku na mchana. Nashangaa hata wakati mwagine watu wanavyowabeza, kazi wanazofanya maaskari wetu ni kubwa sana, wanatulinda usiku tukiwa tumelala, wanalinda maduka mbalimbali, maduka yetu na mali mbalimbali za wananchi wa Tanzania, lakini pia wanatulinda hata sisi Wabunge tuliomo humu ndani. Tunaweza kuongea kwa amani na tukaishi kwa amani humu ndani na tuna uhakika ni kwa sababu askari wetu wametuzunguka huku wanatulinda. Kwa hiyo wanafanya kazi kubwa, hata wanapokosea tutumile maneno mazuri kwa sababu ni binadamu na wakati mwagine sisi wenyewe tunawakwaza na ndiyo maana wakati mwagine wanaghafilita au wanachukua hatua ambazo kidogo kama binadamu wakati mwagine wanapotoka taratibu kwa sababu ya namna sisi wananchi ambao wanatulinda usiku na mchana, wanatumikia muda wote lakini wakati mwagine tunageuka kuwapiga mateke, tunageuka kuwatukana na kuwapa lugha mbayambaya na matusi mbalimbali. Kwa hiyo niombe tuwaheshimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana bado maeneo mengi, mikoa mingi, nyumba za askari haziridhishi na wakati mwagine huwa wanaenda kazini wakiwa na *frustrations* ndiyo maana tunasikia wakati mwagine maaskari wanajiuwa, wanajipiga risasi kwa sababu ya *frustration* ya kukosa makazi. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri

pia niiombe Serikali kwa utaratibu huu ambao Mheshimiwa Rais ameuanza angalau tuanze kujenga nyumba za maaskari hawa kila mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika Mkao wa Njombe kwa mfano, Kituo chetu cha Polisi cha Wilaya pale ni cha zamani sana, ukiangalia hata jengo la kituo lenyewe ni la zamani. Kwa hiyo haiendani na hali halisi ya hatua ilipofikia kwa maana ya ngazi iliyofikia kile kituo. Kile kituo sasa hivi kinatumika kama kituo cha Mkao lakini hadhi ya kituo chenyewe sio nzuri. Nyumba zile ni chakavu, lakini ukiangalia hata makazi ya maaskari kwa kweli ni duni sana. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri tuliangalie hili jeshi, tuangalie maaskari wetu wa Mkao pale Njombe angalau wapate nyumba. Kukaa mitaani sio nzuri sana. Wakati mwingine wanakaa mitaani wanapanga nyumba na wakati mwingine wanaweza kuwa wanapanga nyumba na mhali. Inakuwa ni vigumu sana kumdhhibit huyu kwa sababu wakati mwingine wengine wanashawishika, wanaweza wasifanye kazi vizuri kwa sababu ya mazingira wanayokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wanapokaa mitaani maisha yao yanakuwa hatarini kwa sababu akishajua kwamba askari fulani ndiye aliyenikamata anaweza akamdhuru anaporudi kutoka kwenye shughuli zake ule usiku au anapoamka asubuhi kwenda kufanya shughuli zake zile. Kwa hiyo wakiishi sehemu moja, wakiishi kwenye nyumba nzuri za Serikali watafanya kazi zao vizuri na hatimaye watakuwa na *morale* ya kufanya kazi kwa sababu wanaishi kwenye makazi mazuri. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Kangi na Naibu Waziri na Makatibu Wakuu, nafikiri wawasilliane nao vizuri hawa ili baadaye ikiwezekana bajeti ya makazi iweze kuongezeka na hatimaye maaskari wetu waweze kupata nyumba bora, waweze kuishi vizuri na waweze kuhamasika katika utendaji wao wa kazi wa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Jeshi la Magereza. Ni kweli Jeshi la Magereza wanafanya kazi kubwa lakini ukiangalia kwenye bajeti yao, Fungu lao namba 29, bajeti yao ni ndogo sana kwa hiyo ukomo wao ni mdogo.

Hebu tupanue, tuongeze ukomo wa bajeti ya askari magereza kwa Jeshi la Magereza ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri. Wameeleza Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba kuna shida ya sare za maofisa, hawana sare walio wengi, lakini pia ukiangalia hata maaskari hawana sare, ukiangalia Jeshi la Magereza hawana na wafungwa wetu sare zao nydingi zimechakaa. Kwa hiyo tukiongeza ukomo wa bajeti wataweza kumudu kutekeleza majukumu yao, lakini wataweza kununua vifaa na mavazi ambayo wanatakiwa wayanunue kwa ajili ya askari wetu lakini pia kwa ajili ya maafisa wetu na kwa ajili ya wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hili litiliwe mkazo ili wafungwa wetu, pamoja na kwamba wanakuwa wamefungwa lakini wana haki ya kupewa zile sare. Vilevile maafisa wana haki ya kupewa sare zao na maaskari wana haki ya kupewa sare zao, kwa hiyo tuwatekeleze hii haki ya msingi ya angalau ya kupewa nguo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa akisema mara nydingi kwamba Jeshi la Magereza waanzishe utaratibu wa uzalishaji. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kulismamia hili. Kwanza tuyaitify magereza yetu yalipo, tuzi-*identify*fursa zilizopo katika magereza haya. Tujue kwamba kama ni Dodoma kuna fursa ipi wanaweza wakaifanya na mwishowe wakazalisha. Kama ni Njombe au mikoa kwa mfano yenye mvua nydingi tunaweza tukaanzisha shughuli za kilimo. Kwa hiyo kwenye mikoa hii tuanzishe shughuli za kilimo, lakini hatuwezi kuanzisha shughuli za kilimo bila kupeleka matrektta ya kulimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Kangi akae na wataalam wake wajaribu *ku-identify* maeneo yalipo magereza haya tuangalie ni shughuli gani wanaweza wakazifanya na hatimaye magereza yasiwe tegemezi. Serikali inatumia fedha nydingi sana kwa ajili ya kuwalisha wafungwa, lakini kumbe tukianzisha shughuli watakuwa wanazalisha na hatimaye kuipunguzia gharama Serikali ya kuwatunza hawa wafungwa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kwenye gereza la Idete, kinaweza kuanzishwa kilimo cha umwagiliaji cha mpunga na wakazalisha, halafu huo mpunga au mchele ukasambazwa kwenye magereza mengine, kwa hiyo badala ya kununua chakula basi wakapewa chakula kuititia magereza mengine. Pia kwenye magereza ambako hakuna uzalishaji tunaweza kuanzisha shughuli kama za useremala, kwa mfano, tunesema kwamba hapa Dodoma Msalato tutaanzisha useremala, basi uanze haraka ili waweze kuzalisha hizo bidhaa na waweze kuuza na hatimaye majeshi yetu yaweze kujitegemea kuititia hizo shughuli za kilimo. Kwa hiyo, tukifanya hivyo tutapunguza gharama kubwa ambazo tunazitumia kuwalisha hawa wafungwa. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ili tuweze kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani tuanzishe utaratibu wa adhabu mbadala. Badala ya wote kuwapeleka ndani, kwa mfano, wafungwa wanaokuwa na adhabu ya miezi sita, mwaka mmoja, hawa wanaweza wakatafutiwa shughuli, wakafanya shughuli za maendeleo, wakashiriki kwenye shughuli hizi za ujenzi kwa kuwa sasa hivi jeshi la magereza linashiriki kwenye shughuli za ujenzi na tumeona kazi zao wanafanya vizuri. Tumeona wamejenga hizo nyumba hapo za Mji wa Serikali. Kwa hiyo, kumbe tunaweza tukawatumia hawa wafungwa wale ambao wana vifungo vifupi, badala ya kupelekwa gerezani, wao wakapewa kazi ya kufanya kama vile kushiriki kwenye kazi za ujenzi na hatimaye tukapunguza gharama, tukapunguza msongamano...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bilakwate na Mheshimiwa Alex Gashaza ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote nimshukuru kwanza Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anazozifanya. Kwa kweli nampongeza sana, tumeona mabadiliko makubwa ambayo amekuwa akiyafanya, kwa kweli tunampongeza pamoja na wasaidizi wake, wanafanya kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mimi nilipongeze Jeshi letu la Polisi, kwa kweli pamoja na baadhi ya wenzetu kubeza na kusema hakuna chochote kinachofanyika na wengine wamefika mbali kusema maneno magumu, wanasema Jeshi la Polisi ni kansa, kitu ambacho kwa kweli si jambo zuri na sikutegemea kama Mbunge angeweza kusimama na kusema neno la namna hii. Tuko hapa kwa sababu ya kazi nzuri zinazofanywa na Jeshi letu la Polisi. Ndugu zangu tunaweza tukawa hatuelewi lakini ukiongea na majirani zetu ambao wanapita kwenye nyakati ngumu, ndiyo mnaweza mkajua umuhimu wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri wanazozifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunalala wenzetu wako nje wanang'atwa na mbu na mambo mengine wanayoyafanya. Leo hii tuko hapa tumetulia, hali ni nzuri, ukienda nchi za wenzetu, tulienda kule Burundi, kila mnapozunguka mnatembea na mititu ya bunduki lakini nendeni pale nje hata bunduki hatuzioni ni kwa sababu ya amani iliyopo katika Taifa letu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kuhusu utaratibu, nisaidie Kanuni.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a), Mbunge hatatoa Bungeni maneno yasiyokuwa na ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Bungeni tuko hapa kwa ajili ya....

**MWENYEKITI:** Maneno ambayo siyo ya ukweli ni uongo, si ndiyo?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo uwongo huo. Hakuna mionganoni mwetu hapa ambaye anabeza kazi ya Jeshi la Polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, anachojitungia na kutaka kujipa uhalali kwamba Jeshi la Polisi sisi tunalibeza, hatultitaki au...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwanimekuelewa, sababu ya muda, nimekuelewa, kaa tu, sitaki usimame. Anachosema Mheshimiwa Bilakwate, nimemsikia vizuri sana halafu asubuhi nilimsamehe sana huyu Mheshimiwa Sophia Mwakagenda alitumia neno, Jeshi la Polisi ni kansa, nilimvumilia. Sasa Mheshimiwa Bilakwate anajibu kwa namna hiyo, ndiyo maana sitaki mimi niliendeleze suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Bilakwate, hoja yako imesikika lakini nalikataza hilo, sitaki kufika huko.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niombe sana Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Waziri lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Jeshi letu la Polisi kwa kazi nzuri wanazozifanya waweze kupewa yale ambayo ni mahitaji yao lakini bajeti yao izingatiwe ili waweze kuendelea kutimiza majukumu yao. Vinginevyo tusipowajali hawa wenzetu wanaosema wao wako wengi siku wakianzisha vita, tusipowapa vitendea kazi vizuri ili waweze kuwadhibiti watakapoanzisha vita, tutakuwa tunakwenda pabaya. Kwa hiyo, niombe sana tuwasaidie

Polisi wetu kwani wanayo mahitaji mengi ili waweze kutimiza majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Waziri ulifika Kerwa, ulionamazingira ambayo Polisi wetu wanafanya kazi. Uliona Kituo cha Polisi siyo kizuri na kituo kile ni ofisi za kata, nikuombe sana hili ulizingatie. Sisi tuko mpakani, tunakutana na watu wengi, majirani zetu wanaingia, tusipoimarisha vizuri Jeshi la Polisi mipakani, tunaweza tukaingiza mambo mengine ambayo baadaye yanaweza kuhatarisha amani ya taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kwa upande wa *NIDA*. Kerwa tupo kwenye utaratibu wa kuanza kusajili vitambulisho vya *NIDA*, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, hii mikoa ambayo iko pembezoni muweze kuiangalia kwa umakini sana kwa sababu wako wenzetu wanatamani kuwa Watanzania ambao hawana sifa. Suala hili tuliangalie ilitisijetukaingiza watu ambao hawana sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunahitaji hata kuhubiriana injili au kukemeana mapepo. Naomba nisome hili nenona mwenye akili ataaelewa. Nasoma Kitabu cha Warumi 13:1-7, inasema: "Kila mtu naaitii mamlaka ilio kuu; kwa maanahakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo imeamuriwa na Mungu. Hivyo amwasiye mwenye mamlaka hushindana naagizo la Mungu; nao washindanao watajipatia hukumu. Kwa maana watawalao hawatishi watu kwa sababu ya matendo mema, bali kwa sababu ya matendo mabaya. Basi, wataka usimwogope mwenye mamlaka? Fanya mema, naweutapata sifa kwake. Kwa kuwa ye ye nimtimishi wa Mungu kwako kwa ajili ya mema. Lakini ufanyapo mabaya, ogopa; kwa maana hauchukui upanga bure; kwa sababu ni mtumishi wa Mungu, amlipiziaye kisasi mtenda mabaya kwa ajili ya ghadhabu. Kwa hiyo ni lazima kutii, si kwa sababu ya ile gadhabu tu, ila na kwa sababu ya dhamiri.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kanuni gani?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a), inasema: "...hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli".

**MWENYEKITI:** Hicho ni Kitabu Kitakatifu, Mheshimiwa endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasema sababu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niendelee kusoma mstari, nilikuwa nimefika mstari wa6 unasema: "Kwa sababu hiyo tena mwalipa kodi; kwa kuwa wao ni wahudumu wa Mungu, wakidumu katika kazi iyo hiyo. Wapeni wote haki zao; mtu wa kodi, kodi; mtu wa ushuru, ushuru; astahiliye hofu, hofu; asitahiliye heshima, heshima". Haleluya. (*Makofii*)

**WABUNGE FULANI:** Ameen.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya nafikiri kila mtu ameewela, kama mnataka Jeshi la Polisi lisiwapige na lisizue mikutano lazima muwe watii.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Nyie mnasema mnaonewa kila sehemu, mnaonewa wapi nikwa sababu hamtendi mema. Mabaya mnayoyatenda ndiyo yanayowageuka, tendeni mema muone kama na ninyi hamtatendewa mema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendeleana Mheshimiwa Alex Gashaza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwakunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Ni ukweli usiopingika kwamba Wizara hii ni nyeti na inafanya kazi kubwa ya kuwashudumia Watanzania takribani milioni 55. Tunashukuru kwa ajili ya usalama na utulivu uliopo ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya watu milioni 55, watu wana tabia na akili tofautilakini ukiangalia jinsi ambavyo Wizara hii kupitia Jeshi lake la Polisi imeweza kudhibiti hali ya uhalifu ndani ya nchi hii, tuna kila sababu ya kuwapongeza. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Makamishna Jenerali wa Uhamiaji, Jeshi la Magereza na Jeshi la Zima Moto na Uokoaji kwa kazi kubwa ambayo kwa kweli wameweza kuifanya, tunawapongeza na Mungu awabariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Wakati wote hauwezi ukafanya kwa asilimia 100, *we always do to optimum*. Kwa hiyo, kwa jitihada ambazo zimefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kuhakikisha kwamba utulivu na amani unapatikana kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani, tuna kila sababu ya kusema wamefanya kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba changamoto hazikosi, kwenye Jeshi la Polisi kama wengine ambavyo wamesemakwamba zipo changamoto hususan katika uwezeshejaji wa Jeshi letu la Polisi kutekeleza majukumu yao kulingana na hali ya kijigrafia ya nchi yetu na ukubwa

wa nchi yetu. Tunajua kwamba *resources*, kwa maana ya rasilimali ni kidogo, hasa rasilimali watu lakini pia hata vitendea kazi. Tunamshukuru Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo anaendelea kuguswa kwa namna ya kipekee ili kuiwezesha Wizara hii kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo changamoto ya malazi, kwa maana ya nyumba za Askari wetu, ipo changamoto hata ya matumizi ya kila siku kwa maana *yabills* za umeme, na maji. Niombe Wizara ijaribu kuangalia maeneo ambayo kwa kweli kuna madeni makubwa kama ambavyo Kamati imeweza kushauri, basi waangalie ni namna gani wanaweza kupunguza madeni hayo kwenye maeneo ambayo madeni ya umeme na maji yapo ikiwa ni pamoja na Wilaya yangu ya Ngara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunajua kwamba jiografia zinatofautiana, kwamfano, Wilaya ya Ngara iko mpakani, tunapakana na nchi mbili ambazo hali ya usalama wakati mwininge inakuwa si tulivu na katika mipaka yetu kunakuwa na changamoto ya mwingiliano na wageni kutoka nje. Hii inatokana na kwamba Wilaya ya Ngara kwa muda mrefu *ime-host* wakimbizi, tangu miaka ya 1959. Kwa hiyo, Wilaya ya Ngara ni Wilaya ambayo sasa hata wageni kutoka nchi jirani wameshaizoea kutokana na kwamba wameishi kwa muda mrefu wakiwa wakimbizi, kwa hiyo, hata wanapokwenda ni rahisi kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe vituo vya polisi ambavyo sasakwa jitihada za wananchi kwa kushirikiana na viongozi wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Mkao, tumeanza kujenga kwenye maeneo hasa kata za mpakani, basi Wizara ione namna gani inavyoweza kutuongezea nguvu kwa ajili ya kukamilisha vituo hivyo. Vituo hivyo ni Mkanizi, Mlavyagira, Murubanga, Keza na maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara ina vituo viwili vya pamoja, *OSBP* (*One Stop Border Posts*) kwenye

mpaka Rusumo tunapopakana na Rwanda na mpaka wa Kabanga tunapopakana na Burundi. Kituo hiki cha OSBP-Rusumo, tunahitaji kuwa na *CCTV Cameras*, hakuna, ukienda upande wa Rwanda kila ofisi ina *CCTV Camera*, kwetu pale hakuna hata moja, kwa hiyo, kiusalama ni changamoto kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti,lakini pia tumeppite pale na Kamati ya *LAAC* kuangalia kituo hiki, tunazo *scanners* mbili, *scanner* kwa ajili ya *passengers* na kwa ajili ya *luggage's*. *Scanners* zile zinahitaji moto mwingu wa umeme, wakati mwindinge hazifanyi kazi, kwa hiyo, upekuzi unafanyika *manually*kiasi kwamba kiusalama si hali nzuri, tunahitaji kuboresha maeneo yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda upande waJeshi la Magereza, tuna changamoto kubwa hasa Wilaya yangu ya Ngara, kwanza hawana gari, hata wanapokuwa na wagonjwa kuwasafirisha kuwapeleka hospitali ni tatizo lakini hata kuwapeleka wafungwa kwenye shughuli inakuwa ni gumu, hasa inapokuwa maeneo ya mbali. Kwa hiyo, tunahitaji tupate garikwa ajili ya Jeshi letu la Magereza katika Wilaya yetu ya Ngara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pamoja pia na msongamano wa wafungwa/mahabusu magerezani. Wapo mahabusu ambao hawana sababu ya kuendelea kukaa mle kwamuda mrefu kutokana na kesi zao walizo nazo. Wengine kesi zao zina dhamana, kwa hiyo, tukiweza kuharakisha kufanya upelelezi au wakapewa dhamana wakawa nje wakawa wanahuduria mahakamani, inaweza ikapunguza msongaman. Kwa hiyo, niombe hilo nalo liweze kufuatiliwa na kuangaliwa kwa umakini hii ikiwa ni pamoja na wahamiaji haramu ambao anakamatwa na kuwekwa ndani kwa muda mrefu. Kama inabainika kwamba ni wahamiaji harama hakuna sababu ya kuwahifadhi na kuwagharamia chakula na kadhalika, ni afadhali tukawarudisha kwa sababu wengi wanatokea nchi za jirani, Rwanda na Burundi, ambayo ni *just walking distance*, kutoka Ngara Mjini kwenda borders hizo zote, hazizidi kilomita 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda upande wa Uhamiaji, tunatambua kwamba Sheria ya Uraia wa Tanzania ya mwaka 1995, Sura ya 357 na kama ilivyorejewa mwaka 2002 lakini na Kanuni zake za mwaka 1997, zinazeleza kwamba raia wa Tanzania wanatambuliwa kwa aina tatu: Uraia wa Kuzaliwa; Uraia wa Kurithi lakini na Uraia pia wa Kuandikishwa. Utambuzi huu unazingatia vipindi mbalimbali vya uongoziwa nchi hii. Kuna uraia kabla nabaada ya uhuru, kabla ya mapinduzi na baada ya mapinduzi na baada ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wanasema *ignorance of the law is not excuse* lakini tunahitaji kuendelea kutoa elimukwa wananchi wetu na wakati mwingine kuweza kuhakikisha kwamba haya makundi matatu ya uraia yanajulikana katika jamii. Wakati mwingine hata zinapotolewa taarifa kwamba kuna baadhi ya wahamiaji haramu, unajikuta watu wengine wanapata usumbufu kumbe wako katika *categorieshizi* na hawapaswi kutuhumiwa kama siyo raia lakini ni kutokana nakwamba elimu hii ya uraia kwa wananchiwalio wengi hususan maeneo ya vijiji na hasa maeneo ya mipakani haipo. Kwa hiyo, tuombe Jeshi letu la Uhamiaji wajaribu kujisumbua hasa katika maeneo ya mipakani na vijijinikutoa elimu ya uraia ili kuweza kujua nani anakuwa raia na nani si raia na kwa sababu zippi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru Mheshimiwa Waziri mwanzoni mwaka huu ulifanya ziara katika Wilaya yangu ya Ngara, tumekuwa waathirika wakubwa hususan katika suala zima la uraia. Kuna wapiga kura wangu wengine wanashindwa hata kutembea kwenda Kahama lakini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ile ya Kwanza, Uhuru wa Kuishi, Mtanzania anayo haki ya kuishi mahali popote. Wakati mwingine wananchi wanashindwa kutembea kwa kuhofu kwambaakionekana sehemu fulani ...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gashaza, ahsante sana.  
(*Makofi*)

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuisoma nukuu hii inayosema; "Udikteta wa wengi wape. Udikteta wa wengi wape ni ile hali ambapo Serikali au mamlaka nyingine inayoungwa mkono kidemokrasia na wafuasi wake wengi walio katika vyombo vya maamuzi wanapoamua kutengeneza sera au kuitisha maamuzi yenyewe kufaidisha maslahi yao lakini bila kujali haki wala ustawi wa watu wengine wote walio chini ya utawala wao."

**MWENYEKITI:** Niambie *source* yake.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *source* yake ni kwenye *dictionary*.

**MWENYEKITI:** Niambie *dictionary* ipi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *Oxford Dictionary*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wawakilishi wa walipa kodi na kuna *myth* inataka kutengenezwa katika Bunge hili kwamba sisi wapinzani hatuwapendi polisi. duniani kote polisi wanasi mamia *law and order* na tunahitaji Polisi hakuna mtu ambaye hawataki Polisi, hiyo ieleweke kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanataka kupotosha hapa na kujipendekezapeendekeza kana kwamba sisi hatuwataki polisi, hata sisi tukichukua nchi tutawataka

polisi. Kuna mambo Jeshi la Polisi linafanya kazi vizuri na ndiyo maana kwenye Utawala Bora Mheshimiwa Mollel alisimama hapa kuwatetea wafanyakazi wa umma ambao ni pamoja na polisi wapate mishahara yao. Kwa hiyo, hiyo *mythiondoke kwamba sisi hatuwataki Polisi*, tunawataka polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kubwa tunayojenga dhidi ya polisi ni pale ambapo hawaifiati sheria. Kuna *Police General Order (PGO)* lakini Polisi hawaifiati na sisi hapa ni wajibu wetu kama Wabunge kuhakikisha inafuatwa. Sisi tunasema wafuate sheria ninyi hamtaki, sasa mnataka waendesheje Jeshi, tunataka wafuate sheria kwa sababu hazifuatwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, Mheshimiwa Kangi, nina maswali kadha ambayo lazima uwaambie Watanzania na Mheshimiwa */GP* ananisikia hapa. Mheshimiwa Rais hivi karibuni aliliambia Jeshi la Polisi kwamba Watanzania siyo wajinga, ile *move* ya MO, haieleweki. Tunataka uwaambie Watanzania *exactly what happened?* Kwa sababu polisi kazi yao ni kulinda raia na mali zao, *full stop*. Mimi kama Mtanzania Polisi ana wajibu wa kunilinda, *exactly* tunataka tujue *movehiyo* na Rais alisema, kama mnapinga maamuzi ya Rais sijui, alisema Watanzania siyo wajinga na */GP* akasema baada ya siku tatu atatoa taarifa, sasa hivi muda umepita hiyo taarifa haijatoka, *we want to know that.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *number two*, polisi bado hawajatuambia, *what exactly*, ni kitu gani kilimtokea Roma Mkatoliki, bado tuko gizani hatuna majibu hayo, tutakuwa Wabunge wa hovyo sana kuliruhusu Jeshi la Polisi mambo ya hovyo yanatokea halafu eti tuseme polisi wang'atwa na mbu, hawalali si ndiyo kazi ya polisi, yaani mwanajeshi akienda vitani tuenze *is not doing as a favor that is his job*. Utuambie Roma Mkatoliki kilitokea kitu gani nchi haijui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi haijatambua kuvamiwa kwa *Clouds*, hamjatoa maelezo yoyote *Clouds* ilivamiwa kilitokea gani? Nani alihuksika nani alikamatwa

hatuwezi kukaa kimya halafu tukasifu tu Jeshi la Polisi hapa. Polisi haijasema kuhusu Azory na jana nimesikitika sana kumsikia Mheshimiwa Mwakyembe hapa anasema eti mtu mmoja tu tunaangaika naye. Uhai wa mtu mmoja ni wa thamani sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu ame-*quote* Biblia *out of context* lakini Biblia inasema tumeumbwa kwa *image* ya Mungu, mtu mmoja akipotea Taifa lazima linununike, watu wanaokufa siyo inzi ni binadamu. Polisi hamjasema kitu gani kimetokea kwa Ben Saanane mnabumba bumba mpaka leo. *You must tell us* nani alimuua Mawazo polisi mmekaa kimya, Jeshi la Polisi halijasema Mheshimiwa Kangi, polisi hamjasema mpaka leo dunia nzima mnasema (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MCH. PETER S.MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tundu Lissu anawabagaza Polisi hamjasema nani alimpiga risasi kwa Tundu Lissu...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa huyu.

**MHE. MCH. PETER S.MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uchunguzi tutakaaje kimya tuseme Jeshi la Polisi tunalishangilia matukio makubwa kama haya, dunia inaona, Polisi hawatoi ripoti sasa kazi yao nini? Kazi ya Polisi ni kulinda raia na mali zao ndiyo kazi ya Polisi. Polisi anawajibu wa kulinda raia na atoe ripoti kwa nini raia wameuwawa tuende wapi, wao ndiyo wana mabomu, wao ndiyo wana vitendea kazi, tumewakabidhi watulinde na wapo kwa ajili ya hiyo. Nani alimnyooshea bunduki Mheshimiwa Nape *we are quite*, polisi hawajatoa ripoti nani alionesha bunduki pale amechukuliwa hatua gani? Sasa tukae hapa tuseme hoo wanang'atwa na mbu sasa wana kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma historia duniani wenzetu Marekani ambapo demokrasia imeshamiri George

Washington alivyokuwa anaunda Serikali walitaka kumfanya awe mfalme akasema lazima tuwe na Serikali ambayo itakuwa na nidhamu kwa wananchi. Leo vyombo vya dola tunaonekana kama sisi ni watumwa swali la kujuliza; *are we captive or we are citizen in this county?* Kwa sababu maonezi yanayofanywa kwenye Vituo vya Polisi ni makubwa sana sisemi Jeshi la Polisi lote. Kama mimi Mbunge nimesingiziwa kesi ya kuchoma nyumba, nimesingiziwa kesi ya kubomoa nyumba hawa raia wa kawaida na siyo Mbunge fala, lakini nimesingiziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi zimeenda Mahakamani *within a minute zimefutwa kwa sababu ni uovu, RCO wa Iringa amehamishiwa sasa hivi Pemba anatengeneza kesi za uongo kabisa nimelala mahabusu kwa kuonewa na wengine wenu hapa hamna legitimacy ya kuongelea mambo ya custody wala huko kwenye cell, you have never been there!* Hamjui ukienda *central pale how it looks like? We have been there.* Hamjaenda Segerea mnasema tu hapa hamjaona watu wanavyoteswa kule ndani, hamna hiyo *legit.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea haya mambo kwa sababu tuna *experience*, anasimama leo, leo Kikatiba mtuambie kama Katiba haifuatwi hii, nchi ni ya utawala wa sheria, Katiba inatupa haki ya kuandamana, anasimama RPC, mtumishi wetu, mtumishi wa umma sisi siyo *captive, we are not captive we are citizen anasimama and we pay them* na wamekuja hapa kuomba hela ili tuwalipe...

**MWENYEKITI:** Ongea na Kiti.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes sir,* anasimama kwenye vyombo vya habari anasema nitawatandika nitawachakaza *who he think he is?* Nataka niwaambie Polisi kuna watu amba walifanya makosa katika Vita vya Pili vya Dunia... (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ongea na Kiti, huwezi kuwaambia Polisi ni-*address* mimi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao walifanya makosa katika Vita Vikuu vya Pili vya Dunia leo wanalipa gharama *you never go away* pale ambapo mlipaswa msimamie sheria mkafunika mkadhani sheria haitawafuata; *somewhere in the future* tutakuja tutakukamata kwa sababu sheria inakutaka ufuate sheria, watu wanaoza kwenye vituo, wanakamatwa raia, sheria inasema wakae masaa 48 wanakaa miezi miwili, wanakaa miezi mitatu, tumekuwa na *torturing chamber* katika nchi hii watu wanapigwa, kuna yule mzungu amevunjika miguu, anateswa na mabinti wengine wa kike wanamwambia aoneshe uchi wake wanamtesa, *"how can we live in this county. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tuseme tusikemee haya mambo haya tutasemea wapi? Raia wanakufa kwenye mikono ya Polisi kila wakati halafu tuseme halafu tuseme wapi. *(Makof)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Msigwa ahsante, Mheshimiwa Keissy. *(Makof)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwanza nazungumzia habari ya Jimbo langu la Nkasi Kaskazini, Mheshimiwa Waziri namshukuru sana alifika ziara yake kule akaangalia Gereza la kule kwangu ni la kilimo. Kilimo Kwanza, lakini kilimo hawana dhana za kilimo, wapelekee trekta, Polisi wetu kule mataili ya gari ni shida Polisi Namanyere, petroli, mafuta ya dizeli ni shida ukienda vituo vya pembeni kama vile Kilando na Kabwe ndiyo halikadhalika havifai hata kuviona kwenye macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Idara ya Uhamiaji Kabwe ukienda kuangalia Idara ya Uhamiaji Mheshimiwa Waziri hali yao ni mbaya, wako mpakani Wakongomani wanaingia kila sehemu kwa gari pale Kabwe lakini hawana chochote cha kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri lazima uwafikirie vya pemberi pemberi, kwanza natoa pongezi sana kwa Polisi tuko hapa Bungeni. Nakaa kule Namanyere mke wangu yuko Namanyere analindwa na Polisi wala sina habari nikimpigia simu asubuhi vipi hali anasema hali salama, wote tuko hapa familia zetu ziko Vijijini kule, wanaotulinda kule ni Polisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nashangaa anakaa Mbunge anasema hapa habari ya Polisi ndugu zangu, hivi Polisi wakigoma masaa matatu tu kila mtu atatoka Bungeni hapa atakimbia mbio hakuna atakayebaki hapa, hakuna atakayebaki Polisi waseme leo tunamgommo kama Madaktari walivyogoma vile Muhimbili hakuna atakayebaki hapa. Lazina tuheshimu Jeshi la Polisi ndugu zangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafanya kazikulinda mali zetu na sisi wenyewe tumekaa hapa miezi mitatu tukipiga simu majumbani kwetu hali salama kabisa, hakuna hata mmoja ameingiliwa nyumbani kwake kuvunja nyumba, Namanyere sina hata mlinzi nyumbani kwangu yuko mke wangu na watoto lakini yuko salama kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa unasema habari ya Jeshi la Polisi, ndugu zangu tumefika pabaya ninamheshimu sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa uwamuzi aliouchukua kupiga marufuku mikutano. Tukiwa hapa Bungeni wanakwenda kule Majimboni nilizungumza Awamu ya Nne kuanzia asubuhi magazeti, radio, televisheni kutukana, anatoka na mwendawazimu mmoja anajitia Mwenyekiti anaanzisha mkutano kuanzia asubuhi ni kutukana, anamtukana Diwani, anamtukana Mbunge, anamtukana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli kulikuwa hamna nidhamu wote mnakumbuka hapa tulikuwa wakiita mikutano hawa jamaa ilikuwa ni hatari *peoples* wanaita *peoples*ni uharibifu wa hali ya juu. Nimeshuhudia kule kwangu hawa jamaa wamechoma nyumba, mpaka akinamama

wamepigwa na mimba zimetoka Kilando kwa ushahidi ninao. Leo mnakuja kusema Polisi, milijifanya Polisi nyie mlisika kwenu Sheria mkononi ilikuwa watu hawatembe ndugu zangu mnatishia namsifu Mheshimiwa Dkt. Magufuli amenyoosha nchi vibaya hii ilikuwa nchi imefikia pabaya. Milijifanya nyie madume nyie lakini leo wamewashika kusema kweli tunaishi kwa amani na utulivu, tulikuwa sehemu mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kilando kule mpakani tena ndiyo kulikuwa kubaya zaidi mlikuwa mnakuja vifua mbele leo kusema kweli tunashukuru Serikali ya Awamu ya Tano tunatembea na sisi vifua mbele wakati wetu mlikuwa mnadhalilisha wakati wa uchaguzi mdogo tu mnaiba masanduku ya kura, mnachoma masanduku ya kura ushahidi kabisa Jimbo la Kwela kwa Malocha mlichoma masanduku nyile. Kilando wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa Chadema walichoma masanduku ya kura ilikuwa nchi imeharibika sasa imerudi nidhamu, hii ni nidhamu ya hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Jeshi la Polisi liendelee na mkazo huo huo, mlikuwa mmetupeleka kubaya mpaka wana CCM wanaogopa kuвая mpaka nguo za kijani mnawatishia na nyie sasa ni wakati wenu kuacha kuвая magwanda. Tunakwenda kinidhamu zamu kwa zamu. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Keissy sema!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu lazima tuliona sisi wote nchi ilipofikia tulifikia pabaya nimekaa kule mtu anakuja anaitisha m Kutano mnakaa mnamuona kuanzia asubuhi ni matusi tu anamtukana Rais wa nchi. Nilimwambia Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne mimi Mheshimiwa Jakaya Mliso Kikwete nilimwambia Mheshimiwa takuja kukata mtu kichwa halafu wewe ndiyo utakwenda Mahakamani sitakubali wewe Rais wa nchi unatukanwa nasikiliza na Mapolisi wanasiliza hawachukue hatua yoyote tulifikia pabaya, hata Polisi

walikuwa hawachukue hatua yoyote kwa ushahidi ninao nilizungumza. Wanakumbuka tulikuwa Wabunge Awamu ya Nne hapa nilizungumza, nikamwambia Mheshimiwa Kikwete hawa jamaa wakija kwangu Namanyere wakikutukana tu nitakata kichwa cha mtu, wamezidi hakuna nidhamu dunia nzima hakuna nidhani lazima tuheshimiane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Rais ameweka nidhamu ya hali juu tumuunge mkono na sisi tuendelee tufanye kazi naunga mkono Serikali kusema kweli ndiyo tulisema TV /live namna wanazungumzia hovyohovsky /live gani hii mazungumzo gani haya wana record kwenye *you tube* wanasantaba. Lakini hotuba zote mzee ni kichaka ni kuchochea angalieni ndugu zangu, nchi zingine angalieni Libya tangu leo amefariki Gaddafi miaka mingapi Libya imetulia?

**MBUNGE FULANI:** Hajatulia.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mpaka leo, Libya hajatulia mpaka leo mshukuru ninyi mmekaa hapa familia zenu kule nyumbani mkipiga simu ni salama, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mathayo Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza nikupongeze kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hii hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Lugola, pamoja na Naibu Waziri Masauni pamoja na uongozi wote wa Jeshi la Polisi na Majeshi yote kwa kazi nzuri ambayo mnaendelea kuwatumika watanzania hongereni sana. Yako mambo ambayo ya waziwazi katika hiki kifupi tumeweza kuyaona ambayo watanzania wote naamini watakubaliana na mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja suala la ajali kusema kweli Jeshi la Polisi limezisimamia na zimepungua kwa kiasi kikubwa. Lakini kama hiyo haitoshi leo inaweza kufika saa

hizi saa mbili nikaondoka hapa kwenda zangu Musoma saa mbili za usiku nikafika Musoma salama pasipokuwa na matatizo yoyote kwa sababu Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri sana. Naendelea kazi yangu ni kuendelea tu kuwaombea kwamba hebu endeleeni kufanya kazi hiyo nzuri watanzania waendelee kuishi kwa amani na utulivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe mambo machache ambayo yamezungumziwa katika hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kati ya matatizo ambayo Serikali na Wizara ya Mambo ya Ndani inapaswa kuyafanya kazi imesema hapa vizuri kwenye ukurasa wa 11 kwamba Mheshimiwa Rais bilioni kumi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 400 za maaskari wetu na ni ukweli usiopingika kwamba maaskari wetu ni kati ya watu ambao maeneo yao ya kuishi si mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano pale Musoma kwamba ziko nyumba bahati nzuri baada ya kuwa nimepiga kelele toka mwaka 2005 kweli Serikali ikawa sikivu ikaanza kujenga maghorofa mawili pale ambayo yangebeba maaskari wa kutosha. Lakini nakuambia hadi leo tunavyozungumza yale maghorofa yamekamilika kwa asilimia zaidi ya 85 lakini yameshindwa kumaliziwa mara wanaiba milango, mara wanaiba mabomba ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini hizi nyumba zitakamilika ili walau wale maaskari wachache waweze kujistili kuliko wanavyoishi sasa wanaishi kwanza wengine uraiani, lakini wengine wanaishi kwenye zile nyumba za *full suit* ambapo wanaishi kwa tabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine Mheshimiwa Waziri wewe unafahamu kwamba pale Mjini Musoma pale ndipo Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Mara. Kuna jengo ambalo lilijengwa toka mwaka 2013 jengo la *RPC* lile jengo limeishiwa kwenye *basement* hadi leo jengo hilo liko hapo hapo. Sasa nataka nifahamu mpango wa kulijenga jengo hili ili Jeshi la Polisi waweze kufanya kazi zao vizuri. Lakini

halikadhalika askari Magereza wote bado hawana nyumba na hata maeneo yao ya kuishi si mazuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba Mheshimiwa Waziri haya majibu utaweza kutufafanulia ili watu wa Musoma waweze kujua namna tunavyoweza kuwasaidia katika haya majengo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo moja kubwa ambalo Mheshimiwa Waziri binafsi nilishalileta kwako, na nilishakuja na Mkurugenzi wa maji, Jeshi la Polisi Mkoa wa Mara pamoja na Magereza Polisi wenyewe wanadaiwa zaidi milioni 850 za maji na Magereza wanadaiwa zaidi milioni 360.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matokeo yake katika baadhi ya maeneo mengi ya Musoma Mjini kwenye zile Kata za pembezoni kama Rwamlimi, kama Bweli kule Kwanga mpaka kule Makoko tunakosa maji kwa sababu ziko fedha ambazo Jeshi la Magereza pamoja na Polisi walipata huduma lakini ni kwamba wameshindwa kulipa n hizo fedha kama zingepatikana zingetusaidia katika kuboresha maji katika Mji wetu wa Musoma.

Sasa ningependa kufahamu mpango wa kulipa haya madeni katika bajeti hii utaweza kutulipa ili walau haya matatizo yaweze kupungua. Pamoja na hayo madeni baada ya kuwa yamelipwa ni imani yangu kwamba yatatusaidia sana katika kuboresha Mji wetu wa Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nichangie vilevile kidogo kwenye upande wa Jeshi la Magereza. Nashukuru na tumeangalia pale katika *page 28* Mheshimiwa Rais alifanya kazi kubwa ya kuweza kusema kwamba sasa Jeshi la Magereza lazima wajitosheleze kwa chakula na akaonesha kwamba sasa hivi wanalima mnalima kama eka 4,000 na kitu sasa zitalimwa mpaka eka 12,000 na kusema kweli hii ni kazi nzuri ni kazi ya kupongezwa na niseme tu kwamba Jeshi la Magereza wakijipanga vizuri tatizo la chakula hata kwenye Taasisi zetu za Serikali kama shule hilo tatizo litaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kusema kweli mtu anapofungwa anafungwa mwaka mmoja anafungwa miaka mitatu kulingana na *speed* ya maendeleo, akitoka kule ndani tunategemea kwamba akienda kule ndani apate nafasi ya kujifunza mambo mengi ambayo ni pamoja na kilimo ni pamoja na ufundi. Sasa tunapowafunga tu na kuwaweka kule ndani akitoka huku nje baadhi ya wafungwa wengi wakiachiwa huru wanatamani warudi ndani ya gereza kwa sababu sasa wanakuta huku nje huku maisha yameenda *speed* mambo mengi hawayafahamu sasa wanaona kwamba ni afadhali tena arudi magereza kwa sababu kule magereza anapata chakula cha bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kushauri kwamba mbali na suala la kuwafunza kilimo, vilevile Magereza wanayo nafasi kubwa ya kujifunza mafunzo mbalimbali yanayoweza kuboresha maisha yao. Lakini watakapotoka kule sasa watakuja kwanza wamejirudi lakini watapata mahala pa kuanzia kuliko vile wanavyofungwa, wanakaa mle ndani akitolewa hapo anaenda kusafisha mtalo matokeo yake anatoka kule pasipokuwa na ujuzi. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba tunapokuwa tunawapeleka mtu anapofanya makosa na akapelekwa Magereza tafsiri yake ni kwamba tunataka ajirudi vilevile ajifunze na baada ya hapo aje kuwa raia mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni imani yangu kwamba tukiendelea kuwasaidia hawa Jeshi la Magereza wanaweza wakafanya kazi nzuri zaidi ya kuzalisha na kukuza uchumi wa nchi hii. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge nadhani kwa leo imetosha niwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge kwa mchango wenu ni Wizara muhimu sana hii, naelewa yote mnayoyasema kwa nia njema na ndiyo maana inafika mahali *temperature* inapanda halafu pia inashuka, lakini tupo mikono salama.

Kwa hiyo, sina matangazo niwashukuru sana kwa kunipa msaada tangu saa tatu asubuhi na baada ya hapo tulipoanza tena mchana huu. Kwa hiyo, sina la ziada naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Tarehe 25 Aprili, 2019, siku ya Alhamisi Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi,  
Tarehe 25 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*